# CHANGAMOTO ZA KIMOFOSINTAKSIA MIONGONI MWA WANAFUNZI WA KISWAHILI WA SHULE ZA UPILI WILAYANI MUHANGA, NCHINI RWANDA

**TASNIFU YA**

**NTAWIYANGA SYLVAIN**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**Juni, 2015**

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**UNGAMO**

Utafiti huu ni kazi yangu mwenyewe na haijapata kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

Sahihi………………………………Tarehe……08/06/2015……

Ntawiyanga Sylvain

C50EA/24421/2011

Utafiti huu umewasilishwa katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi.

Sahihi………………………………Tarehe……25/06/2015……

Dkt. Chacha L. M.

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Kenyatta

Sahihi ………………………………Tarehe 25/6/2015……………………

Prof. Mbaabu I.

Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Kenyatta

# IKISIRI

Utafiti huu ulitarajia kuchunguza "Changamoto za kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda". Pamoja na kuzingatia kuwa kipengele cha kimofosintaksia ndicho kiini cha lugha yoyote ile na kuwa vipengele vingine vya sarufi huingiliana nacho na kukitegemea kwa kiwango kikubwa, utafiti huu ulilenga kwanza kubainisha makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi hao. Lengo la pili lilikuwa kuainisha makosa hayo; la tatu, kubainisha vyanzo vya makosa hayo wakati ambapo lengo la nne lilihusu kutathmini mikakati iliyozingatiwa na walimu kwa kupunguza makosa ya wanafunzi wao. Utafiti huu uliongozwa na nadharia za Uchanganuzi Makosa (UM) na Lugha Kadirifu (LK) na unajitokeza katika tafiti za kimaelezo. Data zilikusanywa nyanjani kwa kuzihusisha shule tatu wilayani Muhanga : Groupe Scolaire de Kirwa, Groupe Scolaire de Nyarusange na Groupe Scolaire de Shyogwe. Mbinu ya kimakusudi ilizingatiwa katika usampulishaji na watafitiwa walipatikana kwa kutumia mbinu nasibu. Wanafunzi kumi walichaguliwa katika madarasa ya tano na sita kutoka shule hizo na hojaji na mahojiano ndiyo yaliyozingatiwa kukusanya data kutoka kwa wanafunzi hao na walimu wao. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunza Kiswahili hufanya makosa hasa katika vipengele vya mpangilio wa maneno katika sentensi, upatanishi wa kisarufi na urejeshi wa ngeli katika tungo zao. Makosa mengi yaliyobainishwa yalijikita katika uchopekaji wa vipashio katika tungo, udondoshaji wa vipashio katika tungo, mchanganyiko na matumizi mabaya ya viambishi, mchanganyiko wa aina za maneno na uundaji wa sentensi ndefu. Aidha, uchunguzi wa lugha kadirifu ya wanafunzi ulibainisha pia mikakati ya kisaikolojia waliyoizingatia katika ujifunzaji wao ambapo lugha hii iliathiriwa kwa namna tofauti. Utafiti huu ulidhihirisha kwamba wanafunzi wengi waliweza kuhamisha baadhi ya vipengele vya kiisimu vya Kinyarwanda na kuvitumia katika Kiswahili, kuchanganya ndimi, kujumuisha kanuni za kisarufi za Kiswahili, kutohoa maneno na kutafsiri miundo ya Kinyarwanda hadi Kiswahili. Mbali na hayo, utafiti huu ulibainisha kuwa wanafunzi waliathiriwa na ufundishaji ambapo ukosefu wa vifaa vya kufundishia, mpangilio wa silabasi na muda mfupi uliotengewa ufundishaji wa Kiswahili ulijitokeza kama chanzo msingi cha makosa yao ya kimofosintaksia. Isitoshe, utafiti huu ulichunguza mikakati iliyozingatiwa na walimu katika ufundishaji ambapo mazoezi ya kisarufi, ya utunzi wa insha na masimulizi yaliandaliwa na kutolewa wanafunzi. Hata hivyo, uchunguzi wa mikakati hii ulidhihirisha kwamba nafasi ya wanafunzi katika utambuzi wa makosa waliyoyafanya haikujitokeza bayana na kuwa kazi za makundi hazikupewa kipaumbele katika upunguzaji wa makosa yao. Aidha, utafiti huu ulitoa mapendekezo kwa wadau mbalimbali wa ufundishaji wa Kiswahili ili kuwaita kuchangia katika uimarishaji wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili, nchini Rwanda.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na afya ya kukamilisha utafiti huu. Pili, shukrani zangu za dhati zimwendee Dkt. L. Chacha na Prof. I. Mbaabu ambao waliokubali kuongoza na kusimamia kazi hii. Shukrani zangu pia ziwaendee walimu wote wa Idara ya Kiswahili kwa kunifundisha katika masomo yangu ya uzamili. Baadhi yao ni Prof. King'ei, Dkt. Wafula, Dkt. Maitaria, Prof. Ndungo, Dkt. Ngugi, Dkt.Osore, Dkt. Mwihaki na Bi. Gathenji ambaye alinisaidia sana kwa kuniazima vitabu vyake mwenyewe. Usaidizi wake ulinifaa zaidi kwa kuelekeza utafiti huu kinadharia. Siwezi kuwataja wote hapa, lakini nasema 'asante sana' kwenu nyote mlionisaidia na kunielimisha.

Namshukuru sana mke wangu Denyse Umuhoza kwa kunionyesha mapenzi, kunipa moyo, kuwa karibu nami kila nilipohitaji na hata kuvumilia kukaa peke yake nyumbani na kuendeleza shughuli zote za nyumba na kutimiza wajibu wake wa malezi ya watoto yeye mwenyewe. Ninashukuru sana kwa hayo yote na mengine ambayo siwezi kutaja hapa.

Shukrani ziwaendee wazazi wangu Martin Uwimana na Consolée Nakabonye kwa kuniweka shuleni na walimu wote walionifundisha katika viwango vilivyotangulia kiwango hiki na kuniwekea misingi bora ya elimu. Nawashukuru Yamuragiye, Mukarangwa, Nyirahabineza, Habineza na familia yangu. Maombi na mahimizo yenu yaliniwezesha kufikia kiwango hiki. Aidha, nawashukuru Prof. Nzabarirwa, Prof. Nsanzabiga, Prof. Ntakirutimana, Dkt. Niyomugabo, Dkt. Ahimana, Dkt. Kolbusa, Dkt. Kayi, Bw. Kaniu, Bw. Twilingiyimana, Bw. Kimenyi, Bw. Bazirushaka na

wengine wote mlionifaa sana ili niweze kuendeleza masomo katika kiwango cha uzamili. Maoni yenu na mapendekezo yenu yalinijenga sana katika masomo yangu.

Nashukuru pia Wizara ya Elimu, nchini Rwanda iliyokubali kufadhili masomo yangu, Chuo Kikuu cha Rwanda, Koleji ya Elimu waliokubali kinipa likizo ya kuendeleza masomo yangu. Walimu wakuu, walimu na wanafunzi wa Kiswahili wa Shule za Groupe Scolaire de Kirwa, Groupe Scolaire de Cyeza, Groupe Scolaire de Shyogwe na Groupe Scolaire de Nyarusange nao wanastahili heshima isiyomithilika kwa kukubali kushirikishwa katika utafiti huu. Matokeo yake yatawafaa sana.

Siwezi kuwasahau wanafunzi wenzangu tuliosoma pamoja katika Idara ya Kiswahili. Shukrani zangu ziwaendee Oginda, Onyango, Musotsi, Mwilaria, Haule, Ometty, Anyango, Wambui, Midika, Nanjala, Sigei, Kioko na Omuya kwa jinsi tulivyoshirikiana na kukaa pamoja kwa muda mrefu. Ntawiha, Habinshuti, Twagirimana, Ngugi, Nsengiyumva, Mukarwego, Tuyisenge na wengine mlionifaa sana kwa namna mbalimbali katika masomo yangu, nawashukuru sana. Kuwepo kwenu kulichangia sana katika ufanisi wa masomo yangu.

Mungu awabariki ninyi nyote mliohusika katika utafiti huu.

# TABARUKU

Kwa mke wangu mpendwa Denyse Umuhoza,

Kwa watoto wangu Divine Kwizera Uwacu na David Izere Iradukunda,

Kwa wazazi wangu Martin Uwimana na Consolée Nakabonye,

Kwa ndugu zangu,

Nawatuza kazi hii.

**Mofosintaksia:** Tawi la isimu linalohusisha uchunguzi wa kimofolojia na wa kisintaksia.

**Sintaksia**: Tawi la isimu linalochunguza mpangilio wa maneno katika tungo.

## ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| * | Tungo yenye kosa la kimofosintaksia |
| $A_0$ | Shahada |
| $A_1$ | Stashahada |
| $A_2$ | Cheti cha masomo ya shule ya upili |
| Dham. | Dhamira |
| Kau. | Kauli |
| Kia. | Kiambishi |
| Kiang. | Kiambishi ngeli |
| Kie. | Kielezi |
| Kih. | Kihusishi |
| Kii. | Kiishio |
| Kikan. | Kikanushi |
| Kiony. | Kionyeshi |
| Kip. | Kipatanishi |
| Kirj. | Kirejeshi |
| Kiung. | Kiunganishi |
| Kiv. | Kivumishi |
| Kiw. | Kiwakilishi |
| KN | Kirai Nomino |
| Ksb. | Kisabiki |
| Kt. | Kitenzi |
| Ktesh. | Kitendeshi |

| | |
|---|---|
| L1 | Lugha ya kwanza |
| L2 | Lugha ya pili |
| LK | Lugha Kadirifu |
| LL | Lugha Lengwa |
| MINEDUC: | Wizara ya Elimu |
| Mz. | mzizi |
| Nfs. | Nafsi |
| Ng. | Ngeli |
| Nom. | Nomino |
| UL: | Uchanganuzi Linganuzi |
| UM: | Uchanganuzi Makosa |
| Wkt. | Wakati |
| Wktim. | Wakati uliotimilika |
| Wktpit. | Wakati uliopita |
| Wktuj. | Wakati ujao |
| Wktulp. | Wakati uliopo |
| Wktzo. | Wakati wa mazoea |
| Yam. | Yambwa |

**YALIYOMO**

UNGAMO ........................................ ii

IKISIRI ........................................ iii

SHUKRANI ........................................ iv

TABARUKU ........................................ vi

UFAFANUZI WA ISTILAHI ........................................ vii

ORODHA YA ALAMA NA VIFUPISHO ........................................ ix

YALIYOMO ........................................ xi

ORODHA YA MAJEDWALI ........................................ xviii

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ........................................ 1

1.0 Usuli ........................................ 1

1.1 Suala la utafiti ........................................ 5

1.2 Maswali ya utafiti ........................................ 5

1.3 Malengo ya utafiti ........................................ 6

1.4 Sababu za kuchagua mada ........................................ 6

1.5 Upeo na mipaka ........................................ 9

1.6. Yaliyoandikwa kuhusu mada ........................................ 10

1.7 Misingi ya nadharia ........................................ 17

1.7.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ........................................ 17

1.7.1.1 Historia fupi ya nadharia ya Uchanganuzi Makosa ........................................ 17

1.7.1.2 Mihimili ya nadharia ya Uchanganuzi Makosa ........................................ 19

1.7.1.3 Udhaifu wa nadharia ya Uchanganuzi Makosa ........................................ 21

1.7.2 Nadharia ya Lugha Kadirifu ........................................ 22

1.8 Mbinu za utafiti .......... 25
1.8.1 Muundo wa utafiti .......... 25
1.8.2 Mbinu za usampulishaji .......... 26
1.8.3 Mbinu za kukusanya data .......... 28
1.8.3.1 Hojaji .......... 28
1.8.3.2 Mahojiano .......... 30
1.8.4 Vifaa vya utafiti .......... 31
1.8.4.1 Hojaji .......... 32
1.8.4.2 Kiongozi cha mahojiano .......... 33
1.8.4.3 Kinasa sauti .......... 33
1.8.5 Jaribio la utafiti .......... 34
1.8.6 Uzingativu wa maadili .......... 34
1.8.7 Uchanganuzi wa data .......... 35
1.8.8 Uwasilishaji wa matokeo .......... 36
1.9 Hitimisho .......... 36
SURA YA PILI: MOFOSINTAKSIA YA NGELI ZA NOMINO KATIKA KISWAHILI NA KINYARWANDA .......... 37
2.0 Utangulizi .......... 37
2.1 Dhana ya ngeli .......... 37
2.2 Upatanishi wa kisarufi .......... 38
2.3 Mofosintaksia ya ngeli katika Kiswahili .......... 39
2.3.1 Mtazamo wa kimofolojia wa ngeli .......... 39
2.3.1.1 Msingi wa kutumia viambishi vya nomino .......... 41

2.3.1.2 Msingi wa kutumia viambishi vya umoja na wingi ...... 43
2.3.2 Mtazamo wa kisintaksia wa ngeli ...... 46
2.3.2.1 Matumizi ya viambishi vya ukubalifu katika sentensi ...... 47
2.3.2.2 Utaratibu wa kutumia viambishi vya upatanishi vya umoja na wingi ...... 48
2.3.2.3 Utaratibu wa kutumia vionyeshi ...... 50
2.3.3 Matumizi ya kiambishi cha nomino na kiambishi cha upatanishi ...... 51
2.4 Urejeshi wa ngeli katika Kiswahili ...... 52
2.4.1 Virejeshi vya kati ...... 53
2.4.2 Virejeshi vya mwisho ...... 55
2.4.3 Urejeshi wa ngeli katika vivumishi na viwakilishi ...... 56
2.5 Mofosintaksia ya ngeli za nomino katika Kinyarwanda ...... 58
2.5.1 Muundo wa nomino katika Kinyarwanda ...... 59
2.5.1.1 Kisabiki kiambishi awali ...... 59
2.5.1.2 Kiambishi ngeli ...... 61
2.5.1.3 Mzizi ...... 69
2.5.2 Upatanishi wa kisarufi katika Kinyarwanda ...... 70
2.5.2.1 Nomino na kivumishi ...... 71
2.5.2.2 Upatanishi wa nomino na kiwakilishi ...... 72
2.5.2.3 Upatanishi wa nomino na kitenzi ...... 74
2.6 Ulinganishaji wa mfumo wa ngeli katika Kiswahili na Kinyarwanda ...... 78
2.7 Hitimisho ...... 84
SURA YA TATU: MAKOSA YA KIMOFOSINTAKSIA YA WANAFUNZI ...... 85
3.0 Utangulizi ...... 85

3.1 Makosa ya wanafunzi kutokana na tungo za kukamilisha ..........85
3.1.1 Upatanishi wa nomino na kivumishi ..........86
3.1.1.1 Nomino na kivumishi cha sifa ..........86
3.1.1.2 Nomino na kivumishi kimilikishi ..........88
3.1.1.3 Nomino na kivumishi cha idadi ..........89
3.1.1.4 Nomino na kionyeshi ..........90
3.1.1.5 Nomino na kiulizi ..........91
3.1.1.6 Nomino na vivumishi vya pekee ..........91
3.1.1.7 Upatanishi wa nomino na kiwakilishi ..........93
3.1.2 Nomino na kitenzi ..........94
3.2 Makosa yaliyotokana na uandishi wa insha ..........96
3.2.1 Mpangilio wa maneno katika sentensi ..........96
3.2.2 Makosa ya upatanishi wa kisarufi ..........98
3.2.2.1 Nomino na kivumishi ..........99
3.2.2.1.1 Nomino na kivumishi cha sifa ..........99
3.2.2.1.2 Nomino na kivumishi cha -a unganifu ..........100
3.2.2.1.3 Nomino na kivumishi cha idadi ..........100
3.2.2.1.4 Nomino na kimilikishi ..........101
3.2.2.1.5 Nomino na kionyeshi ..........102
3.2.2.1.6 Nomino na kivumishi cha pekee ..........103
3.2.2.2 Upatanishi wa nomino na kitenzi ..........104
3.2.2.3 Urejeshi wa nomino katika kitenzi ..........105
3.2.3 Jumla ya wanafunzi waliofanya makosa katika uandishi wa insha ..........106

3.3 Makosa kutokana na masimulizi ya wanafunzi ........ 107
3.3.1 Mpangilio wa maneno katika tungo ........ 108
3.3.2 Makosa katika upatanishi wa kisarufi ........ 109
3.3.2.1 Nomino na vivumishi ........ 109
3.3.2.1.1 Nomino na kivumishi cha sifa ........ 109
3.3.2.1.2 Nomino na kivumishi cha a-unganifu ........ 110
3.3.2.1.3 Nomino na kivumishi cha idadi ........ 111
3.3.2.1.4 Nomino na kionyeshi ........ 112
3.3.2.1.5 Nomino na kivumishi kimilikishi ........ 112
3.3.2.1.6 Nomino na kivumishi cha pekee ........ 113
3.3.2.2 Upatanishi wa nomino na kitenzi ........ 114
3.3.2.3 Urejeshi wa nomino katika vitenzi ........ 115
3.3.3 Jumla ya wanafunzi waliofanya makosa katika masimulizi ........ 117
3.4 Aina za makosa yaliyofanywa na wanafunzi ........ 119
3.4.1 Uchopekaji wa vipashio katika tungo ........ 119
3.4.2 Udondoshaji wa vipashio katika tungo ........ 120
3.4.3 Mchanganyiko wa viambishi na matumizi ya viambishi visivyofaa ........ 122
3.4.4 Mchanganyiko wa aina za maneno ........ 123
3.4.5 Uradidi wa vipashio pasipotarajiwa ........ 123
3.4.6 Uhamishaji wa vipashio na mpangilio mbaya wa maneno katika tungo ........ 124
3.4.7 Uundaji wa sentensi ndefu ........ 126
3.5 Hitimisho ........ 127

SURA YA NNE: CHANZO CHA MAKOSA YA WANAFUNZI NA MIKAKATI INAYOZINGATIWA KUYAPUNGUZA........................... 129

4.0 Utangulizi........................................................................................................ 129

4.1 Vyanzo vya makosa ya wanafunzi.................................................................. 129

4.1.1 Uhamishaji wa kiisimu................................................................................ 130

4.1.2 Kuchanganya ndimi..................................................................................... 134

4.1.3 Utohozi usiofaa........................................................................................... 136

4.1.4 Tafsiri........................................................................................................... 137

4.1.5 Uzoefu mdogo na ukosefu wa habari......................................................... 140

4.1.6 Ujumuishaji.................................................................................................. 144

4.2 Utambuzi wa makosa ya wanafunzi na chanzo chake.................................. 152

4.3 Mikakati ya kupunguza makosa ya wanafunzi............................................. 157

4.3 Hitimisho........................................................................................................ 160

SURA YA TANO.................................................................................................. 162

HITIMISHO.......................................................................................................... 162

5.1 Utangulizi........................................................................................................ 162

5.2 Muhtasari wa utafiti........................................................................................ 162

5.3 Matokeo ya utafiti........................................................................................... 165

5.4 Changamoto..................................................................................................... 168

5.5 Mapendekezo................................................................................................... 170

5.5.1 Mapendekezo kuhusu serikali na viongozi wengine................................... 170

5.5.2 Mapendekezo kuhusu walimu...................................................................... 173

5.5.3 Mapendekezo kuhusu wanafunzi................................................................. 174



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

5.5.4 Mapendekezo ya kufanya tafiti zaidi ........ 174

5.6 Hitimisho ........ 175

MAREJELEO ........ 176

VIAMBATISHO ........ 184

KIAMBATISHO A: HOJAJI KWA WANAFUNZI ........ 184

KIAMBATISHO B: HOJAJI KWA WALIMU ........ 186

KIAMBATISHO C: KIONGOZI CHA MAHOJIANO KWA WANAFUNZI ... 188

KIAMBATISHO D: KIONGOZI CHA MAHOJIANO KWA WALIMU ........ 189

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Uainishaji wa ngeli kwa kutumia vimbishi awali vya nomino ............ 42

Jedwali 2.2: Mitazamo ya kuainisha ngeli kimofolojia ........................................ 45

Jedwali 2. 3 Mchango wa vipatanishi vya nomino katika uainishaji wa ngeli ......... 49

Jedwali 2.4: Mtazamo wa kutumia vionyeshi katika uainishaji wa ngeli ................ 51

Jedwali 2.5: Matumizi ya umbo rejeshi "o" katika Kiswahili ................................ 54

Jedwali 2.6: Mfumo wa ngeli katika Kinyarwanda ............................................... 62

Jedwali 2.7: Makundi ya ngeli ya umoja na wingi katika Kinyarwanda ................. 64

Jedwali 2.8: Utambuzi wa mzizi katika Kinyarwanda............................................ 70

Jedwali 2.9: Upatanishi wa kisarufi katika Kinyarwanda ...................................... 76

Jedwali 2.10: Ngeli za Kiswahili na za Kinyarwanda ............................................ 79

Jedwali 2.11: Upatanishi wa ngeli katika vitenzi vya Kiswahili na Kinyarwanda.... 81

Jedwali 3.1: Upatanishi wa nomino na kivumishi cha sifa .................................... 87

Jedwali 3.2: Upatanishi wa nomino na kivumishi kimilikishi ................................ 88

Jedwali 3.3: Upatanishi wa nomino na kivumishi cha idadi ................................... 89

Jedwali 3.4: Upatanishi wa nomino na kionyeshi ................................................. 90

Jedwali 3.5: Upatanishi wa nomino na kiulizi....................................................... 91

Jedwali 3.6: Upatanishi wa nomino na kivumishi cha pekee ........ 92

Jedwali 3.7: Upatanishi wa nomino na kiwakilishi ........ 93

Jedwali 3.8: Upatanishi wa nomino na kitenzi ........ 95

Jedwali 3.9: Wanafunzi waliofanya makosa katika uandishi wa insha ........ 106

Jedwali 3.10: Wanafunzi waliofanya makosa katika masimulizi ........ 117

Jedwali 4.1: Upatanishi wa wanafunzi baada ya kutafsiri KN katika L1 ........ 137

Jedwali 4.2: Tafsiri za moja kwa moja ........ 139

Jedwali 4.3: Kiwango cha masomo cha walimu ........ 145

Jedwali 4.4: Tajiriba ya walimu ........ 146

Jedwali 4. 5: Vitabu vilivyotumiwa na walimu katika ufundishaji wa sarufi ........ 147

Jedwali 4.6: Maoni ya walimu kuhusu vitabu vya sarufi wanavyovitumia ........ 148

Jedwali 4.7: Maoni ya walimu kuhusu mpangilio wa silabasi ya somo la Kiswahili 149

Jedwali 4.8: Maoni ya walimu kuhusu ngeli zinazotatiza wanafunzi ........ 152

Jedwali 4.9: Maoni ya walimu kuhusu chanzo cha makosa ya kimofosintaksia ........ 154

Jedwali 4.10: Mikakati ya walimu ya kupunguza makosa ya kimofosintaksia ........ 157

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli

Lugha kuu zinazotumika nchini Rwanda ni Kinyarwanda ambayo ni lugha ya Taifa na rasmi, Kiingereza na Kifaransa ambazo ni lugha rasmi na Kiswahili ambacho hadhi yake mpaka sasa haijadhihirishwa. Kiswahili ndiyo lugha ya kigeni iliyowasili kwa mara ya kwanza nchini humo na ilianza kufundishwa kuanzia wakati wa ukoloni wa Wajerumani katika shule za msingi mwaka 1907 (Bizimana, 2002). Lugha hii ndiyo ilikuwa inawaunganisha viongozi na raia katika nchi zote za Afrika Mashariki zilizotawaliwa wa Wajerumani kiasi kwamba nchini Rwanda lugha ya Kiswahili ilionekana kama lugha ya uungwana na ujuzi kama wanavyoeleza Karangwa (1986) na Munyakazi (1984). Hali hii ilibadilishwa polepole chini ya utawala wa Wabelgiji mpaka miaka ya 1930 ambapo wakoloni hawa walilenga kufuta athari zote za utawala wa Wajerumani baada yao kushindwa Vita vya Kwanza vya Dunia. Kwa hivyo, hadhi ya Kiswahili ilishushwa na kuachia nafasi Kifaransa ambacho kilitumiwa pamoja na Kinyarwanda katika shughuli zote rasmi (Bizimana, keshatajwa).

Vilevile, baada ya uhuru wa Rwanda, Wanyarwanda wengi walikuwa na mtazamo hasi dhidi ya Kiswahili wakikihusisha na lugha ya wadanganyifu na watu wa mjini ambao hawana nafasi kijijini na mahali pa kufanya kazi. Basigayabo (1992) anasema kuwa jina "Umuswayile" (Mswahili) lilihusishwa na mtu mwenye hila, mkosa kabila, yaani mtu ambaye hafai kutangamana na wengine na kuaminika nao. Hata hivyo, Ntawigira (2011) anaporejelea hali hii, anadhihirisha kuwa mtazamo huu ulianza

kubadilika polepole baada ya mauaji ya kimbari ya mwaka 1994 dhidi ya Watutsi. Wakati huu Wanyarwanda wengi waliokuwa wamekimbilia nchi kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Tanzania, Uganda na Kenya ambako Kiswahili kinatumika walirejea nchini. Hawa walikuwa wakitumia Kiswahili katika maongezi yao na jambo hili liliwaathiri raia wengine na kuwatia hamu ya kukitumia. Mabadiliko hayo ya kimtazamo yalichochewa pia zaidi na kitendo cha nchi ya Rwanda kujiunga na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo raia wengi wa nchi za jumuiya hiyo hutumia Kiswahili. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa watumiaji wa Kiswahili wameongezeka sana ikilinganishwa na vipindi mbalimbali vya awali.

Mbaabu (2005) anatathmini maendeleo ya Kiswahili nchini Rwanda kwa kusema kuwa nchini humo Kiswahili kimeanza kuimarika zaidi kutokana na matarajio ya kujiunga na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zinatumia lugha ya Kiswahili. Anabainisha kuwa nchini Rwanda nafasi ya Kiswahili ni muhimu zaidi hasa wakati huu wa mapinduzi ya kipekee yanayohusu lugha. Rwanda inawafundisha raia wake Kiswahili na Kiingereza kimeshachukua nafasi ya Kifaransa pale ambapo masomo shuleni hufunzwa katika Kiingereza na Kifaransa kufunzwa kama somo (MINEDUC, 2013). Mbaabu anasema kuwa hatua hizi zitawezesha Rwanda kutumia lugha sawia na nchi zingine katika Afrika Mashariki. Kwa hivyo, ni wazi kwamba kutafiti kuhusu Kiswahili ni jambo linaloweza kuchangia mno katika juhudi hizo za kuendeleza na kuimarisha lugha hii nchini Rwanda hasa wakati huu ambapo nchi hii imeshajiunga na Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mnamo mwaka 2008, serikali ya Rwanda ilianzisha mpango wa elimu wa kuifanya elimu ya shule za upili kuwa ni elimu ya msingi kwa wote ambapo kila tarafa kunakuwa na shule angalau moja (MINEDUC, 2013). Kwa kuwa Kiswahili kinafunzwa katika shule za upili, sera hiyo imefanya wanafunzi wengi waweze kufunzwa lugha hii, hasa wale wanaojifunza masomo yao katika muungano wa Kiingereza, Kiswahili na Kinyarwanda. Hata hivyo, miongoni mwa lugha zinazofundishwa, Kiswahili ndiyo lugha inayofunzwa kwa muda wa miaka mitatu peke yake na nyingi za shule zinazokifundisha zimejengwa katika tarafa za vijijini ambapo miundo msingi haijaboreshwa ili kusaidia katika ujifunzaji. Aidha, shule hizi za vijini hupokea mara nyingi wanafunzi ambao hawakuweza kupata alama za kutosha zinazowawezesha kujiunga na shule zenye miundo msingi imara.

Kwa hivyo, kazi hii ilinuia kuchunguza ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili miongoni mwa wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunza lugha hii katika shule za upili, shughuli ya utafiti inayopatikana katika taaluma pana ya Isimu Tumikizi. Alan (2007) analieleza tawi hili la kiisimu kama taaluma inayojishughulisha na maswala mbalimbali ya lugha kwa lengo la kusuluhisha matatizo yanayojitokeza katika maisha halisi ya watumiaji wa lugha hiyo. Hivyo basi, utafiti huu ulichunguza makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi Wanyarwanda katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Kipengele hiki cha mofosintaksia ni kipengele muhimu katika lugha kwani huchunguza vipashio vya kimofolojia vya maneno na kuonyesha jinsi ambavyo vinaweza kuungana kwa ajili ya kuunda kipashio kikubwa zaidi ambacho ni sentensi.

Singleton na Lengyel (1995) wanabainisha kuwa ujifunzaji wa lugha ya pili huwa rahisi kadiri umri wa mwanafunzi ulivyo mdogo. Lakini, silabasi ya Kiswahili inayofuatwa katika shule za upili nchini Rwanda inaonyesha kuwa ujifunzaji wa lugha hii huanzia kidato cha nne hadi cha sita ambapo wanafunzi wanatakiwa kuwa na uwezo wa kuchanganua mambo changamani na ambayo pia ni mengi mno ikizingatiwa kuwa lugha hii ni ngeni kwao. Nao Steinberg na wengine (1982) wanathibitisha kuwa uelewa wa miundo changamano ya lugha huhitaji akili iliyopevuka ya mtumiaji wa lugha hiyo na kuwa mwanafunzi anahitaji mazoezi ya kimazungumzo na kimaandishi ili kutumia kwa njia mwafaka kanuni anazojifunza. Kwa hivyo, ni jambo la kawaida kuweza kutokea wanafunzi Wanyarwanda kufanya makosa ya kimofosintaksia wakati wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Tafiti mbalimbali kama vile Musau (1993), Onyango (1997), Mudhune (1994) na Mutugu (2001) zilionyesha kuwa lugha ya kwanza huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili na kuthibitisha athari za uhamishaji wa vipengele vya kisarufi kutoka lugha ya mama hadi ya pili.

Makosa yanayofanywa na wanafunzi wakati wao wa ujifunzaji wa lugha ya pili huweza kuelezwa kwa namna tofauti. Lakini, maelezo hayo huangukia katika makundi mawili yaliyozungumziwa na Amando na wengine (2007), Corder (1974), Norrish (1983) na Campbell na Wales (1970). Tafiti hizo ziliweza kutofautisha makosa yanayotokana na utendaji wa mtu na yale ya kiumilisi wake. Kundi la kwanza la makosa halihusiani na ujuzi wa mtu bali utendaji wake. Nalo kundi la pili ndilo linalodhihirisha makosa yanayohusiana na ujuzi wa mtu. Makosa huwa ni kielelezo

cha umilisi wa mzungumzaji, yaani dirisha la kuchungulia matukio yaliyomo bongoni na hasa mfumo wa kanuni anazozimiliki mzungumzaji huyo. Kwa hivyo, utafiti huu ulijaribu kueleza na kufafanua makosa ya kimofosintaksia yanayofanywa na wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, kupitia uandishi na uzungumzi wao.

## 1.1 Suala la utafiti

Kimenyi (2003) anaeleza kuwa kuna upungufu mkubwa katika maandalizi na mafunzo ya lugha ya Kiswahili katika shule za upili nchini Rwanda. Anatetea hoja hiyo kwa kusema kuwa kuna ujuzi mdogo wa walimu wanaofunza lugha hiyo na uhaba wa vifaa vinavyohitajika kufunzia lugha yenyewe. Naye Ntawigira (2011) anabainisha jambo hilo anaposema kuwa nchini Rwanda, kutokupewa nafasi kubwa kwa lugha ya Kiswahili kunasababisha kudumaa kwa wanafunzi wanapojifunza lugha hii na kukwamiza juhudi zingine za maendeleo yake. Kwa hivyo, ni wazi kuwa wanafunzi wanatatizika wanapojifunza somo hilo kwa kukumbana na changamoto za aina tofauti zinazostahili kuchunguzwa. Katika utafiti huu, changamoto za kimofosintaksia ndizo zilizochunguzwa ili kudhihirisha vipengele vya sarufi ya Kiswahili vinavyoathirika kutokana na upungufu wa ujifunzaji wa lugha hii kama ulivyogusiwa katika kazi hizo tangulizi. Eneo la msamiati huwa ni rahisi zaidi ikizingatiwa kuwa Kiswahili na Kinyarwanda zote ni lugha za Kibantu na sarufi huwa ndio ufunguo wa mfumo wa lugha yoyote ile (Cook, 1996).

## 1.2 Maswali ya utafiti

Utafiti huu ulilenga kujibu maswali yafuatayo:

1. Ni makosa gani ya kimofosintaksia yanayowakumba wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili, wilayani Muhanga, nchini Rwanda?
2. Kuna aina gani za makosa ya kimofosintaksia yanayofanywa na wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili nchini Rwanda?
3. Nini chanzo cha makosa ya kimofosintaksia yanayofanywa na wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili nchini Rwanda?
4. Ni mikakati ipi inayozingatiwa ili kupunguza au kuondoa makosa ya kimofosintaksia yanayofanywa na wanafunzi wa shule za upili nchini Rwanda?

## 1.3 Malengo ya utafiti

Malengo yafuatayo yaliongoza utafiti huu:

1. Kubaini makosa ya kimofosintaksia yanayofanywa na wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda.
2. Kuainisha makosa ya kimofosintaksia yanayofanywa na wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda.
3. Kuchunguza chanzo cha makosa ya kimofosintaksia yanayofanywa na wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili nchini Rwanda.
4. Kutathmini mikakati inayozingatiwa katika kupunguza makosa ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili nchini Rwanda ili kutoa mapendekezo.

## 1.4 Sababu za kuchagua mada

Ntakirutimana (2000) anabainisha kuwa katika nchi zilizoendelea kuna lugha moja ambayo imekuzwa kimakusudi kwa ajili ya mawasiliano kama vile Kiingereza au

Kifaransa, lakini katika nchi nyingi za Ulimwengu wa Tatu hakuna lugha moja ambayo imekuzwa kwa makusudi kwa ajili hiyo. Kwa hivyo, anapendekeza kuwa Kiswahili kingekuwa Kiingereza cha Afrika ili kiweze kuunganisha Waafrika na dunia nzima. Hali hii ingeyaondoa baadhi ya matatizo ya wananchi wake kwa kuwawezesha kutosheleza mahitaji yao ya msingi kutoka nchi moja hadi nyingine. Hali hii husisitizwa pia na Kiango (2002) anaposema kuwa kuna haja ya kuwepo kwa lugha moja ambayo ingeweza kuwaungaanisha watu wenye tamaduni na lugha mbalimbali kwa ajili ya maingiliano na mashirikiano katika shughuli za biashara na nyinginezo za kijamii. Kwa hivyo, ni wazi kuwa katika jamii zetu kuna haja ya kujifunza Kiswahili na kuinua hadhi yake ili kukiendeleza kulingana na umuhimu wake katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na zile za kijamii.

Katika kazi hii, tulitarajia kuangazia matatizo yanayokwamiza ujifunzaji wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili Wilayani Muhanga. Tuliamini kuwa matokeo ya utafiti wetu yatatusaidia kutoa mapendekezo kwa Serikali ya Rwanda na watu wengine wanaohusika na ufunzaji wa lugha hii kwa jumla ili kuwahimiza kuchukua hatua zinazofaa katika maendeleo ya lugha hii yenye umuhimu wa lugha ya kimataifa barani Afrika na hata nje ya Afrika. Baada ya wanafunzi hawa kufahamu makosa wanayoyafanya na kuanza kutumia Kiswahili kwa njia sahihi ndipo wangeweza kuwafaidi raia wengine wanaowategemea katika ujifunzaji wa lugha hii. Ndiyo sababu kuchunguza makosa yao ya kisarufi kulikuwa jambo lililofaa kutafitiwa.

Rwanda ni mojawapo ya nchi ambapo ingawa Kiswahili kimedhihirishwa kama lugha muhimu kwa wananchi, hakijapewa uzito wake na hadhi yake haijabainishwa wazi kikifananishwa na lugha zingine zinazotumiwa nchini humo. Katika hali kama hii, kutafiti kuhusu Kiswahili kungeweza kusaidia sana kuinua hadhi yake miongoni mwa Wanyarwanda kwa jumla na hasa kwa wanafunzi wa shule za upili wanaojiunga na mafunzo ya lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hawa wakizungumza lugha hii kwa ufasaha wangeweza kufurahia uwezo wao na kuwavutia watu wengine kwa kuwafanya wawe na hamu ya kujifunza pia lugha hii. Kwa hivyo, utafiti huu utaleta mchango katika kupunguza au hata kuondoa vikwazo vinavyojitokeza katika ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili ambayo ndiyo nguzo ya kutumia lugha kwa kufanikisha mawasiliano miongoni mwa watumiaji wake.

Kazi hii itawawezesha wanafunzi kufahamu aina na kiwango cha makosa wanayoyafanya katika sarufi ili kujitahidi kuyarekebisha. Walimu wao pia wataweza kuwa na ufahamu wa vipengele muhimu vinavyofaa kusisitizwa wakati wanapofundisha. Wakuzamitaala nao kwa upande wao wataweza kuelewa namna bora ya kupanga masomo katika silabasi zinazotumiwa katika viwango tofauti vya ujifunzaji na kuandaa vitabu vinavyowafaa kulingana na viwango hivyo. Isitoshe, wapangaji lugha nao wataweza kupata mwangaza wa kuwaelekeza katika ugawaji wa majukumu kwa lugha zinazotumika nchini Rwanda.

Kwa kuwa moja ya malengo ya utafiti huu lilikuwa kutathmini mikakati inayofanywa ili kupunguza makosa ya wanafunzi wa Kiswahili, ni dhahiri kuwa matokeo yake yatawezesha walimu na wakuzamitaala kutafuta vitabu vinavyoafikiana na kiwango

cha ufahamu wa wanafunzi hao kwa kuzingatia vipengele vilivyobainika kuwatatiza katika ujifunzaji wao. Vilevile kazi hii huenda ikasaidia kuboresha mbinu zinazotumiwa katika ufundishaji wa somo la Kiswahili katika mfumo wa wingilugha unaotumiwa nchini Rwanda na kuwachochea watafiti wengine kuendeleza utafiti dhidi ya ujifunzaji wa Kiswahili kwa kuchunguza vipengele vingine vya sarufi ambavyo havikushughulikiwa katika kazi hii au hata na viwango vingine vya lugha kwa jumla.

### 1.5 Upeo na mipaka

Ni kawaida kwa makosa ya kisarufi kuweza kuwa katika matawi yote ya sarufi; yaani fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Hata hivyo, katika utafiti huu zilichunguzwa changamoto za kimofosintaksia kwani aghalabu changamoto katika matawi mengine ya kisarufi hujidhihirisha pia katika matawi ya mofolojia na sintaksia. Mbaabu (1995) anasema kuwa kosa la kimatamshi linaweza pia kuwa la kisarufi na linaweza kuathiri maana ya matamshi au maandishi. Naye Mohamed (1988) anaeleza jambo hili anaposisitiza kuwa maingiliano baina ya vipengele hivyo vya lugha hutegemea kwa kiasi kikubwa mofolojia na sintaksia. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa uchunguzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi katika kiwango cha mofosintaksia huweza kutoa sura kamili inayoweza kuyatatua matatizo mengi yanayokwamiza ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili katika shule za upili nchini Rwanda. Uchunguzi huo ulizingatia hasa matumizi ya ngeli katika vipengele vya upatanisho wa kisarufi na urejeshi wa ngeli hizo kwani hii ni sifa mojawapo muhimu inayozibainisha lugha za Kibantu.

Licha ya kuwa nchini Rwanda, Kiswahili kinafunzwa katika shule za upili na katika vyuo vikuu, utafiti huu uliwahusu wanafunzi wa shule za upili pekee kwa kuwa ngazi hiyo ya awali ndiyo msingi wa ujifunzaji na hivyo kuichunguza na kuijengea msingi mzuri kungewezesha pia ngazi zinazofuata kuwa bora. Shule tatu za upili wilayani Muhanga ndizo zilizohusishwa katika utafiti huu: Shule ya Groupe Scolaire de Kirwa, Groupe Scolaire de Nyarusange na Shule ya Groupe Scolaire de Shyogwe. Shule hizi zinafunza Kiswahili na zimejengwa katika maeneo tofauti pale ambapo shule mbili za kwanza ni za vijijini na ya tatu ni ya mjini. Kwa hivyo, tulitumai kwamba matokeo yetu yangeweza kujumuisha hali halisi ya matatizo ya kimofosintaksia kwa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga.

### 1.6. Yaliyoandikwa kuhusu mada

Watafiti mbalimbali walishughulikia maswala ya aina tofauti kuhusiana na mada hii ya ujifunzaji wa lugha ya pili kwa jumla. Katika tafiti zao, walichunguza viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na msamiati kwa kutumia mikabala tofauti kiasi kwamba maswala yanayosisitizwa katika kazi moja hutofautiana na yale yaliyoshughulikiwa katika kazi nyingine kwani uwanja wa lugha kwa jumla ni mpana na ni vigumu mtafiti mmoja kuuchunguza kikamilifu. Kwa hivyo, kuna maeneo ambayo bado yanahitaji kushughulikiwa ili kuzikamilisha kazi zilizotangulia hii. Katika sehemu hii, tuliangazia mambo yaliyoandikwa katika uwanja wa ujifunzaji wa lugha ya pili kwa jumla na tulijikita hasa katika ufafanuzi wa kazi zilizoshughulikia ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili kwa malengo ya kuonyesha jinsi ambavyo kazi hii inavyoingiliana na kutofautiana na hizo zilizoitangulia.

Skinner (1957) anaeleza kuwa mtu hujifunza lugha kwa njia anayotumia kujifunza aina zingine za tabia. Watoto wanajifunza kutembea, kukimbia, kula, kuimba na kadhalika. Baadaye wataweza kujifunza stadi zingine kama vile kupika na kuendesha baiskeli. Kwa hivyo, Skinner anadhihirisha kuwa ujifunzaji wa lugha hufanywa kama mtoto anavyojifunza tabia hizo na ndiyo sababu dhana ya urudiaji ni muhimu. Chomsky (1959) alitupilia mbali mtazamo huu wa Skinner na kusema kuwa unafanya ujifunzaji uweze kuangukia katika ujumlishaji ambao ndio chanzo cha makosa yanayofanywa na wanaojifunza lugha. Kwa hivyo, alipendekeza kuwa ujifunzaji wa lugha uhusishwe na maelekezo ya kanuni ambazo ndizo zinazoongoza. Ujifunzaji unahusisha sana vigezo vya ndani badala ya kuangalia vigezo vya nje kwani mtoto anaelekezwa na kiunzi msingi cha ujifunzaji. Chomsky alishikilia kuwa ujifunzaji wa lugha utegemee vigezo hivyo vya ndani na kubainisha kuwa watoto wanazaliwa na kiunzi msingi kinachowawezesha kujifunza lugha. Ujifunzaji wa lugha unaongozwa na kanuni na unahusisha michakato iliyo changamano.

Lado (1957) alionyesha kuwa katika uchunguzi wa ujifunzaji wa lugha ya kwanza (L1) na lugha ya pili (L2), miundo fanani na ile inayotofautiana ni lazima iangaziwe. Miundo ya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na hata mifumo ya kitamaduni ni lazima ichunguzwe kwa lengo muhimu la kuweza kutabiri miundo inayoweza kurahisisha ujifunzaji na ile inayoweza kutatiza. Anazidi kusema kuwa uhamishaji ni jambo muhimu linalofaa kuchukuliwa hatua na ndiyo maana anatoa wito kwa walimu ili waweze kufundisha vipengele hivyo vinavyotofautiana kwani ndivyo chanzo cha makosa yanayojitokeza katika L2. Kwa hivyo, anasisitiza kuwa matatizo ya



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

wanafunzi katika ujifunzaji wao yatatofautiana kadiri lugha zao za kwanza zinavyotofautiana.

Ellis (1985, 1994) alijadili kwa upana nadharia mbalimbali za ujifunzaji wa L2 na kutoa maelezo msingi yanayoweza kuzingatiwa katika ujifunzaji wa L2. Pamoja na tafiti zingine zilizotajwa hapo juu, kazi hizi zitatufaa zaidi katika utafiti wetu kwa kutuelekeza kinadharia na kubainisha mipaka ya utafiti huu. Nguvu na udhaifu wa nadharia zilizozungumziwa katika kazi hizo ndizo zilizingatiwa kuchagua nadharia mwafaka zilizotuongoza. Hata hivyo, tafiti hizi ni tofauti na utafiti wetu kwa kuwa zilizingatia mwelekeo wa kinadharia bila kuingia katika utendakazi wa nadharia zenyewe ambapo utafiti wetu ulitumia nadharia teule na kuzitumia katika mazingira mahususi ya ujifunzaji wa L2.

Mbaabu (1995) alizungumzia usahihishaji wa makosa katika Kiswahili na kubainisha kuwa makosa yanayofanywa huweza kugawanywa katika makundi manne ambayo ni kundi la kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi. Kazi hii ilionyesha kuwa makundi haya huingiliana na kuwa chanzo cha makosa mengi ya kimatamshi ni maingiliano ya L1 na Kiswahili sanifu. Makosa mengine ya kisarufi yanahusu kuchanganya viambishi vya ngeli tofauti. Nayo makosa ya kimaana yanasababishwa na upungufu wa msamiati pamoja na athari za L1. Ujuzi wa L1, unyonge wa kutojitahidi katika kuyatamka maneno ambao hujitokeza katika maandishi na upungufu wa msamiati na mazoezi ya matumizi ya lugha ndiyo mambo yanayosababisha makosa ya kisauti katika maandishi ya wanafunzi wengi. Utafiti huu unaingiliana na wetu kwa kuwa unahusu makosa yanayofanywa na wanafunzi wa L2

ambayo ni Kiswahili. Tofauti kati ya utafiti huo na wetu ni kwamba unazungumzia makosa yanayofanywa na wanafunzi kwa kuzingatia matawi tofauti ya sarufi ya Kiswahili na kuonyesha jinsi yanavyoweza kusahihishwa kupitia mazoezi mbalimbali. Utafiti wetu ulijikita katika makosa ya kimofosintaksia katika mazingira mahususi ya wanafunzi wa Kiswahili, yaani wilayani Muhanga, nchini Rwanda.

Musau (1993) alishughulikia ujifunzaji wa kifonolojia kwa wanafunzi Wanandi, Wakamba, Wakikuyu, Wabukusu, Wasomali, Wamasai na Waluo wa shule za msingi nchini Kenya na kubainisha makosa yanayojitokeza kwa makundi hayo tofauti. Utafiti wake ulidhihirisha kuwa wanafunzi hawa wanapojifunza fonolojia ya Kiswahili wanatatizwa kutokana na msingi walio nao wa lugha zao za mama. Uhamishaji na ujumuishaji ni baadhi ya mbinu zinazotumiwa na wanafunzi hawa kujiundia lugha kadirifu au fonolojia ya kati ya lugha za mama na Kiswahili. Tofauti kubwa kati ya utafiti huo na wetu ni kwamba ulijikita katika uchunguzi wa makosa ya kifonolojia ambapo utafiti wetu ulichunguza makosa ya kimofosintaksia.

Mudhune (1994) alifanya uchunguzi linganuzi wa mofosintaksia ya Kiswahili kwa wanafunzi Waluo na kudhihirisha kwamba tofauti za kisarufi kati ya Kiswahili na Kiluo ni changamoto kubwa kwa wanafunzi hao wanapojifunza Kiswahili. Chanzo cha makosa mengi yanayofanywa na wanafunzi hao kilikuwa tofauti hizo. Utafiti huo ulijikita katika uchunguzi wa kiulinganuzi ambao unawiana na utafiti wa Onyango (1997) ambaye naye alibainisha tofauti za kisarufi zilizopo kati ya Kinyala na Kiswahili. Watafiti hawa wote wanakubaliana kuwa makosa mengi yaliyofanywa na wanafunzi yalitokana hasa na athari za lugha za kwanza za wanafunzi waliotafitiwa.

Tafiti hizo zinahusiana na utafiti wetu kwani zote zinahusu ujifunzaji wa Kiswahili kama L2. Hata hivyo, utafiti wetu ni tofauti na hizo kwani eneo lililotafitiwa ni tofauti na maeneo yaliyozingatiwa katika tafiti hizo. Vilevile misingi ya kinadharia ni tofauti pale ambapo wao wamezingatia nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (UL) kama nguzo iliyowaelekeza katika tafiti zao ambapo utafiti wetu ulijikita haswa katika nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM).

Mutugu (2001) alishughulikia makosa ya kileksia na chanzo chake miongoni mwa wanafunzi Waembu. Utafiti wake ulionyesha kuwa makosa yanayofanywa hufuata mikondo mbalimbali kama vile yale yanayohusiana na L1 ya wanafunzi hawa ambayo ni Kikikuyu. Matokeo aliyoyapata ni kuwa wanafunzi waliweza kuchanganya sauti hasa zile ambazo zipo katika Kiswahili na ambazo hazipo katika Kikikuyu. Makosa ya uhamishaji na ujumuishaji yalijitokeza pale ambapo wanafunzi wanahamisha misemo moja kwa moja kutoka lugha ya Kikikuyu na hata Kiingereza hadi Kiswahili na pale ambapo wanajumuisha matumizi ya sheria wanazozimudu katika L1 na kuzitumia katika miktadha ambayo haifai. Ingawa utafiti huo ulishughulikia ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 ni tofauti na wetu kwani ulichunguza eneo la kileksia ambapo utafiti wetu ulichunguza eneo la kisarufi.

Cheruiyot (2011) alizungumzia matatizo ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa Kikipsigis wanaojifunza Kiswahili sanifu. Katika utafiti wake alibainisha kuwa utaratibu wa muundo wa sentensi za Kiswahili na ule wa Kikipsigis ni tofauti kwani lugha hii siyo lugha ya Kibantu. Kwa hivyo, alionyesha kuwa makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi wengi hutokana na athari za lugha ya kwanza. Utafiti

wake ulidhihirisha kuwa wanafunzi wa Kikipsigis walitatizika sana katika upatanishi wa kisarufi kwani lugha ya Kikipsigis haina sifa hii. Makosa mengine yalitokana na ujumuishaji mno wa maumbo ya sarufi ya Kiswahili. Utafiti huu unahusiana na wetu kupitia nadharia ya Lugha Kadirifu (LK) iliyozingatiwa kueleza chanzo cha makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi watakaotafitiwa. Hata hivyo, utafiti huo ni tofauti na wetu kwani nadharia msingi ya utafiti wetu ni UM. Vilevile utafiti huo ulichunguza makosa yanayofanywa na wazungumzaji wa L1 ambayo ni Kikipsigis ambacho huhesabiwa katika lugha za Kinailoti ambapo L1 ya watafitiwa wetu, Kinyarwanda, ni lugha ya Kibantu.

Kwa jumla, tafiti hizo hapo juu zilifanywa nchini Kenya na zinakubaliana kuwa kujifunza lugha ya pili kuna changamoto kubwa za kisarufi hususan kutokana na athari ya lugha ya kwanza, jambo ambalo linatarajiwa kudhihirika pia kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili nchini Rwanda ikizingatiwa kuwa lugha hii siyo ya kwanza kwao. Changamoto hizo za kisarufi zilikuwa muhimu zichunguzwe ili kuweza kujenga mazingira mazuri ya kuzitatua na hivyo kuwawezesha wanafunzi hao kuifahamu kwa ufasaha sarufi ya lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, tafiti hizo ni tofauti na utafiti wetu kutokana na mazingira tofauti ya ujifunzaji wao. Wengi wa waliotafitiwa katika kazi hizo za awali huwa mara nyingi wamekwenda shuleni wakiwa na ufahamu wa aina fulani wa Kiswahili na ujifunzaji wao wa Kiswahili huanzia shule za msingi. Wengi wa wanafunzi Wanyarwanda hukuta Kiswahili shuleni tu kutoka kwa walimu wao na ujifunzaji wake huanzia rasmi katika darasa la

nne la shule za upili kiasi kwamba matatizo wanayokumbana nayo miaka hiyo mitatu ni mengi.

Nchini Rwanda, tafiti mbalimbali zilifanywa kuhusu lugha ya Kiswahili kwa jumla. Miongoni mwa kazi muhimu tunazoweza kutaja hapa ni pamoja na Ntawigira (1997) na (2011), Niyibizi (1980), Nyabaguma (1984), Karangwa (1986), Kalisa (1992), Niyomugabo (1992), Basigayabo (1992), Kimenyi (2003). Nyingi ya kazi hizo zilijikita katika uchunguzi wa nafasi na matumizi ya Kiswahili katika asasi mbalimbali kama vile utangazaji, dini na mashirika ya kibiashara kama vile MAGERWA na zilichukua mwelekeo wa kiisimujamii kwa jumla. Kazi chache tu ndizo zilichunguza nafasi ya Kiswahili katika uwanja wa elimu na hazikujishughulisha na ujifunzaji wake kama lugha ya pili.

Miongoni mwa tafiti tulizozichukulia kuwa muhimu ni Ntawigira (2011). Kazi hii ilichunguza sera ya lugha nchini Rwanda kwa kudhihirisha lugha zinazotumiwa katika shughuli za umma na asasi zingine. Vilevile, ilichunguza mielekeo ya Wanyarwanda kuhusu matumizi ya lugha zote nne zinazofunzwa shule za upili; Kiswahili, Kinyarwanda, Kiingereza na Kifaransa. Kwa hivyo, kazi hiyo ilijaribu kuonyesha nafasi ya Kiswahili katika shule za upili hasa ikilinganishwa na lugha zingine zinazofunzwa. Utafiti huu unahusiana sana na ule uliofanywa na Kimenyi (2003) kwani naye alizungumzia hali ya Kiswahili katika elimu ya shule za upili nchini Rwanda na kubainisha umuhimu wake kwa wanafunzi Wanyarwanda.

Kwa hivyo, ni wazi kwamba nchini Rwanda hakuna utafiti uliofanywa na kudhihirisha hali ya ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi

Wanyarwanda kwa kuzingatia makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi hawa wakati wanapojifunza Kiswahili. Hilo ni pengo lililohitajika kuzibwa kupitia utafiti huu hasa wakati huu wa baada ya Rwanda kuanzisha mfumo mpya wa elimu ya msingi ya miaka kumi na miwili kwa wote.

### 1.7 Misingi ya nadharia

Sehemu hii inahusu misingi ya nadharia zilizozingatiwa katika utafiti huu. Kwa hivyo, nadharia za Uchanganuzi Makosa (UM) na Lugha Kadirifu (LK) zilifafanuliwa ili kudhihirisha jinsi zilivyoweza kukamilishana katika kazi hii.

#### 1.7.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa

Ili kuelewa vyema nadharaia hii ya UM, ni bora kwanza kuzingatia historia yake kwa kifupi na kubainisha sababu zilizotuchochea kuichagua dhidi ya nadharia zingine zinazohusika na ujifunzaji wa L2. Mihimili iliyozingatiwa katika utafiti huu imeelezwa na hatimaye udhaifu wake nao ukajadiliwa ili kuonyesha mapengo yaliyozibwa na nadharia ya Lugha Kadirifu (LK) kwa kufanikisha kazi hii.

##### 1.7.1.1 Historia fupi ya nadharia ya Uchanganuzi Makosa

Uchanganuzi Makosa (UM) ni nadharia iliyopata mwelekeo miaka ya 1970 wakati ambapo ilichukua nafasi ya nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi (UL) ambayo ilikuwa ikizingatiwa katika tafiti nyingi juu ya ujifunzaji wa L2 kuanzia miaka ya 1940 hadi miaka ya 1960. Hata hivyo, Ellis (1994) anasema kuwa uchunguzi wa makosa ulikuwepo tangu muda mrefu na ulikuwa ukichukuliwa kama sehemu moja ya mbinu za ufundishaji wa lugha. Ellis (keshatajwa) anasema kuwa French (1949), kwa mfano, alikuwa amejaribu kutoa maelezo kuhusu makosa ya kijumla ya

wanafunzi na kuwa Lee (1957) naye alikuwa amefafanua makosa katika maandishi ya wanafunzi na kuyapanga katika kategoria tofauti.

Mbali na hayo, nadharia ya UM ilitolewa mwelekeo kutokana na kutangazwa kwa makala ya Corder (1974) wakati ambapo utafiti juu ya L2 ulileta mtazamo mpya. Tangu wakati huu, nadharia hii ilianza kutambulika kama sehemu ya Isimu Tumikizi. Makosa katika nadharia ya UL iliyokuwa ikizingatiwa hapo mbeleni yalikuwa yakitazamwa tu kama matokeo ya maingiliano ya L1 na L2 na mwalimu aliweza kutabiri makosa ya wanafunzi ili kulenga kufundisha tofauti za kiisimu kati ya L1 na L2. Kwa hivyo, wakati ambapo nadharia ya UL ilizingatia miundo sahihi ya L1 na L2, nadharia ya UM ilitilia mkazo mbinu za kuichunguza lugha ya mwanafunzi. Makosa katika nadharia ya UM huchukuliwa kama ishara kwamba mwanafunzi anajaribu kujifunza na kuelewa mfumo wa lugha lengwa (LL). Kwa hivyo, nadharia ya UM inampatia mwanafunzi nafasi ya kutosha katika ujifunzaji kwa kuchunguza makosa anayoyafanya katika ujifunzaji wake.

Tafiti mbalimbali zilizofanywa kuhusu ujifunzaji wa L2 miaka hiyo ya 1970 zilizidi kuonyesha kuwa makosa mengi hayangeweza kufafanuliwa tu kwa msingi wa uhamishaji wa L1 katika mchakato wa kujifunza L2 kama ilivyokuwa ikifanywa katika UL (Dulay na Burt, 1973 na 1974). Vilevile, tafiti hizo zilidhihirisha kuwa maswali mengi yalikuwa yakibaki bila maelezo yoyote katika nadharia ya UL. Hivyo basi, nadharia ya UM ilianza kuchukua nafasi ya UL kwa uwezo wake wa kuchanganua makosa ya aina mbalimbali ya wanafunzi wa L2 bila kujikita tu katika makosa yanayotokana na athari za L1.

### 1.7.1.2 Mihimili ya nadharia ya Uchanganuzi Makosa

Kwa mujibu wa Ellis (1994), hatua zifuatazo tano ndizo muhimu katika UM: kukusanya data, kubainisha makosa, kuyafafanua, kuyaeleza na kuyatathmini.

*Ukusanyaji wa data*

Katika hatua hii ya kwanza data hukusanywa katika njia ya maandishi au masimulizi. Hii ni hatua muhimu kwani makosa ya kimasimulizi na yale ya kimaandishi huweza kutofautiana ikizingatiwa kuwa watu mara nyingi huwa makini hasa wanapoandika kuliko wanavyoweza kufanya wanapozungumza.

*Kubainisha makosa*

Hii ni hatua ya pili ambapo mtafiti huyabainisha makosa baada ya kulipata kongoo kutoka kwa lugha ya mwanafunzi. Hatua hii humwezesha mtafiti kwanza kuamua mapema mambo muhimu au sifa zinazoyabainisha makosa ya mwanafunzi. Pili, mtafiti anajiwekea kanuni za kuzingatia katika uchunguzi wake wa kuyabainisha makosa. Tatu, uamuzi hufanywa kwa kuzingatia makosa yaliyo bayana na yale yasiyo bayana. Hayo ya kwanza hutokea pale ambapo mwanafunzi anafanya makosa ya kiumilisi na hayo ya pili huhusu fani zinazodhihirishwa kama makosa lakini zikawa tofauti na kile kilichomo bongoni au akilini mwa mwanafunzi.

*Kufafanua makosa*

Kulingana na Ellis (1994), maelezo kuhusu makosa ya mwanafunzi yanaleta ulinganishaji wa semi za mwanafunzi na miundo inayopaswa kuzingatiwa katika lugha lengwa. Mara nyingi hali hii huambatana sana na uainishaji wa makosa yaliyobainishwa katika hatua iliyotangulia. Burt na Krashen (1982) katika Ellis



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

(1994) wamejaribu kuonyesha vigezo vifuatavyo vinavyoweza kuzingatiwa katika ufafanuzi wa makosa.

| **Kategoria** | **Maelezo** |
|---|---|
| Udondoshaji | Hali ambapo kipashio hudondoshwa katika muundo sahihi |
| Uchopekaji | Hali ya kuongeza kipashio kisichotarajiwa katika muundo sahihi |
| Ukosefu wa habari | Matumizi mabaya ya muundo, mofimu isiyofaa au muundo usiofaa |
| Mpangilio usio sahihi | Hali mbaya ya mfuatano wa mofimu au kifungu cha mofimu katika usemi |

Ellis (1994 : 56)

Mifano hii inaonyesha kuwa ufafanuzi wa makosa huambatana na uainishaji wake pale ambapo makosa hupangwa katika kategoria totaufi kulingana na vigezo alivyojiwekea mtafiti. Vilevile, katika hali hii ya ufafanuzi wa makosa ya mwanafunzi ndipo mtafiti huweza kuonyesha pia kiwango cha makosa hayo ili kudhihirisha makosa yanayotokea kwa nadra na yale yanayotokea mara kwa mara na kufanyiwa uchunguzi wa kina katika hatua inayofuata.

***Kueleza makosa***

Hatua ya nne katika UM ni kueleza makosa yaliyobainishwa na kufafanuliwa. Ellis (1994) anadhihirisha kuwa kuyaeleza makosa kunachangia sana katika kuonyesha chanzo cha makosa hayo. Kwa hivyo, uchanganuzi makosa unaleta uwezo mkubwa wa kupata maelezo ya makosa ya mwanafunzi wa L2 hasa kwa kuzingatia vipengele viwili: kipengele cha undani wa lugha na kipengele cha kati au maingiliano ya lugha. Makosa katika hiki cha pili yanaweza kutokana na lugha ya kwanza kwani yanahusisha mifumo ya lugha tofauti.

Nayo makosa ya undani lugha hujitokeza wakati yanapotokana na lugha yenyewe inayofunzwa au inayochunguzwa. Haya ni makosa ya kimaendeleo katika muktadha

wowote wa ujifunzaji lugha. Mara nyingi kosa linalofanywa na mwanafunzi katika mfano huu ni la ujumuishaji wa baadhi ya kanuni za kisarufi anazozimudu mwanafunzi.

***Kutathmini makosa***

Ellis (1994) anasema kuwa hatua hii ya kutathmini makosa ni jambo linalohusiana na kuchunguza athari za makosa kwa mwanafunzi anayetafitiwa kwa ajili ya kuboresha mikakati ya ufundishaji wa lugha. Kwa hivyo, ni lazima kuangalia upande wa mwanafunzi anayejifunza lugha hiyo ili kujua kama ni mzawa wa lugha hiyo au la. Vilevile, kunazingatiwa umahiri wa wanaohusika katika ufunzaji kama vile walimu na kuchunguza ikiwa maamuzi yanayofanywa yanalenga kiini au kiwango cha makosa husika. Zaidi ya hayo, sababu za utokeaji wa makosa fulani zinaangaliwa pia ili kutambua uzito wa makosa fulani miongoni mwa makosa yote yaliyobainishwa. Hapa ndipo tunakuta kuwa njia za kuepuka makosa hayo huweza kupendekezwa kama suluhisho kwa makosa yaliyobainishwa. Sharma (1980) katika Khansir (2012) anasema kuwa UM huweza kuwa mbinu nzuri ya kupunguza au kuondoa matatizo katika ufundishaji kwa kuonyesha nguvu na udhaifu wa silabasi inayofuatwa.

### 1.7.1.3 Udhaifu wa nadharia ya Uchanganuzi Makosa

Matumizi ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa yanabainisha upungufu wa aina tofauti ambao ni lazima kuujadili katika sehemu hii ili kuonyesha jinsi ulivyoweza kufidiwa na nadharia ya LK katika kazi hii. Ellis (1994) anasema kuwa tafiti nyingi zilizozungumzia udhaifu wa nadharia hii zilirejelea kwamba UM hutilia mkazo

michakato ya ufundishaji wa L2 na kuichukulia kama kifaa kisichoweza kuonyesha picha kamili ya lugha ya mwanafunzi.

Schachter na Mriane (1977) wanaeleza kuwa nadharia ya UM inasisitiza kuhusu uchanganuzi wa makosa na kupuuza matumizi sahihi yanayojitokeza kwa upande wa mwanafunzi na jitihada zake katika ujifunzaji wake wa L2. Jambo hili linatiliwa mkazo na Ellis (1994) anapodhihirisha kuwa UM huchunguza lugha inayozungumzwa na mwanafunzi wa L2 bila kuzingatia hatua mbalimbali za maendeleo ambazo mwanafunzi huyu huzipitia wakati wa kujifunza lugha hiyo.

Aidha, wanaojifunza lugha hujiongezea ujuzi hatua baada ya hatua na mifumo ya lugha ya mwanafunzi hubadilikabadilika kulingana na vipindi tofauti vya ujifunzaji wake. Jambo hili halitiliwi maanani katika UM na linaingiliana na changamoto nyingine inayoweza kujitokeza pale ambapo mwanafunzi huweza kukwepa kutumia miundo anayoiona kuwa migumu kwake na kutumia ile ambayo ana uhakika nayo kuwa sahihi (Khansir, 2012). Kwa hivyo, mtafiti huweza kupata ugumu wakati wa kuchunguza vyanzo vya makosa hayo na kuyatathimini kwa ukamilifu. Mapengo haya ndiyo yaliyozibwa kwa kutumia nadharia ya Lugha Kadirifu (LK) ambayo ilijadiliwa katika sehemu hii inayofuata.

### 1.7.2 Nadharia ya Lugha Kadirifu


Nadharia ya Lugha Kadirifu (LK) ilitolewa mwelekeo na Selinker (1972) baada ya kugusiwa na watafiti mbalimbali waliotumia istilahi tofauti kumaanisha lugha kadirifu. Kwa mfano, Nemser (1971) alikuwa amezungumzia mifumo kadirifu, James (1971) lugha ya kati na Corder (1971) lahaja ya kipekee. Nadharia hii ya LK

inaashiria mfumo wenye utaratibu katika ujifunzaji wa lugha ya pili na inazingatia lugha anayojiundia mwanafunzi wakati wa ujifunzaji wake. Norrish (1983) anaeleza kuwa Lugha Kadirifu inahusishwa na mfumo ulioundwa na mwanafunzi na ambao anajiwekea wakati wa kujifunza lugha. Mfumo huu wa mwanafunzi unajengwa na elementi tofauti za kiisimu ambazo hutokana na L1 na L2 wakati ambapo zingine hazina chanzo chochote kati ya hivyo.

Wananadharia kama vile Corder (1974) na Nemser (1971) wanaiona lugha kadirifu kama mfumo unaobadilikabadilika. Kulingana nao, lugha kadirifu ni istilahi inayotumiwa kurejelea sarufi mpito inayoundwa na wanaojifunza L2 katika mwelekeo wao wa kuijua lugha lengwa (LL). Jambo linalojitokeza hapa ni kwamba lugha kadirifu inajengwa kupitia kipindi fulani mwanafunzi anapojaribu kwa mfano kutumia mbinu tofauti za undani lugha kwa kuzingatia data alizo nazo kuhusu L2 na kudhibiti matumizi yake. Kwa hivyo, mwanafunzi wa L2 atakuwa na miundo tofauti ya lugha kadirifu kwa viwango vya ujifunzaji wake. Katika hali hii, Corder (1974) na Nemser (1971) wanasema kuwa mwanafunzi anabainisha umilisi wa mpito na kuwa lugha kadirifu inalenga kuelezea mfumo wa lugha ya mwanafunzi katika kipindi fulani.

Selinker (1972) alipendekeza kuwa LK hujitokeza kati ya L1 na L2 na kudhihirisha kuwa wanafunzi wengi wa lugha ya pili wafikao asilimia 95 hushindwa kufikia moja kwa moja umilisi wa lugha lengwa (LL). Ujifunzaji wa lugha hii huchukuliwa kama mchakato unaoendelea na usiokatizwa mpaka mwanafunzi anapoweza kuimudu. Mwanafunzi anayejifunza kwa mfano Kiswahili kama L2, atakuwa na uwezo wa

kuzungumza lugha kadirifu tofauti kabla afikie kiwango cha kuzungumza Kiswahili kamili kama mzaliwa wake. Krezeszowski (1981) katika Musau (1993) anatoa kielelezo kifuatacho kwa kuzingatia mchakato wa uundaji wa LK uliobainishwa na Selinker (1972) na huweza kutudhihirishia hali halisi ya utendakazi wa nadharia ya LK.




Kutokana na kielelezo hicho cha uhusiano kati ya L1, LK na LL, tunaweza kupata kuwa mwanafunzi huweza kujiundia mifumo tofauti katika ujifunzaji wake kabla afikie mfumo tarajiwa wa LL. Selinker (keshatajwa) anadai kuwa miundo fiche ya kisaikolojia ndiyo hufanya kazi wakati mwanafunzi anapojaribu kujifunza L2. Kulingana na Selinker (1972), mchakato wa kwanza unadhihirisha kuwa mwanafunzi anaweza kuhamisha vipengele vya kisarufi kutoka L1 na kuvitumia katika lugha yake kadirifu. Mchakato wa pili unahusu kuhamisha ujifunzaji pale ambapo elementi za LK hutokana na jinsi ambavyo mwanafunzi huvyofunzwa. Kwa hivyo, miundo na kanuni potofu anazozitumia ni matokeo ya vipengele vinavyozingatiwa katika ujifunzaji wake.

Mchakato wa tatu unahusu mbinu za ujifunzaji wa LL. Katika mchakato huu, mwanafunzi anajaribu kutumia mbinu tofauti ili kurahisisha mfumo wa LL na

kujiundia mtazamo wake kutokana na jambo analostahili kufunzwa. Mchakato wa nne unahusishwa na mikakati ya kimawasiliano wakati ambapo mwanafunzi anatambua mbinu zinazomwezesha kuwasiliana na wazawa wa LL. Nao mchakato wa tano ni ujumuishaji pale ambapo elementi za LK hutokana na kujumuisha kanuni na sifa za LL na kuzitumia pasipotarajiwa. Michakato hiyo mitano ndiyo Selinker (keshatajwa) anaiona kuwa humfanya mwanafunzi adumae katika lugha yake kadirifu.

Mchango wa nadharia hii ya LK kwa utafiti huu ulijikita haswa katika kuchunguza na kueleza vyanzo vya makosa yaliyofanywa na wanafunzi kwa kuzingatia lugha yao kadirifu. Michakato mitano iliyobainishwa hapo juu ilizingatiwa ili kuchunguza vyanzo hivyo na kiwango cha utokeaji wa makosa ya mwanafunzi.

### 1.8 Mbinu za utafiti

Utafiti wowote ni lazima uzingatie mbinu mbalimbali ili mtafiti aweze kufikia malengo yake. Mbinu hizo ndizo zinamwongoza na kumwezesha kufanikisha utafiti wake. Katika sehemu hii, vipengele vya muundo wa utafiti, usampulishaji, vifaa vya utafiti, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data vilijadiliwa na kuelezwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu.

#### 1.8.1 Muundo wa utafiti

Creswel (2009) anaeleza kuwa miundo ya utafiti ni mipango na michakato ya utafiti ambayo huzingatia kwa pamoja maamuzi yanayofanywa na mtafiti na mbinu zote anazozitumia kukusanya, kuwasilisha na kuchanganua data. Nao Mugenda na Mugenda (2012) wanasema kuwa muundo wa utafiti ni mpango unaobainisha

vipengele muhimu vya kazi inayotarajiwa kufanywa katika utafiti mzima. Kwa hivyo, muundo wa utafiti unadhihirisha taratibu na mikakati ya mtafiti katika uchunguzi wa malengo ya mada anayoishughulikia. Miundo mbalimbali ya utafiti huweza kuzingatiwa katika utafiti, lakini yote huangukia katika makundi makuu matatu ya utafiti yaliyozungumziwa na Creswel (2012) ambayo ni tafiti za kitakwimu, tafiti za kimaelezo na tafiti zenye miundo changamani; yaani tafiti zinazohusisha miekeleo ya kitakwimu na ya kimaelezo.

Katika utafiti huu, mtafiti alinuia kuchunguza changamoto za kimofosintaksia zilizokumba wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda. Kwa hivyo, utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo kwa kiwango kikubwa ingawa matafiti alihitaji takwimu mbalimbali kuhusu kiwango cha makosa yaliyofanywa na wanafunzi. Aidha, baada ya kukusanya, kuchunguza na kuchanganua data, mtafiti alitoa maelezo na fafanuzi mwafaka kulingana na matokeo aliyoyapata. Data hizo zilizochanganuliwa na kuelezwa zilipatikana kutoka nyanjani kwa kuhusisha mbinu za hojaji na mahojiano. Vitabu, magazeti na makala mengine vilisomwa maktabani ili kumwezesha mtafiti kutoa maelezo kamili kufuatana na matokeo ya data hizo.

### 1.8.2 Mbinu za usampulishaji

Bickman na Rog (2011) wanasema kuwa shughuli ya usampulishaji huanzia pale ambapo mtafiti ameshaamua kuhusu wakati na mahali pa kufanyia uchunguzi wake, watu wa kushirikisha na aina ya habari anazozihitaji katika utafiti wake. Naye Seale (2012) anadhihirisha kuwa sampuli hutakikana kuwa kiwakilishi kamili cha jamii nzima ili kumwezesha mtafiti kujumuisha matokeo ya utafiti wake kwa jamii nzima.

Hivyo basi, sampuli ni idadi ndogo inayochaguliwa na mtafiti ili kuwakilisha jamii lengwa ya utafiti wake. Katika utafiti huu sampuli yetu ilikuwa shule, wanafunzi na walimu na ilipatikana kutokana na mbinu ya kimakusudi.

Orodho (2009) anasema kuwa mbinu ya kimakusudi hulenga watoa habari wenye ujuzi maalum kuhusu jambo linalotafitiwa na ambao hukubali kumjulisha mtafiti habari walizo nazo. Kwa hivyo, uteuzi wa sampuli yetu ulizingatia shule zilizofunza Kiswahili na wanafunzi walikuwa wale waliosoma lugha hiyo. Miongoni mwa shule saba zilizofundisha Kiswahili wilayani Muhanga, shule zilizoteuliwa ni Shule ya Groupe Scolaire de Nyarusange, Groupe Scolaire de Kirwa na Groupe Scolaire de Shyogwe. Shule hizi zilijitokeza katika maeneo tofauti kiasi kwamba tulipata data za kutosha zilizoweza kudhihirisha picha kamili ya changamoto za kimofosintaksia za wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga.

Shule ya kwanza na ya pili ni za vijijini na shule ya tatu ni ya mjini. Mugenda na Mugenda (2003) wanaeleza kuwa angalau asilimia 10 ya watafitiwa hutosha katika tafiti za kimaelezo. Katika utafiti huu, shule mbili za vijijini hulingana na 40% ambapo shule moja ya mjini hulingana na 50% kwani shule zilizofundisha Kiswahili zilikuwa saba ambapo shule tano ni za vijijini na mbili za mjini. Tofauti na shule za kwanza, hizi za pili mara nyingi ndizo zenye kuwa na walimu wa kutosha na miundo msingi iliyo imara. Vilevile, uchunguzi wetu ulifanywa miongoni mwa wanafunzi 10 wa darasa la tano na 10 wa darasa la sita. Jambo hili lilitokana na hali kwamba wanafunzi hawa ndio walikuwa wameshapata msingi wa lugha ya Kiswahili kwani ufundishaji wa lugha hii huanzia kirasmi kidato cha nne. Aidha, idadi ya wanafunzi

10 nayo ilitosheleza kwani wanafunzi waliohesabiwa katika madarasa yote yaliyochunguzwa walikuwa kati ya 20 na 45. Kwa hivyo, watafitiwa wetu walihesabiwa kati ya wanafunzi asilimia 50 na 20.

Mbinu ya nasibu ndiyo iliyozingatiwa kuchagua waliotafitiwa. Kulingana na mbinu hii, kila mwanajumuia alikuwa na uwezekano sawa wa kushiriki katika utafiti. Kwa hivyo, karatasi kumi zilipewa nambari moja na nambari mbili ikapewa karatasi zingine kulingana na idadi ya wanafunzi waliobaki katika darasa husika. Waliopata nambari moja ndio walioshirikishwa katika utafiti huu kiasi kwamba jumla ya idadi ya wanafunzi waliohusika ilikuwa wanafunzi sitini kutoka madarasa yote ya shule tatu zilizoteuliwa.

### 1.8.3 Mbinu za kukusanya data

Data zilizokusanywa ni makosa ya kimofosintaksia na mikakati iliyofanywa kupunguza makosa hayo. Seale (2012) anadhihirisha kuwa uchaguzi wa mbinu za kukusanya data hutegemea kwa kiasi fulani aina ya utafiti unaolengwa kufanywa. Kwa hivyo, anaeleza kuwa mbinu mseto huweza kutumiwa katika utafiti na kubainisha kuwa kila mbinu inayozingatiwa huwa na udhaifu na manufaa yake. Katika utafiti huu, mbinu zilizotumiwa kuzikusanya data zetu ni pamoja na hojaji na mahojiano.

#### 1.8.3.1 Hojaji

Seale (2012) anasema kuwa hojaji ni mbinu ya kukusanya data ambapo mtafitiwa hupewa muda wa kukaa peke yake na kujibu mwenyewe maswali yaliyompelekewa. Katika hali hii, ni lazima maswali yanayoulizwa yawe sahili, finyu na yaeleweke

vizuri ili kumrahisishia mtafitiwa kujaza hojaji aliyoipewa. Vilevile, mtafitiwa hana muda wa kuuliza pale pasipoeleweka. Hata hivyo, mbinu hii ina faida ya kumfanya mtafitiwa ajisikie huru katika kutoa maoni yake na hupunguza gharama ya utafiti kwa kumwezesha mtafiti kukusanya data kutoka mahali pengi pasipokaribiana na kuzichunguza kwa muda mfupi.

Katika utafiti huu, hojaji zilipelekwa kwa wanafunzi na walimu ili kujibu maswali yaliyoandaliwa. Katika kukusanya data kutoka kwa wanafunzi, mtafiti alijumuika kwanza na watafitiwa kwa kuwaeleza malengo yake katika utafiti huu. Aliwaonyesha kwamba matokeo ya utafiti alionuia kufanya yangeweza kuwanufaisha wote na kuwa mazoezi waliyotarajia kufanya hayakuwa mtihani. Walielezwa vilevile kuwa hawakutakiwa kuandika majina yao kwenye hojaji hizo kwani mtafiti hakuwa na lengo la kujua majina yao. Kwa hivyo, waliweza kujibu maswali hayo kwa utulivu bila wasiwasi wowote.

Hatua ya pili ilikuwa kuwapatia hojaji ambazo zilikuwa na maswali  ya aina mbili. Katika aina ya kwanza ya maswali, wanafunzi walipewa sentensi za Kiswahili ambapo walitakiwa kuzikamilisha kwa kutumia viambishi mwafaka vya upatanishi wa kisarufi. Jambo hili lilimwezesha mtafiti kujua kiwango chao cha uhamishaji kutoka L1 na kile cha matumizi yao ya kanuni za sarufi ya Kiswahili wanazojifunza darasani, hasa matumizi ya viambishi vya upatanishi wa kisarufi.

Hatua ya tatu ilihusiana na uandishi wa insha. Wanafunzi walipewa mada moja, *Ufugaji kijijini mwangu*, na kuishughulikia. Wanafunzi walipewa uhuru wa kufikiria kwa makini lile walililoliandika. Hatua hii ilikuwa muhimu sana kwani ilimwezesha

mtafiti kutambua makosa yaliyofanywa na wanafunzi katika uandishi wao kwani mara nyingi mtu huandika kwa namna tofauti na vile anavyozungumza.

Walimu wa Kiswahili pia walipewa hojaji zenye maswali yaliyolenga kuchunguza mikakati iliyofanywa kupunguza makosa ya wanafunzi wao. Hojaji hizi zilikuwa na maswali ya aina mbili; yaani maswali funge na maswali wazi ambapo mwalimu alitakiwa kueleza maoni yake.

#### 1.8.3.2 Mahojiano

Mugenda na Mugenda (2012) wanaeleza kuwa mahojiano hushirikisha mtafiti anayeuliza maswali na mhojiwa anayejibu. Katika matumizi ya mbinu hii, ni lazima mtafiti awe makini kumsikiza mhojiwa ili aweze kumfafanulia yale ambayo hayaelewi vizuri. Vilevile, mtafiti anaweza kumwomba mhojiwa akamilishe majibu yake kwa kutoa maelezo zaidi pale panapohitajika. Seale (2012) anasema kuwa ingawa mahojiano huchukua muda mwingi, ni mbinu nzuri inayoruhusu uzingatifu wa mazingira na muktadha kuliko zilivyo hojaji na huweza pia kusaidia kukusanya habari nyingi zinazohitajika.

Katika utafiti huu, kila mwanafunzi alipewa fursa ya kusimulia wengine kisa chochote alichokipenda na kujibu maswali ya wenzake kuhusu kisa hicho. Jambo hili lilimshawishi msimuliaji kujieleza zaidi na mtafiti aliweza kupata data aliyoihitaji kutoka kwa walioliza maswali pia. Mazungumzo hayo yalirekodiwa na kunukuliwa na mtafiti baadaye ili kuyachunguza kwa misingi ya nadharia zilizopendekezwa kutumiwa katika utafiti huu.

Kabla ya kufikia hatua hii ya kukusanya data kwa njia ya masimulizi ya wanafunzi, mtafiti aliwafafanulia pia malengo yake kwamba utafiti huu ulinuia kuwanufaisha baadaye kwa kuchangia katika maandilizi ya vitabu vya kufunzia lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, jambo hili liliwatayarisha wanafunzi hawa kurekodiwa bila wasiwasi. Aidha, mtafiti aliwachochea kwa kuwapendekezea mifano ya mada zilizoweza kuwavutia zaidi ili waweze kujichagulia wao wenywe bila kuwafunga katika mada yoyote.

Kwa mujibu wa Seale (2012), mahojiano ya ana kwa ana ni mbinu nzuri ya kukusanya data katika tafiti za kimaelezo ambapo maswali changamani huweza kuulizwa na kuelezwa. Kwa hivyo, sehemu ya pili ya matumizi ya mbinu ya mahojiano iliwalenga walimu wa Kiswahili wa shule teule. Mtafiti aliwahoji walimu hao kwa kutaka kupata data zilizohusiana na makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi wao pamoja na mikakati waliyoizingatia katika kupunguza makosa hayo. Mahojiano haya yalimwezesha mtafiti kupata maelezo kamili kuhusiana na maswala mbalimbali ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili nchini Rwanda kwa jumla.

### 1.8.4 Vifaa vya utafiti

Creswell (2009) anasema kuwa matumizi ya vifaa vya utafiti huzingatia data inayotarajiwa kukusanywa na muundo wa utafiti wenyewe. Kwa hivyo, vifaa vilivyotumiwa katika utafiti huu ni pamoja na hojaji, kiongozi cha mahojiano na kinasasauti.

#### 1.8.4.1 Hojaji

Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2012), hojaji ni kifaa muhimu cha kukusanya data kinachozingatia maswali mbalimbali yenye kulenga habari zote zinayohitajika na mtafiti katika uchunguzi wake. Maswali hayo yaweza kuwa ya aina mbili: maswali funge na maswali huru. Katika utafiti huu, hojaji zilipelekewa wanafunzi na walimu. Hojaji kwa wanafunzi zilikuwa na sehemu kuu mbili ambapo walitakiwa kukamisha sentensi katika sehemu ya kwanza na kutunga insha katika sehemu nyingine.

Hojaji zilizosambazwa kwa walimu zilizingatia kundi la maswali funge na kundi la maswali huru. Katika maswali funge, mtafitiwa alitakiwa kujibu ndiyo au hapana au kuchagua jibu sahihi kati ya majibu yaliyopendekezwa na mtafiti. Ingawa aina hii ya kukusanya data humfunga mtafitiwa katika maswali ya mtafiti peke yake, ni bora pia kwani humwezesha mtafiti kuchunguza mambo mengi iwezekanavyo kwa muda mfupi. Aina ya pili ya maswali ilikuwa maswali huru ambapo mtafiti aliundia maswali kuhusu mambo msingi yaliyomwezesha kuchunguza makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi na mikakati iliyozingatiwa na walimu ili kuyapunguza makosa hayo.

Hivyo basi, maswali kwa walimu yalihusu kuchunguza maoni ya kijumla dhidi ya ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kwa wanafunzi wao. Maswali haya ndiyo yalituwezesha kutambua changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo katika ufundishaji wao na ambazo ndizo zinaathiri lugha kadirifu ya wanafunzi wao. Maswali mengine yalilenga kudhihirisha mikakati iliyozingatiwa na walimu hawa katika upunguzaji wa makosa ya wanafunzi wao ili kuweza kuitathmini makosa ya

wanafunzi kwa mujibu wa nadharia ya UM na kutafuta chanzo cha makosa hayo. Kwa hivyo, maswali ya aina hii yalitusaidia kubainisha vipengele vingine visivyo vya kiisimu ambavyo viliweza kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili ili kutoa mapendekezo mwafaka kuhusiana na matokeo ya utafiti wetu.

#### 1.8.4.2 Kiongozi cha mahojiano

Mugenda na Mugenda (2012) wanaeleza kuwa kiongozi cha mahojiano ni kifaa kinachotumiwa na mtafiti ili kutekeleza mahojiana yaliyo wazi. Kifaa hicho kinazingatia maswali yaliyopangwa kwa mtiririko unaomwezesha mtafiti kuuliza maswali yenye mantiki. Katika utafiti huu, kiongozi cha mahojiano kilitumiwa kuwahoji walimu na mazungumzo yaliyofanywa yalichukua ya ana kwa ana ambapo mtafiti alimwendea mtafitiwa na kumhoji kwa kutumia maswali mseto. Katika hali hii, mtafitiwa aliweza kujibu maswali aliyoulizwa na kujieleza au kufafanua jibu lake kadiri alivyopenda. Maswali haya ndiyo yalimwezesha mtafiti kupata habari za kutosha kuhusu mambo kadhaa yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu na pia kuibua maswali mbalimbali yaliyohusiana na makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi watafitiwa.

#### 1.8.4.3 Kinasa sauti

Ili kufanikisha utafiti huu, kinasa sauti kilikuwa muhimu katika kutekeleza mbinu ya mahojiano hasa wakati wa masimulizi ya wanafunzi na pia kwa kuwahoji walimu wao. Baadaye, mtafiti aliweza kunukuu mahojiano na masimulizi hayo ili yaweze kuchanganuliwa.

### 1.8.5 Jaribio la utafiti

Megenda na Mugenda (2012) wanasema kuwa jaribio la utafiti ni muhimu kwani humwezesha mtafiti kuchunguza na kuelewa hali za wanatafitiwa wake ili baadaye aweze kuondoa vipengele vyote vinavyoweza kuwatatanisha na kuwakanganya. Hivyo basi, ili kufanikisha kazi hii, mtafiti alifanya utafiti mdogo kwenye Shule ya Groupe Scolaire de Cyeza, wilayani Muhanga, nchini Rwanda. Kutokana na matokeo ya utafiti huo mdogo, mtafiti aliweza kuandaa maswali ya utafiti kwa njia iliyofaa na kuyapanga ipasavyo. Vilevile, jaribio hili ndilo lilichangia sana katika kuwekea mipaka kazi hii na kuboresha matumizi ya mbinu na vifaa vilivyoteuliwa kutumiwa katika utafiti huu. Kwa hivyo, mwalimu wa Kiswahili wa shule ya Groupe Scolaire de Cyeza na wanafunzi wake wa madarasa ya tano na sita walishirikishwa katika utafiti huo mdogo.

### 1.8.6 Uzingativu wa maadili

Bickman na Rog (2009) wanaeleza kuwa uzingatifu wa maadili katika utafiti ni jambo msingi pale ambapo haki ya kutoingiliwa kwa wanaotafitiwa humtaka mtafiti ajiwekee mipaka katika utafiti wake. Kwa hivyo, mtafiti anatakiwa kuzingatia njia halali zilizowekwa kulingana na vipengele vya kitamaduni, kielimu na kimaendeleo. Katika utafiti huu, mtafiti aliomba kwanza idhini ya kufanya utafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta, shule inayohusika na Shahada za Juu. Hapo aliandikiwa baruwa iliyopelekwa kwa Wizara ya Elimu nchini Rwanda ambapo kwa upande mwingine Wizara hii nayo ilimwandikia barua ya kumruhusu kuenda nyanjani kukusanya data.

Baadaye, viongozi waliosimamia shule tatu teule walikabidhiwa barua hiyo kutoka kwa Wizara ya Elimu ili waweze kuwaruhusu walimu wa Kiswahili na wanafunzi wao kushiriki katika utafiti huu. Kabla ya kukusanya data zilizohitajika, watafitiwa walihakikishiwa kwamba data hizo zingetumiwa tu kwa ajili ya utafiti huu na kuambiwa kwamba hawangetakiwa kuandika majina yao kwenye hojaji walizopewa au kutaja majina yao wakati wa mahojiano.

### 1.8.7 Uchanganuzi wa data

Mugenda na Mugenda (2012) wanasema kuwa katika mchakato wa kuchanganua data, mtafiti anatakiwa kwanza kupanga data yake kwa utaratibu unaomwezesha kupata maana ya habari alizonazo. Aidha, uchanganuzi wa data huwa na mitazamo mbalimbali inayojumuisha mbinu tofauti zinazotumiwa kulingana na muundo wa utafiti. Katika kazi hii, mtafiti alichanganua data yake kuhusiana na makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi wa Kiswahili na mikakati ya kuyapunguza makosa hayo kwa mujibu wa nadharia zilizojadiliwa katika §1.7. Kwa hivyo, uchanganuzi wa data ulizingatia hatua zifuatazo: Kwanza, makosa na mikakati ya kuyapunguza ilinukuliwa kwa utaratibu maalum; pili, makosa yalibainishwa kwa kuzingatia kategoria za kimofosintaksia zilizoathirika na viwango mbalimbali vya utokeaji wake kwa asilimia. Hatua ya tatu ilikuwa kuyafafanua makosa hayo na kuyaainisha. Hatua ya nne ilikuwa kuchunguza vyanzo vyake na kuvitolea maelezo. Hatua ya mwisho ilikuwa kutathmini utokeaji wa makosa na kuchunguza mikakati iliyozingatiwa na walimu kuyapunguza makosa hayo ili kutoa mapendekezo yaliyohitajika.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

### 1.8.8 Uwasilishaji wa matokeo

Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2012), uwasilishaji wa matokeo unaingiliana na shughuli ya kuelewa, kueleza na kufasiri data iliyochanganuliwa. Kwa njia hii, mtafiti anadhihirisha na kueleza maana ya matokeo yake katika hali halisi ya jambo lililochunguzwa. Katika utafiti huu, uwasilishaji wa matokeo ulifanywa kwa njia ya maelezo. Majedwali yalitumika kuweka bayana maelezo yetu, kiwango cha utokeaji wa makosa na idadi ya wanafunzi waliofanya makosa hayo kwa asilimia. Kwanza, matokeo ya kukamilisha tungo yaliwasilishwa kwa kuzingatia kategoria mbalimbali za kimofosintaksia. Pili, yale ya utungaji wa insha nayo yalichunguzwa kivyake; tatu, yale yaliyopatikana katika masimulizi yakadhihirishwa. Hali hii ilituwezesha kuthibitisha matokeo yetu kwa urahisi na kuchunguza kipengele cha kimofosintaksia kilichoathirika zaidi.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imetoa utangulizi wa utafiti huu kwa kubainisha mambo muhimu yaliyozingatiwa na mtafiti katika kuichagua mada na jinsi alivyoikabili kwa ajili ya kuyafikia malengo yake. Kwa hivyo, usuli wa mada, swala la utafiti, malengo ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, nadharia zilizomwongoza na mbinu zilizotumika katika utafiti huu zimedhihirishwa na kufafanuliwa ili kuupa mwelekeo utafiti huu.

# SURA YA PILI

# MOFOSINTAKSIA YA NGELI ZA NOMINO KATIKA KISWAHILI NA KINYARWANDA

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tulibainisha ngeli za nomino za Kiswahili na Kinyarwanda ili kuonyesha jinsi zinavyotawala aina zingine za maneno na kuleta upatanishi wa kisarufi katika sentensi. Kwa hivyo, urejeshi wa ngeli unaopatikana katika vitenzi, vivumishi na viwakilishi ulijadiliwa kwa lengo la kuonyesha nafasi kubwa ya ngeli katika mofosintaksia ya lugha hizo mbili. Mjadala wetu katika sehemu hii ulieleza kwa kina mofosintaksia ya ngeli katika Kiswahili na Kinyarwanda ingawa maswala mengine muhimu ya kisemantiki katika mifumo miwili yaliweza kudokezwa pale palipohitajika. Jambo hii lilitokana na kisio letu kwamba makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi yalitokana na miundo fanani na tofauti zilizopo kati ya mfumo wa ngeli za Kiswahili na Kinyarwanda ambapo maswala ya kimofolojia, ya kisintaksia na kisemantiki huingiliana na kukamilishana kiasi cha kumkanganya mwanafunzi.

## 2.1 Dhana ya ngeli

Mgullu (1999) na Kapinga (1983) wanaeleza kuwa "ngeli" ni istilahi iliyoundwa kutokana na neno la lugha ya Kihaya "engeli" lenye kumaanisha aina ya kitu au aina ya vitu. TUKI (1981) nao wanafafanua "ngeli" kama utaratibu wa taaluma ya sarufi ya lugha katika kupanga aina za majina (nomino) kama vile *ki, vi, ma* na kadhalika. Ngeli hurejelea kundi moja la majina yaliyo na upatanishi wa kisarufi unaofanana

kupitia misingi tofauti inayoweza kuzingatiwa katika kuziainisha nomino hizo. Kwa hivyo, fafanuzi nyingi za istilahi hii 'ngeli' zinatuelekeza katika maoni yaliyotolewa na Kihore na wengine (2003) waliposema kuwa neno 'ngeli' linamaanisha mgawanyo wa aina mbalimbali za nomino katika mtazamo wa kisarufi. Watafiti hawa walieleza kuwa ngeli za nomino huhusu makundi ya majina; kila kundi likiwa na mabadiliko ya aina moja ya viambishi vya umoja na wingi vyenye kuleta upatanishi wa kisarufi wa namna moja katika vitenzi, vivumishi na viwakilishi.

Kila jina linaingizwa katika kundi fulani au familia moja ya nomino kutokana na hali kwamba kuna sifa ambazo zinajumuishwa kwa nomino hizo zinazoshirikishwa katika kundi moja ambalo ndilo ngeli. Sifa hizo zaweza kuwa za kisemantiki, za kimofolojia au za kisintaksia na "ngeli" ni sifa mojawapo muhimu inayozibainisha lugha za Kibantu ingawa kila lugha inayotumia utaratibu wa ngeli huwa na idadi fulani. Kihore na wengine (keshatajwa) hutuambia kuwa lugha nyingi za Kibantu zina ngeli zisizopungua kumi na zisizozidi ishirini.

## 2.2 Upatanishi wa kisarufi

Mdee (1986) anaeleza upatanishi wa kisarufi kama tabia ya kufungamanisha maneno yaliyo katika tungo na kusema kwamba mfungamano huu hujitokeza katika viambishi vilivyo katika maneno tofauti yanayohusiana. Uhusiano huo wa viambishi vya maneno tofauti katika sentensi ndio unaojenga mfumo wa mshikamano wa maneno katika lugha ambao huitwa upatanishi wa kisarufi. Lugha za Kiswahili na Kinyarwanda hutumia mfumo wa ngeli ambapo viambishi vya ngeli ndivyo vinatawala mahusiano ya nomino na maneno mengine katika sentensi. Kila neno

linaloandamana na nomino na kutawaliwa nayo kisarufi huchukua kiambishi chake kutegemea aina ya ngeli ya nomino hiyo. Kwa hivyo, nomino ndiyo huamua aina ya kiambishi kinachoambikwa kwa kitenzi, kivumishi na kiwakilishi ili kuleta mshikamano katika tungo. Mdee (1986) anaeleza kwamba tungo za mtu ambaye hajamiliki upatanishi wa kisarufi huwa na mkengeuko usiokubaliwa na mzawa wa lugha na kwamba hali hii hujitokeza kwa wageni wanaojifunza Kiswahili.

### 2.3 Mofosintaksia ya ngeli katika Kiswahili

Katika Kiswahili, idadi na majina ya ngeli hutegemea mtazamo unaozingatiwa na mwainishaji; yaani mtazamo wa kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia. Hata hivyo, utafiti wetu utajikita kwenye sifa za kimofolojia na zile za kisintaksia za ngeli za majina ya lugha hii ili kutuwezesha kuzielewa changamoto za kimofosintaksia zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda.

#### 2.3.1 Mtazamo wa kimofolojia wa ngeli

Katamba (1993) anaeleza kuwa mofolojia ni tawi la kiisimu ambalo hushughulikia miundo ya ndani au maumbo ya maneno. Kwa hiyo, ngeli zinapotazamwa kwa msingi huu wa kimofolojia, nomino hugawanywa kwa kuzingatia mofolojia yake na viambishi awali vya idadi vya umoja na wingi katika nomino hizo ndivyo vinachunguzwa (Mgullu, 1999). Baadhi ya wanaisimu ambao waliainisha ngeli kwa kutumia msingi huu wa kimofolojia ni pamoja na Krapf (1850), Steere (1865), Ashton (1944), Polome (1967), Myachina (1981), Mbaabu (1978, 1985), Mgullu (1999), Mohammed (2001), Kihore na wengine (2003) na Habwe na Karanja (2004).

Adewole (1986) anakibainisha kigezo hiki cha uainishaji kama "*Kigezo cha kifonolojia*" na kuonyesha kuwa nomino zinagawanywa kwa kuzingatia mfanano wa kifonolojia unaohusisha viambishi awali vya nomino. Nomino ambazo zina viambishi awali vyenye sifa ya unazali zinawekwa pamoja wakati ambapo zingine zenye vibadala kama *{ki-ch; u-w}*, nazo huwekwa pamoja. Kwa mfano, nomino kama *mti* na *mlango*zinapangwa pamoja ilhali nomino *kitabu, chakula* nazo huunda kundi jingine.

Mawazo hayo ya Adewole hayatofautiani sana na yale ya Mgullu (keshatajwa) anapodhihirisha kuwa nomino zote zilizo na viambishi awali vya umoja na wingi vinavyofanana huwekwa katika kundi moja ambalo huitwa ngeli. Mgullu anasema kuwa utaratibu huu ndio umekuwa ukitumiwa na wanaisimu wengi walioshugulikia lugha za Kibantu. Nao Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa uanishaji wa ngeli kwa kuzingatia mtazamo huu unajikita katika mfanano wa kimaumbo wa viambishi awali vya umoja na /au wingi; jambo linalotufanya tuyapange pamoja majina kama *kijana/vijana, kitabu/vitabu, kiwete/viwete, kiongozi/viongozi.* Majina haya yote yana kiambishi awali {ki} cha umoja na {vi} cha wingi.

Mgullu (1999) akiyajumuisha mawazo yaliyogusiwa na watafiti wa hapo mwanzoni kama vile Krapf (1850), Ashton (1944), Brain (1969) na Polomé (1967) anadhihirisha makundi yafuatayo ya ngeli:

1. Ngeli ya M-WA: **m**toto/**wa**toto; **mw**alimu/**wa**limu; **mu**ungwana/**wa**ungwana (Kiambishi awali cha umoja *m* katika mifano hii, kinaweza kujidhihirisha katika maumbo mengine (alomofu: m/mw/mu).
2. Ngeli ya M-Mi: **m**ti/**mi**ti; **m**chungwa/**mi**chungwa; **m**tume/**mi**tume

3. Ngeli ya JI-Ø/MA: **ji**cho/**ma**cho ; Økasha/**ma**kasha ; Øbalozi/**ma**balozi (Katika mifano hii, tunapata kuwa kiambishi awali cha umoja *ji* kinaweza kudhihirishwa kwa mofu kapa (Ø))

4. Ngeli ya KI/VI: **ki**ti/**vi**ti; **ch**akula/**vy**akula; **ki**jana/**vi**jana (Hapa kiambishi cha umoja *ki* huweza kudhihirishwa katika alomofu *ch* na kiambishi *vi* kikadhihirishwa katika alomofu *vy*).

5. Ngeli ya U/N/(MA): **u**fa/**ny**ufa; **u**devu/**n**devu ; **u**gonjwa/**ma**gonjwa ; **u**zuri/**u**zuri

6. Ngeli ya KU (Vitenzijina): **ku**cheza; **ku**imba (Majina ya ngeli hii ni yale yanatokana na vitenzi).

7. Ngeli ya PA/MU/KU : hapa/hapo ; humu/humo ; huku/huko

Mbali na hayo, tukiwarejelea Kihore na wengine (2003) utaratibu huu wa kuainisha ngeli za nomino kimofolojia huweza kudhihirisha mielekeo miwili: Msingi unaotumia viambishi vya nomino na ule unaotumia jozi ya viambishi vya umoja na wingi.

#### 2.3.1.1 Msingi wa kutumia viambishi vya nomino

Msingi huu wa kutumia viambishi vya nomino unadhihirisha maumbo ya viambishi yanayofanana kwa kila ngeli ambazo hujipanga katika umoja kwanza na wingi katika ngeli inayofuata. Lakini, kuna majina ambayo hayabainishi viambishi vya umoja na wingi wakati ambapo mengine hupata wingi wake katika ngeli tofauti na zile zinazofuatana nazo kama tunavyopata katika Jedwali 2.1.

**Jedwali 2.1: Uainishaji wa ngeli kwa kutumia vimbishi awali vya nomino**

| **Umoja** | | **Wingi** | |
|---|---|---|---|
| **Na** | **Ngeli** | **Na** | **Ngeli** |
| I | mu-/mw-/m- (muuguzi, mwalimu, mtoto) | ii | wa- (wauguzi, walimu, watoto) |
| Iii | mu-/mw-/m- (muungu, mwembe, mti) | Iv | mi- (miungu, miembe, miti) |
| V | ji-/Ø (jiwe, panga) | Vi | ma- (mawe, mapanga) |
| Vii | ki- (kiti, kiatu, kikombe) | viii | vi- (viti, viatu, vikombe) |
| Ix | N- (nyumba) | X | N- (nyumba) |
| Xi | u- (ubao, ukuta) | X | N-Ø (mbao, kuta) |
| Xiv | u- (ugonjwa, ukubwa) | Vi | ma (magonjwa, -) |
| Xv | ku- (kucheza) | | |
| Xvi | pa- (pale) | | |
| Xvii | ku- (huku) | | |
| Xviii | mu- (humu) | | |

Kulingana na mtazamo huu wa uainishaji wa ngeli, tunaweza kutambua kwamba baadhi ya ngeli huwa na viambishi vinavyofanana katika umoja na wingi (ng. za 9/10) ilhali nomino kama ***ukubwa*** (ng. 14) na *kucheza* (ng. 15) hazibadiliki kutoka umoja hadi wingi. Majina kama ***u****bao* (ng. 11) huchukua wingi wake ***m****bao* katika ngeli ya 10 wakati ambapo kuna mengine yanayochukua kiambishi kapa kama ilivyo katika mfano wa **u**kuta (ng. 11)/**Ø**kuta (ng. 10).

Mbaabu (1992) anasema kuwa nomino za ngeli ya 14 ni za hisi kwa kuzingatia nomino za vitu visivyoweza kuguswa. Baadhi ya nomino zake huweza kuchukua viambishi vya ngeli ya 6 katika hali ya wingi kama tunavyopata katika mfano 2.1.

*(2.1) ugonjwa/magonjwa, uovu/maovu; ulezi/malezi*

Nomino zenye kimbishi ngeli {u} hujitokeza katika makundi mawili; yaani kundi la 11/10 na lile la 14. Kundi la kwanza huchukua viambishi vya wingi katika ngeli ya 10 wakati ambapo zile za 14 hazionyeshi kiambishi chochote cha wingi. Ngeli ya 14 huwa na nomino ambazo hazina umoja wala wingi. Mbaabu (1992) anasema kuwa nomino nyingi huweza kuanza na {u} lakini kuna zingine zinazoanza na {w}:

*(2.2) U: uzuri, umaskini, uzembe*
*W: wali, wino*

Vilevile, ngeli ya 15 huzingatia nomino ambazo huundwa kutokana na vitenzi kwa kupachika kiambishi {ku} mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi na hazina umoja wala wingi. Nazo ngeli za 12 {ka} na 13 {tu} hazitumiki katika Kiswahili lakini zinapatikana katika lugha zingine za Kibantu kama vile Kinyarwanda na zinaashiria udogo wa vitu au kudunishwa kwa vitu, watu, wanyama na wadudu. Mbaabu (keshatajwa) anaeleza kuwa ngeli hizi zilipotea katika Kiswahili na badala ya {ka} na {tu}, Kiswahili kikatumia ngeli ya KI/VI. Kwa hiyo, Kiswahili kitatumia *kitoto kile* badala ya *katoto kale; vitoto vile* badala ya *tutoto tule.*

#### 2.3.1.2 Msingi wa kutumia viambishi vya umoja na wingi

Mgullu (1999) anabainisha makundi makuu manne ya ngeli kwa kuzingatia utaratibu huu wa kutumia jozi ya viambishi vya nomino katika umoja na wingi:

a) Ngeli sita za nomino zilizo na viambishi awali vyote viwili yaani: kiambishi awali cha umoja na kiambishi awali cha wingi:

Ngeli ya MU/M/MW-WA: *mtu/watu; mtoto/watoto*; Ngeli ya MU-MI: *mti/miti, mtume/mitume, mkono/mikono*, Ngeli ya JI/MA: *jicho/macho, jiwe/mawe*; Ngeli ya KI-VI: *kiti/viti, ki-akula/vi-akula*; Ngeli ya U-N: *ubawa (u-bawa)/mbawa (n-bawa)*; Ngeli ya U-MA: *ugonjwa/magonjwa; uasi/maasi,* na kadhalika. Kundi la ngeli za nomino hizi linabainika kuwa kamili kuliko ngeli za nomino zingine kwani ndilo lenye nomino zenye viambishi vyote viwili.

b) Ngeli ya nomino zilizo na kiambishi awali cha umoja tu na mofu kapa ya wingi.

Majina yanayoingizwa katika kundi hili ni kama *ukingo/Økingo; ufunguo/Øfunguo; ukuta/Økuta; upembe/Øpembe; ukucha/Økucha,* na kadhalika.

c) Ngeli ya nomino zilizo na kiambishi awali cha wingi tu pamoja na mofu kapa ya umoja.

Nomino za aina hii ni pamoja na *Ødebe/madebe; Økasha/makasha ; Øjembe/majembe ; Øbepari/mabepari ; Øbibi/mabibi* na kadhalika.

d) Ngeli za nomino zisizo na Kiambishi awali hata kimoja.

Mgullu (1999) husema kuwa nomino zilizo katika ngeli hii hazina kiambishi chochote kwani maumbo yake katika umoja na wingi yanafanana. Hizi ni nomino ambazo haziwekewi viambishi vyovyote vya idadi iwe ya umoja au ya wingi kwani maumbo yake hayaonyeshi mabadiliko yoyote.

*(2.3) ndama/ndama, mbuzi/mbuzi, nguo/nguo, nyumba/nyumba, nyanya/nyanya.*

Kulingana na maelezo ya watafiti mbalimbali kuhusu uainishaji wa ngeli kimofolojia, jedwali (2.2) huweza kutudhirishia picha kamili ya utaratibu huu.

**Jedwali 2.2: Mitazamo ya kuainisha ngeli kimofolojia**

| **Mtazamo wa kutumia viambishi vya nomino** | | | **Mtazamo wa kutumia viambishi vya umoja na wingi** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Kia./Ngeli moja moja** | **Mifano** | **Na** | **Ngeli/umoja** | **Ngeli/wingi** | **Mifano** |
| i | mu-/mw-<br>/m- | **mu**uguzi,<br>**mw**alimu, **motto** | i | mu-<br>mw<br>m | wa<br>wa<br>wa | **mu**uguzi.....**wa**uguzi<br>**mw**alimu....**wa**limu<br>**m**toto......**wa**toto |
| ii | wa- | **wa**uguzi, **wa**limu,<br>**wa**toto | ii | mu<br>m- | mi<br>mi | **mu**ungu......**mi**ungu<br>**m**ti......**mi**ti |
| iii | mu-/mw-<br>/m- | **mu**ungu, **m**ti;<br>**mw**embe | iii | ji<br>Ø | ma<br>ma | **ji**we.....**ma**we<br>**Ø**panga......**ma**panga |
| iv | mi- | **mi**ungu, **mi**ti,<br>**mi**embe | iv | ki- | vi | **ki**ti......**vi**ti |
| v | ji-/Ø | **ji**we, Øpanga | v | N- | N- | **n**yumba......**n**yumba |
| vi | ma- | **ma**we, **ma**panga, | vi | u- | N | **u**zi......**n**yuzi |
| vii | ki- | **ki**ti, **ki**atu,<br>**ki**kombe | vii | ka* | tu-* | (**ka**toto*)...(**tu**toto*) |
| viii | vi- | **vi**ti, **vi**atu,<br>**vi**kombe | viii | u-<br>u- | u-<br>ma- | **u**nene......**u**nene<br>**u**gonjwa....**ma**gonjwa |
| ix | N- | **n**yumba, **n**yama | ix | ku- | ku- | **ku**cheza.....**ku**cheza |
| x | N- | **n**yumba, **n**yufa,<br>**m**bao | x | pa | pa | Mahali ha**pa** |
| xi | u- | **u**bao, **u**fa, **u**nywele | xi | ku | ku | mahali hu**ku** |
| xiv | u- | **u**gonjwa, **u**chungu | xii | mu | mu | mahali hu**mu** |
| xv | ku- | **ku**cheza, **ku**imba | | | | |
| xvi | pa- | mahali **pa**le | | | | |
| xvii | ku- | mahali hu**ku** | | | | |
| xviii | mu | mahali hu**mu** | | | | |

Jedwali hili linaonyesha kuwa viambishi vya nomino ndivyo vinavyozingatiwa kwa kuzipanga nomino katika makundi tofauti ambayo ni ngeli. Ngeli ya kwanza huwa na maumbo tofauti katika hali ya umoja ambayo ni *m, mw* na *mu* na hali hii hujidhihirika pia katika ngeli ya 3 ambapo tunapata *m; mw* na *mu*. Mabadiliko haya yanatokana na mifanyiko ya kifonolojia (kama vile udondoshaji na uyeyushaji) kutegemea aina ya sauti inayotangulia shina la nomino husika. Hali hii hutokea vilevile katika ngeli ya *n* wakati inapojitokeza kwa maumbo ya *{n}* na *{m}* kulingana na usimilisho wa nazali ambapo nazali huathiriwa na konsonanti inayoifuata kulingana na mahali pa kuitamkia. Kwa hivyo, {n} itatumiwa katika nomino zenye mashina yanayoanza na

konsonanti ghuna kama vile *{d, j, g}* wakati ambapo alomofu *{m}* itapatikana katika nomino zenye mizizi inayotanguliwa na konsonanti ghuna *{b}*, na *{v}:*

*(2.4) ndoto, njia, ngano, mbao, mvua*

Kutokana na mtazamo wa kwanza wa uainishaji ngeli kimofolojia, ngeli za (i), (iii) na (xviii) hutumia kiambishi {mu}, ngeli za *ix* na *x* hutumia {n}, ngeli za (xi) na (xiv) zinatumia kiambishi {u} na ngeli za (xv) na (xvii) hutumia {ku}. Nao mtazamo wa pili wa uanishaji ngeli nao unadhihirisha viambishi vya umoja na wingi vinavyofanana kama ilivyo katika ngeli za (v), (ix), (x), (xi) na (xii). Mbaabu (1992) anadhihirisha kuwa nomino nyingi za {n/n} hazina kiambishi awali ambacho ndicho kitambulishi cha ngeli na jambo lili lilimfanya Kithuku (2012) aseme kwamba sifa hiyo ilizifanya nomino nyingi za kigeni kuingizwa katika kundi hili la ngeli.

*(2.5) redio, tarakilishi, maktaba, shati*

Ingawa nomino hizi huingizwa katika ngeli ya 9/10 hazionyeshi viambishi awali vinavyoweza kumwelekeza mwanafunzi kuzipanga nomino hizo katika ngeli hizo. Ili kutambua ngeli zake, inampasa mwanafunzi kuchunguza upatanishi wa kisarufi kwani kisintaksia nomino hizo huendelezwa kwa njia sawa na nomino zinazodhihirisha kiambishi {n} cha umoja na wingi katika kundi la ngeli za 9/10.

### 2.3.2 Mtazamo wa kisintaksia wa ngeli

Kwa kuzungumzia uainishaji ngeli wa kisintaksia, Adewole (1986) anasema kuwa upangaji wa nomino katika makundi kadha unategemea kwa kiasi kikubwa uhusiano uliopo baina ya nomino na maneno mengine. Uhusiano huo unaozingatiwa ni ule unaojitokeza kwa mfano kati ya nomino na kitenzi.

*(2.6) Watoto <u>wa</u>melala; Rafiki yangu <u>a</u>takuja; Mtoto <u>a</u>nakuja; Vijana <u>wa</u>metoroka.*

Katika mifano hii, uhusiano kati ya nomino na maneno mengine unachunguzwa kwa kuzingatia vipashio vilivyopigiwa mstari chini na ambavyo ni viambishi awali vya nafsi vya vitenzi. Vimbishi hivi ndivyo vinapitiwa ili kuzigawa nomino hizo katika ngeli fulani. Kwa hiyo, *mtoto* na *rafiki* zitaunda ngeli moja, *watoto* na *vijana* nazo zitaunda ngeli nyingine. Hata hivyo, taratibu mbalimbali zilitumiwa na watafiti tofauti kuziainisha ngeli kisintaksia pale ambapo tunawakuta waliotumia viambishi vya ukubalifu unaojitokeza katika vipashio vinavyotawaliwa na nomino katika sentensi, viambishi vya nomino pamoja na vipatanishi vyake katika vitenzi au vionyeshi vya karibu na mzungumzaji.

### 2.3.2.1 Matumizi ya viambishi vya ukubalifu katika sentensi

Ukubalifu katika sentensi ulizungumziwa na Adewole (1986) alipozingatia udhaifu na kasoro alizoziona katika kazi za Steere (1865), Ashton (1944) na watafiti wengine wa awali ambazo zilionekana kuchanganya vigezo katika uainishaji wa ngeli. Kwa hivyo, Adewole alipendekeza uainishaji wa nomino unaozingatia kiambishi awali cha kitenzi ambacho ndicho kinachorejelea jina au kiima katika kitenzi hicho. Kiambishi hicho ndicho kinachoonyesha ukubalifu katika nomino na kitenzi au kiima na kiarifu na huwa kinafanana ikiwa majina yanayorejelewa yanajitokeza katika kundi moja ambalo ndilo ngeli. Pale ambapo kuna mabadiliko huwa yamesababishwa na kirai nomino (KN) kilichotumiwa kuashiria hali tofauti.

*(2.7) Mtoto **a**nalia; Toto **li**nalia; Kitoto **ki**nalia.*

Tungo ya kwanza ni ya hali ya kawaida, ya pili, hali ya kukuza na ya tatu ikawa katika hali ya kudunisha. Kwa hivyo, mifano hii inadhihirisha kuwa ukubalifu unajitokeza katika sentensi hizo ambazo zinatumia mzizi "toto" kupitia viambishi *{a,*



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

*li, ki}* kuashiria maana tatu tofauti zinazojitokeza katika viambishi hivyo. *a* inawakilisha mtoto katika hali yake ya kawaida, *li* inawakilisha hali ya kukuza na *ki* inawakilisha hali ya kumdunisha mtoto. Adewole anasema kuwa ukubalifu unachukuliwa katika viambishi nomino na mabadiliko huamuliwa katika KN na kusababisha mabadiliko ya maana; yaani mzizi mmoja unaweza kutumiwa pamoja na vibainishi vya ukubalifu wa aina tofauti ili kuashiria maana tofauti. Kila sentensi inaunganishwa kwa kuzingatia sifa ya ukubalifu wa nomino au KN na vipashio vingine vya sentensi. Ukubalifu wa kiima ndio unadhihirisha ngeli ya nomino inayohusika katika mazingira hayo ya kisintaksia.

> *(2.8) Kiti* ***ki****mevunjika/viti* ***vi****mevunjika, Mtu huyu* ***a****nasafiri/Watu hawa* ***wa****nasafiri, Tunda hili* ***li****meharibika/Matunda haya* ***ya****meharibika, miti imekatwa, nguo imechanika.*

Kulingana na Adewole (1986), viambishi awali vya kila nomino kwa kila ngeli inayohusika husaidia kubainisha ngeli za nomino zenye viambishi vya ukubalifu vinavyofanana.

> *(2.9) a)* ***mi****ti* ***i****mekatwa*
> *b)* ***n****guo* ***i****mechanika*

Katika mifano hii, ngeli *{i-}* inawakilisha *miti* (2.9 a) kwa kupitia kiambishi *{mi}* cha nomino *miti* wakati ambapo ngeli ya *{i}* inasimamia *{n}* ya jina *nguo* katika mfano (2.9 b).

**2.3.2.2 Utaratibu wa kutumia viambishi vya upatanishi vya umoja na wingi**

Utaratibu huu wa uainishaji wa ngeli unazingatia viambishi vinavyoambikwa hasa kwa vitenzi katika umoja na wingi wakati wa kuzigawa nomino katika makundi tofauti. Mbaabu (1992) anabainisha umuhimu wa utaratibu huu anaposema kuwa

nomino za binadamu ambazo zilitawanywa katika ngeli mbalimbali kulingana na viambishi vya nomino (1/2; 3/4; 5/6; 7/8 na 9/10) peke yake huweza kuwekwa pamoja kwa kutumia viambishi vya upatanishi vilivyo sawa. Umoja wa nomino hizi za ngeli za 1, 3, 5, 7 na 9 hutumia viambishi sawa katika sentensi wakati ambapo ngeli za 2, 4, 6, 8 na10 za wingi nazo hutumia viambishi sawa. Kwa hivyo, viambishi hivi ndivyo vinapaswa kuzingatiwa katika kuzipanga nomino katika ngeli tofauti kwani vinafanana kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo ya umoja na wingi (Mbaabu, 1992).

**Jedwali 2. 3 Mchango wa vipatanishi vya nomino katika uainishaji wa ngeli**

| Ngeli | Sentensi katika umoja | Ngeli | Sentensi katika wingi |
|---|---|---|---|
| 1 | **M**zee huyo mfupi **a**listaajabu | 2 | **Wa**zee hao wafupi **wa**listajabu |
| 3 | **Mt**ume huyo **a**listaajabu | 4 | **Mi**tume hao **wa**listaajabu |
| 5 | Nabii huyo **a**listaajabu | 6 | **Ma**nabii hao **wa**fupi wamestaajabu |
| 7 | **Ki**lema huyo mfupi **a**listaaajabu | 8 | **Vi**lema hao wafupi **wa**listaajabu |
| 9 | Askari huyo mfupi **a**listaajabu | 10 | Askari hao wafupi **wa**listaajabu |

Usuli: Mbaabu, 1992

Kulingana na jedwali hili, ni dhahiri kuwa nomino zenye viambishi awali tofauti katika umoja na wingi zimeingizwa katika kundi moja kwa kuzingatia kipatanishi *a* katika umoja na *wa* katika wingi. Vilevile, mifano hiyo hutuwezesha kutambua kwamba ingawa nomino hizo zinaonyesha viambishi awali vinavyoweza kuzifanya ziingizwe katika ngeli tofauti ikiwa kigezo cha kimofolojia kinatumika, uzingatifu huo wa vipatanishi katika umoja na wingi husaidia kuziweka katika kundi moja la *A/WA*.

Isitoshe, kigezo hiki cha uainishaji wa ngeli kilizungumziwa pia na Kihore na wenzake (2003). Kazi yao ilifuata utaratibu wa kutumia kiambishi cha upatanishi wa

kisarufi, yaani jozi ya umoja na wingi kwa kuziainisha nomino katika ngeli tofauti na kiambishi kilichochaguliwa kutumika ni kile kinachoambikwa kwenye vitenzi kama ilivyodhihirishwa hapo juu. Kwa hivyo, utafiti wao unauchukulia utaratibu huu kama unaokidhi haja kwa sababu ngeli zote zina majina yanayozibainisha. Hata hivyo, wanabainisha kuwa mtazamo huu unadhihirisha matatizo ya aina mbili pale ambapo nomino zinahesabiwa katika jozi ya umoja na wingi wakati ambapo kwa upande mwingine zinahesabiwa kama ngeli moja moja. Kwa hivyo, walipendekeza mtazamo wa kutumia kwa pamoja kiambishi cha nomino na kiambishi cha upatanishi wa kisarufi.

**2.3.2.3 Utaratibu wa kutumia vionyeshi**

Utaratibu wa kutumia vionyeshi ni mtazamo uliozungumziwa na Mbaabu (1992) alipolenga kuyatatua baadhi ya matatizo yaliyodhihirishwa katika mitazamo tofauti ya uainishaji wa ngeli. Kwa hivyo, makundi manane ya ngeli yaliyomo katika jedwali lifuatalo yaliweza kudhihirishwa.

**Jedwali 2.4: Mtazamo wa kutumia vionyeshi katika uainishaji wa ngeli**

| **Makundi ya ngeli** | **Mifano** | |
|---|---|---|
| huyu na hawa | huyu | mtu, mtume, nabii, kipofu, ndugu, seremala, mbwa, paka, mbu, nzi |
| | hawa | watu, mitume, manabii, vipofu, ndugu, maseremala, mbwa, paka, mbu, nzi |
| huu na hii | huu | mti, mkarafuu, mgomba, mkeka, mkono, mguu, mlima, mto, msitu, udogo, ukuta, uzee, uzuri, wali, unga, unyevu, nyumba, nyundo, barabara |
| | hii | miti, mikarafuu, migomba, mikeka, mikono, miguu, milima, mito, misitu |
| hili na haya | hili | jani, jino, ua, tunda, neno, jumba, joka, jisu |
| | haya | majani, meno, maua, matunda; majumba, majoka, majisu, maji, maziwa, mafuta, mate, matope |
| hiki na hivi | hiki | kifagio, kifuniko, kitanda, kijiji (mji), kijiti (mti), kibakuli (bakuli), kibata (bata); Kiswahili, Kireno, Kiingereza. |
| | hivi | vifagio, kifuniko, vitanda |
| hizi | nyumba, picha, redio, nyuso (uso), nyuta (uta), mbao (ubao), nyembe (wembe), mbavu (ubavu). | |
| huku | kucheza, kuimba, huku kwetu | |
| hapa | Hapa mezani | |
| humu | Humu chumbani | |

Usuli: Mbaabu, 1992

Mbaabu anasema kuwa mtazamo huu wa kuainisha majina katika Kiswahili unasaidia kuleta pamoja nomino nyingi ambazo hapo awali zilikuwa zimetawanyika katika ngeli nyingi kulingana na hali kwamba zinaonyesha viambishi awali sawa katika maumbo yake. Kwa hivyo, anasema kuwa mtazamo huu unaosaidia kutatua tatizo la nomino kama *ng'ombe* na *ngoma* ambazo zingeweza kuwa katika ngeli moja ikiwa tunazingatia viambishi vyake awali kwani *ng'ombe* litaingizwa katika kundi la *huyu* wakati ambapo jina *ngoma* linaingizwa katika kundi la *hii*.

### 2.3.3 Matumizi ya kiambishi cha nomino na kiambishi cha upatanishi

Utaratibu huu ulizungumziwa na Kihore na wenzake (2003) walipolenga kubainisha mtazamo wa uainishaji ngeli ambao ungezibainisha wazi na kuyapanga majina ya Kiswahili bila utata wowote. Kwa hivyo, walizingatia matumizi ya viambishi awali vya nomino pamoja na viambishi vinavyowakilisha nomino hiyo katika kitenzi katika kuunda makundi tofauti ya ngeli. Kulingana na hayo, ni wazi kwamba huu mtazamo

unashirikisha kwa pamoja mofolojia ya jina husika na sintaksia yake kwani kiambishi cha nomino hiyo hutumiwa pamoja na kiambishi cha upatanishi wa kinachoambikwa kwa kitenzi.

(2.10) ***Wa**tu **wa**nalima (wa-wa); **Mi**ti **i**mekatwa (mi-i), **U**nene **u**napendeza (u-u).*

Kihore na wengine wanautetea utaratibu huu wakisema kuwa ngeli zote zinajibainisha vizuri kuliko taratibu nyingine zilizowahi kutumika. Hata hivyo, kuna tatizo la baadhi ya nomino ambazo hazionyeshi viambishi vyake awali.

(2.11) *Sungura amechinjwa (Ø-a), kalamu imenunuliwa (Ø-i).*

Aidha, nomino zingine nazo zina upatanishi wa kipekee.

*(2.12) **Ki**ziwi **a**nafurahi (ki-a)/ **Vi**ziwi **wa**nafurahi (vi-wa), **m**tume **a**mefika (m-a)/ **mi**tume **wa**mefika (mi-wa), Nabii **a**nahubiri (Ø-a)/**Ma**nabii **wa**nahubiri (ma-wa).*

Katika mifano hii, ngeli za {a} na {wa} zinatumiwa pamoja na viambishi awali tofauti pale ambapo tuna {ki-a/vi-wa, m-a/mi-wa, Ø-a/ma-wa}.

Kulingana na hayo yote na mengine yaliyozungumziwa katika sehemu hii, ni wazi kwamba ni vigumu kuuchagua mtazamo mmoja wa uainishaji wa ngeli unaoweza kukidhi haja ya kila mzungumzaji wa Kiswahili na ambao unaweza kupendekezwa kama mtazamo bora wa kuwarahisishia wanaojifunza lugha hii kuitumia ipasavyo. Kwa hivyo, mitazamo hiyo huweza kukamilishana na jambo muhimu kwa mwalimu anayefunza ni kuichagua misimamo isiyoweza kuwakanganya wanaojifunza lugha hii kulingana na kiwango chao cha masomo.

## 2.4 Urejeshi wa ngeli katika Kiswahili

Massamba (2004) anaeleza kuwa urejeshi ni uhusiano wa kisarufi uliopo baina ya vipengele vya kisarufi kama vile uhusiano baina ya kirai nomino na kiwakilishi

chake. Aidha, Mbaabu (1995) naye anafafanua kwamba katika Kiswahili, nomino huweza kurejelewa katika kitenzi kwa kutumia virejeshi vya ngeli vya kati na virejeshi vya mwisho kulingana na mahali kiambishi kinachorejelea nomino hizo hujitokeza. Hivyo basi, kuna haja kubwa ya kuzungumzia urejeshi huo wa kati, wa mwisho katika vitenzi na uhusiano kati ya nomino na viwakilishi vyake katika vivumishi na viwakilishi. Mbali na mitazamo ya ngeli iliyojadiliwa hapo juu, uhakiki wa aina hii utatusaidia pia kuelewa ipasavyo upatanisho wa kisarufi katika Kiswahili ambao tunauchukulia kama msingi wa uchunguzi wetu kuhusu makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunza lugha hii katika shule za upili.

### 2.4.1 Virejeshi vya kati

Kitenzi huwa na viambishi vya aina kuu tatu; yaani viambishi awali, viambishi vya kati na viambishi tamati au vya mwisho. Miongoni mwa viambishi vinavyojitokeza katikati mwa kitenzi ni virejeshi vinavyotumiwa kurejelea nomino mtenda au mtendwa. Muundo wa viambishi hivi hutegemea ngeli ya nomino hiyo inayorejelewa kama tunavyopata katika mfano (2.13)

(2.13) *Mwanafunzi anasoma kitabu/vitabu* /*Mwanafunzi anakisoma/anavisoma*

Kulingana na mifano hii, sentensi ya kwanza ni sawa na ya pili. Katika sentensi ya pili, viambishi *{ki/vi}* ndivyo virejeshi vya kati; yaani viambishi vinavyorejea nomino mtendwa (kitabu/vitabu) katika ngeli za *{ki}* na *{vi}*.

Isitoshe, Kiswahili kinatumia aina nyingine ya kirejeshi kati *{o}* kinachorejelea nomino ambayo imetajwa kabla ya kitenzi chenyewe kutajwa. Mgullu (1999)

anaeleza kuwa urejeshi huo hutegemea aina ya nomino inayorejelewa na kwa mantiki hiyo, hutegemea ngeli ya nomino inayorejelewa. Kwa kawaida, umbo rejeshi hili huundwa kwa kutumia kipatanishi cha ngeli ya nomino na mofimu {o} ya urejeshi kama inavyoonekana katika jedwali hili linalofuata:

**Jedwali 2.5: Matumizi ya umbo rejeshi "o" katika Kiswahili**

| Ngeli | Mofu | Mifano |
|---|---|---|
| yu +a+wa | ye<br>wa+o o | mtu aliyepigwa<br>watu waliopigwa |
| u+i | u+o o<br>i+o yo | mti uliokatwa<br>miti iliyokatwa |
| li+ya | li+o lo<br>ya+o yo | jicho lililoumia<br>macho yaliyoumia |
| ki+vi | ki+o cho<br>vi+o vyo | kiti kilichovunjika<br>viti vilivyovunjika |
| i+zi | i+o yo<br>zi+o zo | nguo iliyopasuka<br>nguo zilizopasuka |
| U | u+o o | uvivu uliomponza |
| u+ya | u+o o<br>ya+o o | ugonjwa ulioenea<br>magonjwa yaliyoenea |
| u+zi | u+o o<br>zi+o zo | ufa uliozibwa<br>nyufa zilizozibwa |
| ku | ku+o ko | kuimba kulikoskika |
| pa<br>mu<br>ku | pa+o po<br>mu+o mo<br>ku+o ko | mahali paliposifika<br>mahali mlimosifika<br>mahali kulikosifika |
| ya | ya+o yo | maji yaliyochotwa |
| i | i+o yo | chai iliyochemshwa |

Usuli: Mgullu (1999:195)

Mgullu (1999) anaeleza kuwa mofu rejeshi hizi zinahusisha nomino iliyokwisha kutajwa au ambayo bado haijatajwa, yaani mrejeosabiki au kidokezi na kuwa nomino hizo zinazohusishwa zinaweza kuwa na uamilifu wa aina mbalimbali kama vile nomino mtendwa (wali**o**pigwa), yambwa tendewa (ali**ye**jengewa), vitendana (wali**o**pigana), vitendeshwa (wana**o**fundishwa), kitendeka (kili**cho**vunjika), na kadhalika. Mgullu anazidi kusema kuwa katika kundi hili pia ndimo tunakuta mofu rejeshi ya namna vi+o {vyo} kama tunavyopata katika mfano *namna ali**vyo**cheza*.

Aidha, ni vyema kubainisha hapa kwamba mofu rejeshi hizi ndizo huandamana na matumizi ya shina *"amba"* katika kuunda kiwakilishi cha nomino iliyotajwa.

(2.14) *Ua ambalo limekatwa/ lililokatwa, nyumba ambazo zimejengwa/ zilizojengwa, mti ambao umeanguka/ ulioanguka.*

Mifano hii huweza kutuonyesha jinsi ambavyo mofu {o} hutumiwa katika Kiswahili na vile shina *amba* huandamana na viambishi vya ngeli za majina vinavyobadilikabadilika kutoka ngeli moja hadi nyingine. Mohamed (2001) anasema kuwa kiambishi cha wakati *-me-* ambacho hakiendi sambamba na matumizi ya virejeshi vinapotumiwa katika vitenzi hukubaliwa kutumika katika kitenzi ikiwa *amba-* imetumika.

(2.15) *a) *Wanafunzi wameokisoma kitabu kile ni wengi.*
*b) Wanafunzi ambao wamekisoma kitabu kile ni wengi.*

Kulingana na mifano hii, tunapata kwamba sentensi ya kwanza haikubaliki katika Kiswahili kwani haina usarufi ilhali sentensi ya pili ni sahihi.

### 2.4.2 Virejeshi vya mwisho

Katika Kiswahili, matumizi ya viambishi virejeshi vya nomino huweza kuruhusiwa mwishoni mwa kitenzi au kiunganishi *na* kama tunavyopata katika mifano hii ifuatayo.

(2.16) *a) Mtoto aliye mgonjwa ndiye huyu.*
*b) Mwalimu wetu ni mmoja tu: naye ndiye Kristo*
*c) Kitabu asomacho kila siku ndicho hiki.*

Katika mifano hii, *{ye}* ni kiwakilishi kirejeshi cha nomino *mtoto* katika (2.16 a) na *mwalimu* katika (2.16 c) wakati ambapo *{cho}* ndicho kiwakilishi kirejeshi cha nomino *kitabu* katika (2.16 b). Viambishi hivi vinajitokeza mwishoni mwa vitenzi (*aliye, ndiye* na *asomacho)* na huchukuliwa kama virejeshi vya mwisho. Muundo

*naye* unadhihirisha kuwa viwakilishi vya nafsi huweza kuwekwa pia mwishoni mwa kiunganishi *na* ili kuunda kiwakilishi. Mbaabu (1995) anadhihirisha kuwa virejeshi hivyo hurejelea nomino za ngeli tofauti na kuwa hutegemea ngeli za nomino hizo zinazorejelewa.

**2.4.3 Urejeshi wa ngeli katika vivumishi na viwakilishi**

Steere (1969) anaeleza kuwa kivumishi ni neno linalotumiwa kufafanua kile kinachoelezwa na nomino au kutoa maelezo zaidi kuhusu sifa ya nonimo hiyo. Katika utafiti wake, alibainisha kwamba viambishi awali vya vivumishi katika Kiswahili vinafanana na vile vya nomino isipokuwa ngeli ya ***u*** katika umoja.

*(2.17) a) **mtu mrefu, mbwa mkali, kiti kizuri, mtoto mnene, mlima, mrefu.***
*b) **ufa mrefu, ukuta mchafu.***

Steere (keshatajwa) anasisitiza kuwa ikiwa jina la ngeli ya KI-VI linarejelea mtu, kivumishi kitapata upatanishi ulio sawa na ule wa ngeli ya MU-WA.

*(2.18) kijana mrefu, kipofu mdogo, kiziwi mmoja.*

Vivumishi huwekwa baada ya jina linalovumishwa na huundwa kwa msingi unaoleta ukubalifu wa viambishi awali vya nomino na vile vya vivumishi vyenyewe. Hata hivyo, Steere anaeleza kuwa kuna vivumishi ambavyo havikubali kupokea viambishi vya nomino.

*(2.19) bora, hakika, rahisi, safi, hodari, kamili, lazima, radhi, sahihi, ghali, kila, amini, haba, imara, huru, marufu, halali, hafifu, dhahiri, uchi, faradhi, wazi, tele, maskini, tayari, kanuni, tajiri, salama, laini, kweli, haramu, dhaifu.*

Vivumishi hivi havichukui viambishi awali vya ngeli za majina vinapotumiwa pamoja na majina hayo na vingi vya vivumishi hivi ni vya sifa. Aina nyingine ya vivumishi vyenye sifa hii ya kutokubali kuchukua viambishi awali vya nomino na baadhi ya vivumishi vya idadi ipo katika mifano (2.20 b).

(2.20) a) *mtoto mmoja, kisu kimoja, miti mitatu, watoto wanne, wanawake watano*
b) *milima sita, watu saba, wanafunzi tisa, walimu kumi.*

Kulingana na mifano hii, vivumishi sita, saba, tisa na kumi haviendelezwi kwa njia sawa na vivumishi vingine vya idadi (2.20 a) kwani havichukui viambishi vya nomino zinazovumishwa. Aidha, Steere (1969) anabainisha pia kwamba vivumishi vya kuuliza huchukua viambishi vya nomino zinazovumishwa, lakini ndani ya kundi hili la vivumishi hivi kuna kivumishi *gani* ambacho hakina kiambishi chochote cha nomino.

(2.21) a) *watu wangapi, viti vingapi, mtu yupi, miti ipi, kiti kipi, nyumba ipi.*
b) *watu gani, miti gani.*

Kulingana na mifano hii, kivumishi kiulizi *gani* hakionyeshi kiambishi chochote cha jina linalovumishwa. Nacho kivumishi kiulizi *-pi* huchukua umbo wakilishi la nomino inayovumishwa nacho. Kihore na wengine (2003) wanauchukulia muundo wa kundi hili la vivumishi kama njia ya kuvipanga katika kundi la viwakilishi na kuingiza ndani mwake aina zingine zote zenye miundo kama hii. Miongoni mwa maumbo hayo ni pamoja na maneno yote yenye kueleza zaidi nomino inayozungumziwa na kubainisha sifa hiyo ya matumizi ya umbo wakilishi badala ya umbo fanani la kiambishi awali cha nomino.

(2.22) *miti yote, miti yoyote, miti yenyewe, ufa wenyewe, nyufa zenyewe.*

Tofauti na mifano (2.20.a), mfano (2.22) unadhihirisha kuwa, kimofolojia, maumbo *ote, o-ote, enyewe* huchukua viambishi vyenye muundo ulio tofauti na viambishi awali vya nomino husika kama lilivyo umbo *-pi* katika (2.21.a).

Katika utafiti huu, tumeamua kuzingatia mtazamo uliobainishwa na Mgullu (1999) na ambao unakichukulia kivumishi kama neno lolote linaloeleza zaidi juu ya nomino

kwa kufafanua kitu, mtu, sifa, hali au tendo linalowakilishwa na nomino hiyo. Navyo viwakilishi vinachukuliwa kama maneno ambayo hutumiwa badala ya jina. Mgullu anaeleza kwamba kwa kawaida viwakilishi vinapotumika nomino zinazowakilishwa na viwakilishi hivyo huwa hazitajwi kwani maneno haya huziwakilisha nomino hizo na ndiyo maana huitwa viwakilishi.

Kwa hivyo, tunaweza kuhakikisha kwamba vivumishi ni vya aina tofauti katika Kiswahili na huchukua upatanishi wa kisarufi kulingana na jina linalovumishwa au kutolewa habari. Mara nyingi viambishi vinavyotumiwa kwa vivumishi hivi hufanana na viambishi awali vya nomino inayofafanuliwa na kuelezwa navyo. Lakini, kuna kundi jingine la vivumishi (ote, o-ote, enyewe, a- unganifu) ambavyo hupata viambishi vya upatanishi wa kisarufi au umbo wakilishi badala ya kutumia viambishi vya nomino vinavyoandamana nayo.

## 2.5 Mofosintaksia ya ngeli za nomino katika Kinyarwanda

Kinyarwanda ni lugha inayozungumzwa katika Afrika ya kati hasa katika eneo kubwa la Maziwa Makuu. Shimamungu (1998) anasema kuwa wengi wa wazungumzaji wa lugha hii ni Wanyarwanda wanaoishi nchini Rwanda na wale wanaokaa katika maeneo yanayopakana na nchi ya Rwanda kama vile sehemu kubwa ya mashariki mwa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na kusini mwa Uganda (Gishari, Bwishya na Bufumbira). Shimamungu anabainisha kuwa lugha zingine kama vile Kirundi kinachozungumzwa nchini Burundi na Kiha kinachozungumzwa nchini Tanzania ni lugha zinazofanana sana na lugha ya Kinyarwanda kiasi kwamba zaweza kuchukuliwa kama lahaja za lugha moja.

Kama ilivyo katika lugha nyingi za Kibantu, Kinyarwanda nacho kinatumia mfumo wa ngeli. Mtazamo wa ngeli ulioshughulikiwa na watafiti wengi katika lugha ya Kinyarwanda ni ule wa kimofolojia ambapo Kinyarwanda hutumia ngeli zipatazo 19. Ngeli hizi ndizo hutawala mahusiano yote kati ya nomino na maneno mengine kama vile vivumishi, viwakililishi na vitenzi katika uundaji wa vipashio vikubwa ambavyo ni virai, vishazi na sentensi.

Ili kuelewa vizuri mfumo huo wa ngeli za Kinyarwanda ni vyema kuchunguza muundo wa nomino na vipashio vyake kwa jumla.

### 2.5.1 Muundo wa nomino katika Kinyarwanda

Nomino katika Kinyarwanda huwa na sehemu tatu : kisabiki kiambishi awali, kiambishi kati ambacho ndicho kiambishi cha ngeli na shina la nomino hiyo.

#### 2.5.1.1 Kisabiki kiambishi awali

Hiki ni kiambishi kinachotangulia viambishi vingine katika mpangilio wa vipashio vinavyounda nomino na hutumiwa kuyabainisha majina ya kijumla. Muundo wake huwa ni irabu *a, u* na *i*. Irabu hizi ndizo silabi za kwanza katika mpangilio wa vipashio vya nomino za Kinyarwanda. Uchaguzi wa irabu inayofaa kutumiwa kama kisabiki kiambishi awali cha jina hutegemea irabu inayotumiwa katika silabi ya pili ya jina hilo ambayo ndiyo kiambishi cha ngeli kama anavyoeleza Nkusi (1983).

*(2.23)* ***umugabo/abagabo*** (mwanamme/wanaume)

Katika mfano huu, mofu *{-mu-}* na *{-ba-}* hutegemea sana miundo ya irabu *{u-}* na *{a-}* zinazotangulia nomino husika. Irabu hizi ndizo visabiki viambishi awali

ambavyo hufanana na irabu *-u-* na *-a-* zinazojitokeza katika silabi za pili ambazo ndizo pia viambishi kati vya ngeli za nomino hizo.

Kisabiki kiambishi awali cha nomino huweza kudondoshwa pale jina linapotanguliwa na baadhi ya aina za maneno kama vile kikanushi « nta », vionyeshi kama *uyu* (huyu), *unó* (huyu), *waá* (yule), na kadhalika. Vilevile, kiambishi hiki huweza kudondoshwa ikiwa msemaji anatumia nomino jumuishi kumwita mtu, wakati ambapo msemaji anamtaka mtu kuwa makini ili aweze kuzingatia kile anachotaka kumfahamisha au ikiwa tungo imeundwa katika dhamira amrishi. Mifano inayofuata huweza kutudhihirishia jambo hilo:

*(2.24) a) U-yu-Ø mu-nyéeshuúri a-Ø-kuund-a kw-íig-a (Uyu munyéeshuúri akuunda kwíiga)*
*Ksb-kip-mz-kiang-mz-kip-wktulp-mz-kii-ku-mz-kii.*
*Huyu mwanafunzi anapenda kusoma.*
*b) Nta mu-nyéeshuri n-a-Ø-boon-yé u-yu-Ø mu-nsi (Nta munyéeshuúri naboónyé uyu muúnsi)*
*kikan-kiang-mz-nfs1-wktim-nfs3-mz-kii-ksb-kip-mz-kiang-mz..*
*Sijamuona mwanafunzi hii leo (leo hii).*
*c) Mw-aána u-a, íig-a néezá u-záa-tsiind-é (Maána wa.., iga néazá uzáatsiindé)*
*kiang-mz-kip-kiv unganifu-dham.amrishi/nasihi-mz-kii-kie-nfs2-wktuj-dham.amrishi/nasihi-mz-kii.*
*Mwanangu, kajifunze vizuri ili uweze kufaulu mitihani yako.*

Katika mifano hii, ni dhahiri kuwa matumizi ya baadhi ya aina za maneno hukifanya kisabiki kiambishi awali cha nomino kudondoshwa. Katika kipashio *uyu munyéeshuúri* 2.24 a, kisabiki kiambishi awali *{u}* kimedondoshwa katika nomino *umunyéeshuúri* kutokana na matumizi ya kionyeshi *uyu* wakati ambapo katika mfano 2.24 b, kikanushi *nta* kimekifanya kisabiki *{u}* kidondoshwe katika nomino *umunyéeshuúri*. Mfano *2.24 c* unatudhihirishia pia kwamba kisabiki kiambishi awali {u} cha jina *umwáana* kimedondoshwa kwa kuwa msemaji anamwita mtoto ili kumnasihi au kumwamrisha kujifunza vizuri.

Aidha, matumizi au udondoshaji wa kiambishi hiki huweza kuifanya nomino kutoka katika kundi la nomino za jumla na kuingizwa katika nomino za pekee.

(2.25) a) *Munyéeshuúri a-Ø-kuund-a kw-íig-a (Munyéeshuúri akuunda kwíiga)*
*nom.pekee-kip-wktulp/wktzo-mz-kii-ku-mz-kii.*
*Munyéeshuri anapenda kusoma*
b) *U-mu-nyéeshuri a-Ø-kuund-a kw-íig-a (Umunyéeshuúri akuunda kwíiga)*
*ksb-kiang-mz-kip-wktulp/wktzo-mz-kii-kiang-mz-ku-mz-kii.*
*Mwanafunzi anapenda kusoma*

Kutokana na tungo hizi, tunapata kwamba matumizi na udondoshaji wa kisabiki kiambishi awali {u} huzifanya tungo hizi zitofautiane pale ambapo katika tungo *25 a*, *Munyéeshuúri* ni nomino ya pekee ya mtu ilhali katika tungo *25 b*, jina *umunyéeshuúri* litakuwa na maana ya kijumla; yaani mwanafunzi yeyote. Kwa hivyo, matumizi na udondoshaji wa kiambishi hiki huongeza au kupunguza maana kwenye nomino inayohusika.

**2.5.1.2 Kiambishi ngeli**

Hiki ni kiambishi ambacho kinatumiwa hasa kuyapanga majina ya Kinyarwanda katika makundi tofauti ambayo ndiyo ngeli. Kiambishi hiki ndicho hutawala upatanishi wa kisarufi unaojitokeza katika sentensi. Kinyarwanda kina ngeli zipatazo 19 zinazoweza kugawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza huzingatia viambishi ngeli vya majina kuanzia ngeli ya kwanza hadi ya 16. Katika kundi hili viambishi ngeli ndivyo silabi za pili katika mpangilio wa vipashio vya majina hayo. Kundi la pili huundwa na viambishi ngeli za 17, 18 na 19 ambavyo muundo wake hutofautina kidogo na huo wa kwanza. Viambishi vya ngeli hizi ndivyo vipashio vya kwanza katika muundo wa majina na mara nyingi hujitenga na majina husika ingawa huchukuliwa kama sehemu ya majina yenyewe. Jedwali 2.6 huweza kutupa picha kamili ya muundo wa viambishi hivi.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**Jedwali 2.6: Mfumo wa ngeli katika Kinyarwanda**

| Jina la ngeli | | Mfano wa jina | | Mfano wa sentensi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | mu | u-mu-gabo<br>u-mu-áarimu | umugabo (mwanamme)<br>umwáarimu (mwalimu) | Umugabo munini yaaje hano (Mwanamme mnene amekuja hapa)<br>Umwáarimu mwiza arúgiisha (Mwalimu mzuri anafundisha) |
| 2 | ba | a-ba-gabo | abagabo (wanaume) | Abagabo baníni baaje hano (wanaume wanene wamekuja hapa) |
| 3 | mu | u-mu-twé<br>u-mu-eénge | umutwé (kichwa)<br>umweénge (tundu) | Umutwé waawe ufite uruhára (kichwa chako kina upara)<br>Umweénge uri muri uru rukuta ni wo uteera imbeho muri iyi nzu (tundu lililopo kwenye ukuta huu ndilo linasababisha baridi nyumbani humu) |
| 4 | mi | i-mi-twé | imitwé (vichwa) | Imitwé yáanyu ifite uruhára (vichwa vyenu vina upara) |
| 5 | ri<br>Ø | i-ri-íinyo<br>i-Ø-gí | iryíinyo (jino)<br>igí (yai) | Iryíinyo ryaanjye ryaakúutse (jino langu limeng'oka)<br>Igi riraryóoha (yai ni tamu) |
| 6 | ma | a-ma-íinyo | améenyo (meno) | Améenyo yáacu yaakúutse (meno yetu yameng'oka) |
| 7 | ki | i-ki-úuma | icyúuma (kisu) | Icyúuma kirakeba (kisu kinakata) |
| 8 | bi | i-bi-úuma | ibyúuma (visu) | Ibyúuma birakeba (visu vinakata) |
| 9 | N | i-n-táre | intáre (simba) | Intáre iratoontoma (kimba anangurума) |
| 10 | N | i-n-táre | intáre (simba) | Intáre ziratoontoma (samba wananguruma) |
| 11 | ru | u-ru-kutá | urukutá (ukuta) | Urukutá rwaaguuye (ukuta umeanguka) |
| 12 | ka | a-ka-áana | akáana (kitoto) | Akáana karaaje (kitoto kinakuja) |
| 13 | tu | u-tu-áana | utwáana (vitoto) | Utwáana turaaje (vitoto vinakuja) |
| 14 | bu | u-bu-éenge | ubwéenge (akili) | Ubwéenge buríiyongeera (akili inaongezeka) |
| 15 | ku | u-ku-guru | ukuguru (mguu) | Ukuguru kuraandyá (mguu unaniuma) |
| 16 | ha | a-ha-ntu | ahaantu (mahali) | Aha haantu harasukuuye (mahali hapa pamesafishwa) |
| 17 | ku | ku (nzu) | kuu nzu (kwenye nyumba) | Kuu nzu harasukuuye (kwenye nyumba kumesafishwa) |
| 18 | mu | mu (nzu) | muu nzu (nyumbani) | Muu nzu harasukuuye (nyumbani mmesafishwa) |
| 19 | i | i (Kigali)<br>i-muhirá | i Kigali (Kigali)<br>imuhirá (nyumbani, kwangu) | I Kigalí harasukuuye (Kigali kumesafishwa)<br>Imuhirá hari abaashyitsi beénshi (Nyumbani kwangu kuna wageni wengi) |

Jedwali 2.6 linadhihirisha kuwa lugha ya Kinyarwanda ina ngeli 19. Ngeli katika umoja ndiyo hutangulia na kufuatwa na ngeli katika wingi isipokuwa ngeli za 14, 16, 17, 18 na 19 ambazo zina miundo ya kipekee ya kujitenga na mizizi ya majina au kutoonyesha umoja wala wingi wa majina hayo. Hata hivyo, kila jina huhesabiwa katika kundi fulani kulingana na muundo wa viambishi hivyo vya ngeli ambavyo pia ndivyo msingi wa upatanishi wa kisarufi katika tungo za Kinyarwanda. Mfano 2.26 unatuelezea hali hii.

*(2.26)* *a) U-mw-áarimú mw-iizá a-ra-íig-iish-a (Umwáarimú mwiíza aríigisha)*
*ksb-kiang-mz-kip-mz-kip-wktulp-mz-ktesh-kii.*
*Mwalimu mzuri anafundisha*
*b) A-bá-áarimú ba-iizá ba-ra-íig-iish-a (Abáarim beéza baríigiisha)*
*ksb-kiang-mz-kip-mz-kip-wktulp-mz-ktesh-kii.*
*Walimu wazuri wanafundisha*

Sentensi hizi hutudhihirishia kwamba kiambishi cha ngeli katika nomino ndicho kinatawala upatanishi wa kisarufi katika sentensi nzima. Mabadiliko ya kiambishi ngeli {mu} katika mfano *2.26* a na {ba} katika *2.26 b* husababisha pia mabadiliko ya vipatanishi vyote vinavyotumiwa katika sentensi nzima kuzirejelea nomino ambamo viambishi hivyo vimetumiwa. Wakati ambapo kisabiki kiambishi awali huweza kudondoshwa kulingana na nia ya mzungumzaji, kiambishi ngeli hakidondoshwi ingawa tunayakuta majina yaliyo na viambishi ngeli visivyo bayana. Katika majina ya aina hii, mfano *2.27* unatuonyesha kuwa utambuzi wa ngeli hudhihirishwa kupitia upatanisho wa kisarufi uliomo katika tungo nzima.

*(2.27)*
*I-Ø-zúuru* ***ri****-raá-n-ri-a (Izúuru riraándya)/A-ma-zuuru a-raa-tu-ri-a (Amazúuru araándya)*
*ksb-kiang-mz-kip-wktulp-nfs1-mz-kii./ksb-kiang-mz-kip-wktulp-nfs1 mz-kii.*
*Pua linaniuma/ Mapua yanatuuma*

Kulingana na mfano *2.27*, ni dhahiri kuwa kiambishi ngeli cha jina *izuru* hakionekani kwani kinasimamiwa na mofu kapa {Ø}. Kwa hivyo, ngeli ya jina hili inatambulika kupitia kipatanishi {ri} ambacho ndicho pia kiambishi nafsi cha kitenzi *-rya*.

Bizimana (2002) anadhihirisha kwamba nomino za Kinyarwanda huweza kuainishwa katika makundi tofauti ya umoja na wingi kama tunavyopata katika jedwali hili.

**Jedwali 2.7: Makundi ya ngeli ya umoja na wingi katika Kinyarwanda**

| **Kundi** | **Mifano** | |
|---|---|---|
| 1/2 mu/ba | Mu | u**mu**gabo (u-mu-gabo/mwanaume, u**mu**márayíka (u-mu-árayíka) -Malaika |
| | Ba | a**ba**gabo (a-ba-gabo), mwanamume, a**ba**márayíka (a-ba-márayíka) -malaika |
| 3/4 mu/mi | Mu | u**mu**heto (u-mu-het-o) -uta, u**mu**ríma (u-mu-ríma) -shamba, u**mu**sega -mbwa aliyekonda |
| | Mi | i**mi**heto (i-mi-het-o)/nyuta, i**mi**ríma (i-mi-ríma) -mashamba, i**mi**sega -mbwa waliokonda, i**mi**korére (i-mi-kór-ir-e) -hali ya kutenda au utendaji wa jambo |
| 5/6 ri/ma | Ri | igí (i-Ø-gí) -yai, isokó (i-Ø-sokó) -soko, i**ryí**inyo (i-ri-íinyo) -jino, ihíinga (i-Ø-híing-a)/ -ukulima, |
| | Ma | a**ma**gí (a-ma-gi) -mayai, a**ma**sokó (a-ma-sokó), a**mée**nyo (a-ma-íinyo) -meno, a**ma**híinga (a-ma-híing-a)-ukulima |
| 7/8 ki/bi | Ki | i**ki**biíndi (i-ki-bindi) –mtungi, i**gi**tí (i-ki-ti)/ -mti, i**ki**gabo (i-ki-gabo) -mwanamume mwenye unene wa kuchukia, i**ki**réma (i-ki-réma) -mlemavu, i**gi**pfáamatwí (i-ki-pfú-a-ma-twí) -kiziwi |
| | Bi | i**bi**biíndi (i-bi-biíndi) -mitungi, i**bi**tí (i-bi-tí) –miti, i**bi**gabo (i-bi-gabo) -wanamume wenye unene wa kuchukia, i**bi**réma (i-bi-réma) -walemavu, i**bi**pfáamatwí (i-bi-pfú-a-ma-twí) -viziwi |
| 9/10 n/n | N | i**n**ká (i-n-ka) -ng’ombe, i**m**beba (i-n-beba) -panya, i**n**kokó (i-n-kokó) -kuku, i**n**tébe (i-n-tébe) -kiti, ishaáti, (i-n-shaáti) -shati, isáahá (i-n-sáahá) –saa |
| 11/8 ru/bi | Ru | u**rw**áana (u-ru-áana) -kitoto kibaya |
| | Bi | i**by**áana (i-bi-áana)- vitoto vibaya |
| 11/10 ru/n | Ru | u**ru**kutá (u-ru-kutá), ukuta/ u**ru**báahó (u-ru-báahó) -ubao, u**ru**rími (u-ru-rimi), -ulimi |
| | N | i**n**kutá (i-n-kutá) - kuta, i**m**báahó (i-n-báahó) -mbao, i**n**dími (i-n-rími)-ndimi |
| 12/13 ka/tu | Ka | a**ká**ana (a-ka-áana / kitoto/- a**ka**ríma (a-ka-ríma)/ -kishamba |
| | Tu | u**tw**áana (u-tu-áana) - vitoto; u**tu**ríma (u-tu-ríma) –vishamba |
| 14 bu | Bu | u**bu**sáaza (u-bu-sáaz-a) -uzee, u**bu**rwáayi (u-bu-rwáar-yi) –ugonjwa |
| 15/6 ku/ma | Ku | u**ku**bóko (u-ku-bóko)/ -mkono/ u**ku**guru (u-ku-guru)/ -mguu |
| | Ma | a**ma**bóko (a-ma-bóko) -mikono, a**ma**guru (a-ma-guru) –miguu |
| 15 ku | Ku | **gu**kina (ku-kin-a) -kucheza, **ku**ríriimba (ku-ríriimb-a) –kuimba |
| 16, 17, 18, 19 ha, ku, mu, i | Ha | A**ha** **haa**ntu **ha**rashyúushye (mahali hapa pana joto) |
| | Ku | **Ku** musózi **ha**rakóonje (kwenye mlima kuna baridi. |
| | Mu | **Mu** ishuúri **ha**rashyúushye (Darasani mna joto) |
| | I | **I** Muhaanga **ha**ri abaantu beénshi (Muhanga kuna watu wengi). |

Kulingana na mifano katika jedwali hili, ni dhahiri kwamba upangaji wa ngeli za majina katika Kinyarwanda huzingatia mofolojia ya majina hayo kwa kiwango kikubwa. Sifa za jumla za kimofolojia, yaani mfanano wa viambishi awali vya

majina, ndio unazingatiwa ingawa sifa hizi huwa wakati mwingine zimechanganywa na zile za kisemantiki ili kuyapambanua maumbo mbalimbali yanayofanana. Kwa mfano, kundi la ngeli la *{mu/ba}* linazingatia nomino zenye kutaja watu au viumbe wenye akili wakati ambapo *{mu/mi}* huingiza majina ya mimea, vifaa, baadhi ya sehemu za mwili, na kadhalika. Bizimana (2002) husema kuwa kiambishi {mi} huweza pia kurejelea hali ya kufanya kitu kama ilivyo katika jina *imikorére (i-mi-kór-ir-e)* -hali ya kutenda na wakati huo jina lenambalo halibainishi hali ya umoja.

Nomino katika ngeli za {ri/ma} huhusisha majina yenye kiambishi ngeli {ri} katika umoja na {ma} katika wingi. Majina mengine yasiyobainisha kiambishi ngeli hasa yale yaliyoundwa kutokana na vitenzi kama *ihíinga (i-Ø-híing-a)* -ukulima ambapo *ihíinga* huundwa kutokana na kitenzi *guhíinga* (kulima) na umoja wa majina kama *igí* (i-Ø-gí) -yai na *isokó* (i-Ø-sokó) -soko nayo huingizwa katika kundi hili.

Kundi la {ki/vi} huzingatia nomino zenye kuwa na viambishi ngeli {ki} katika umoja na {vi} katika wingi. Hili ni kundi ambalo linazingatia majina ya vifaa vya kawaida, baadhi ya mimea, na kadhalika. Katika kundi hili pia tunaweza kuyakuta majina mengine yenye dhana ya ukubwa usiopendelewa au yenye dhana ya kudharau kitu au kiumbe chochote kama vile *ikigabo (i-ki-gabo)* -mwanamume mwenye unene wa kuchukia na *igiká (i-ki-ká)* -ng'ombe mwenye unono wa kuchukia.

Aidha, majina ya watu wenye upungufu wa aina fulani nayo huingizwa katika kundi hili. Kwa hivyo, majina kama *ikiréma (i-ki-réma)* -mlemavu, *igipfáamatwí (i-ki-pfú-a-ma-twí)* -kiziwi, *ikimúga (i-ki-múga)* -mtu mwenye upungufu wa aina yoyote kwa mwili wake, yote huhesabiwa katika kundi hili. Ingawa majina haya ni ya binadamu,

kisintaksia hayaendelezwi kama majina mengine ya ngeli za kundi la kwanza *{mu/ba}* ambalo ndilo kundi linalozingatia majina ya watu au ya viumbe wenye akili. Majina haya yanachukua *{ki/bi}* kama vipatanishi vyake kwa vitenzi badala ya *{a/ba}* vinavyotumiwa kwa majina ya binadamu.

*(2.28)*
*(Ntibavuga): I-ki-réma ki-mwé ki-aa-z-ye há-no (Ikiréma kimwé cyaaje háno)*
*(Usiseme): kbs-kiang-mz-kip-mz-kip-wktim-mz-kii.-kiang-mz.*
*Mlemavu mmoja amekuja hapa.*
*(Ntibavuga): I-bi-pfu-á-ma-twí bi-biri bi-ríig-á (Ibipfáamatwí bibiri biríiga)*
*(Usiseme): ksb-kiang-mz-ksb-kiang-mz-kip-mz-kip-wktulp-mz.kii.*
*Viziwi wawili wanasoma*

Kulingana na mfano *2.28*, ni dhahiri kwamba jina *ikiréma* na *igipfáamatwí* yameendelezwa kama majina mengine ya ngeli za kundi la *{ki/vi}*. Kwa hivyo, upatanishi wa kisarufi katika Kinyarwanda hujikita zaidi katika mtazamo wa kimofolojia wa majina husika badala ya kuzingatia sifa za kisemantiki za majina hayo. Hali hii ndiyo inatufanya tuendeleze pia kwa namna sawa majina ya wanyama na yale yanayotaja vifaa au vitu mbalimbali kama ilivyo katika 2.29.

*(2.29)*
*a) I-n-ká i-ra-ríish-a/I-n-ká zi-ra-ríish-a*
*ksb-kiang.-mz.-kip-wktulp-mz.kii./ ksb-kiang-mz-kip-wktulp-mz-kii.*
*Ng'ombe anakula majani/ Ng'ombe wanakula majani*
*b) I-n-koni i-ra-bábar-y-a (inkoni irabábaza)/i-n-koni zi-ra-bábar-y-a (Inkoni zirabábaza)*
*ksb-kiang-mz-kip-wktulp/wktzo-mz-kau.tendeshi-kii./ ksb-kiang-mz-kip-wktulp/wktzo-mz.-kau.tendeshi-kii*
*Fimbo inaumiza/huumiza/Fimbo zinaumiza/huumiza.*

Mifano *2.29* inaonyesha kwamba majina ya wanyama katika *2.29 a* huendelezwa kisintaksia kwa namna sawa na majina yenye kutaja vitu mbalimbali kama tunavyopata katika *2.29 b*. Jambo hili hutokana na muundo wa viambishi ngeli vya majina hayo unaofanana katika umoja na wingi. Ushahidi wa kuyapanga majina haya katika kundi moja unapatikana pia pale ambapo kimofosintaksia majina *inká* (2.29 a) na *inzu* (2.29 b) hudhihirisha miundo ya {n-i} katika umoja na {n-zi} katika wingi.

Aidha, katika kundi hili la {n/n}, kuna majina ya mkopo ambayo hayaonyeshi kiambishi chochote katika umoja na wingi wakati ambapo mengine hupata wingi wake katika katika ngeli ya 6.

*(2.30)*
*a) I-n-módoká i-ra-héend-a (imódoká irahéenda)/i-n-módoká zi-ra-héend-a (Imódoká zirahéenda)*
*ksb-kiang-mz-kip-wktulp-mz-kii./ ksb-kiang-mz-kip-wktulp-mz-kii.*
*b) I-n-sáahá i-a-iib-w-ye (Isáahá yiíbwe)/i-n-sáahá zi-a-iib-w-ye (Isáahá ziíbwe)*
*kbs-kiang-mz-kip-wktim-mz.-kau tendwa-kii./kbs-kiang-mz-kip-wktim-mz-kau.tendwa-kii.*
*c) I-n-sáahá i-mwé-i-ra-shír-ye (isáahá imwe irashíze)/A-ma-sáahá a-biri a-ra-shír-ye (Amasáahá abiri arashize)*
*ksb-kiang-mz-kip-mz-kip-wktulp-mz.-kii./ ksb-kiang-mz-kip-mz-kip-wktulp-mz-kii.*
*Saa moja inakwisha/Saa mbili zinakwisha*

Kwa mujibu wa mifano 2.30, ni wazi kwamba kiothografia, nomino nyingi za mkopo hazionyeshi kiambishi ngeli. Kwa hivyo, upatanishi wa kisarufi unaotumiwa katika tungo nzima ndio unathibitisha ikiwa jina husika limo katika ngeli fulani. Mifano hiyo pia inatudhihirishia kwamba nyingi za nomino za mkopo katika Kinyarwanda huingizwa katika ngeli ya 9 {n} katika umoja na ya 10 {n} katika wingi, ingawa, kiothografia, hazionyeshi kiambishi ngeli chochote (2.30 a, 2.30 b). Pengine, baadhi ya nomino hizo huweza pia kupata wingi ama katika ngeli ya 10 {n} au ngeli ya 6 {ma} kama ilivyo katika 2.30 c ambapo nomino *isáahá* lenye muundo wa *isáahá* katika wingi (2.30 b) limeweza kuwa pia *amasáahá*.

Kundi la 16, 17, 18 na 19 (Jedwali 2.7) huwa na majina yote yanayorejelea mahali. Mzungumzaji huweza kudhihirisha mahali waziwazi kwa kutumia *{ha}* au kuzungumzia juu ya kitu, ya sehemu ya mwili wa mtu au mnyama pale ambapo anatumia kiambishi ngeli *{ku}*. Vilevile, mahali penyewe panaweza kuzungumziwa kwa umbali au kwa jumla pale ambapo kiambishi *{i}* hutumiwa. Aidha, kundi hili

linahusu pia undani wa mahali na mzungumzaji atatumia kiambishi ngeli *{mu}* kuashiria undani huo.

*(2.31)*

*a) A-ha-Ø haa-*ntu *ha-ra-shyúuh-ye (Aha haantu harashyúushye)*
*ksb-kiang-mz.-kip-wktulp-mz-kii.*
*Mahali hapa pana joto.*

*b) Ku mu-sózi ha-ra-kóonj-ye (Ku musózi harakóonje)*
*kih-kiang-mz-kip-wktulp-mz-kii.*
*Kwenye mlima kuna baridi.*

*c) I Muhaanga ha-ri a-ba-ntu ba-iínshi (I Muhaanga hari abaantu beénshi)*
*kih-nom.pekee-wktulp-mz-kiang-mz-kiang-mz.*
*Muhanga kuna watu wengi.*

*d) Mu i-Ø-shuúri ha-ra-shyúuh-ye (Mu ishuúri harashyúushye)*
*kih-ksb-kiang-mz-kip-wktulp-mz-kii.*
*Darasani mna joto.*

Kulingana na mifano yote iliyotolewa, ni wazi kwamba majina katika ngeli hizi za mahali huendelezwa kisintaksia kwa kutumia kipatanishi *{ha}* kinachoambikwa kwa vitenzi bila kujali tafauti kati ya miundo ya viambishi ngeli katika majina husika. Isitoshe, uchunguzi wa matumizi ya nomino katika kundi hili unatudhihirishia kuwa ngeli hizi huweza pia kuingiza dhana za nyakati.

(2.32)

a) *Mu w'2010 ha-á-baa-ye i-bi-ntu bi-iínshi bi-iíza (Mu w'2010 haabaye ibiintu byiínshi byiíza)*
*kie-kip-wktpit-mz-kii-ksb-kiang-mz-kip-mz-kip-mz.*
Mnamo mwaka 2010 palitokea vitu vingi vizuri.

*b) Kurí Páasíka ha-á-baa-ye n-misa i-mwé (Kuri Páasíka haábaaye misa imwé)*
*kie-kip-wktpit-mz-kii-kiang-mz-kip-mz.*
*Siku kuu ya Pasaka palisomwa misa moja*

*c) Keéra ha-á-baa-ye-hó u-mu-gabo n á u-mu-goré (Keéra haábaayehó umugabo n'úmugoré)*
*kie-kip-wktpit-mz-kii-kiw.wakati-ksb-kiang-mz-kiung-ksb-kiang.-mz.*
*Hapo zamani palitokea mme na mke.*

Mbali na makundi hayo madogo madogo ya ngeli, Bizimana (2002) anabainisha kuwa uainishaji wa ngeli za majina katika Kinyarwanda huweza kujikita katika makundi makubwa mawili. Kundi la kwanza ni la nomino kamili na kundi la pili linazingatia nomino ambazo ni pungufu. Katika kundi hilo la kwanza nomino zina sehemu zote tatu zinazodhihirika katika muundo wa kawaida wa nomino za

Kinyarwanda; yaani kisabiki kiambishi awali, kiambishi cha ngeli na shina. Kundi la pili la ngeli linazingatia nomino zenye upungufu wa aina fulani. Kuna nomino zenye kukosa kisabiki kiambishi awali, zile zenye kukosa kisabiki kiambishi awali na kiambishi cha ngeli kisichoonekana na nomino zenye kiambishi cha ngeli kisichoonekana.

*(2.32)* *a) umutwé (u-mu-twé)- kichwa*
*b) mushíki (Ø-mu-shíki)* -dada
*c) so (Ø-Ø-só)* -babako ; *nyoko (Ø-Ø-nyoko)*- mamako
*d) ifi (i-n-fi)* -samaki ; *izúuba (i-Ø-zuba)*- jua, *ihíinga (i-Ø-híinga)*

Mfano wa kwanza (2.32 a) unawakilisha majina katika kundi la kwanza lenye majina yanayobainisha mofimu zote tatu. Mifano mingine ni ya kundi la pili ambapo kuna majina yenye kukosa mofimu moja au mbili: kisabiki kiambishi awali kama ilivyo katika *2.32 b*, kiambishi ngeli kama ilivyo katika *2.32 d* au viambishi vyote viwili kama tunavyopata katika *2.32 c*. Ingawa baadhi ya majina hayo hayaonyeshi kiambishi chochote cha ngeli, ngeli zake hutambuliwa kupitia upatanishi wake wa kisarufi kama tunavyopata katika *2.26*. Katika mfano huu, jina *izúuru (i-Ø-zúuru)* linaingizwa katika kundi la ngeli *{ri/ma}* kutokana na kiambishi kiwakilishi chake katika kitenzi {ri}. Vilevile, wingi wake ni *amazuru (a-ma-zúuru)* ambapo kiambishi ngeli *{ma}* hutumika pamoja na kiambishi nafsi *{a}* katika kitenzi.

#### 2.5.1.3 Mzizi

Mzizi ndiyo sehemu ya jina ambayo huchukuliwa kama kiini chake kwa kuwa ndiyo inazingatia maana ya jina hilo. Sehemu hii haibadiliki kulingana na hali kwamba jina limeingizwa katika hali tofauti kama vile hali ya kudunisha, kukuza au hali ya umoja na ya wingi. Jina huweza kuwekwa katika hali hizo kwa kubadilisha viambishi vyake

awali, lakini mzizi wake haubadiliki kwani unazingatia maana msingi ya jina hilo. Mifano katika Jedwali 2.8 lindhihirisha jambo hilo.

**Jedwali 2.8: Utambuzi wa mzizi katika Kinyarwanda**

| Kundi la ngeli | | Nomino | Mfano |
|---|---|---|---|
| 1/2 | mu/ba | Umw**áana**/ab**áana** | Umw**áana** araaje/ab**aána** baraaje (mtoto anakuja/Watoto wanakuja) |
| 7/8 | ki/bi | Icy**áana**/iby**áana** | Icy**áana** kiraaje/iby**áana** biraaje (mtoto mbaya anakuja/watoto wabaya wanakuja) |
| 11 | ru/bi | Urw**áana**/iby**áana** | Urw**áana** ruraaje/iby**áana** biraaje (toto linakuja/matato yanakuja) |
| 12/13 | ka/tu | Ak**áana**/utw**áana** | Ak**áana** karaaje/Utw**áana** turaaje (kitoto kinakuja/vitoto vinakuja) |

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba mzizi wa jina haubadiliki. Viambishi awali na vya kati vya mzizi {-áana} vimebadilishwa kutokana na dhana inayolengwa na mzungumzaji pale ambapo hali ya kawaida ni *umw**áana*** katika umoja na *ab**áana*** katika wingi; hali ya kudunisha *ak**áana**/utw**áana*** hali ya kukuza *urw**áana**/**iby**áana* na *icy**áana** /**iby**áana*. Mifano hii miwili ya mwisho huweza kuleta pia dhana ya kumdharau mtu kulingana na muktadha. Kwa hivyo, jina *"umwáana"* (mtoto) huweza kuingizwa katika ngeli tofauti na kupewa maana tofauti katika ngeli hizo lakini mzizi wake haubadiliki. Maana kusudiwa hutokana hasa na kiambishi cha ngeli kinachobadilikabadilika kwa ajili hiyo ya kuleta maana hizo tofauti.

### 2.5.2 Upatanishi wa kisarufi katika Kinyarwanda

Kama tulivyobainisha katika §2.2, muundo wa tungo za lugha za Kinyarwanda na Kiswahili hutawaliwa na upatanishi wa kisarufi au mshikamano unaojitokeza kati ya nomino na maneno mengine yanayounda sentensi na kuathiriwa nayo kimuundo; yaani kivumishi, kiwakilishi na kitenzi. Kwa hivyo, sehemu hii itachunguza jinsi ambavyo upatanishi wa kisarufi ulivyo katika Kinyarwanda ili kutuwezesha kuelewa

athari za lugha hii kwa mwanafunzi Mnyarwanda anayejifunza Kiswahili kama lugha yake ya pili. Ili kukikabili kipengele hiki katika sehemu hii, tutazingatia mtazamo wa Bizimana (2002) na Shimamungu (1998) kuhusu fafanuzi wanazozitoa kuelezea kivumishi na kiwakilishi. Tafiti zao zinatilia mkazo mofolojia au muundo wa maneno haya katika kuyatofautisha na kuayaainisha ingawa katika maelezo yao, uamilifu wake katika tungo, nao hugusiwa.

### 2.5.2.1 Nomino na kivumishi

Bizimana anasema kuwa vivumishi ni maneno yanayotoa maelezo zaidi kwa nomino hiyo kwa kubainisha sifa, hali na namna nomino hiyo ilivyo. Neno hilo huchukua kiambishi awali kinachofanana na kile cha nomino inayoelezewa na kuandamana nalo. Mizizi ya vivumishi katika Kinyarwanda ni kamili:

> *(2.33) gufí (fupi), bí (baya), kurú (kubwa), tó (dogo), iiza (zuri), hiíre (zuri sana), ké (chache), iínshi (ingi), bísi (bichi), sa (bila kuchanganywa), shyá (pya), níni (kubwa), zima (zima)* na *garí (pana).*

Hivi ndivyo vivumishi katika Kinyarwanda na vinapotumika katika tungo ni lazima vichukue viambishi vya ngeli vinavyofanana na vile vya nomino zinazovumishwa navyo.

> *(2.34) **umusóre muguf**í* (kijana mfupi); *umusózi **mureemure*** (mlima mrefu), *iryíinyo **riguf**í* (jino fupi), ***urukutá rwiíza*** (ukuta mzuri).

Majina mengine yasiyobainisha kiambishi chochote cha ngeli hutumia kiambishi kinachofanana na kile cha majina mengine yaliyomo katika kundi moja.

> *(2.35) igí **riníni**/amagí **maníni** (yai kubwa/mayai makubwa).*

Katika mfano huu, jina *igí (i-Ø-gí)/amagí (a-ma-gí)* -yai/mayai hupata upatanishi wa kisarufi katika *{ri/ma}* kama ilivyo katika majina mengine ya kundi hili. Ingawa

muundo wa kawaida wa kivumishi hubainisha mofu mbili; yaani kiambishi awali cha ngeli na mzizi, wakati mwingine huweza kuchukua muundo wa kawaida wa nomino kinaposimama badala ya jina. Mifano katika *2.36* huweza kututhibitishia jambo hilo.

*(2.36) (a) A-ba-byéeyi ba-iíza ba-Ø-kuund-a a-ba-áana (Ababyéeyi beéza bakuunda abáana)*
*ksb-kiang-mz-kip-mz-kip-wktulpo/wktzo-mz-kii-ksb-kiang-mz.*
*Wazazi wazuri wanapenda/hupenda watoto.*
*(b) A-ba-iíza ba-Ø-kuund-a a-ba-áana (abéezá bakuunda abáana)*
*ksb-kiang-mz-kip-wktulpo/wktzo-mz-kii-ksb-kiang.-mz.*
*Wazuri hupenda watoto.*

Kama tunavyopata katika mifano hii, kivumishi *beéza* (ba-iíza) kinatoa maelezo zaidi kuhusu sifa ya nomino *ababyéeyi* (a-ba-byéeyi). Mfano *2.36 a* unaonyesha kuwa kivumishi chenyewe kimeandamana na jina linalofafanuliwa nacho wakati ambapo mfano *2.36 b* unadhihirisha zaidi uamilifu wa kusimama badala ya jina linalotolewa maelezo nacho. Kwa hivyo, uamilifu huu wa pili wa kusimama badala ya jina ndio umekifanya kivumishi hicho kuchukua muundo wa kawaida wa jina; yaani kisabiki kiambishi awali, kiambishi awali cha ngeli na mzizi (§2.4.1).

### 2.5.2.2 Upatanishi wa nomino na kiwakilishi

Kiwakilishi ni neno linalotumiwa kuirejelea nomino fulani, kuikamilisha kwa kuifafanua zaidi au kuieleza (Shimamungu, 1998). Kiwakilishi huwa na kipashio wakilishi cha nomino hiyo na kudhihirisha uhusiano uliopo kati ya nomino na kiwakilishi chenyewe. Kwa hivyo, muundo wa kiwakilishi huwa na sehemu kuu mbili ambazo ni kiambishi wakilishi cha nomino na mzizi wa kiwakilishi. Wakati mwingine kiwakilishi huweza kuwekewa kisabiki kiambishi awali na kusimama badala ya nomino inayorejelewa kama ilivyo katika mifano *2.37.*

*(2.37) (a) A-ba-ntu ba-biri ba-a-iic-ye u-mu-ntu u-mwé (Abaantu babiri biishe umuuntu umwé*
*ksb-kiang-mz-kip-wktpit-mz-ksb-kiang-mz-kip-mz.*
*Watu wawili walimuua mtu mmoja*

*(b) A-ba-bíri ba-a-iic-ye u-mwé (Ababíri biishe umwé)*
*ksb-kiang-mz-kip-wktpit-kip-mz.*
*Wawili walimuua mmoja.*

Kulingana na mifano hii hapo juu, kiwakilishi *babiri* (ba-biri) kimetumiwa kukamilisha au kueleza zaidi kuhusu idadi ya nomino *abaantu* (watu). Katika mfano wa kwanza (2.37 a) kiwakilishi *babíri* (wawili) kimetumika pamoja na jina linalotolewa maelezo na kiwakilishi chenyewe *abaantu* (watu) ilhali katika mfano wa pili (2.37 b) kiwakilishi hicho kimetumika bila kuandamana na jina lenyewe. Katika hali hiyo, kiwakilishi *babiri* kimechukua kisabiki kiambishi awali *{a}* na kuunda kiwakilishi *ababiri (a-ba-biri)* chenye mofu tatu zinazotumika kubainisha miundo ya kawaida ya majina ya Kinyarwanda (§2.4.1).

Shimamungu (1998) anadhihirisha kuwa viwakilishi katika Kinyarwanda ni vya aina mbili: viwakilishi vijalizo na viwakilishi visimamizi. Kundi la kwanza huzingatia viwakilishi vinavyotumiwa pamoja na majina yanayotolewa maelezo navyo. Kundi la pili la viwakilishi husimamia viwakilishi vyote vinavyotumiwa bila kuandamana na nomino zinazofafanuliwa na viwakilishi hivyo au pengine vikaitangulia nomino hiyo badala ya kuifuata.

*(2.38) a) I-n-ká yíi-ndi i-aa-báag-w-ye (Inká yiíndi yaabáazwe)*
*ksb-kiang-mz-kip-mz-kip-wktim-mz-kii.*
*Ng'ombe mwingine amechinjwa*
*b) I-yíi-ndi n-ká i-aa-báag-w-ye (Iyiíndi nká yaabázwe)*
*ksb-kiang-mz-kiang-mz-kip-wktim-mz-kii.*
**Mwingine ng'ombe amechinjwa*
*Ng'ombe mwingine amechinjwa*
*c) I-yíi-ndi i-aa-báag-w-ye (Iyiíndi yaabázwe)*
*ksb-kiang-mz-kip-wktim-mz-kii.*
*Mwingine amechinjwa.*

Katika mfano *2.38 a*, kiwakilishi *-ndi* hakionyeshi kisabiki kiambishi awali na kimefuata nomino inayoelezwa nacho wakati ambapo katika mfano *2.38 b*,

kiwakilishi hiki kimetumia kisabiki na kutangulia jina linaloelezwa na kuandamana nacho. Mfano *2.38 c* unadhihirisha pia kwamba kiwakilishi hiki *-ndi* huweza kutumia kisabiki wakati kinaposimama badala ya jina linalorejelewa nacho. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba matumizi ya kisabiki kiambishi awali katika viwakilishi hutegemea muundo wa tungo nzima.

Aidha, kulingana na mifano iliyotolewa hapo juu, ni bayana kwamba tofauti kubwa kati ya vivumishi na viwakilishi vya Kinyarwanda huegemezwa zaidi kwenye muundo wa maneno hayo na uamilifu wake katika tungo. Vilevile, idadi ya vivumishi ni kamili na mizizi yake hujulikana wakati ambapo viwakilishi ni vya aina mbalimbali na huweza kutangulia jina au kulifuata kwa kulitolea maelezo kuhusu idadi, hali, umbali wa kitu kinachozungumziwa, umilikaji wake, na kadhalika. Isitoshe, vivumishi hutumia viambishi vya ngeli vinavyofanana na vile vya ngeli ya jina linayovumishwa wakati ambapo viwakilishi huwa na viambishi ambavyo ni umbo wakilishi la jina husika.

**2.5.2.3 Upatanishi wa nomino na kitenzi**

Katika Kinyarwanda, ngeli ya jina ndiyo inayotumiwa kuamua kiambishi mwafaka kinachoambikwa kwa kitenzi kama kiambishi nafsi au kiambishi rejeshi yambwa. Urejeshi huo ni wa aina mbili: kuna urejeshi wa mwanzoni mwa kitenzi ambao hutumia kiambishi nafsi cha ngeli ya jina linalosimama kama kiima cha kitenzi hicho na urejeshi wa kati ambao hutumia kiambishi cha ngeli cha jina hilo kama kiambishi mtendwa au yambwa.

(2.39) a) *U-mw-áana a-ra-z-ye n-ra-mú-bon-a (Umwáana araaje ndamúbona)*
*ksb-kiang-mz-kip-wktulp-mz-kii-nfs1-wktulpo-nfs3-mz-kii.*
*Mtoto anakuja ninamuona*
b) *A-ba-áana ba-ra-z-ye n-ra-bá-bon-a (Abáana baraaje ndabábona)*
*ksb-kiang-mz-kip-wktulipo-mz-kii-nfs1-wktulp-nfs3-mz-kii.*
*Watoto wanakuja ninawaona*
c) *U-tw-áana tu-ra-z-ye n-ra-tú-bon-a (Utwáana turaaje ndatúbona)*
*ksb-kiang-mz-nfs3-wktulp-mz-kii-nfs1-wktulp-nfs3-mz-kii.*
*Vitoto vinakuja ninaviona*

Katika tungo hizi tunapata kwamba viambishi nafsi vya vitenzi *{a, ba, tu}* hurejelea nomino *umwaana* (2.39 a), *abaána* (2.39 b) na *utwáana* (2.39 c) na nomino hizi ndizo viima vya vitenzi *araaje, baraaje* na *turaaje.* Kwa upande mwingine, viambishi yambwa *{mu, ba, tu}* vimewekwa katikati mwa kitenzi, yaani kati ya viambishi awali vingine na mzizi wa kitenzi, *ndamúbona* (2.39 a), *ndabábona* (2.39 b) na *ndatúbona* (2.39 c), ili kuzirejelea nomino *umwáana* (mtoto), *abáana* (watoto) na *utwáana* (vitoto). Kwa hivyo, matumizi ya kiambishi nafsi mtenda na yambwa hutegemea sana kiambishi ngeli cha jina linalorejelewa katika kitenzi husika.

Kwa kuhitimisha sehemu hii, Jedwali 2.9 laweza kutupa picha kamili ya hali halisi ya upatanishi wa kisarufi na urejeshi wa nomino katika Kinyarwanda:

**Jedwali 2.9: Upatanishi wa kisarufi katika Kinyarwanda**

| **Ngeli na Kip./ kiv.** | **Upatanishi wa nomino na kivumishi** | **Upatanishi wa nomino na Kiwakilishi** | | **Upatanishi wa nomino na kitenzi** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Mfano wa nomino na kiv.** | **Kip kiw** | **Mfano wa kiwakilishi** | **Kip nfs** | **Mfano wa kitenzi** | **Kirj. yam** | **Mfano wa kitenzi** |
| 1 mu | U**mu**untu **mu**tó (mtu mdogo) | u | **u**ríiya muuntu (mtu yule) | a/u | **a**raaje /ujé (yule anakuja/anayekuja) | mu | naa**mú**bonye (nimemuona) |
| 2 ba | a**ba**antu **ba**tó (watu wadogo) | ba | **bá**riíya baantu (watu wale) | ba | **ba**ajé (wale wanaokuja) | ba | naa**ba**bóonye (nimewaona) |
| 3 mu | u**mu**ríma **mu**tó (shamba dogo) | u | **u**ríiya murimá (shamba lile ) | u | **u**híingwa (linalolimwa) | wu | naa**wu**bóonye (nimeliona) |
| 4 mi | i**mi**ríma **mi**tó (mashamba madogo) | i | **i**rúiya mirimá (mashamba yale ) | i | **i**híingwa (linalolimwa) | yi | naa**yi**bóonye (nimeyaona) |
| 5 ri | i**ry**íinyo **ri**tó (jino dogo) | ri | **rí**riíya ryíinyo (jino lile) | ri | **ry**aakuutsé (lililong'oka) | ri | naa**ri**bóonye (nimeliona) |
| 6 ma | a**mé**enyo **ma**tó (meno madogo) | a | **a**rúiya méenyo (meno yale) | a | **y**akuutsé (yaliyong'oka) | ya | naa**ya**bóonye (nimeyaona) |
| 7 ki | i**gi**tí **gi**tó (mti mdogo)<br>i**ki**rema **gi**tó (mlemavu mdogo) | ki | **kí**riíya gití (mti ule)<br>**kí**riíya kiréma (mlemavu yule) | ki | **cy**aatemwé (uliokatwa)<br>**cy**aaje/cyaáje (aliyekuja) | ki | naa**ki**bóonye (nimeuona)<br>naa**ki**boonye (nimemuona) |
| 8 bi | i**bi**tí **bi**tó (miti midogo) | bi | **bí**riíya bití (miti ile)/biriiya **bi**réme (walemavu wale) | bi | **by**aatemwé (iliyokatwa) | bi | naa**bi**bóonye (nimeiona) |
| 9 n | i**n**ká **n**tó (ng'ombe mdogo) | i | **i**rúiya nká (ng'ombe yule) | i | **i**raríisha/iríisha (anayekula majani) | yi | naa**yi**bóonye (nimeiona) |
| 10 n | i**n**ká **n**tó (ng'ombe wadogo) | zi | **zí**riíya nká (ng'ombe wale) | zi | **zi**riishá (wanaokula majani) | zi | naa**zi**bóonye (nimeziona) |
| 11 ru | u**ru**kutá **ru**tó (ukuta mdogo) | ru | **rú**riíya rukutá (ukuta ule) | ru | **rw**aaguuyé (umeanguka/ulioanguka) | ru | naa**ru**bóonye (nimeuona) |
| 12 ka | a**ká**ana **ga**tó (kitoto kidogo) | ka | **ká**riíya káana (kitoto kile kile) | ka | **ka**ajé (kinachokuja) | ka | naa**ka**bóonye (nimekiona) |
| 13 tu | ut**w**áana **du**tó (vitoto vidogo) | tu | **tú**riíya twáana (vitoto vile) | tu | **tu**raaje/tuujé (vinavyokuja) | tu | naa**tu**bóonye (nimeviona) |
| 14 bu | u**bu**níni **bw**iizá (unene mzuri) | bu | **bú**riíya buníni (unene ule) | bu | **bu**ukuundwá (unaopendwa) | bu | naa**bu**bóonye (nimeiona) |
| 15 ku | u**ku**guru **gu**tó (mguu mdogo)<br>**ku**geenda **kw**iizá (kutembea kuzuri) | ku | **kú**riíya kuguru (mguu ule)<br>**kú**riíya kugeenda (kutembea kule) | ku | **kw**aakoméretse (uliojeruhiwa)<br>**gu**shiimíisha (kunakofurahisha) | ku | naa**ku**bóonye (nimeuona)<br>naa**ku**bóonye (nimekuona) |
| 16 ha | a**ha**antu **hee**zá (mahali pazuri) | ha | **há**riíya haantu (mhali pale) | ha | **ha**asukúuwe (paliposafishwa) | ha | naa**ha**bóonye (nimepaona) |
| 17 ku/ha | **ku** rukutá **hee**zá (kwenye ukuta kuzuri) | ha | **há**riíya ku rukutá (kwenye ukuta kuna) | ha | **ha**asukúuwe (kulikosafishwa) | ha | naa**ha**bóonye (nimekuona) |
| 18 mu/ha | **mu** nzu **hee**zá (nyumbani mzuri) | ha | **há**riíya muu nzu (nyumbani mle) | ha | **ha**asukúuwe (mlimosafishwa) | ha | naa**ha**bóonye nimemuona) |
| 19 i/ha | **i** Kigalí **hee**zá (Kigali kuzuri) | ha | **há**riíya i Kigali (Kigali kule) | ha | **ha**asukúuwe (kulikosafishwa) | ha | naa**ha**bóonye (nimekuona) |

Jedwali 2.9 linadhihirisha tofauti za upatanishi unaojitokeza au mahusiano yaliyopo kati ya nomino na kivumishi, nomino na kiwakilishi na nomino na kitenzi. Kwa hivyo, ni dhahiri kuwa upatanishi wa kisarufi katika Kinyarwanda hutawaliwa na nomino kwa kutumia viambishi tofauti kulingana na aina ya neno linaloandamana na nomino hiyo.

*(2.40) i**mi**rimá **mi**tó (milima midogo), i**ry**íinyo ritó (jino dogo) na i**gi**tí **gi**tó (mti mdogo)*

Katika mifano (2.40), viambishi vinavyorejelea nomino katika vivumishi hufanana na viambishi ngeli vya majina yanayovumishwa ambapo miundo ya kivumishi *tó* hutegemea mofimu za ngeli za majina yaliyotumika; yaani, *{mi}* katika nomino *imirimá* (i-mi-rimá), *{ri}* katika *iryíinyo* (i-ri-íinyo) na *{ki}* katika *igití* (i-ki-tí).

Aidha, jedwali 2.9 linaonyesha pia kwamba viwakilishi, kwa upande wake, hutumia maumbo wakilishi ya nomino zinazoelezwa navyo.

*(2.41) a) A-ríiya ma-íinyo a-aa-kúuk-ye (Aríiya méenyo yaakúutse)*
*kip-mz-kiang-mz-kip-wktim-mz-kii.*
*Yale meno yameng'oka*
*b) U-ríiya mu-rimá u-ra-híing-w-a (Uríiya murimá urahíingwa)*
*kip-mz-kiang-mz-kip-wktulpo/wktzo-mz-kau.tendwa-kii.*
*Lile shahamba linalimwa/hulimwa*

Kupitia mifano (2.41), ni dhahiri kwamba viwakilishi *aríiya* na *uríiya* vimeendelezwa kwa namna tofauti na vivumishi katika 2.26 na 2.40 ambapo viwakilishi hutumia umbo wakilishi wakati ambapo vivumishi hutumia umbo fanani na lile la kiambishi ngeli cha jina husika. Viambishi ngeli vinavyotumiwa katika viwakilishi ni vile vinavyoambikwa pia kwa vitenzi kama viambishi nafsi au vipatanishi. Kwa hivyo, mofu {a} katika kiwakilishi *aríiya* (2.41 a) hurejelea jina *amenyo* na umbo la mofu hii ndilo pia hutumiwa kama kiambishi nafsi kipatanishi cha jina hilo kwa kitenzi

*yaakúutse* (a-a-kuuk-ye). Halikadhalika, mfano *2.41 b* unadhihirisha kwamba kipashio {u} kinasimia nomino *umurima* katika kitenzi *urahíingwa*.

Urejeshi wa nomino katikati mwa kitenzi nao unabainisha maumbo yaliyo tofauti kama tunavyoona katika 2.42.

*(2.42) a) U-mu-ntu, n-aa-mu-bóon-ye (Umuuntu, naamubóonye)*
*ksb-kiang-mz-nfs1-wktim-nfs3-mz-kii*
*Mtu, nimemuona.*
*b) U-mu-rima, n-aa-wu-bóon-ye (Umurima, naawubóonye)*
*ksb-kiang-mz-nfs1-wktim-nfs3-mz.-kii.*
*Shamba, nimeliona.*

Katika *2.42 a*, kiambishi *{mu}* katika kitenzi *naamuboonye* (n-aa-mu-bóon-ye) kimetumiwa kuwakilisha jina *umuuntu* la ngeli ya kwanza {mu} wakati ambapo umbo *{wu}* linawakilisha nomino *umurimá* (2.42 b) ya ngeli ya tatu {mu} katika kitenzi *nawubóonye (n-aa-wu-bóon-ye)*.

## 2.6 Ulinganishaji wa mfumo wa ngeli katika Kiswahili na Kinyarwanda

Kama tulivyoeleza katika sehemu hii, Kiswahili na Kinyarwanda ni lugha za Kibantu ambazo zinatumia mifumo ya ngeli inayofanana sana. Upatanishi wa kisarufi katika lugha hizi hutegemea sana ngeli za majina ambazo ndizo nguzo ya usarufi wa tungo zinazoundwa na watumiaji wa lugha hizi kama tunavyopata katika Jedwali 2.10.

**Jedwali 2.10: Ngeli za Kiswahili na za Kinyarwanda**

| Kiswahili | | | Kinyarwanda | |
|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Ngeli** | **Mifano** | **Ngeli** | **Mifano** |
| I | mu-/mw-/m- | **mu**uguzi, **mw**alimu, **m**toto | mu (mw) | **umu**sáaza (mzee) /**umw**áarimu (mwalimu) |
| II | wa- | **wa**uguzi, **wa**limu, **wa**toto | ba | **aba**sáaza (wazee)/**ab**áarimu (walimu) |
| III | mu-/mw-/m- | **mu**ungu, **m**to; **mw**embe | mu (mw) | **umu**gezi (mto)/**umw**eembe (mwembe) |
| IV | mi- | **miungu,** **mi**to, **mi**embe | mi (my) | **imi**gezi (mito)/**imy**eembe (miembe) |
| V | ji-/Ø | **ji**we, Øpanga | ri (ry)/Ø | **iry**úinyo (jino)/**iØ**buye (jiwe) |
| VI | ma- | **ma**we, **ma**panga | ma | **amé**enyo (meno)/**ama**buye (mawe) |
| VII | ki- | **ki**tabu | ki (cy) | **igi**tabo (kitabu)/**icy**úuma (kisu) |
| VIII | vi- | **vi**tabu | bi (by) | **ibi**tabo (vitabu)/ **iby**úuma (visu) |
| IX | n- | **n**yumba | n | **in**zu (nyumba) |
| X | n- | **n**yumba/**m**bao/**m**vua | n | **in**zu (nyumba)/**im**baahú (mbao)/**im**vúra |
| XI | u | **u**bao | ru | **uru**baahú (ubao) |
| XII | - | - | ka | **aká**ana (kitoto) |
| XIII | - | - | tu | **utw**áana (vitoto) |
| XIV | u- | **u**gonjwa | bu (bw) | **ubu**rwáayi (ugonjwa)/ubwéenge (akili) |
| XV | ku- | **ku**imba | ku | **ku**ríriimba (kuimba) |
| XVI | pa- | mahali **pa**le | ha | **aha**antu (mahali) |
| XVII | ku- | mahali hu**ku** | ku | **ku** rukutá (kwenye ukuta) |
| XVIII | mu | mahali hu**mu** | mu | **muu** nzu (nyumbani) |
| XIX | - | | i | **i** Muhaanga (Muhanga) |

Jedwali hili linadhihirisha kwamba maumbo mengi ya ngeli za majina katika Kiswahili na Kinyarwanda yanafanana. Katika ngeli ya kwanza na ya tatu, Kiswahili hutumia alomofu *{mu, mw, m}* wakati ambapo Kinyarwanda kinatumia *{mu}* na *{mw}*. Maumbo ya ngeli za 12, 13 na 19 hayamo katika Kiswahili. Badala ya kutumia {ka} na {tu} za kudunisha katika Kinyarwanda, Kiswahili hutumia ngeli za 7 na 8, {ki} na {vi}, kuelezea dhana hiyo. Nalo umbo la {i} la ngeli ya 19 ya kueleza umbali wa mahali katika Kinyarwanda hutumia kiambishi {ku} katika Kiswahili kurejelea dhana hiyo. Maumbo mengine ni sawa isipokuwa tofauti ndogo za matumizi ya konsonanti zinazojidhihirisha katika ngeli za 2, 5, 8, 11, 14 na 16 ambapo Kiswahili hutumia *{wa, ji, vi, u, u, pa}* ilhali Kinyarwanda hutumia maumbo ya *{ba, ri, bi, ru, bu, ha}*.

Tunapochunguza mtazamo wa kisintaksia wa ngeli za Kiswahili na Kinyarwanda, hasa urejeshi wa ngeli hizi katika upatanishi wa kisarufi, tunatambua kwamba mifumo yote miwili hufanana pia. Matumizi ya viambishi nafsi vinavyoambikwa kwa vitenzi na virejeshi vya ngeli katika vitenzi huzingatia taratibu zinazofanana na maumbo yenyewe hufanana sana kwa upande mmoja na kubainisha tofauti ndogo kwa upande mwingine. Jedwali 2.11 laweza kutupa picha kamili ya hali hiyo.

**Jedwali 2.11: Upatanishi wa ngeli katika vitenzi vya Kiswahili na Kinyarwanda**

| Kiswahili | | | Kinyarwanda | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Ngeli** | **Umoja** | **Wingi** | **Ngeli** | **Umoja** | **Wingi** |
| 1 yu-a-wa | Mtu **yu**aja<br>Mtu **a**nakuja, | Watu **wa**nakuja | a/u-ba | Umuuntu **u**jé/araaje (mtu anayekuja/Mtu anakuja) | Abaantu **baajé**/baraaje (Watu wanaokuja/ wanakuja) |
| | Ng'ombe **a**mechinjwa | Ng'ombe **wa**mechinjwa | | - | - |
| | Kiziwi **a**natembea | Viziwi **wa**natembea | | - | - |
| 2 u-i | Mto **u**mefurika | Mito **i**mefurika | u-i | Umurimá **u**rahúngwa (shamba linalimwa) | Imiríma irahúngwa (Mashamba yanalimwa) |
| 3 li-ya | Jicho **li**nauma | Macho **ya**nauma | Ø/ri-a | iØjúsho **ri**rareeba (jicho linaona) | Amáaso **a**rareeba (macho yanaona) |
| 4 ki-vi- | Kisu **ki**nakata | Visu **vi**nakata | ki-bi | Icyúuma **ki**rakeba (Kisu kinakata | Ibyúuma **bi**rakeba (visu vinakata) |
| | - | - | | Ikiréma **ki**rakóra (mlemavu anafanya kazi) | ibiréma **bi**rakóra (walemavu wanafanya kazi) |
| 5 i-zi | Nguo **i**napasuka | Nguo **zi**napasuka | i-zi | Inzu **i**rúubakwa (nyumba inajengwa) | Inzu **zi**rúubakwa (nyumba zinajengwa) |
| | - | - | | Inká **i**rarúsha (Ng'ombe anakula majani) | Inká **zi**rarúsha (ng'ombe wanakula majani) |
| 6 u-zi | Ufa **u**nazibwa | Nyufa **zi**nazibwa | ru-zi | Urukutá **ru**rúubakwa (ukuta unajengwa) | Inkutá **zi**rúubakwa (kuta zinajenhgwa) |
| 7 u-ya | Ugonjwa **u**meenea | Magonjwa **ya**meenea | i-a | Ifi **i**ranywá amáazi (samaki anakunywa maji) | Amafi **a**ranywá amáazi (samaki wanakunywa maji) |
| 8 u | Unene **u**nazidi | - | bu | Ubugwaari **bu**riyoongera (uzembe unazidi) | - |
| 9 | - | - | ka-tu | Akáana **ka**raaje (kitoto kinakuja) | Utwáana **tu**raaje (vitoto vinakuja) |
| 10 ku | Kuimba **ku**nafaa | - | ku/bi | Kuríriimba **ku**rakíza/ Kuríriimba birakíza (kuimba kunatajirisha) | - |
| 11 | - | - | ku-a | Ukuguru **ku**rageenda (mguu unatembea) | Amaguru **a**rageenda (miguu inatembea) |
| 12 pa | Pahali hapa **pa**napendeza | - | ha | Aha haantu **ha**rahúngwa (mahali hapa panalimwa) | - |
| 13 mu | Mjini humu **m**metulia | - | | Muu nzu **ha**rashyúushye (nyumbani humu mna joto) | - |
| 14 ku | Kwenu **ku**natisha | - | | Ku rukutá **ha**rasukuurwa (kwenye ukuta kunasafishwa) | - |
| | - | - | | I Muhaanga **haá**teeye imbere (Muhanga kumeendelea) | - |

Jedwali 2.11 linabainisha kwamba nomino za Kiswahili na Kinyarwanda huendelezwa kisintaksia kwa namna inayofanana sana. Viambishi vingi ambavyo huambikwa kwa vitenzi ni sawa. Pale ambapo mtazamo wa kimofolojia hushindwa kutofautisha viambishi vya ngeli tofauti vinavyofanana katika lugha hizi, utaratibu wa kisintaksia huweza kusaidia. Kwa mfano, ngeli za 9 na 10 zitatofautiana pale ambapo mzungumzaji atatumia *{i}* kama kipatanishi cha nomino katika 9 na *{zi}* katika 10 wakati ambapo ngeli za 1 na ya 3 zitapata tofauti zake katika vipatanishi *{a}* katika ngeli ya 1 na *{u}* katika ngeli ya 3.

Halikadhalika, vipatanishi vya nomino katika ngeli navyo hufanana sana. Kwa mfano, Kinyarwanda hutumia {a/ba} katika ngeli ya 1 {mu} na pili {ba} wakati ambapo Kiswahili hutumia {a/wa}. Hata hivyo, kuna tofauti ndogo kati ya mifumo hii miwili ambapo utambuzi wa majina yanayoingizwa katika kundi hili hustahili kufanywa kwa uangalifu. Katika Kinyarwanda, majina yanayoingizwa katika kundi hili la {a/ba} ni yale yenye kubainisha kiambishi ngeli {mu} katika umoja na {ba} katika wingi. Kiswahili, kwa upande wake, kitatumia upatanishi ulio sawa katika nomino kama *mtu/watu, ngombe/ng'ombe, kiziwi/viziwi* wakati ambapo Kinyarwanda kitachunguza ikiwa nomino husika zina viambishi ngeli {mu/ba} au la. Kwa hivyo, jina kama *inká* (ng'ombe), *inzu* (nyumba) yatachukua {i} kama kipatanishi katika umoja na {zi} katika wingi.

Aidha, ingawa ngeli ya 15 *{ku}*, Kiswahili na Kinyarwanda hutumia *{ku}* kama kipatanishi chake na kitenzi, Kinyarwanda huweza kutumia muundo mwingine wa kipekee *{bi}* badala ya {ku} kama ilivyo katika mfano 2.43.

(2.43) *Ku-ririimb-a ku-ra-kir-y-a (Kuririmba kurakiza)/Ku-ririimb-a bi-ra-kir-y-a (Kuririimba birakiza)*
*kiang-mz-kii-kiang-wktzo/ kiang-mz-kii-kiang-wktzo-mz-kii.*
*Kuimba kunatajirisha*

Kulingana na mfano 2.43, Kinyarwanda huruhusu vipatanishi viwili {ku} na {bi} kuweza kubadilishana nafasi katika muundo huo wa vitenzijina.

Isitoshe, uchunguzi wetu umetubainishia kwamba, matumizi ya ngeli za mahali nayo ni jambo muhimu la kuzingatia katika mfumo wa ngeli za Kinyarwanda na wa Kiswahili. Viambishi *{pa, mu ku}* ndivyo vinavyotumiwa katika Kiswahili ilihali Kinyarwanda hutumia maumbo ya *{pa, mu, ku, i}*. Vilevile, Kinyarwanda hutumia kipatanishi kimoja {ha} kwa ngeli hizo zote zinazorejelea mahali ilhali Kiswahili hutumia vipatanishi tofauti kwa kila ngeli; yaani *{pa, mu ku}*, kama tunavyopata kutokana na Jedwali 2.11.

Kuhusina na urejeshi wa nomino katika vitenzi, ni vyema kubainisha kwamba Kinyarwanda hakiruhusu urejeshi wa ngeli mwishoni mwa kitenzi.

(2.44)
(Kinyarwanda): *a) U-mw-áana u-Ø-kúund-a ku-nyo-á a-ma-tá a-ra-z-ye (Umwáana ukúunda kunywa amatá araaje)*
*ksb-kiang-mz-kip-wktzo-mz-ku-mz-kii-ksb-kiang-mz-kip-wktulp-mz-kii.*
(Kiswahili): *b) Mtoto apendaye kunywa maziwa anakuja*
*c) Mtoto anayependa kunywa maziwa anakuja*
*d) Mtoto ambaye anapenda kunywa maziwa anakuja*

Kutokana na mifano katika 2.44, ni wazi kwamba Kiswahili kina namna mbili za kurejelea nomino kiima katika kitenzi mbali na kutumia kiambishi awali cha nafsi. Urejeshi huu huweza kufanywa mwishoni mwa kitenzi kama ilivyo katika *apendaye* (2.44 b) au katikati mwa kitenzi kama ilivyo katika *anayependa* (2.44 c). Isitoshe, kiwakilishi *amba-* nacho huweza kutumiwa kuirejelea nomino kiima kama ilivyo katika *ambaye* (2.44 c). Kinyarwanda, kwa upande wake, hakitumii mfumo huo. Badala yake, Kinyarwanda hutumia wakati wa mazoea unaowakilishwa na kiambishi



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kapa *{Ø}* pamoja na toni ya juu kwenye silabi ya kwanza ya mzizi wa kitenzi ili kuashiria hali hiyo kama ilivyo katika mfano *2.44 a*. Urejeshi wa ngeli mwishoni utaruhusiwa tu ikiwa jina linalorejelewa ni la mahali kama tunavyopata katika 2.48.

*(2.48) a) A-ba-ntu a-aa-saang-ye-yó (Abaantu yasaánzeyó)*
*ksb-kiang-mz.-kip-wktim-mz-kii-kiw.mahali*
*Watu aliowakuta pale.*
*b) I-n-zu a-aa-iinjir-ye-mó (Inzu yiinjíyemó)*
*ksb-kiang-mz-kip-wkt uliotimilika-mz.-kii.-kiw.mahali*
*Nyumbani alimoingia*
*c) U-ru-kutá a-aa-kor-ye-hó (Urukuta yakozehó)*
*ksb-kiang-mz-kip-wkttim-mz-kii-kiw.mahali.*
*Kwenye ukuta alikogusa.*

Katika tungo hizi, maumbo ***{yó, mó, hó}*** ndiyo yanayorejelea mahali na yamewekwa mwishoni mwa vitenzi.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii, uchunguzi wa mofosintaksia ya ngeli katika Kiswahili na Kinyarwanda umedhihirisha kuwa lugha hizi huhusiana sana kimofolojia na kisintaksia. Taratibu za uanishaji wa ngeli zilizodhihirishwa katika lugha hizi mbili zimebainisha kuweko kwa mielekeo tofauti ya uainishaji wa ngeli. Uchunguzi wa upatanishi wa kisarufi na urejeshi wa ngeli katika lugha hizi umetudhihirishia kwamba matumizi bora ya ngeli ndiyo uti wa mgongo wa utunzi wa sentensi sahihi kiasi kwamba ni lazima mzungumzaji wa lugha amiliki mifumo hiyo kikamilifu ili aweze kujiepusha makosa ya kimofosintaksia katika matamshi na maandishi yake. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba kubainisha mofosintaksia ya ngeli katika lugha hizi mbili kulitusaidia kuujengea msingi imara uchunguzi wetu wa changamato za kimofosintaksia zinazowakumba wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunza Kiswahili katika shule za upili. Hivyo basi, sura ifuatayo itazungumzia makosa ya kimofosintaksia yanayofanywa na wanafunzi hawa.

# SURA YA TATU

# MAKOSA YA KIMOFOSINTAKSIA YA WANAFUNZI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili yalidhihirishwa kupitia majibu waliyoyatoa kwenye hojaji, utunzi wa insha na masimulizi yao. Kwa kuzingatia nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM), makosa yalibainishwa kwa kuzingatia kategoria tofauti za kimofosintaksia, yakaelezwa na hatimaye kuainishwa. Kwa hivyo, idadi ya wanafunzi waliofanya makosa ilikadiriwa kwa asilimia na kuwasilishwa katika majedwali ili kuonyesha kiwango cha makosa yaliyofanywa na wanafunzi kutoka madarasa yote mawili yaliyotafitiwa; yaani darasa la tano na la sita. Kila zoezi lililopewa wanafunzi lilichunguzwa kivyake ili kutuwezesha kutambua kipengele cha ufundishaji kilichowatatiza zaidi wanafunzi. Katika sehemu ya kwanza, makosa yaliyojitokeza katika tungo za kukamilisha yalibainishwa. Sehemu ya pili ilizungumzia yale yaliyotokana na uandishi wa insha nayo sehemu ya tatu ikadhihirisha makosa yaliyojitokeza katika zoezi la masimulizi ya wanafunzi.

## 3.1 Makosa ya wanafunzi kutokana na tungo za kukamilisha

Lengo kuu la zoezi hili la kukamilisha tungo mbalimbali kwa kutumia viambishi mbalimbali lilikuwa kuutathmini uwezo wa wanafunzi wa kupatanisha nomino na maneno mengine yanayoandamana nayo na kutawaliwa nayo katika upatanishi wa kisarufi. Kwa hivyo, matokeo yafuatayo yanathibitisha jinsi ambavyo wanafunzi walipatanisha nomino na vivumshi na nomino na vitenzi kwa kutumia viambishi

mwafaka. Ili kulikabili tatizo linalojitokeza katika mitazamo tofauti ya uainishaji wa ngeli, tumeamua kuzingatia mitazamo ya matumizi ya viambishi awali vya nomino (§2.3.1.2) na vya upatanishi vya wa kisarufi vya umoja na wingi ambavyo hurejelea nomino kiima katika kitenzi husika (§2.3.2.2).

Mbali na kuwa kazi hii ilidhamiria kuchunguza makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi, uamuzi wa kuzingatia mielekeo hii miwili ulitokana na hali kwamba kulikuwa na majina yasiyobainisha viambishi awali vyovyote wakati ambapo mengine hupata upatanishi sawa na makundi ya majina yenye viambishi awali tofauti. Kwa hivyo, ilitubidi kuendeleza mjadala wetu kwa kushirikisha mtazamo wa kimofolojia wa ngeli pamoja na mtazamo wa kisintaksia.

### 3.1.1 Upatanishi wa nomino na kivumishi

Kutokana na majibu tuliyotolewa na wanafunzi kwenye hojaji zao, upatanishi wa nomino na vivumishi mbalimbali ulidhihirisha matatizo tofauti ambayo yalipangwa na kubainishwa kwa misingi ya nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM). Kwa mujibu wa nadharia hii, makosa ya mwanafunzi hudhihirishwa kwanza ili kuelezwa na kuainishwa katika hatua ya pili (§1.7.1.2).

#### 3.1.1.1 Nomino na kivumishi cha sifa

Kulingana na Mbaabu (1995), matumizi ya vivumishi vya sifa huwatatiza watu kwa kuwa muundo kamili wa vivumishi hivyo hutegemea upatanishi wa nomino. Katika utafiti wetu, wanafunzi walitakiwa kukamilisha tungo kwa kutumia viambishi vya upatanishi wa nomino na kivumishi cha sifa. Hivyo basi, jedwali lifuatalo

linatuonyesha hali halisi ya matatizo yanayowakumba wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunza Kiswahili katika kipengele hiki cha kimofosintaksia.

**Jedwali 3.1: Upatanishi wa nomino na kivumishi cha sifa**

| Kivumishi | Kundi la ngeli | Majibu sahihi | Idadi ya wanafunzi waliofanya makosa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Darasa la 5 | % | Darasa la 6 | % | Jumla /60 | % |
| Sifa | li/ya | koti zuri | 27 | 90 | 26 | 86.6 | 53 | 88.3 |
| | u/zi | udevu mrefu | 16 | 53.3 | 16 | 53.3 | 32 | 53.3 |
| | i/zi | nyumba ndefu | 13 | 43.3 | 3 | 10 | 16 | 26.6 |
| | u/i | mwili safi | 26 | 86.6 | 16 | 53.3 | 42 | 70 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu 2014

Kulingana na majibu yaliyotolewa na wanafunzi, ni wazi kuwa upatanishi wa nomino na kivumishi cha sifa katika kundi la *{li/ya}* uliwatatiza wanafunzi wengi. Kundi hili linazingatia majina yenye viambishi awali *{ji/Ø-ma}* na yanapotumiwa katika umoja pamoja na vivumishi vya sifa hayaathiri muundo wa vivumishi hivi. Matokeo ya utafiti wetu yametubainishia kuwa wanafunzi wafikao asilimia 88.3 walishindwa kupatanisha vizuri jina *koti* na kivumishi *zuri*. Wengi wao walikuwa wakitoa majibu kama *koti nzuri* na *koti lizuri*. Nayo nomino *mwili* ya kundi la *{u/i}* iliwatatiza wanafunzi 70% walioshindwa kupatanisha jina hili kwa kivumishi *safi* wakati ambapo asilimia 53.3 walitatizika katika kupatanisha jina *udevu* na kivumishi *refu*.

Baadhi ya miundo potofu iliyotolewa na wanafunzi wengi ni kama *mwili msafi*, *mwili usafi* katika upatanishi wa kwanza na *udevu urefu* au *udevu ndefu* katika upatanishi huo wa pili. Muundo wa nomino za kundi la *{i/zi}* kama vile *nyumba* uliwatatiza wanafunzi asilimia 26.6 waliokosa jibu sahihi kwa kutumia kiambishi mwafaka kipatanishi cha jina hili na kivumishi *refu*. Aidha, uchunguzi wa matokeo yetu umetubainishia pia kwamba idadi kubwa ya wanafunzi wa darasa la sita ilionekana

kudumaa katika miundo mibovu. Wanafunzi 86.6% wa darasa hili walishindwa kupatanisha jina *koti* na kivumishi *zuri* wakati ambapo 66 % walishindwa kupatanisha nomino *mwili* na kivumishi *safi*.

#### 3.1.1.2 Nomino na kivumishi kimilikishi

Wanafunzi walipopewa sentensi tano ili kuzikamilisha kwa kutumia kiambishi kipatanishi cha nomino na kivumishi kimilikishi, walifanya makosa kwa viwango tofauti kama inavyoonekana katika Jedwali 3.2.

**Jedwali 3.2: Upatanishi wa nomino na kivumishi kimilikishi**

| Kivu mishi | Kundi la ngeli | Majibu sahihi | Idadi ya wanafunzi waliofanya makosa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Darasa la 5 | % | Darasa la 6 | % | Juml a /60 | % |
| Kumi liki | a/wa | Ng'ombe wangu | 17 | 56. 6 | 13 | 43. 3 | 30 | 50 |
| | | Mama yake | 8 | 26. 6 | 9 | 30 | 17 | 28. 3 |
| | ki/vi | Kisu changu | 6 | 20 | 3 | 10 | 9 | 15 |
| | u/i | Mwili wake | 13 | 43. 3 | 9 | 30 | 22 | 36. 6 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kulingana na matokeo katika Jedwali 3.2, maswali yaliyoulizwa kuhusu upatanishi wa nomino na kivumishi kimilikishi yanadhihirisha kuwa kundi la ngeli za *{a/wa}* ndilo liliwatatiza wanafunzi wengi. Asilimia 50 walishindwa kutumia kiambishi mwafaka kiwakilishi cha jina *ng'ombe* katika kimilikishi "-angu" kwani mengi ya majibu yao yaliangukia katika muundo wa *ng'ombe yangu*. Katika kundi hili, wanafunzi wapatao 28.3% ndio walitatizika kupatanisha vizuri jina *mama* na kimilikishi "-ake" wakati ambapo 36.6% walitatizika kupatanisha pia jina *mwili* na kimiliskishi "-ake" katika kundi la ngeli za *{u/i}*. Miongoni mwa majibu tuliyoyapata kutoka kwa wanafunzi waliofanya makosa haya ni kama *mama wake, mwili yake* na

*mwili mke*. Ngeli iliyoonekana kuwa rahisi katika kipengele hiki ni ile ya majina ya kundi la *{ki/vi}* kwani asilimia 15 peke yao ndio walioshindwa kutumia kiambishi sahihi kiwakilishi cha jina *kisu* katika kimilikishi "-angu".

### 3.1.1.3 Nomino na kivumishi cha idadi

Wanafunzi walipewa pia maswali mawili ili kuchunguza jinsi wanavyoweza kupatanisha nomino na kivumishi cha idadi. Kwa hivyo, majibu yao ndiyo tumebainisha katika jedwali 3.3:

**Jedwali 3.3: Upatanishi wa nomino na kivumishi cha idadi**

| **Kivumishi** | **Kundi la ngeli** | **Majibu sahihi** | **Idadi ya wanafunzi waliofanya makosa** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Darasa la 5** | **%** | **Darasa la 6** | **%** | **Jumla /60** | **%** |
| Idadi | a/wa | Mbuzi wanne | 19 | 63.3 | 11 | 36.6 | 30 | 50 |
| | | Kipofu mmoja | 20 | 66.6 | 17 | 56.6 | 37 | 61.6 |
| | li/ya | Jiwe moja | 12 | 40 | 15 | 50 | 37 | 61.6 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kulingana na matokeo katika jedwali hili, wanafunzi 61.6% walishindwa kutoa jibu sahihi kuhusu upatanishi wa majina *kipofu* na *jiwe* na kivumishi cha idadi *moja*. Jina *kipofu* linatanguliwa na kiambishi awali *{ki}* katika umoja lakini hukiuka kanuni ya kawaida ya kupatanisha kwa kutumia *{ki}* katika umoja *na* *{vi}* katika wingi. Badala ya kutumia viambishi hivi, jina hili huendelezwa kwa namna moja kama majina mengine ya binadamu katika kundi la *{a/wa}*. Kwa hivyo, wanafunzi wengi walitoa majibu yaliyoangukia katika muundo wa *kipofu kimoja* badala ya *kipofu mmoja*. Nayo majibu yaliyotolewa kuhusu upatanishi wa *jiwe* na *moja* yalikuwa *jiwe limoja*. Upatanishi wa jina *mbuzi* na kivumishi cha idadi *nne* ulionekana kuwatatiza pia wanafunzi kwa kiwango cha asilimia 50. Wengi wa wanafunzi waliofanya makosa haya walitumia muundo *mbuzi nne* au *zinne* badala ya *mbuzi wanne*.

#### 3.1.1.4 Nomino na kionyeshi

Maswali matano yalitumiwa ili kutathmini uwezo wa wanafunzi wa kupatanisha nomino na kivumishi kionyeshi. Jedwali lifuatalo linadhihirisha hali halisi ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi katika kategoria hii ya kimofosintaksia:

**Jedwali 3.4: Upatanishi wa nomino na kionyeshi**

| Kivumishi | Kundi la ngeli | Majibu sahihi | Idadi ya wanafunzi waliofanya makosa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Darasa la 5 | % | Darasa la 6 | % | Jumla /60 | % |
| Kionyeshi | u/i | mchele huu | 18 | 60 | 13 | 43.3 | 31 | 51.6 |
| | u/zi | ufa ule | 11 | 36.6 | 9 | 30 | 20 | 33.3 |
| | m | mahali humu | 23 | 76.6 | 22 | 73.3 | 45 | 75 |
| | ku | Msituni huku | 27 | 90 | 22 | 73.3 | 49 | 81.6 |
| | a/wa | muuguzi huyu | 4 | 13.3 | 3 | 10 | 7 | 11.6 |
| | ya | maji haya | 9 | 30 | 5 | 16.6 | 14 | 23.3 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kulingana na majibu ya wanafunzi, ni dhahiri kwamba ngeli za mahali ndizo ziliwatatiza wanafunzi kwa kiwango cha juu. Asilimia 75 walishindwa kutoa majibu sahihi kwa kutumia kiambishi kinachofaa kwa kutumia *humu*. Nao wanafunzi 81% walishindwa kupatanisha *msituni* na *huku*. Miongoni mwa majibu yaliyotolewa na wanafunzi ni kama *mahali huu, mahali huo, mahali haya* au *mahali huyu* badala ya *mahali humu*. Pengine, miundo kama *msituni huyu*, *msituni huu* na *msituni humu* ndiyo ilipendelewa na wanafunzi wengi badala ya *msituni huku*. Isitoshe, kupatanisha jina *mchele* na kivumsihi *hu-* nako kuliwatatiza wanafunzi wafikao 51.6% wakati ambapo jina *ufa* liliwatatiza wanafunzi 33.3% walioshindwa kutumia kiambishi mwafaka kwa kupatanisha jina hili na kionyeshi *-le*. Jina *muuguzi* la kundi la *{a/wa}* ndilo halikubainisha matatizo mengi pale tunapokuta wanafunzi 11.6% peke yao ambao walishindwa kutumia kiambishi sahihi cha jina hili katika kionyeshi *hu-*.

#### 3.1.1.5 Nomino na kiulizi

Viulizi navyo vilitumiwa ili kutathmini uwezo wa wanafunzi wa kutumia viambishi sahihi katika kupatanisha nomino na vivumishi hivi. Kwa hivyo, maswali mawili yalitumiwa na matokeo ya majibu yao ndiyo yamewasilishwa katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali 3.5: Upatanishi wa nomino na kiulizi**

| **Kivumishi** | **Kundi la ngeli** | **Majibu sahihi** | **Idadi ya wanafunzi waliofanya makosa** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Darasa la 5** | **%** | **Darasa la 6** | **%** | **Jumla /60** | **%** |
| Kiulizi | a/wa | mkulima yupi | 20 | 66.6 | 14 | 46.6 | 34 | 56.6 |
| | u | ukubwa upi | 19 | 63.3 | 5 | 16.6 | 24 | 40 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Matokeo ya utafiti wetu yalionyesha kuwa wanafunzi 56.6% ndio hawakuweza kupata jibu sahihi katika kupatanisha kiulizi "-pi" na nomino *mkulima* ya kundi la {a/wa}. Wengi wao walipendelea miundo kama *mkulima mpi, mkulima wapi* na *mukulima upi* badala ya *mkulima yupi*. Nayo ngeli ya *u* iliwatatiza wanafunzi kwa kiwango cha 40% ambapo wanafunzi wengi walitumia miundo ya *ukubwa wapi* na *ukubwa kupi*. Uchunguzi wa majibu yaliyotolewa na wanafunzi umetudhihirishia kuwa lugha kadirifu ya wanafunzi hawa hubadilika kutoka miundo mibovu kuelekea miundo iliyo sahihi pale tulipowapata wanafunzi 63.3% wa darasa la tano dhidi ya 16.6% wa darasa la sita walioshindwa kupatanisha vizuri jina hili *ukubwa* na kivumishi "-pi". Aidha, asilimia 66.6 wa darasa la tano dhidi ya 46.6 wa darasa la sita ndio walitatizika katika kupatanisha nomino *mkulima* na kivumishi "-pi".

#### 3.1.1.6 Nomino na vivumishi vya pekee

Habwe na Karanja (2004) wanasema kuwa vivumishi hivi vina matumizi mengine ya pekee zaidi ya kuwa vivumishi vya majina. Kila kimoja cha vivumishi hivi huwa na

sheria za pekee katika upatanisho wa kisarufi licha ya sheria za jumla za viambishi ngeli mbalimbali. Kwa hivyo, maswali matano yalitumiwa ili kuchunguza uwezo wa wanafunzi wa kutumia vivumishi vya pekee.

**Jedwali 3.6: Upatanishi wa nomino na kivumishi cha pekee**

| Kivumishi | Kundi la ngeli | Majibu sahihi | Idadi ya wanafunzi waliofanya makosa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Darasa la 5 | % | Darasa la 6 | % | Jumla /60 | % |
| Enyewe | I | chai yenyewe | 28 | 93.3 | 27 | 90 | 55 | 91.6 |
| | u/zi | ukuni wenyewe | 21 | 70 | 19 | 63.3 | 40 | 66.6 |
| | u/i | mkono wenyewe | 14 | 46.6 | 15 | 50 | 29 | 48.3 |
| | U | wali wote | 11 | 36.6 | 10 | 33.3 | 21 | 35 |
| | ku | mahali kwenyewe | 29 | 96.6 | 21 | 70 | 50 | 83.3 |
| o-ote | i/zi | Nguo yoyote | 18 | 60 | 14 | 46.6 | 32 | 53.3 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Matokeo ya majibu ya wanafunzi katika jedwali hili yanadhihirisha kuwa vivumishi vya pekee viliwatatiza sana wanafunzi. Kutokana na uchunguzi wetu, asilimia 91.6 walishindwa kutoa jibu sahihi pale walipotakiwa kupatanisha nomino *chai* na kivumishi "-enyewe". Majibu mengi tuliyoyapata kutoka kwa wanafunzi hawa yalikuwa *chai chenyewe*. Jina *mahali* ndilo lilichukua nafasi ya pili katika kuwatatiza wanafunzi kwani asilimia 83.3 walishindwa kutumia kiambishi mwafaka kwa kupatanisha jina hili na kivumishi "-enyewe". Majibu mengi kuhusu upatanishi wa jina hili na kivumishi hiki yalikuwa *mahali yenyewe, mahali mwenyewe* na *mahali wenyewe.* Vilevile, wanafunzi 66.6% nao walikosa jibu sahihi katika kupatanisha nomino *ukuni* na kivumishi hiki wakati ambapo majibu mengi waliyoyatoa yalikuwa *ukuni kwenyewe, ukuni mwenyewe* na *ukuni yenyewe*.

Nomino *nguo* iliwatatiza wanafunzi 53.3% walioshindwa kuipatanisha na kivumishi "o-ote". Wanafunzi waliokosa jibu sahihi katika muundo huu wa kivumishi "o-ote" walitoa majibu yaliyohitilafina sana kama vile *nguo yote, nguo zoote, nguo zote, nguo lolote, nguo ote,* na kadhalika. Katika kundi la *{u/i}*, wanafunzi 48.3% ndio waliotatizika kupatanisha nomino *mkono* na "-enyewe" wakati ambapo asilimia 35 walikanganywa na muundo wa *wali wote*. Mengi ya majibu yao yalikuwa *mkono mwenyewe* katika upatanishi wa kwanza na *wali yote, wali yoyote* au *wali zote* katika upatanishi huo wa pili. Isitoshe, uchunguzi wetu umethibitisha kwamba kipengele hiki cha kimofosintksia kiliwatatiza wanafunzi wengi wa madarasa yote yaliyotafitiwa. Idadi kubwa ya wanafunzi wa darasa la sita wamedumaa katika miundo mibovu iliyotumiwa pia na wanafunzi wa darasa la tano kama vile *ukuni kwenywe, mahali henyewe* na *chai chenyewe.*

### 3.1.1.7 Upatanishi wa nomino na kiwakilishi

Ili kuchunguza uwezo wa wanafunzi wa kupatanisha nomino na viwakilishi, maswali mawili yalitolewa kama tunavyopata katika Jedwali 3.7.

**Jedwali 3.7: Upatanishi wa nomino na kiwakilishi**

| **Kiwakilishi** | **Kundi la ngeli** | **Majibu sahihi** | **Idadi ya wanafunzi waliofanya makosa** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Darasala 5** | **%** | **Darasa la 6** | **%** | **Jumla /60** | **%** |
| ndiye | a/wa | huyu ndiye muuguzi | 17 | 56.6 | 17 | 56.6 | 34 | 56.6 |
| ambaye | li/ya | shamba ambalo | 22 | 73.3 | 15 | 50 | 37 | 61.6 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Matokeo katika Jedwali 3.7 yanadhihirisha kuwa kiwakilishi *amba* kiliwatatiza wanafunzi 61.6% walioshindwa kupatanisha jina *shamba* na kiwakilishi hicho. Miongoni mwa miundo iliyotolewa na wanafunzi waliofanya makosa ni pamoja na



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

*shamba ambao, shamba ambaye, shamba wamba,* na kadhalika. Hata hivyo, uchunguzi wetu ulitudhihirishia kwamba wanafunzi wengine wengi walikosa kuandika jibu lolote lile au wakarudia muundo wenyewe *shamba amba* bila kukamilisha kwa kutumia kiambishi kirejeshi *lo* kilichostahili kutumiwa.

Aidha, wanafunzi 56.6% walishindwa kutoa jibu sahihi kwa kurejelea jina *muuguzi* katika kitenzi kipungufu *ndi* ambacho hushirikiana na kiambishi wakilishi cha jina linalorejelewa ili kuunda kiwakilishi. Mengi ya majibu ya wanafunzi yalikuwa *huyu ndiyo, huyu ndi* au *huyu ndiwe, huyu ndimi, huyu ndiko,* na kadhalika. Idadi nyingine ya wanafunzi ilishindwa kuandika jibu lolote kuihusu miundo iliyotakikana ya *shamba ambalo* na *huyu ndiye*. Hivyo basi, uchunguzi wetu ulitubanishia kwamba kategoria hii ya kimofosintaksia ilikuwa mojawapo ya miundo yenye changamoto kubwa kwa wanafunzi wa madarasa yote mawili.

### 3.1.2 Nomino na kitenzi

Matumizi ya ngeli katika Kiswahili humtaka mzungumzaji amudu jinsi ambavyo viambishi mbalimbali huambikwa kwa vitenzi kulingana na nomino inayotumiwa kama kiima cha kitenzi hicho. Kwa hivyo, mtafiti alitathmini uwezo wa wanafunzi wa kupatanisha nomino mbalimbali na vitenzi kwa kutumia kiambishi mwafaka. Matokeo ya majibu yao ndiyo yamewasilishwa katika Jedwali 3.8.

**Jedwali 3.8: Upatanishi wa nomino na kitenzi**

| Kundi la ngeli | Majibu sahihi | Idadi ya wanafunzi waliofanya makosa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Darasa la 5 | % | Darasa la 6 | % | Jumla /60 | % |
| a/wa | Ng'ombe anakula majani | 11 | 36.6 | 6 | 20 | 17 | 28.3 |
| | Mbuzi wanne wameuzwa | 12 | 40 | 10 | 33.3 | 22 | 36.6 |
| | Mkulima amevuna | 14 | 46.6 | 8 | 26.6 | 22 | 33.3 |
| | Kipofu amefika | 20 | 66.6 | 17 | 56.6 | 37 | 61.6 |
| u/i | Mkono umevunjika | 6 | 20 | 6 | 20 | 12 | 20 |
| li/ya | Jiwe lilitupwa | 13 | 43.3 | 5 | 16.6 | 18 | 30 |
| | Shamba litalimwa | 15 | 50 | 9 | 30 | 24 | 40 |
| ki/vi | Kisu kimepotea | 10 | 33.3 | 6 | 20 | 15 | 25 |
| i/zi | Nyumba itajengwa | 7 | 23.3 | 1 | 3.3 | 8 | 13.3 |
| i | Chai imepikwa | 29 | 96.6 | 27 | 90 | 56 | 93.3 |
| u | Ukuta umebomolewa | 12 | 40 | 7 | 23.3 | 19 | 31.6 |
| u/zi | Udevu umekatwa | 11 | 36.7 | 2 | 6.7 | 13 | 21.7 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kulingana na matokeo ya majibu ya wanafunzi kama yanavyoonekana katika Jedwali 3.8, ni dhahiri kwamba ngeli ya {i} katika jina *chai* ndiyo iliwashinda wanafunzi wengi kwani asilimia 93.3 walishindwa kutoa kiambishi sahihi cha upatanishi wa jina hilo kwa kitenzi *mepikwa*. Majibu mengi ya wanafunzi hawa yalikuwa *chai kimepikwa* na *chai chimepikwa* badala ya *chai imepikwa*. Jina *kipofu* ndilo lilichukua nafasi ya pili kati ya majina mengine yaliyowakanganya wanafunzi kwani asilimia 61.6 walishindwa kutumia kiambishi nafsi {a} kinachostahili kutumiwa katika kitenzi *mefika*.

Wengi wa wanafunzi waliofanya makosa walikuwa wakitoa jibu kama *kipofu kimefika*. Nalo jina shamba liliwatatiza wanafunzi 40% walioshindwa kutumia kiambishi nafsi {li} kiwakilishi cha jina katika kitenzi *-talimwa* wakati ambapo asilimia 36.6 walitatizika katika kupatanisha KN, *mbuzi wanne* kwa kitenzi *meuzwa*. Miundo kama *shamba italimwa, shamba utalimwa* na *mbuzi zinne zimeuzwa* ndiyo ilijidhihirisha sana miongoni mwa majibu ya wanafunzi waliofanya makosa.

Pengine, majina *kisu, udevu, ngombe* na *mkono* hayakuwatatiza sana wanafunzi kwani walioshindwa kutumia viambishi mwafaka kwa vitenzi husika walikadiriwa kuwa kati ya asilimia 20 na 30 ya wanafunzi wote. Katika kundi la {a/wa}, upatanishi wa jina *mkulima* uliwakanganya wanafunzi wafikao 33.3% wakati ambapo ule wa jina jiwe uliwatatiza wanafunzi 30%. Kundi la hii ndilo lilionekana kuwa rahisi kwa wanafunzi kwani asilimia 13.3 ndio walishindwa kutumia kiambishi nafsi sahihi kwa kurejelea jina nyumba katika kitenzi *-tajengwa*. Isitoshe, uchunguzi wetu umetubainishia kwamba katika kipengele hiki cha kimofosintaksia, wanafunzi wa darasa la tano walifanya makosa mengi kuliko yale yaliyofanywa na wanafunzi wa darasa la sita.

### 3.2 Makosa yaliyotokana na uandishi wa insha

Kulingana na nadharia ya UM iliyoongoza utafiti huu, uandishi ni mojawapo ya hatua zinazoweza kuzingatiwa na mtafiti wakati anapochunguza makosa yanayofanywa wanafunzi wa L2. Kwa hivyo, zoezi la kuandika insha kuhusu "Ufugaji kijijini mwangu" lilipewa wanafunzi kwa lengo la kuchunguza umilisi wao wa Kiswahili katika njia ya maandishi. Kwa kuwa utafiti huu ulilenga kuchunguza changamoto za kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi waliotafitiwa, makosa yaliyojitokeza yalipangwa katika kategoria za mpangilio wa sentensi zilizoundwa na wanafunzi pamoja na upatanishi wa kisarufi.

#### 3.2.1 Mpangilio wa maneno katika sentensi

Massamba (2004) anaeleza kuwa mpangilio wa maneno ni utaratibu utumikao katika kuyaweka maneno ya lugha pamoja ili kuunda tungo kubwa zaidi. Ingawa sentensi za

Kiswahili hupangwa kwa njia iliyo sawa na zile za Kinyarwanda, matokeo ya utafiti wetu kuhusu mpangilio wa maneno katika sentensi za insha zilizotungwa na wanafunzi yalidhihirisha matatizo tofauti katika uundaji wa sentensi zao kama tunavyopata kutokana na mifano ifuatayo:

***(3.1) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*hiki kijijini kiko watu wengi wako ufugaji sababu kila mtu wa kijijini mwangu ana ng'ombe, hicho kitendo ni kimoja kiko vitendo vya kiongozi wetu anapanga kwamba kila mtu apate ng'ombe ili naye aweze kupata kila kitu anachotaka kujisaidie wakati muda mrefu* | Kijiji hiki kina wafugaji wengi. Kila mtu anafuga ng'ombe angalau mmoja kwani kiongozi wetu alianzisha sera ya kuwapatia ng'ombe raia wote wasiojiweza. Jambo hili liliwasaidia sana raia hawa kwa kukidhi maslahi yao ya kila siku na kuwawezesha kujitegemea wao wenyewe. |
| b)**Wakati wa kufanya ufugaji kutaka kuwa na mtajiri* | Mtu anapofuga anatajirika. |
| *(c)**ni lazima kutengeneza na kufuga kijijini kwangu ni muhimu mengi* | Ufugaji kijijini mwangu una umuhimu mkubwa |
| d)**ufugaji kijijini mwangu ni kuona muhimu kwa sababu kuona hivyo kutaka* | Ufugaji kijijini mwangu una umuhimu kwa kuwezesha wafugaji kutosheleza mahitaji yao |
| e)**watu wana wanyama wanafuga lakini kuna wengine hana mnyama mmoja* | Kuna watu wanaofuga wanyama wengi ilhali wengine hawana mnyama hata mmoja |
| f) *Kwa kijijini mwangu palikuwa na wafugaji wengi* | Kijijini mwangu mna wafugaji wengi |

***(3.2) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*ufugaji kijijini unasaidia watu kupata chakula kwa sababu wanyama wanafugwa wa mbolea ya kutumia katika ukulima wetu na tukapata mvuno mkubwa na hatuna mawazo ya vyakula, tunawala ng'ombe, kondoo, kukuu na mayai* | Ufugaji unawasaidia wanakijiji kupata chakula kwa sababu wanyama wanaofugwa huwaletea mbolea inayotumiwa katika shughuli zao za kilimo. Ufugaji huu unatuwezesha pia kula mayai, nyama ya ng'ombe, ya kondoo na ya kuku kiasi kwamba kijijini mwangu hamna matatizo ya chakula. |
| b)**ufugaji ni kazi kazuri ka kufuga wanyama mbalimbali tofauti vinaletea mapato au mavuno wafugaji lakini waweza kukutana na matatizo mbalimbali kwa ufugaji wako* | Ufugaji ni kazi nzuri ya kuwatunza wanyama mbalimbali. Ingawa ufugaji una faida nyingi, wafugaji hukumbana pia na matatizo ya aina tofauti |
| *c) *tunaona umuhimu wa ufugaji katika kijijini mwangu utusaidia kuona fedha* | Unaona kuwa ufugaji una umuhimu sana kijijini kwa kuwasaidia wanakijiji kupata pesa nyingi |
| d)**wakati wanyama zetu zinagonjwa hatuwezi kuona watu watusaidia kuona dawa ni ngumu* | Wwakati wanyama wetu wanapopata magonjwa hatuwezi kupata waganga wa kutusaidia |

Kutokana na mifano hii, makosa mengi yanayojitokeza katika sentensi za wanafunzi yanahusu namna wanafunzi wanavyoyapanga maneno na vipashio vyake katika sentensi. Kuna sentensi ambazo zimetumia mpangilio wa nomino na vitenzijina kama ilivyo katika (3.1 b) na (3.1 d) wakati ambapo tungo zingine zinadhihirisha kwa kiwango cha juu matumizi mabaya wa maneno *katika, kwa* na kipashio *ni*. Tungo kama (3.1 f), (3.2 c), (3.2 e) zimetolewa na wanafunzi wengi wa madarasa yote ; la

tano na la sita. Vilevile, tunakuta kwamba sentensi (3.1 c), (3.1 e), (3.1 f) na (3.2.b) na (3.2 e) zinaonyesha kwamba wanafunzi hawa wana upungufu mkubwa katika kuyapanga maneno na vipashio vyake katika sentensi. Sentensi kama hizo zilitungwa na wanafunzi ambao hawakuzingatia nafasi ya viunganishi, vivumishi na viwakilishi katika sentensi zao.

Isitoshe, sentensi (3.1 a, 3.2 a na 3.2 b) ni ndefu mno. Mbali na kupanga vibaya maneno yaliyomo katika tungo hizo, wanafunzi waliofanya makosa ya kuandika sentensi ndefu sana hawakuzingatia kamwe matumizi ya vituo kama vile alama ya mkato, nukta na mkato, nukta na alama zingine zinazohitajika katika uandishi sahihi. Urefu huu ndio hasa unamfanya msomaji asielewe ujumbe uliokusudiwa kutolewa na mwanafunzi. Vilevile, kosa hili lilionekana kuathiri upatanishi wa kisarufi kiasi kwamba msomaji anapata tabu katika kuelewa jina linalorejelewa katika vitenzi, vivumishi au viwakilishi vilivyotumiwa. Kulingana na nadharia ya Lugha Kadirifu, matokeo haya hutudhihirishia kiwango cha chini cha matumizi ya Kiswahili ya wanafunzi waliofanya makosa hayo. Kulingana na Selinker (1972), mchakato wa ujifunzaji lugha ya pili (L2) huanzia pale ambapo mwanafunzi huitumia miundo mibovu inayozidi kudilika kadiri anavyojifunza kuelekea muundo sahihi wa lugha lengwa (LL).

### 3.2.2 Makosa ya upatanishi wa kisarufi

Miongoni mwa makosa yaliyofanywa katika uandishi wa insha za wanafunzi, upatanishi wa kisarufi umejitokeza kama kipengele muhimu kinachotakiwa kujadiliwa katika sehemu hii. Wengi wao walishindwa kupatanisha nomino na

kivumishi, nomino na kiwakilishi au nomino na kitenzi kwa kutumia kiambishi mwafaka.

### 3.2.2.1 Nomino na kivumishi

Mjadala wetu katika sehemu hii utazingatia jinsi ambavyo wanafunzi walipatanisha nomino na aina mbalimbali za vivumishi zilizojitokeza katika uandishi wao wa insha.

#### 3.2.2.1.1 Nomino na kivumishi cha sifa

Katika kipengele hiki wanafunzi walitunga sentensi zenye makosa ya kupatanisha nomino kwa kivumishi cha sifa kama inavyodhihirika katika sentensi zifuatazo:

***(3.3) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a) *Ufugaji ni nzuri* | ufugaji ni mzuri |
| *b) *ufugaji ni umuhimu kwa kijijini na mjini na watu anayofuga* | ufugaji ni muhimu kwa kwa wafugaji wenyewe na kwa wanakijiji kwa jumla) |
| *c) *Wafugaji wengi ndiye watajiri kijijini mwangu* | wafugaji ndio matajiri tulio nao kijijini mwangu |
| *d) *Walikuwa watajiri sana....* | walikuwa matajiri sana.... |
| *e) *.....ili waone muvuno nzuri* | ili wapate mavuno mazuri |
| *f) *wafugaji wana maisha nzuri* | wafugaji wana maisha mazuri |

***(3.4) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a) *Wameona mvuno kubwa* | Wamepata mavuno makubwa |
| *b) *Ukimuona mtu msikini huo anaweza kukuambia kwamba anakuwa na maisha nzuri* | Ukimuona maskini huyo anaweza kukuambia kwamba ana maisha mazuri |
| *c) *ufugaji katika kijijini ni uzuri* | ufugaji kijijini ni mzuri |
| *d) *ufugaji ni kazi kazuri ka kufuga wanyama mbalimbali* | ufugaji ni kazi nzuri ya kutunza wanyama mbalimbali |
| *e) *Kijijini mwangu watu wanakuwa watajiri* | kijijini mwangu watu wengi ni matajiri |
| *f) *Mtu asiyefuga si mtajiri, mtu afugaye ni mtajiri kwa nyumbake* | mtu asiyefuga si tajiri wakati ambapo yule anayefuga ni tajiri |
| *g) *kufuga ni vizuri vinaweza kukuokoa katika shida* | ufugaji ni muhimu kwa sababu unaweza kukuokoa katika shida |

Kama inavyoonekana katika mifano hii, wanafunzi wa madarasa ya tano na sita walifanya makosa yanayofanana pale ambapo walishindwa kutumia viambishi sahihi katika kupatanisha nomino na kivumishi cha sifa. Vipashio kama *ufugaji ni nzuri* (3.3 a), *ufugaji ni uzuri* (3.4 c), *ufugaji ni umuhimu* (3.3 b), *mtu mtajiri* (3.4 f), *watu*

*watajiri* (3.3 c), *kazi kazuri* (3.4 d), *mtu msikini* (3.4 b), *maisha nzuri* (3.3 f) vilijitokeza katika tungo za wanafunzi wengi katika madarasa yote mawili.

### 3.2.2.1.2 Nomino na kivumishi cha -a unganifu

Nomino huweza kutumiwa pamoja na kivumishi hiki cha –a unganifu kuonyesha kuwa kitu au mtu ni mali ya kitu au ya mtu fulani. Katika hali hii, kivumishi cha -a unganifu hutumiwa kwa kuweka kiambishi kinachofaa kulingana na jina la kitu au mtu anayemilikiwa. Mifano inayofuata inadhihirisha kuwa wanafunzi walifanya makosa walipotumia kipengele hiki cha kisarufi.

***(3.5) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*kuona mahali ya kupata chakula* | kuona mahali pa kupata chakula |
| *b)*ng'ombe ya maskini.....* | Ng'ombe wa maskini...... |
| *c)*unaona mtoto anafanya kazi ka nguvu nyingi* | unaona mtoto anayefanya kazi ya nguvu nyingi |
| *d)*wanaweza kuona maji kwenye eneo ya kijiji hicho* | wanaweza kuona maji kwenye eneo la kijiji hicho |

***(3.6) Kidato cha sita***

| | |
|---|---|
| *a)*utakutana na tatizo za kukosa nyasi* | utakutana na matatizo ya kukosa nyasi |
| *b)*kwa sababu ya kuwa na shamba ya nyasi* | kwa sababu ya kuwa na shamba la nyasi |
| *c)*kwa kijijini wangu ninaona hakuna tatizo cha ufugaji* | ninaona kwamba hakuna tatizo la ufugaji kijijini mwangu |
| *d)*watatutafutia suluhisho ya tatizo hiyo* | watatutafutia suluhisho la tatizo hilo |

Mifano hii inadhihirisha kuwa baadhi ya wanafunzi wana shida katika matumizi yao ya kivumishi hiki cha -a unganifu. Mifano 3.5 inadhihirisha kuwa baadhi ya wanafunzi walitatizika katika kutambua kiambishi wakilishi cha jina husika na kutoa viapashio kama *eneo ya kijiji* (3.5 d), *tatizo za kukosa nyasi* (3.6 a), *shamba ya nyasi* (3.6 b), *tatizo cha ufugaji* (3.6 c), *suluhisho ya tatizo* (3.6 d), *ng'ombe ya maskini* (3.5 b), *mahali ya kupata chakula* (3.5 a), na kadhalika.

### 3.2.2.1.3 Nomino na kivumishi cha idadi

Kivumishi cha idadi nacho kilionekana kuwakanganya baadhi ya wanafunzi katika uandishi wao wa insha na mifano inayofuata inadhihirisha jambo hili:

***(3.7) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*ninaona ufugaji wa wanyama nyingi sana* | ninaona ufugaji wa wanyama wengi sana |
| *b)*katika kijijini tunafuga wanyama mengi* | kijijini tunafuga wanyama wengi |
| *c)*ng'ombe inaweza kutupa rutuba, ikatusaidia kuona mavuno nyingi* | ng'ombe anaweza kutupa rutuba inayotuwesha kupata mavuno makubwa |
| *d)*watu walikuwa na ng'ombe nyingi sana* | watu walikuwa na ng'ombe wengi sana |
| *e)*wanayama hao hawapatwa na ugonjwa nyingi* | wanyama hao hawapatwi na magonjwa mengi |

***(3.8) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*tuna wanyama nyingi, zote zilipata chakula* | tuna wanyama wengi, wote wanapata chakula |
| *b)*wana mifungo nyingi sana* | wana mifugo mingi |
| *c)*katika kijiji tulikuwa tuna shamba nyingi* | katika kijiji changu tuna mashamba mengi |
| *d)*tulikutana na tatizo nyingi* | tulikutana na matatizo mengi |
| *e)*mtu moja ana ng'ombe tano, mbuzi nane na kondoo nne kwa mifano* | kwa mfano mtu mmoja ana ng'ombe watano, mbuzi wanne na kondoo wanne |

Kulingana na mifano iliyoandikwa hapo juu, ni wazi kuwa makosa ya wanafunzi wa kidato cha tano hayatofautiani sana na yale yaliyofanywa na wanafunzi wa kidato cha sita. Baadhi ya wanafunzi wa madarasa haya walishindwa kupatanisha vizuri kivumishi hiki cha idadi kwa kutumia kiambishi kinachofaa kutokana na nomino iliyotumiwa kama jina tawala la kivumishi hicho. Miongoni mwa vipashio vinavyodhihirisha jambo hili ni pamoja na *mifugo nyingi* (3.8 b), *wanyama nyingi* (3.8 a), *ugonjwa nyingi* (3.7 e), *ng'ombe nyingi* (3.7 d), *wanyama mengi* (3.7 b), *tatizo nyingi* (3.7 d), *mavuno nyingi* (3.7 c), *mtu moja* (3.8 e), *ng'ombe tano* (3.8 e), *mbuzi nne* (3.8 e), *kondoo nne* (3.8 e), na kadhalika.

### 3.2.2.1.4 Nomino na kimilikishi

Uandishi wa insha za wanafunzi ulidhihirisha pia kuwa walifanya makosa ya kupatanisha nomino na vivumishi vimilikishi walivyovitumia katika tungo zao. Mifano ifuatayo inathibitisha jambo hilo.

***(3.9) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*kufuga kijijini si vigumu kwa sababu tuna nyasi yazo* | kufuga kijijini si vigumu kwa sababu tunaweza kupata nyasi zao |
| *b)*wafugaji wanafuga ng'ombe kwa kijijini mwangu waliona nyasi za kulisha ng'ombe zao* | kijijini mwangu wafugaji wa ng'ombe wanaweza kupata nyasi za kuwalisha ng'ombe wao |

***(3.10) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*ni lazima kufuga mifugo hapa nchini yetu* | ni lazima kuwa na mifugo nchini mwetu |

| | |
|---|---|
| *b) *kwa hitimisho yangu* | kwa kuhitimisha kwangu/katika hitimisho langu |
| *c) *tunaona rutuba nyingi za kujilimisha katika shamba zetu* | tunapata rutuba nyingi ya kutuwezesha kulima mashamba yetu |
| *d) *watu wakataja tatizo zao......* | watu wakataja matatizo yao |
| *e) *ufugaji kijijini wangu unatusaidia kuona muhimu* | ufugaji kijijini mwangu unatusaidia kupata faida |

Mifano hii inatuonyesha kuwa wanafunzi walitunga sentensi zenye makosa walipotakiwa kupatanisha nomino na kivumishi kimilikishi. Vipashio vya tungo zao vilivyokuwa na makosa ya aina hii ni kama *hitimisho yangu* (3.10 b), *nchini yetu* (3.10 a), *nyasi yazo* (3.9 a), *ng'ombe zao* (3.9 b), *kijijini wangu* (3.10 e), *tatizo zao* (3.10 d), *shamba zetu* (3.10 c).

#### 3.2.2.1.5 Nomino na kionyeshi

Mifano inayofuata inaonyesha makosa yaliyoyafanywa katika kategoria hii ya kupatanisha nomino kwa kivumishi kionyeshi:

***(3.11) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a) *ufugaji wa ng'ombe ni yule anapewa vitu vyingi sana* | ufugaji wa ng'ombe unahitaji vitu vingi sana |
| *b) *ufugaji katika hiki kijijini mwangu....* | ufugaji kijijini mwangu |
| *c) * hiyo mazao inatupatia fedha nyingi sana* | mazao hayo yanatuletea pesa nyingi sana |
| *d) *kuku huo wanapewa vyakula tofauti* | kuku huyo anapewa vyakula tofauti |
| *e) *tunaweza kupata maziwa kutoka kwa ng'ombe hii* | tunaweza kupata maziwa kutoka kwa ng'ombe huyu |
| *f) *wanyama hizi ni nguruwe, ng'ombe, sungura,* | wanyama hawa ni nguruwe, ng'ombe na sungura. |
| *g) *wafugaji wanafanya kazi hako katika zizi* | wafugaji wanafanya kazi hii zizini |

***(3.12) Kidato cha sita***

| | |
|---|---|
| *a) *mifugo hao* | mifugo hiyo |
| *b) *tukakosa mganga huo* | tutakosa mganga huyo |
| *c) *kazi hilo linawasaidia* | kazi hiyo inawasaidia |
| *d) *kijijini chetu watu wengi wanapenda kufuga* | kijijini mwetu mna watu wengi wanaopenda kufuga |
| *e) *hizi wanyama ziliwa na umuhimu kwetu, zilitusaidia afya yetu* | wanyama hawa wana umuhimu kwetu kwani hutusaidia kwa afya yetu |
| *f) *yule ufugaji ni vizuri* | ufugaji ule ni muhimu |

Mifano iliyobainishwa hapo juu inathibitisha kuwa baadhi ya wanafunzi walifanya makosa katika matumizi yao ya nomino na kivumishi kionyeshi. Mbali na kutumia kiambishi kisichofaa kwa vivumishi hivyo, mifano mingi inadhihirisha kuwa wanafunzi hawa walitumia muundo wa kivumishi+nomino kama ilivyo katika *hiyo*

*mazao* (3.11 c), *hizi wanyama* (3.12 e), *hiki kijijini* (3.11 b) na *yule ufugaji* (3.12 f). Makosa haya yamejitokeza miongoni mwa wanafunzi wengi katika madarasa yote mawili. Kuhusiana na matumizi mabaya ya viambishi vipatanishi vya nomino na kivumishi kionyeshi, vipashio kama *ufugaji wa ng'ombe ni yule* (3.11 a) *mifugo hao* (3.12 a), *ng'ombe hii* (3.11 e), *kazi hilo* (3.12 c), *kuku huo* (3.11 d), *mganga huo* (3.12 b), *mifugo hao* (3.12 a), *kazi hako* (3.11 g), *wanyama hizi* (3.11 f), vinaweza kutupa picha ya makosa yaliyofanywa katika kategoria hii ya mofosintaksia.

**3.2.2.1.6 Nomino na kivumishi cha pekee**

Kipengele hiki cha kimofosintaksia nacho kilidhihirisha makosa mbalimbali katika insha za wanafunzi. Baadhi ya makosa hayo yaliyofanywa ndiyo haya yafuatayo :

***(3.13) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*ufugaji ni jambo chenye mtu kuwa na wanyama* | ufugaji ni shughuli ya kuwatunza wanyama |
| *b)*ninataka kusema watu wengi wana matatizo ya vyakula visivyo na uzuri wote* | ninataka kusema kwamba watu wengi wana matatizo ya vyakula visivyo na uzuri wowote |
| *(c)*hizo wanyama zote zinatuletea mazao mbalimbali* | wanyama hao wote wanatuletea mazao mbalimbali. |

***(3.14) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*kuna ufugaji wengine wa aina yengine hapa kijijini* | kijijini humu mna ufugaji wa aina nyingine |
| *b)*tuna ufugaji wa ng'ombe kuliko ufugaji nyingine* | watu wengi wanapenda ufugaji wa ng'ombe kuliko ufugaji wa wanyama wengine |
| *c)*hii ufugaji ni vizuri kwa mtu yote* | ufugaji huu ni mzuri kwa mtu yeyote |
| *d)*tuna wanyama nyingi zote zilipata chakula hatuna tatizo* | tuna wanyama wengi lakini wote hupata chakula bila tatizo |
| *e)*bantu benye banatoka kijijini* | watu wanaotoka kijijini |

Mifano 3.13 na 3.14 inatuonyesha kuwa wanafunzi walikuwa na shida katika matumizi yao ya nomino na vivumishi vya pekee. Miongoni mwa makosa waliyoyafanya, kuchanganya kivumishi "-ote" na "o-ote" kumejidhihirisha sana katika insha za wanafunzi wengi. Vilevile, mifano kama *aina yengine* (3.14 a), *mtu yote* (3.14 c), *wanyama nyingi zote* (3.14 d), *hizo wanyama zote* (3.13 c), *jambo chenye mtu* (3.13 a), *visivyo na uzuri wote* (3.13.b), *kuliko ufugaji nyingine* (3.14 b),

*bantu benye* (3.14 e) huweza kuthibitisha hali hiyo ya kutomudu matumizi bora ya kivumishi hiki katika uandishi wao.

### 3.2.2.2 Upatanishi wa nomino na kitenzi

Katika kategoria hii, makosa ambayo yalifanywa na wanafunzi yanaweza kudhihirishwa kupitia mifano hii inayofuata:

***(3.15) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*mavuno atasaidia kupata zaidi nzuri katika maishani* | mavuno yatasaidia kupata faida maishani |
| *b)*ufugaji kwa kijijini ni vizuri kwa sababu binasaidia watu binatupatia mazao* | ufugaji kijijini ni mzuri kwa sababu unasaidia watu kupata mazao |
| *c)*kijijini mwangu kinasaidia mtu kwa kupata chakula* | kijijini mwangu mnasaidia watu kupata chakula |
| *d)*ufugaji kijijini mwangu ni kufuga wanyama yafuatayo* | wanyama wanaofugwa kijijini mwangu ni hawa wafuatao |
| *e)*maziwa ya ng'ombe ana umuhimu mwingi* | maziwa ya ng'ombe yana umuhimu sana kwetu |

***(3.16) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)* mapato anaweza kuongezeka* | mapato yanaweza kuongezeka |
| *b)*kufuga vinatusaidia kutuletea faida nyingi* | kufuga kunatuletea faida nyingi |
| *c)*mfugaji mnaweza kufuga wanyama akaanzia kwa wanyama watoto* | mfugaji anaweza kufuga wanyama kuanzia kwa wanyama wadogo |
| *d)*ukitaka kujenga zizi utapa miti karibu yao kwa sababu kijijini palikuwa na milima lina misitu* | ukitaka kujenga zizi utapata miti karibu kwa sababu kijijini mna milima yenye misitu |
| *e)*hizo wanyama zinakula majani mbalimbali* | wanyama hao wanakula majani ya aina mbalimbali |
| *f)*ng'ombe ina faida nyingi* | ng'ombe ana faida nyingi |

Mifano hii inadhihirisha kuwa kategoria hii ya kupatanisha nomino kwa kitenzi katika utunzi wa insha iliwatatiza sana wanafunzi. Wanafunzi walitunga sentensi nyingi zenye makosa mengi kwa kutumia kipatanishi kisichofaa kama vile *kufuga vinasaidia* (3.16 b), *kijijini palikuwa na milima lina misitu* (3.16 d), *hizo wanayama zinakula* (3.16 e), *mavuno atasaidia* (3.15 a), *mapato anaweza* (3.16 a), *kijijini mwangu kinasaidia* (3.15 c), *wanyama yafuatayo* (3.15 d), *ng'ombe ina faida* (3.16 f), *mfugaji mnaweza kufuga* (3.16 c), *maziwa ya g'ombe ana faida* (3.15 e) na kadhalika. Majina ya wanayama yanayohesabiwa katika kundi la ngeli la {a/wa} na yale ya kundi ya {*li/ya}* ndiyo yalitumiwa sana katika insha zao na yalionekana kuwatatiza wanafunzi wengi. Isitoshe, tunapata kwamba idadi nyingine ya wanafunzi haikuweza kutumia

kiambishi mwafaka kupatanisha vitenzijina na vitenzi na hata majina ya mahali na vitenzi. Viambishi kama *{ku}* cha kitenzijina na {pa, mu, ku} vya mahali viliwakanganya wanafunzi katika uandishi wao.

### 3.2.2.3 Urejeshi wa nomino katika kitenzi

Katika kategoria hii ya urejeshi wa ngeli za majina, wanafunzi walitunga sentensi zenye makosa ya aina tofauti kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo.

***(3.17) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)**unanunua vitu vingi unataka* | unanunua vitu unavyotaka |
| *b)**tuna viterineri anatusaidia kukingia wanyama wetu* | tuna daktari wa mifugo wanaotusaidia kwa kuwapa chanjo wanyama wetu |
| *c)**ili binadamu aone chochote anataka* | ili binadamu apate chochote anachotaka |
| *d)**ninaenda kuwajulisha jinsi ufugaji unaofanywa katika kijiji mwangu* | ninataka kuwajulisha jinsi ufugaji unavyofanywa kijijini mwangu |
| *e)**hakuna mtoto anaweza kugonjwa* | hakuna mtoto anayeweza kupatwa na ugonjwa |
| *f)**tunafuga pahali halipojengwa vizuri ; tunaoita zizi* | tunafugia mahali palipojengwa vizuri ; tunapaita zizi |
| *g)**mbuzi nazo zinaweza kutupa ngozi na mbolea* | mbuzi nao wanaweza kutupa ngozi na mbolea |

***(3.18) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)**mfugaji anaweza kukosa mahali anaweza kupanda majani ya ng'ombe* | mfugaji anaweza kukosa mahali pa kupanda nyasi za ng'ombe |
| *b)**hakuna mifugo inatosha* | hakuna mifugo inayotosha |
| *c)**unaweza kuona mtu akikinja mnyama alikuwa akifuga* | unaweza kuona mtu akichinja mnyama aliyekuwa akifuga |
| *d)**namna wanyama wanafugwa sasa* | namna wanyama wanavyofugwa sasa |
| *e)**tunachukua vitu vingi vinatusaidia* | tunachukua vitu vingi vinavyotusaidia |
| *f)**ufugaji ni neno linatoka kwa kitenzi inayosema kufuga* | ufugaji ni neno linalotoka kwa kitenzi kufuga |

Mifano hii inatudhihirishia kuwa wanafunzi walitunga sentensi zenye makosa mengi ya kategoria hii ya urejeshi wa ngeli. Mbali na kuwa walitumia kipatanishi kisichofaa kama tunavyopata katika *jinsi ufugaji unaofanywa* (3.17 d), *mbuzi nazo* (3.17 g), *kitenzi inayosema* (3.18 g), *tunafuga pahali halipojengwa...tunaoita zizi* (3.17 f), mifano mingine hapo juu imetubainishia kwamba urejeshi wa ngeli katika vitenzi ni changamoto kubwa kwa wanafunzi wengi. Tuliweza kuzipata tungo kama *viterineri atusaidia* (3.17 b), *hakuna mifugo inatosha* (3.18 b), *vitu vingi unataka* (3.17 a),

*mahali anaweza kupanda* (3.18 a) na *vitu vingi vinatusaidia* (3.18 e) ambamo mwanafunzi alidondoa viambishi virejeshi vya ngeli za majina.

### 3.2.3 Jumla ya wanafunzi waliofanya makosa katika uandishi wa insha

Kupitia uchunguzi wa insha za wanafunzi tumebainisha kuwa makosa mbalimbali yalijitokeza katika uandishi wao. Kwa hivyo, pamoja na kuzingatia kategoria za kimofosintaksia ambazo tumezijadili hapo juu, idadi ya wanafunzi waliofanya makosa katika zoezi hili yaweza kutuelezea mengi kuhusiana na umilisi wa wanafunzi hawa katika uandishi wao. Shahim (2011) anasema kuwa kiwango cha utokeaji wa makosa hubainishwa katika kuyachunguza na kuwa ndiyo hupitiwa katika nadharia ya UM ili kudhihirisha ujuzi wa mwanafunzi wa L2.

**Jedwali 3.9: Wanafunzi waliofanya makosa katika uandishi wa insha**

| **Kategoria** | | **Darasa** | | | | **Jumla /60** | **%** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Tano** | **%** | **Sita** | **%** | | |
| Mpangilio maneno katika tungo | | 30 | 100 | 26 | 86.6 | 56 | 93.3 |
| Upatanishi wa nomino na kivumishi | Nomino na sifa | 19 | 63.3 | 17 | 56.6 | 36 | 60 |
| | Nomino na kionyeshi | 11 | 36.6 | 15 | 50 | 26 | 43.3 |
| | Nomino na kiv. Cha pekee | 12 | 40 | 11 | 36.6 | 23 | 38.3 |
| | Nomino na kiv.kimilikishi | 12 | 40 | 17 | 56.6 | 29 | 48.3 |
| | Nomino na idadi | 10 | 33.3 | 7 | 23.3 | 17 | 28.3 |
| | Nomino na kiv. cha -a unganifu | 11 | 36.6 | 17 | 56.6 | 28 | 46.6 |
| Upatanishi wa nomino na kitenzi | | 21 | 70 | 22 | 73.3 | 43 | 71.6 |
| Urejeshi wa nomino katika kitenzi | | 24 | 80 | 23 | 76.6 | 47 | 78.3 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kutokana na matokeo ya uchunguzi wa insha zilizotungwa na wanafunzi, ni wazi kwamba kategoria ya mpangilio wa maneno katika tungo ndiyo imechukua nafasi ya kwanza miongoni mwa kategoria zilizowatatiza wanafunzi. Asilimia 93.3 ya madarasa yote ya tano na sita walipata shida katika kupanga maneno kwa njia sahihi ili kuwasilisha mawazo yao. Urejeshi wa nomino katikati mwa kitenzi au mwishoni nao uliwakanganya wanafunzi wengi. Asilimia 78.3 walishindwa kurejelea nomino

kwa kutumia kiambishi mwafaka katika kitenzi au kwa kutumia kiwakilishi *amba-*. Walioshindwa kupatanisha vizuri nomino na kitenzi ni wanafunzi 71.6% wakati ambapo 60% hawakuweza kutumia kiambishi sahihi kwenye kivumshi cha sifa. Nao upatanishi wa nomino na vivumishi vya kuonyesha, kumiliki na cha a- unganifu uliwatatiza wanafunzi 43.3% kwa kivumishi cha kwanza, 48.3% cha pili na 46.6% kwa kivumishi cha tatu.

Aidha, kiwango cha makosa katika upatanishi wa nomino na aina zingine za maneno katika uandishi wa insha kilikuwa cha juu au cha chini kulingana na jinsi ambavyo insha za wanafunzi zilivyokuwa ndefu au fupi. Vivumishi vya idadi na vya pekee havikutumiwa na wanafunzi wengi katika uandishi wao. Kwa hivyo, kiwango cha makosa kuhusu matumizi ya vivumishi hivi, hakikuwa cha juu sana pale tulipotapata wanafunzi 38.3% ambao walishindwa kutumia kivumishi cha pekee kwa namna inayofaa ilhali 28.3% walitatizika katika matumizi sahihi ya nomino na idadi katika tungo zao.

### 3.3 Makosa kutokana na masimulizi ya wanafunzi

Kama tunavyoelekezwa na nadharia za Uchanganuzi Makosa (UM) na Lugha Kadirifu (LK), mtafiti hukusanya data kupitia lugha ya masimulizi ya mwanafunzi na kuipanga vizuri ili aweze kuichanganua na kubainisha makosa. Kwa hivyo, wanafunzi walipewa mazoezi ya kusimuliana visa tofauti kulingana na tajiriba ya kila mmojawapo au jambo lolote alilolipenda kuwajulisha wanafunzi wenzake. Masimulizi hayo yalinukuliwa baadaye na mtafiti kwa utaratibu maalumu ili kuweza kubashiri makosa yaliyofanywa na wanafunzi wa kila darasa. Hivyo basi, makosa

yaliyojitokeza katika lugha kadirifu ya wanafunzi hawa ndiyo yalipangwa katika kategoria za kimofosintaksia zinazofuata.

### 3.3.1 Mpangilio wa maneno katika tungo

Matokeo ya utafiti wetu yalidhihirisha kwamba wanafunzi wengi walifanya makosa katika kategoria hii kwa kupanga maneno kwa namna isiyofaa katika tungo zao. Mengi ya makosa hayo yaliyojitokeza ni kama haya yanayofuata:

***(3.19) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*katika upande mwingine nimeenda mahali pengine nimeona mimea tofauti* | kwa upande mwingine nilienda mahali pengine palipokuwa na mimea tofauti |
| *b)*wakati uliopita nilipoenda kwa mji Kigali* | wakati nilipoenda mjini Kigali |
| *c)* nilienda mahali alipo mtungi huo* | nilienda mahali ambapo palikuwa mtungi huo |
| *d)* Muhanga ni mjini lakini si mjini mrefu kwa mjini wa Kigali* | Muhanga ni mji mdogo kuliko mji wa Kigali |
| *e)* hakuna mtu aliwaambia historia….* | kwa kuwa hakuna mtu aliyewazungumzia kuhusu historia….. |
| *f)* kwa jioni tunacheza* | jioni tulicheza |
| *g)* nyimbo ni za muhimu kwa maisha ya mtu* | nyimbo ni muhimu kwa maisha ya mtu |

***(3.20) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)* Yesu atakuja atasimama kwenye hewani* | Yesu atarudi na kusimama angani |
| *b)*ninataka msaada wa kusaidia mimi ukafundisha mimi msamiati* | ninahitaji msaada wako wa kunifundisha msamiati |
| *c)*baada ya hivyo nikafikiri kwa moyoni wangu hawa ni wajangili* | baada ya mambo hayo, nilifikiria moyoni mwangu kuwa hao walikuwa majangili |
| *d)* kwa barabara halikuwa ajili* | kulikuwa na ajali barabarani |
| *e)* ndugu yangu aliniona mimi akacheka* | ndugu yangu aliponiona alicheka |
| *f)* lakini nasi kama watu tumefanyiwa utafiti huo tumepata faida* | Vilevile, nasi kama watu tuliotafitiwa, tumefaidika kutokana na utafiti huu |
| *g)*katika nyumbani tuko watoto kumi na mbili* | nyumbani kwetu tuko watoto kumi na wawili |
| *h)* nikaenda kwenye mjini niliona watu wengi wanasema lugha mbalimbali* | nilipoenda mjini nilikutana na watu waliokuwa wakizungumza lugha mbalimbali |
| *i)*mama alikuwa yeye mmoja nilikuwa na mzazi mwenyewe kwani babangu naye alifariki dunia awali* | nina mzazi mmoja, mamangu, kwani babangu alifariki kitambo |

Mifano hiyo hapo juu inadhihirisha kwamba wanafunzi walifanya makosa mengi ya kutunga sentensi zenye mpangilio mzuri. Kuna wanafunzi waliochanganya maneno *katika, kwenye* na *kwa* (3.19 a, 3.19 b, 3.19 c, 3.19 e, 3.20 a, 3.20 c, 3.20 d, 3.20 g, 3.20 h) na kuyatumia vibaya katika tungo zao wakati ambapo wengine walishindwa kutumia ipasavyo kiambishi *"ni"* (3.19 d, 3.20 g, 3.20 h). Vilevile, matokeo yetu yamebainisha kwamba baadhi ya sentensi za wanafunzi zimeonyesha kwamba wana

matatizo katika kutumia baadhi ya aina za maneno kama vile *viunganishi, vihusishi na viwakilishi.* Miongoni mwa mifano inayoweza kutudhihirishia jambo hili ni kama *kwa jioni* (3.19 f), *katika nyumbani* (3.20 g), *kwenye mjini* (3.20 h) na *ninataka msaada wa kusaidia mimi* (3.20 b). Aidha, tungo kama *hakuna aliyewaambia historia* (3.20 d) nazo zilionekana kukosa vihusishi au viunganishi kama *kuhusu, kwa kuwa, na* na *kwa sababu.*

### 3.3.2 Makosa katika upatanishi wa kisarufi

Katika kipengele hiki cha kimofosintaksia, wanafunzi walifanya makosa tofauti katika kupatanisha nomino na kivumishi, nomino na kitenzi au kuirejelea nomino katika kitenzi.

#### 3.3.2.1 Nomino na vivumishi

Uchunguzi wetu kuhusu upatanishi wa nomino na kivumishi ulidhihirisha kwamba wanafunzi hawakuweza kutumia viambishi mwafaka katika masimulizi yao na kuwa makosa mengi yaliyofanywa katika uandishi wa insha yalirudiwa na wanafunzi wengi katika masimulizi yao. Mifano ifuatayo inaweza kutupa picha kamili ya makosa yaliyofanywa katika zoezi la masimulizi ya wanafunzi.

##### 3.3.2.1.1 Nomino na kivumishi cha sifa

Kulingana na matokeo ya utafiti huu, wanafunzi waliotatizika kwa kupatanisha nomino na kivumishi cha sifa walifanya makosa kama haya yanayojitokeza katika tungo hizi.

***(3.21) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *(a)*ufugaji katika kijijini ni uzuri* | ufugaji kijijini ni mzuri |
| *(b)*nikasema hapa ni hazuri* | nikasema kuwa pale palikuwa pazuri |
| *(c)*wanaweza kulima shamba ndogo sana* | wanaweza kulima shamba dogo sana |

| | |
|---|---|
| *(d)*nina lengo nzuri* | nina lengo zuri |
| *(e)*nimeona manyumba marefu* | niliona nyumba ndefu |
| *(g)*swali hiyo ni swali nzuri* | swali hilo ni swali zuri |

***(3.22) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *(a) *safari yangu ilikuwa vizuri kwa sababu mtu nilimtaka nilimuona* | safari yangu ilikuwa nzuri kwa sababu mtu niliyemtarajia nilimuona |
| *(b)*wanaweza kulima shamba ndogo sana* | wanaweza kulima shamba dogo sana |
| *(c)*tulikuwa na mwalimu mhodari sana* | tulikuwa na mwalimu hodari sana |
| *(d)*lugha ya Kiingereza na Kinyarwanda ni umuhimu lakini lugha ya Kiswahili ni lugha ya muhimu sana* | lugha za Kiingereza na Kinyarwanda ni muhimu kakini lugha ya Kiswahili ni muhimu zaidi |

Mifano hii inadhihirisha kwamba wanafunzi kutoka madarasa yote yaliyotafitiwa walifanya makosa kwa kupatanisha vibaya nomino na vivumishi vya sifa. Kwa hivyo, walitunga vipashio kama *shamba ndogo* (3.22 b), *swali nzuri* (3.21 h) na *lengo nzuri* (3.21 d) ambapo majina ya ngeli za {li/ya} yalichukuliwa kama ya ngeli za {i/zi}. Isitoshe, wanafunzi wengine hawakujali tofauti kati nomino na kivumishi ambapo walitumia nomino badala ya kivumishi kama ilivyo katika tungo *ufugaji ni uzuri* (3.21 b). Vilevile, wanafunzi walitumia viambishi visivyofaa katika vivumishi kama ilivyo katika vipashio *hapa ni hazuri* (3.21.b), *manyumba marefu* (3.21 e) na *mwalimu mhodari* (3.22 c).

### 3.3.2.1.2 Nomino na kivumishi cha a-unganifu

Ingawa makosa katika kategoria hii ya kimofosintaksia hayakuwa mengi, mifano inayofuata hutudhihirishia kwamba wale waliokitumia walikumbana na matatizo tofauti katika upatanishi wa nomino na kivumishi hiki.

***(3.23) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*nilipotembelea jijini wa Kigali* | nilipotembelea jijini Kigali |
| *b)*ninataka kuwaambia kitu cha muhimu* | ninataka kuwambia kitu muhimu |

***(3.24) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*katika mauaji wa kimbari utangazaji ulitumiwa sana* | wakati wa mauaji ya kimbari, utangazaji ulitumiwa sana |
| *b)*hiyo ni tatizo ya michezo* | hilo ni tatizo la michezo |

Mifano hii inatuonyesha kuwa wanafunzi waliofanya makosa kwa kupatanisha nomino na kivumishi cha -a unganifu walitumia kipatanishi kisicho sahihi au pengine wakatumia kivumishi hiki mahali pasipotarajiwa. Vipashio *kama mjini wa Kigali* (3.23 a), *kitu cha muhimu* (3.23 b), *mauaji wa kimbari* (3.24 a), *tatizo ya michezo* huweza kutupa picha kamili ya matatizo yaliyowakumba wanafunzi katika kategoria hii ya kimofosintaksia.

#### 3.3.2.1.3 Nomino na kivumishi cha idadi

Upatananishi wa nomino na kivumishi nao ulibainisha matatizo mbalimbali katika masimulizi ya wanafunzi kama tunavyopata katika mifano ifuatayo.

***(3.25) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*timu ya Rwanda inashinda magori moja kwa sufuri ya timu ya Uganda* | timu ya Rwanda ilishinda goli moja kwa sufuri ya timu ya Uganda. |
| *b)*nina sungura mbili* | nina sungura wawili |
| *c)*nilikutana na mzee moja* | nilikutana na mzee mmoja |

***(3.26) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*tulitangulia kwa msamiati chache* | tulianza na msamiati mchache |
| *b)*baada ya miaka tano nilienda shuleni* | baada ya miaka mitano nilienda shuleni |
| *c)*baba yangu ameoa wake wapili* | babangu alioa mke wa pili |
| *d)*tulijifunza tukapata msamiati nyingi* | ulijifunza na tulipata msamiati mwingi |

Uchunguzi wetu wa makosa yaliyofanywa na wanafunzi katika kategoria hii ya kimofosintaksia ulithibitisha kwamba vipatanishi visivyo sahihi vilitumiwa na wanafunzi kutoka madarasa yote mawili yaliyotafitiwa. Mifano hapo juu inatuonyesha kwamba wanafunzi hawa hawakuzingatia viambishi vinavyotakiwa kutumiwa kwa kupatanisha aina tofauti za nomino na vivumishi vya idadi iliyo dhahiri kama *magori moja* (3.25 a), *sungura mbili* (3.25 b), *mzee moja* (3.25 c), *miaka tano* (3.26 b), *wake wapili* (3.26 c), iau isiyo dhahiri kama ilivyo katika vipashio *msamiati chache* (3.26 a) na *msamiati nyingi* (3.26 d).

### 3.3.2.1.4 Nomino na kionyeshi

Katika upatanishi wa nomino na kionyeshi, mifano inayofuata ni baadhi ya tungo zenye makosa zilizotumiwa na wanafunzi:

| | |
|---|---|
| ***(3.27) Darasa la tano*** | |
| *a) *nilikosa hali ya kushuka huyu mti* | nilikosa namna ya kushuka mti huu |
| *b) *daktrari huo ni mzuri sana kwa sababu alinipa mimi dawa nzuri* | daktari huyo ni mzuri kwa sababu alinitibu vizuri |
| *c) *ukiona ile shimo* | ukiona shimo lile |
| *d) *huo msichana tunatoka mu tumbo moja* | msichana huyo ni dadangu |
| *e) *nikasomea hapa nchi Rwanda* | nikasomea nchini humu |
| ***(3.28) Darasa la sita*** | |
| *a) *hiyo ndiyo lengo yangu* | hilo ndilo lengo langu |
| *b) *nimefurahi kuchaguliwa kujidffunza darasani hapo* | nilifurahia kuchaguliwa kujifunza darasani humu |
| *c) *asanteni kwa muda huyu* mlionipa | Asanteni kwa kunipa muda huu |
| *d) *kwa kuzungumzia watu wanaosema lugha hilo* | kwa kuzungumzia watu wanaosema lugha hiyo |

Mifano hapo juu inadhihirisha kwamba wanafunzi walifanya makosa katika kupatanisha nomino na kionyeshi ambapo nomino za kundi la {u/i} na {a/wa} zilichanganywa kama tunavyoapata katika vipashio *huyu mti* (3.27 a), *huo msichana* (3.27 d), *muda huyu* (3.28 c), *daktari huo* (3.27 b). Vilevile, uchunguzi wa mifano iliyotolewa katika sehemu hii, unadhihirisha kwamba wanafunzi hawakuzingatia vizuri viambishi vinavyostahili katika upatanishi wa nomino za mahali na vionyeshi au ule wa nomino za kundi la {li/ya} na{ i/zi}. Vipashio *ili shimo* (3.27 c), *darasani hapo* (3.28 a), *lugha hilo* (3.28 d) na *hiyo ndiyo lengo (3.28.a)* huweza kuthibitisha jambo hilo.

### 3.3.2.1.5 Nomino na kivumishi kimilikishi

Katika kategoria hii ya kimofosintaksia, mifano inayofuata inaweza kutuonyesha matatizo yaliyowakumba baadhi ya wanafunzi katika masimulizi yao.

***(3.29) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*tunafanya kazi kake huo msichana tunapata zawadi* | tulifanya kazi ya msichana huyo na alitupa zawadi |
| *b)*baada ya hivyo nikafikiri kwa moyoni wangu hawa ni wajangili* | nilifikiria moyoni mwangu kuwa hao walikuwa majangili |

***(3.30) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*lengo yangu ni kusoma* | lengo langu ni kusoma |
| *b)*ninakwenda kuzuru shangazi wangu* | nilikwenda kumtembelea shangazi yangu) |
| *c)*mimi ninatoka nyumbani yangu* | nilitokana nyumbani mwangu |

Kama tunavyopata kutokana na mifano hii, upatanishi wa nomino na kimilikishi ulitatiza wanafunzi kwa kutozingatia viambishi mwafaka vilivyotakiwa kutumiwa kulingana na aina ya nomino iliyotumiwa. Hivyo basi, vipashio kama *kazi kake* (3.29 a), *moyoni wangu* (3.29 b), *lengo yangu* (3.30 a), *shangazi wangu* (3.30 b), *nyumbani yangu* (3.30 c) ni baadhi ya makosa ya kupatanisha nomino na kimilikishi yaliyofanywa na wanafunzi katika masimulizi yao.

### 3.3.2.1.6 Nomino na kivumishi cha pekee

Upatanishi wa nomino na kivumishi cha pekee nao ulibainisha makosa mbalimbali kama tunavyopata katika mifano hii inayofuata.

***(3.31) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*ninamsaidia kwa kazi yote anafanya* | ninamsaidia kwa kazi yoyote anayoifanya |
| *b)*wakati nimejifunza kiswahili, ninaweza kujua vitu vingine* | kujifunza Kiswahili kuliniwezesha kujua vitu vingi |
| *c)*alizunguluka kwa mjini wote akisema….* | alizunguka mjini kote akisema…. |

***(3.32) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*nchini yote panaonekana redio inayotangaza habari* | nchini kote kunapatikana redio zinazotangaza habari |
| *b)*dada zenu zote ni watu wenye mali sana* | dada zetu wote ni watu wenye mali sana |
| *c)*mimi nilienda kufuata basi ingine barabarani sinapata muda wa kurudi hapo* | nilienda kutafuta basi nyingine na sikupata muda wa kurudi hapo |
| *d)*ninataka vitambulisho vizuri nikakuja nikavitafuta mahali popote* | nilihitaji vitambulisho halali nikaja kuvitafuta mahali pote |
| *e)*ni lini watangazaji wote duniani popote watakuwa na uhuru* | ni lini watangazaji wote duniani kote watakuwa na uhuru |

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba makosa mbalimbali yalifanywa na wanafunzi katika kategoria ya kupatanisha nomino na kivumishi. Mengi ya makosa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

hayo yalihusu kuchanganya vivumishi kama vile *-ote* na *o-ote*, *ingi* na *ingine* kama ilivyo katika kazi yote anafanya (3.31 a), *nikavitafuta mahali popote* (3.32 d), *duniani popote* (3.32 e), *vitu vingine* (3.31 b). Makosa mengine mengi yalijitokeza katika kutumia viambishi visivyofaa kulingana na aina ya nomino au ngeli inayoelezwa katika vivumishi hivyo. Vipashio kama *mjini wote* (3.31 c), *nchini yote* (3.32 a), *basi ingine* (3.32 c) na *dada zenu zote* (3.32 b) huweza kutuelezea zaidi kuhusu makosa hayo ya wanafunzi.

### 3.3.2.2 Upatanishi wa nomino na kitenzi

Katika masimulizi ya wanafunzi, makosa ya kupatanisha nomino na kitenzi nayo yalijitokeza. Baadhi ya wanafunzi waliofanya makosa haya walishindwa kuchagua viambishi mwafaka kulingana na ngeli ya nomino-kiima cha kitenzi husika kama tunavyoona katika mifano inayofuata :

***(3.33) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*sungura ilisaidia kuona pesa yalisaidia kununua kalamu na vitu vingine* | sungura ilisaidia kupata pesa zilizoniwezesha kununua kalamu na vitu vingine |
| *b)*wakasema Kiswahili sikijapiga hatua ndefu* | wakasema kwamba Kiswahili hakijapiga hatua kubwa |
| *c)*shimo ile ilipita ndani ya mlima* | shimo lile lilipitia ndani ya mlima |
| *d)*ninasoma masomo anayopendeza* | ninasoma masomo yanayopendeza |
| *e)*hapa hana magari mengi* | hapa pana magari mengi |
| *f)*katika nchini Uganda wana mimea tofauti* | nchini Uganda mna mimea tofauti |
| *g)*sisi hajatumia nguvu nyingi* | sisi hatujatumia nguvu nyingi |
| *h)*serikali hajatia nguvu kwenye lugha hii* | serikali haijatia nguvu kwenye lugha hii |

***(3.34) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*niliona kwamba mchepuo huo huna faida* | niliona kwamba mchepuo huo hauna faida |
| *b)*tumeona watu kupiga hatua kupenda mchezo wa kandanda* | tumeona kwamba watu walipiga hatua kwa kupenda mchezo wa kandanda |
| *c)*katika miaka iliyopita nchini yetu palikuwa na redio chache* | miaka iliyopita nchini mwetu mlikuwa na redio chache |
| *d)*tukasema mambo anayotufurahisha* | tukasema mambo yanayotufurahisha |

Kulingana na mifano hii, ni wazi kuwa baadhi ya ngeli ziliwatatiza wanafunzi pale waliposhindwa kupatanisha vizuri nomino na kitenzi kwa kutumia kiambishi nafsi

kinachofaa. Tatizo kubwa miongoni mwa wanafunzi waliofanya makosa katika kategoria hii lilijitokeza pale walipotaka kutunga sentensi katika hali kanushi. Wengi wao walikuwa wakishindwa kuweka kiambishi cha ngeli au cha nafsi iliyostahili baada ya kikanushi « ha » na kutoa vipashio kama *serikali hajatia nguvu* (3.33 h), *sisi hajatumia nguvu* (3.33 g) au wakadondosha « a » ya kikanushi « ha » kama ilivyo katika mfano *mchepuo huo huna faida* (3.34 a). Vilevile, ngeli zinazorejelea wanyama na mahali nazo zilionekana kuwakanganya pale ambapo tungo kama *sungura ilisaidia* (3.33 a), *nchini yetu palikuwa na redio chache* (3.34 c), *hapa hana magari mengi* (3.33 e) na *shimo ile ilipita ndani* (3.33 c) zilionekana kuwa jambo la kawaidia kutokea miongoni mwao.

Pengine, wanafunzi waliofanya makosa haya walishindwa kutumia kipatanishi kinachofaa kwa kutozingatia ngeli iliyorejelewa katika kitenzi kama ilivyo katika mifano *sungura ilisaidia* (3.33 a), *kuona pesa yalisaidia* (3.33 a), *shimo ile ilipita ndani ya mlima* (3.33 c), *masomo anapendeza* (3.33 d), *mambo anayotufurahisha* 3.34 d).

### 3.3.2.3 Urejeshi wa nomino katika vitenzi

Makosa yaliyofanywa na wanafunzi kuhusu kategoria ya urejeshi wa ngeli katika vitenzi ni kama haya yafuatayo:

***(3.35) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*kitu kilinifurahisha* | kitu kilichonifurahisha |
| *b)*ninasema sherehe ya msichana tunatoka mu tumbo moja* | ninazungumzia sherehe ya msichana ambaye tulizaliwa pamoja. |
| *c)*mimi ninapenda jinsi Wanyarwanda wanatangaza habari* | mimi ninapenda jinsi Wanyarwanda wanavyotangaza habari |
| *d)*watu walitoka Tanzania walikuwa tatizo la kuona nguo* | watu waliotoka Tanzania walikuwa na tatizo la kupata nguo |
| *e)*palikuwa watu wawili hawajui majina yao* | palikuwa na watu wawili ambao hawakujua majina yao |

| | |
|---|---|
| *f)*hakuna mtu aliwaambia historia* | hakuna mtu aliyewazungumzia kuhusu historia |
| *g)*siku hiyo ilifuata tunaenda sokoni* | siku hiyo iliyofuata tulienda sokoni |
| *h)*ninataka kuonyesha jinsi ninapenda utangazaji* | tunataka kuonyesha jinsi tunavyopenda utangazaji |

***(3.36) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*ukiangalia nchini yetu unaweza kujua vitu vinaweza kusaidia* | ukiangalia nchi yetu, unaweza kujua vitu vinavyoweza kutusaidia/ambavyo vinaweza kutusaidia |
| *b)*kuna wantu wengi walipoteza maisha yao kwa kutokana na utangazaji* | kuna watu wengi waliopoteza maisha yao/ambao walipoteza maisha yao kutokana na utangazaji wa habari. |
| *c)*kintu cha tatu ninataka kusema* | kitu cha tatu ninachotaka kuzungumzia |
| *d)*kutoka nilikuwa mtoto hadi sasa* | tangu nilipokuwa mtoto hadi sasa |
| *e)*niliende kusoma masomo yanahusiana na sayansi* | nilienda kusoma masomo yanayohusiana na sayansi |
| *f)*neno linaonekana katika kitabu cha Matayo* | neno linaloonekana katika kitabu cha Matayo |

Kategoria hii ya urejeshi wa nomino katika vitenzi ilionekana kuwa na makosa mengi yaliyofanywa pia na wanafunzi wengi wa madarasa yote ya tano na sita. Wanafunzi hawa hawakuweza kutunga sentensi kamili zinazotumia viambishi sahihi katikati na mwishoni mwa kitenzi ili kuirejelea nomino husika pale palipohitajika. Mifano kama *kitu kilinifurahisha* (3.35 a), *msichana tunatoka mu tumbo moja* (3.35 b) na *watu walitoka Tanzania* (3.35 c) ni baadhi ya tungo zenye makosa hayo.

Isitoshe, uchunguzi wetu wa mifano iliyotolewa hapo juu, umebainisha kuwa wanafunzi wengi hawajamudu matumizi ya kiwakilishi *amba*. Sentensi kama *kuna wantu wengi walipoteza maisha yao* (3.36 b), *kutoka nilikuwa mtoto hadi sasa* (3.36 d), *neno linaonekana* (3.36 f) na *hakuna mtu aliwaambia historia* (3.35 f) zinaweza kutuonyesha jinsi wanafunzi hawa walivyotatizika katika masimulizi yao kuhusiana na matumizi ya urejeshi uliotakiwa kuzingatiwa katika tungo zao.

### 3.3.3 Jumla ya wanafunzi waliofanya makosa katika masimulizi

Kama tunavyoelekezwa na nadharia ya UM, ni vyema mtafiti abainishe kiwango cha makosa yanayofanywa na wanafunzi ili kuwezesha kudhihirisha yale yanahitaji uangalifu mkubwa katika ufundishaji wa L2 (Allwright, 1975). Kwa hivyo, uchunguzi wa masimulizi yaliyofanywa na wanafunzi katika utafiti huu ulionyesha kwamba kiwango cha utokeaji wa makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi huweza kudhihirishwa kwa namna ifuatayo katika Jedwali 3.10.

**Jedwali 3.10: Wanafunzi waliofanya makosa katika masimulizi**

| **Kategoria** | | **Darasa** | | | | **Jumla /60** | **%** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Tano** | **%** | **Sita** | **%** | | |
| Mpangilio maneno katika tungo | | 30 | 100 | 30 | 100 | 60 | 100 |
| Upatanishi wa nomino na kivumishi | Nomino na kionyeshi | 14 | 46.6 | 19 | 63.3 | 33 | 55 |
| | Nomino na sifa | 9 | 30 | 10 | 33.3 | 19 | 31.6 |
| | Nomino na kiv. cha pekee | 5 | 16.6 | 8 | 26.6 | 13 | 21.6 |
| | Nomino na kivumishi kmilikishi | 8 | 26.6 | 11 | 36.6 | 19 | 31.6 |
| | Nomino na idadi | 5 | 16.6 | 7 | 23.3 | 12 | 20 |
| | Nomino na –a unganifu | 9 | 30 | 7 | 23.3 | 16 | 26.6 |
| Upatanishi wa nomino na kitenzi | | 9 | 30 | 18 | 60 | 27 | 45 |
| Urejeshi wa nomino katika kitenzi | | 23 | 76.6 | 21 | 70 | 44 | 73.3 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Jedwali hili linatudhihirishia kwamba makosa mengi yalifanywa katika kategoria ya mpangilio wa maneno katika tungo ambapo wanafunzi 100% walishindwa kuyapanga maneno ipasavyo katika sentensi zao. Kategoria hii ilifuatwa na ile ya urejeshi wa nomino katika kitenzi kwani wanafunzi 73.3% walishindwa kutumia viambishi virejeshi vya nomino katika sentensi zao. Upatanishi wa nomino kwa kivumishi kionyeshi nao uliwatatiza wanafunzi 55% ilhali 31.6% yao walitumia viambishi visivyo sahihi kwa kivumishi cha sifa. Vilevile, uchunguzi wetu ulionyesha kwamba asilimia 45 ya wanafunzi walishindwa kutumia kiambishi nafsi kinachofaa kwa kupatanisha nomino-kiima na kitenzi.

Ijapokuwa makosa haya yanafanana na yale yaliyobainishwa katika uandishi wa insha za wanafunzi, uchunguzi wetu ulitudhihirishia kwamba makosa katika masimulizi ya wanafunzi yalikuwa mengi mno hasa katika kategoria ya mpangilio wa maneno katika tungo. Vilevile, uchunguzi wetu umetubainishia kuwa wanafunzi wa darasa la sita walifanya makosa mengi kuliko wanafunzi wa darasa la tano hasa kuhusu baadhi ya kategoria za kimofosintaksia. Jambo hili lilitokana na hali kwamba wanafunzi wa darasa la sita ndio walioweza kujieleza zaidi kuliko wanafunzi wa darasa la tano ambao mara nyingi walikuwa wakisitasita katika matamshi yao. Kwa mfano, katika kategoria ya nomino na kitenzi, wanafunzi hawa walipendelea muundo wa nafsi ya kwanza kuliko nafsi zingine na nyingi za tungo zao hazikupendelea kugusia vivumishi tofauti.

Ingawa mtafiti alichochea wanafunzi watafitiwa kusimulia visa mbalimbali na kuwapatia mifano inayoweza kuwavutia, wengi wao, hasa wa darasa la tano walipendelea mada zilizoelekea kwa shughuli zao likizoni, ujifunzaji wao na hali za familia zao. Halikadhalika, changamoto hii ilijitokeza zaidi miongo mwa wanafunzi wa shule zisizo na miundo msingi imara kuliko ilivyokuwa katika shule zenye miundo msingi iliyoimarishwa. Uchunguzi wetu ulitubainishia kwamba wanafunzi waliopata changamoto kuitambua mada mwafaka ya kuzungumzia, walikuwa na udhaifu mkubwa katika maongezi. Uamuzi huu ulitokana na kwamba wanafunzi hao walikuwa wakitafuta kuyarudia yale yaliyokuwa yamezungumziwa na wenzao, hali aliyomlazimisha mtafiti kurudia mara kwa mara maelekezo ya zoezi walilokuwa wakifanya. Pengine, ilimbidi kuwauliza maswali kadhaa kuhusiana na tajiriba yao ya

maisha ili kuwapatia mifano mingine ya mada ambazo wangeweza kuzizungumzia. Jambo hili lilitubainishia kwamba changamoto zilizowakumba wanafunzi hawa katika masimulizi yao zilikuwa nyingi ilhali darasa la tano ndio mwaka unaotangulia kikomo cha masomo yao ya shule za upili.

### 3.4 Aina za makosa yaliyofanywa na wanafunzi

Kama ilivyodhihirishwa hapo juu, wanafunzi walifanya makosa mbalimbali katika kategoria tofauti za kimofosintaksia. Kwa kuzingatia hatua za nadharia ya UM ambapo makosa hubainishwa na kupangwa kabla ya kuelezwa, tumedhihirisha kategoria za kimofosintaksia ambamo makosa yalijitokeza na kutoa ufafanuzi wa makosa hayo yaliyofanywa. Vilevile, tumeweza kutambua viwango vya utokeaji wa makosa ya wanafunzi watafitiwa pale tulipodhihirisha lugha kadirifu za wanafunzi wa madarsa ya tano na darasa la sita.

Baada ya kubainisha makosa yaliyofanywa na wanafunzi kwa kuzingatia kategoria mbalimbali za kimofosintaksia, ni muhimu kueleza na kufafanua makosa hayo kwa kuyaainisha kama tunavyopata kulingana na nadharia ya Uchanganuzi Makosa (UM). Jambo hili ndilo linatiliwa mkazo na Ellis (1994) anaposema kuwa kuyaeleza makosa kunasaidia kuchunguza chanzo chake na hatimaye kuyatathmini . Hivyo basi, uchunguzi wetu ulibainisha aina saba za makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunza Kiswahili.

#### 3.4.1 Uchopekaji wa vipashio katika tungo

Makosa ya uchopekaji yalijitokeza pale ambapo wanafunzi waliingiza kipashio kisichotakiwa katika sentensi zao. Kipashio hicho chaweza kuwa kiambishi au neno

linalowekwa pahali pasipotarajiwa. Miongoni mwa sentensi zilizodhihirisha aina hii ya makosa ni kama hizi zinazofuata:

***(3.37) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a) *ufugaji katika kijijini mwangu vilitufikisha sana kwa maendeleo* | kijijini mwangu, ufugaji ulitufikisha kwenye maendeleo |
| *b) *kitu cha muhimu anaweza kutaka* | kitu muhimu anachoweza kuhitaji |
| *c) *aliyeona mwenye kipofu aliyemungojea* | aliona kipofu aliyekuwa akimngoja |
| *d* shamba lile ambalo alilonunua ni langu* | shamba lile alilonunua ni langu |
| *e) *kwa kufika Muhangani* | kufika Muhanga |
| *f) *nilipenda kujenga nyumba katika majiwe* | nilipenda kujenga nyumba kwa mawe |

***(3.38) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a) *bantu benye banatoka kijijini* | watu wanaotoka kijijini |
| *b) *katika nyumbani tuko watoto kumi na mbili* | Nyumbani tuko watoto kumi na wawili |
| *c) *kitu cha jambo la pili* | kitu cha pili |
| *d) *nikapata basi nikaenda kwenye mjini* | nikapata basi nikaenda mjini |
| *e) *nilipotembelea jijini wa Kigali* | nilipoenda jijini Kigali |

Kulingana na mifano hii, tunatambua kuwa wanafunzi walifanya makosa kwa kuchopeka au kuongeza vipashio mbalimbali visivyotarajiwa katika tungo zao. Vipashio hivyo ni kama kiambishi *-ni* cha undani (3.37 a, 3.38 b, 3.38 d), vihusishi *katika, kwa* na *kwenye*, (3.37 a, 3.37 e, 3.37 f, 3.38 b, 3.38 d) vivumishi kama *–enye, -a unganifu* (3.37 b, 3.37 c, 3.38 a, 3.38 c, 3.38 e) na viwakilishi virejeshi kama *-ye-* na *amba-* (3.37 c, 3.37 d, 3.38 a). Vilevile, kuna nomino ambazo zimechopekwa katika sentensi ijapokuwa hazileti maana mpya katika tungo. Tungo kama *kitu cha jambo la pili* (3.38.c) badala ya *jambo la pili* au *kitu cha pili* yaweza kuthibitisha jambo hili.

### 3.4.2 Udondoshaji wa vipashio katika tungo

Aina hii ya makosa ilijitokeza pale ambapo mwanafunzi alidondosha kiambishi katika neno au neno likadondoshwa katika tungo nzima. Mifano inayofuata inaweza kutudhihirishia jambo hilo.

***(3.39) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a) *ninayo furaha kupata mzungumzo huu* | ninayo furaha ya kupata muda huu wa kuzungumza |
| *b) *mimi ninaenda kuwaambia ajali niliyokutana* | Mimi ninataka kuwasimulia kuhusu ajali |

| | |
|---|---|
| *mhula uliopita* | niliyoipata/niliyokutana nyayo/ambayo nilipata/ nilikutana nayo mhula uliopita |
| *c)*nilikutana na mtu alivunjika mguu* | nilikutana na mtu aliyevunjika/ambaye alivunjika mguu |
| *d)*hakuna mtu aliwaambia historia…..* | kwa kuwa hakuna mtu aliyewazungumzia/ambaye aliwazungumzia kuhusu historia….. |

***(3.40) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*kitu kilinifurahisha* | kitu kilichonifurahisha/Kitu ambacho kilinifurahisha |
| *b)*kitu cha tatu ninataka kusema* | kitu cha tatu ninachotaka kusema/Kitu cha tatu ambacho ninataka kusema |
| *c)*kuna watu wengi walipoteza maisha yao* | kuna watu wengi waliopoteza maisha yao/Kuna watu wengi ambao walipoteza maisha yao |
| *d)*tunajua hizi wanyama ziliwa na umuhimu kwetu, zilitusaidia afia yetu* | Wanyama hawa walikuwa na umuhimu kwetu kwani walitusaidia kutunza afya yetu |
| *e)*ninapa shauri watu hawataki kufuga* | Ningependa kutoa shauri kwa watu ambao hawataki kufuga |
| *f)*tunajua wanyama zinawa umuhimu* | tunajua kuwa wanyama wana umuhimu |

Matokeo haya yanatudhihirishia kwamba wanafunzi walitatizwa sana na matumizi ya kiwakilishi *amba-* au viambishi virejeshi na hata viambishi vya nyakati katika vitenzi vya tungo zao. Tungo kama (3.39 d), (3.39 c), (3.40 d), (3.40.e), (3.40 a), (3.40 b) na (3.40 e) zinaweza kutuonyesha picha kamili ya makosa ya aina hii.

Mbali na kudondosha vipashio hivi, wanafunzi walidondosha pia baadhi ya *vivumishi, viunganishi, viwakilishi, vihusishi* na aina zingine za maneno zinazoweza kuleta urari na uwiano wa mawazo katika tungo zao. Tungo kama (3.39 a), (3.39 d), (3.40 d) na (3.39 b) ni mifano mizuri ya aina hii ya makosa ya wanafunzi ambapo maneno kama *kuwa, kwamba, kwa sababu, na, kwa kuwa* na *kuhusu* yamedondoshwa. Aidha, tumetambua kuwa katika hali hii, mwanafunzi anafululiza maneno bila kujali umuhimu wa vipengele hivyo vya kimofosintaksia ambavyo huhitajika ili kuleta uwiano wa mawazo ya mzungumzaji.

### 3.4.3 Mchanganyiko wa viambishi na matumizi ya viambishi visivyofaa

Matokeo ya uchunguzi wa mazoezi yaliyofanywa yamedhihirisha kwamba wanafunzi walifanya makosa kwa kutumia viambishi visivyofaa hasa kwenye vivumishi, viwakilishi na vitenzi. Mifano 3.41 na 3.42 inathibitisha jambo hilo.

***(3.41) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*shamba alinunua ni yangu* | shamba alilonunua ni langu |
| *b)*mtu nilimtaka nilimuoana* | mtu niliyemtaka nilimuona |
| *c)*kusoma vina thamani kubwa* | kusona kuna thamani kubwa |
| *d)*ng'ombe inaweza kutuletea maziwa* | ng'ombe anaweza kutuletea maziwa |
| *e)*ninaenda kuwajulisha jinsi ufugaji unaofanywa katika kijiji mwangu* | ninataka kuwajulisha jinsi ufugaji unavyofanywa kijijini mwangu |
| *f)*shamba ambao utalimwa* | shamba ambalo litalimwa |

***(3.42) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*nguruwe ile ina jicho limoja, lingine hakuoni* | nguruwe yule ana jicho moja kwani jingine halioni |
| *b)*kazi hilo linawasaidia* | kazi hiyo inawasaidia |
| *c)*kufuga vinaweza kukuokoa katika shida* | kufuga kunaweza kukuokoa katika shida |
| *d)*hapa kijijini chetu tunakosa waganga* | kijijini humu mnakosa waganga |
| *e)*unaona mtu anafanya kazi ka nguvu* | unaona mtu anayefanya kazi ya nguvu |

Kulingana na mifano hii, ni wazi kwamba wanafunzi walifanya makosa ya kuchanganya viambishi vilivyostahili kuwekwa kwa vivumishi, viwakilishi na vitenzi. Mifano ya tungo za aina hii ya makosa ni pamoja na *nguruwe ile* (3.42 a), *jicho limoja* (3.42 a), *hapa kijijini* (3.42 d), *shamba yangu* (3.41 a), *kufuga vinaweza* (3.42 c), *jicho hakuoni* (3.42 a) na *kusoma vina thamani* (3.14 c). Isitoshe, tuliweza kutambua kwamba baadhi ya matatizo yaliyojitokeza katika kategoria ya kimofosintaksia ya urejeshi wa nomino katika vitenzi yaliuhusu pia mchanganyiko wa viambishi vilivyotumiwa pale ambapo wanafunzi walitoa tungo kama *jinsi ufugaji unaofanywa* (3.41 e), *mtu nilimtaka* (3.41 b), na kadhalika.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

### 3.4.4 Mchanganyiko wa aina za maneno

Katika aina hii ya makosa, tumetambua kuwa wanafunzi walichanganya maneno kwa kutumia kategoria isiyofaa kulingana na nafasi ambapo neno linatokea katika tungo. Mifano inayofuata inatupa picha kamili ya makosa ya aina hii.

***(3.43) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*shamba anayenunua ni ya mimi* | shamba alilonunua ni langu |
| *b)*ufugaji ni umuhimu kwa kijijini na mjini na watu anaofuga* | ufugaji ni muhimu kwa wafugaji wenyewe na hata kwa wakazi wote wa vijijini na mijini |
| *c)*ninamsaidia kwa kazi yote anafanya* | nilimsaidia kwa kazi yoyote aliyoifanya |
| *d)* nilifaulu nzuri* | nilifaulu vizuri |
| *e)*Watu wowote waliko kijijini ni wafugaji* | watu wote wanaoishi kijijini |

***(3.44) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*ufugaji ni umuhimu kwa watu wanafanya kazi hiyo* | ufugaji ni muhimu |
| *b)*kwa sababu ni vitu vya rahisi* | kwa sababu ni vitu rahisi |
| *c)*yule ufugaji ni vizuri* | ufugaji ule ni mzuri |

Mifano hii inathibitisha kwamba wanafunzi walifanya makosa kwa kuchanganya aina za maneno waliyoyatumia katika tungo zao. Baadhi yao walichanganya vivumishi na vielezi kama ilivyo katika mifano (3.44 c), (343 d), nomino na vivumsihi kama tunavyopata katika vipashio *vitu vya rahisi* (3.44 b) na *ufugaji ni umuhimu* (3.43 b), vivumishi na viwakilishi kama ilivyo katika tungo (3.43 a). Vilevile, uchunguzi wetu umedhihirisha kwamba baadhi ya aina za vivumishi kama *-ote* na *o-ote* zilichanganywa pale tulipoona kuwa mwanafunzi aliunda vipashio *kazi yote anafanya* (3.43 c) badala ya *kazi yoyote anayoifanya*, *watu wowote waliko kijijini* (3.43 e) badala ya *watu wote wanaoishi kijijini*.

### 3.4.5 Uradidi wa vipashio pasipotarajiwa

Uradidi ni hali ya kuyarudia maneno au vipashio fulani katika tungo. Uchunguzi wa makosa yaliyofanywa na wanafunzi ulidhihirisha  kuwa walirudiarudia baadhi ya

maneno au vipashio vya maneno katika tungo zao kama tunavyopata kutokana na mifano ifuatayo :

***(3.45) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*ufugaji ni kazi kazuri ka kufuga wanyama mbalimbali* | ufugaji ni kazi nzuri ya kutunza wanyama mbalimbali |
| *b)*tumefika mjini Kigali tumeona vitu vingi tofauti katika mjini* | tulipofika mjini Kigali tuliona vitu vingi |

***(3.46) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*ninataka msaada wa kusaidia mimi ukafundisha mimi msamiati* | ninahitaji msaada wa kunifundisha msamiati |
| *b)*ndugu yangu aliniona mimi akacheka* | ndugu yangu aliponiona alicheka |
| *c)*Muhanga ni mjini lakini si mjini mrefu kwa mjini wa Kigali* | mji wa Muhanga ni mdogo kuliko ule wa Kigali |
| *d)*swali hiyo ni swali nzuri* | swali hilo ni zuri |

Mifano 3.45 na 3.46 inadhihirisha kwamba wanafunzi walifanya makosa kwa kurudiarudia baadhi ya vipashio vya tungo zao. Uchunguzi wetu ulituthibitishia kwamba uradidi huo wa vipashio vya tungo ulikuwa kikwazo kikubwa katika kuziunda sentensi zenye mpangilio sahihi. Tungo kama *ninataka msaada wa kusaidia mimi* (3.46 a), *aliniona mimi* (3.46 b), *tulifika mjini Kigali..tumeona... mjini* (3.45 b) na *ni mjini lakini si mjini mrefu kwa mjini* (3.46 c) zinaweza kutupa picha kamili ya uwezo mdogo wa kujieleza kwa njia bora kwa wanafunzi waliofanya makosa haya ya uradidi wa baadhi ya vipashio vya tungo zao.

### 3.4.6 Uhamishaji wa vipashio na mpangilio mbaya wa maneno katika tungo

Uhamishaji wa vipashio katika tungo nao ni mojawapo ya aina za makosa yaliyofanywa na wanafunzi. Katika aina hii ya makosa, wanafunzi waliweza kuliweka neno fulani mwishoni mwa tungo badala ya kuliweka mwanzoni au pengine wakaweka kiambishi katika nafasi isiyofaa kama tunavyopata katika mifano ifuatayo :

***(3.47) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)*hapa ndiyo nilionapo ng'ombe wawili wanene* | hapa ndipo niliona ng'ombe wawili wanono |
| **(b) hiki kijijini kiko watu wengi wako wafugaji* | kijijini humu mna watu wengi ambao ni wafugaji |
| *c)*hiyo mazao inatupatia pesa nyingi sana* | mazao hayo yanatuletea pesa nyingi sana |
| *d)*ababu kuona hivyo kutaka* | ufugaji kijijini mwangu ni muhimu kwani humsaidia mtu kupata vitu anavyotaka |
| *e)*wakati wa kufanya ufugaji kutaka kuwa na mtajiri* | wakati mtu anapofuga lengo lake ni kuwa tajiri |

***(3.48) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*mtu moja ana ng'ombe tano, mbuzi nane na kondoo nne kwa mifano* | kwa mfano, mtu mmoja anaweza kuwa na ng'ombe watano, mbuzi wanne na kondoo wanne |
| *b)*hizo wanyama ni ng'ombe, mbuzi, nguruwe* | wanyama hao ni ng'ombe, mbuzi na nguruwe |
| *c)*Moja siku nilitembea mji kuzuru ndugu yangu* | siku moja nilienda mjini kumtembelea ndugu yangu |

Kulingana na mifano 3.47 na 3.48 hapo juu, ni dhahiri kwamba vipashio mbalimbali vya tungo vilihamishwa na wanafunzi katika tungo zao kwa kuviweka katika nafasi zisizofaa. Miongoni mwa vipashio vilivyowatatiza ni pamoja na vivumishi ambapo wanafunzi walitumia muundo wa *kivumishi +nomino* badala ya *nomino +kivumishi*. Mifano kama *moja siku* (3.48 c), *hizo wanyama* (3.48 b) na *hiyo mazao* (3.47 c) huweza kutupa maelezo zaidi kuhusu kosa hili la kimofosintaksia. Vilevile, tunapata kwamba kuna viambishi ambavyo vilihamishwa na kuwekwa kwenye nafasi zisizostahili kama *nilionapo* (3.47 a) badala ya *nilipoona*. Tungo zingine zilitolewa zikiwa na mfuatano wa vitenzi katika nia isiyotajwa. Katika hali hii, mwanafunzi alifulululiza maneno bila kujali kanuni za kisarufi za kupatanisha nomino na kitenzi au akatumia njeo isiyostahili ili aweze kujieleza ipasavyo. Sentensi kama **ufugaji kijijini mwangu ni kuona muhimu kwa sababu kuona hivyo kutaka* (3.47 d) au *wakati wa kufanya ufugaji kutaka kuwa na mtajiri* (3.47 e) ni mifano mizuri ya aina hii ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi hawa.

### 3.4.7 Uundaji wa sentensi ndefu

Uundaji wa sentensi ndefu umejitokeza kama changamoto kubwa kwa wanafunzi waliotafitiwa. Kutokana na matokeo ya uchunguzi wetu, tulipata kwamba wanafunzi wote wa madarasa ya tano na la sita walikuwa na shida kubwa ya kutunga sentensi nyepesi. Sentensi nyingi zilikuwa ndefu sana kiasi kwamba msomaji hupata tabu kuzielewa kama tunavyoona katika mifano ifuatayo:

***(3.49) Darasa la tano***

| | |
|---|---|
| *a)* mimi ninatawambia kuhusu ufugaji kijijini mwangu ni vizuri sana kwa sababu niliona kufuga wanyama yote watu walifuga hao wanyama hatakuwa na matatizo walikutana* | Ningependa kuwaambia kwamba shughuli ya ufugaji kijijini mwangu imeimarishwa sana. Jambo hili linathibitishwa na hali nzuri ya mifugo na maisha mazuri ya wafugaji |
| *b)*kwa hivyo, mbona kufuga hawo wanyama walikuwa watajiri kwa sababu mtu anaefuga anaweza kupata mfuno unaotoka kwa ufugaji wenu akaununua akauona pesa za kumsaidia kufanya vintu anataka kwa hivyo mbona ufugaji kijijini mwangu hakuna tatizo mbona ni vizuri sana* | Kwa hivyo, wafugaji ndio matajiri sana. Kwa kawaida, mtu anayefuga anaweza kupata faida nyingi. Wakati anapokosa pesa, anaweza kuuza baadhi ya mifugo yake na kufanya jambo lolote analotaka. Hivyo basi, ufugaji kijijini mwangu ni shughuli muhimu sana. |

***(3.50) Darasa la sita***

| | |
|---|---|
| *a)*ufugaji kijijini unasaidia watu kupata chakula kwa sababu wanyama wanafugwa wa mbolea ya kutumia katika ukulima wetu na tukapata mvuno mkubwa na hatuna mawazo ya vyakula, tunawala ng'ombe, kondoo, kukuu na mayai* | Ufugaji unawasaidia wanakijiji kupata chakula kwa sababu wanyama wanaofugwa huwaletea mbolea inayotumiwa katika shughuli zao za kilimo. Ufugaji huu unatuwezesha pia kula mayai, nyama ya ng'ombe, ya kondoo na ya kuku kiasi kwamba kijijini mwangu hamna matatizo ya chakula. |
| *b)*kuna tatizo la kukosa mganga wa wanyama kama ng'ombe hao wanapatwa na magonjwa tofauti lakini tukakosa mganaga huo wa kuwapatia dawa* | kuna tatizo la kupata la kukosa daktari wa mifugo. Ikiwa ng'ombe wanashikwa na ugonjwa fulani wafugaji hawapati madaktari hawa kwa urahisi. |

Kutokana na matokeo haya, ni dhahiri kwamba wanafunzi walifanya makosa ya aina tofauti katika sentensi moja. Mbali na kuchanganya viambishi (3.49 a, 3.49 b, 3.50 b), kupanga vibaya maneno na kutumia aina za maneno katika nafasi zisizostahili (3.49 a, 3.49 b, 3.50 a, 3.50 b), sentensi zao ni ndefu sana. Urefu huu ndio unamfanya mwanafunzi akose kurejelea nomino kwa kutumia kiambishi mwafaka. Katika hali hii mwanafunzi hajali kuwa maneno yaliyomo katika lugha hufanya kazi za aina tofauti

katika tungo zao na kuwa hutekeleza majukumu mbalimbali kama wasemavyo Obuchi na Mukhwana (2010).

Hivyo basi, nyingi za sentensi za wanafunzi zilibainisha mfululizo wa maneno unaomfanya msomaji akose ujumbe uliokusudiwa. Tunapochunguza mfano 3.49 a, tunapata kuwa msomaji hawezi kuelewa kwa urahisi nomino zinazorejelewa katika vipashio vya sentensi: *ni vizuri*, *yote*, *hatakuwa na matatizo,* na kadhalika. Vilevile, mbali na kuwa mwanafunzi hajali uafikishaji katika tungo zake, vipashio katika (3.49 b) kama *mbona kufuga hawo wanyama walikuwa watajiri, mfuno unaotoka kwa ufugaji wenu akaununua akauona pesa za kumsaidia* navyo vinabainisha matatizo ya kumfanya msomaji asitambue kwa urahisi jambo linalozungumziwa na mwanafunzi. Katika sentensi (3.50 a), kivumishi cha a-unganifu *wa,* kimilikishi *wetu* na kitenzi *hatuna,* humwacha msomaji katika hali ya kujiuliza jambo ambalo analizungumzia mwanafunzi. Nayo sentensi (3.50 b) inabainisha kwamba mwanafunzi alirudiarudia kipashio *kukosa mganga* ambacho huifanya sentensi yake ikose mantiki na uwiano wa mawazo anayoyazungumzia.

### 3.5 Hitimisho

Katika sura hii, makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi yamedhihirishwa kwa kuzingatia viwango vya utokeaji wake kwa asilimia. Kila zoezi lililotolewa wanafunzi limechunguzwa kivyake na kuonyesha vipengele vya kimofosintaksia vilivyoathirika zaidi. Zoezi la kuzikamilisha tungo za wanafunzi limesaidia sana kubashiri matatizo ya upatanishi wa kisarufi yanayowakumba wanafunzi. Zoezi la utungaji wa insha limedhihirisha jinsi ambavyo wanafunzi wanatatizika kujiundia wenyewe tungo

kamili wakati ambapo zoezi la kusimulia visa mbalimbali limeonyesha uwezo wao wa kujieleza kwa njia ya mazungumzo na matatizo ya kimofosintaksia yanayowakumba. Kwa hivyo, makosa yalibainishwa, kisha kufafanuliwa na kuainishwa kama tunavyopata kutokana na misingi ya nadharia ya UM iliyozungumziwa katika (§1.7.1.2). Katika sura inayofuata, tutabainisha chanzo cha makosa hayo ya wanafunzi na kutathmini mikakati inayozingatiwa katika kuyapunguza makosa hayo.

# SURA YA NNE

# CHANZO CHA MAKOSA YA WANAFUNZI NA MIKAKATI INAYOZINGATIWA KUYAPUNGUZA

## 4.0 Utangulizi

Baada ya kudhihirisha makosa ya kimofosintaksia yanayofanywa na wanafunzi na kuonyesha aina na kiwango cha utokeaji wake katika sura iliyotangulia, sura hii imechunguza vyanzo vya makosa hayo na mikakati inayozingatiwa na walimu ili kuyapunguza makosa hayo. Kupitia nadharia za Uchanganuzi Makosa (UM) na Lugha Kadirifu (LK), tofauti za kiisimu zinazosisitizwa katika nadharia ya kwanza na michakato ya kisaikolojia iliyozungumziwa na Selinker (1972) katika ujifunzaji wa L2 ndiyo imeelekeza uchunguzi wetu katika sura hii. Lugha kadirifu ya mwanafunzi hubadilikabadilika kutoka pale anapotumia miundo mibovu kuelekea kiwango ambapo atakuwa na miundo sahihi au inayokaribia sana muundo kamili wa L2. Hivyo basi, kwa mujibu wa nadharia ya UM na LK, sehemu ya kwanza ya sura hii imejadili vyanzo mbalimbali vya makosa yanayofanywa na wanafunzi katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Sehemu ya pili ya sura hii imetathmini mikakati inayozingatiwa na walimu katika jitihada zao za kuyapunguza makosa ya wanafunzi wao.

## 4.1 Vyanzo vya makosa ya wanafunzi

Kwa hakika, ni vigumu kudhihirisha kuwa kosa fulani limetokana na kitu fulani. Norrish (1983) anabainisha kuwa makosa katika ujifunzaji wa lugha huweza kutokana na uteuzi wa vifaa vya kufundishia na utaratibu unaozingatiwa katika ufundishaji, mpangilio wa mifano inayotolewa na mazoezi ya utekelezaji au mchakato

unaozingatiwa na mwanafunzi katika ujifunzaji wake. Hata hivyo, kwa kuzingatia misingi ya nadharia za UM na LK, uchunguzi wa data yetu umedhihirisha kuwa makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi watafitiwa yalikuwa na vyanzo vyake katika uhamishaji wa kiisimu, kuchanganya ndimi, upungufu wa msamiati, utohozi usiofaa, tafsiri, kutojali, uzoefu mdogo na ukosefu wa habari, ujumuishaji na uhamishaji wa ufundishaji.

### 4.1.1 Uhamishaji wa kiisimu

Richards (1974) anaeleza uhamishaji kama mojawapo ya mbinu anazozitumia mwanafunzi katika ujifunzaji wake wa L2 na kuhakikisha kwamba jambo hili hutokea mara kwa mara katika tungo za mwanafunzi huyo. Kwa hivyo, uhamishaji unaweza kuelezwa kama utaratibu unaozingatiwa na mwanafunzi katika ujifunzaji wake pale anapokitoa kiambajengo cha tungo katika L1 na kukitumia katika L2. Katika hali hii, mwanafunzi hufanya makosa kwani hajali tofauti za kiisimu zilizopo kati ya L1 na L2. Kulingana na uchunguzi wa matokeo ya utafiti wetu, wanafunzi Wanyarwanda wameathiriwa na miundo ya Kinyarwanda katika ujifunzaji wao wa Kiswahili kwa kuvihamisha vipengele vya kimofosintaksia vya Kinyarwanda na kuvitumia katika Kiswahili kama tunavyopata kutokana na mifano 4.1.

(4.1)

| | |
|---|---|
| *a)*ng'ombe yangu inakula majani tuna wanyama nyingi, zote zilipata chakula* | ng'ombe wangu anakula majani tuna wanyama wengi, wote wanapata chakula |
| *b)*Kwa sababu wanapata waganga wa kuzipatia dawa* | kwa sababu wanapata madaktari wa mifugo wanaowatibu |
| *c)*hizo wanyama ni ng'ombe, mbuzi, nguruwe na kadhalika* | Wanyama hao ni ng'ombe, mbuzi, nguruwe, na kadhalika. |
| *d)* Mapato anaweza kuongezeka* | Mapato yanaweza kuongezeka |
| *e)*ili maziwa asambazwe katika nchi nzima* | Ili maziwa yasambazwe katika nchi nzima |
| *f)*maziwa ya ng'ombe ana umuhimu mwingi* | Maziwa yana umuhimu sana |
| *g)* kufuga vinatusaidia kutuletea faida nyingi* | Kufuga kuna faida nyingi kwa maisha yetu |
| *h)*kufuga binasaidia kuona vyakula* | Kufuga kunasaidia kupata chakula |

| | |
|---|---|
| *i)*kufuga vinatuletea uchumi* | Kufuga kunatufanya tuendelee kiuchumi |
| *j)* kijijini hataonekana* | Kijijini mnaonekana, |
| *k)*tunafuga pahali halipojengwa* | Tunafugia mahali palipojengwa. |

Kutokana na mifano katika (4.1.a-c), wanafunzi wengi walitumia viambishi *{i/zi}* vya ngeli za 9 na 10 za Kinyarwanda katika tungo za Kiswahili zenye majina ya wanyama. Katika tungo hizi, wanafunzi walipatanisha nomino za wanyama na vivumishi au vitenzi kwa kuzingatia miundo ya viambishi vinavyotumiwa katika lugha ya Kinyarwanda ambapo nomino za wanyama za ngeli za 9 na 10 *{N/N}* huendelezwa kwa namna sawa na nomino zingine za ngeli hizi (Angalia Jedwali 2.9).

Ngeli zingine ambazo zilionekana kuwatatiza wanafunzi katika muktadha huu wa uhamishaji wa vipengele vya kisarufi vya Kinyarwanda katika Kiswahili, ni ngeli ya 6 inayotumia kiambishi *{ma}*. Kwa kuwa lugha ya Kinyarwanda hutumia muundo wa *{ma/a}* katika kupatanisha nomino hizo kwa vitenzi, baadhi ya wanafunzi Wanyarwanda walishindwa kutunga sentensi sahihi pale walipohamisha muundo huo wa Kinyarwanda katika tungo zao za Kiswahili kama tunavyopata katika mifano (4.1.d-f). Uhamishaji mwingine ulijitokeza kuhusu kiambishi *{ku}* cha vitenzi jina. Kama tulivyoeleza katika §2.4.1.2, lugha ya Kinyarwanda huruhusu kurejelea vitenzi jina katika vitenzi kwa kutumia kiambishi nafsi *{bi}* ambacho aghalabu hutumiwa katika muundo wa majina yenye kiambishi *{bi}* cha ngeli ya 8. Kwa hivyo, athari ya Kinyarwanda kwa wanafunzi ilijitokeza pale walipounda vitenzi vyenye viambishi nafsi *{bi/vi}* kurejelea kitenzi jina kiima kama ilivyo katika mifano (4.1 g-i). Muundo wa kwanza unaonyesha kuwa mwanafunzi anajaribu kuzingatia kuwa Kiswahili hutumia kiambishi *{vi}* pale Kinyarwanda kinapotumia *{bi}* ilhali katika muundo wa pili mwanafunzi hajali tofauti hiyo na kutumia *{bi}* ya ngeli ya 8 ya Kinyarwanda.

Nayo mifano (4.1 j na 4.1 k) inabainisha matumizi ya kipatanishi {ha} cha ngeli za mahali {ha, ku, mu, i} katika Kinyarwanda (Jedwali 2.6).

Isitoshe, uchunguzi wa matokeo ya utafiti wetu ulibainisha kuwa miundo mingine ya ngeli za makundi ya {li/ya}, {a/wa} na {pa/mu/ku} iliathiriwa sana na miundo ya ngeli za Kinyarwanda.

(4.2)

| | |
|---|---|
| a)**jiwe limoja limetupwa* | jiwe moja limetupwa |
| *b) *koti rizuri/lizuri* | koti zuri |
| *c) *ng'ombe yangu* | ng'ombe wangu |
| *d) *mbuzi zinne* | mbuzi wanne |
| *e) *kipofu kimoja* | kipofu mmoja |
| *f) *) Mahali henyewe hamesafishwa* | mahali penyewe pamesafishwa |
| *g) *barabarani halikuwa ajali* | kulikuwa na ajali barabarani |

Makosa katika miundo hii potofu ya wanafunzi yana vyanzo vyake katika miundo ya Kinyarwanda pale ambapo, katika (4.2 a-e), mwanafunzi anaathiriwa na muundo wa Kinyarwanda kinachoruhusu kipatanishi cha ngeli ya 5 *{ri}* kutumiwa katika vivumishi vyote; kipatanishi cha ngeli ya 9/10 *{i/zi}* katika vitenzi na viwakilishi hata kama nomino zinazorejelewa ni za wanyama (Angalia Jedwali 2.7). Kipatanishi cha ngeli ya 7 *{ki}* kurejelea jina *kipofu* nacho kimeonekana kuwatatiza baadhi ya wanafunzi kwani L1 yao huyaruhusu majina yote yanayotanguliwa na *{ki}* kurejelewa katika vitenzi, vivumishi na viwakilishi kwa kutumia kipatanishi hicho (Jedwali 2.7). Katika tungo za (4.2 f na 4.2 g), athari ya Ll inajidhihirisha pale ambapo mwanafunzi ana habari kwamba nomino zote za mahali husimamiwa na kiambishi *{ha}* kama kipatanishi chake kwa vivumishi, viwakilishi na vitenzi. Kwa hivyo, mwanafunzi huyu anakumbana na changamoto kubwa sana anapotakiwa kutumia kiambishi mwafaka cha mahali husika. Kwa hivyo, badala ya kutumia *{pa, mu, ku}* kulingana na

aina ya mahali panapozungumziwa, mwanafunzi anatumia *{ha}* kwani L1 haitofautishi mahali penyewe (Angalia majedwali 2.2, 2.5 na 2.7).

Aidha, uchunguzi wetu ulibainisha kuwa baadhi ya wanafunzi hawakuzingatia matumizi ya urejeshi wa nomino katika maneno mengine yanayounda sentensi kama tunavyopata katika mifano hii.

(4.3)

| | |
|---|---|
| *a) *Wafugaji wana milima ina nyasi ya wanyama* | Wafugaji walio na milima ya nyasi za wanyama. |
| *b) *Vitu vinaweza kuleta wageni* | vitu vinavyoweza kuleta wageni |
| *c) *Nataka kuonyesha jinsi ninapenda utangazaji* | ninataka kuwaonyesha jinsi ninavyopenda utangazaji |
| *d) *Kuna wantu wengi walipoteza maisha yao* | kuna watu wengi waliopoteza maisha yao |

Kutokana na tungo hizo ni dhahiri kwamba makosa ya kimofosintaksia waliyoyafanya wanafunzi yalitokana na athari za L1 ambapo nomino kiima hairuhusiwi kurejelewa katikati mwa kitenzi (Angalia Jedwali 2.7). Katika mifano (4.3), mwanafunzi anashindwa kurejelea nomino kiima kwa kutumia kirejeshi *{o}* kinachoweza kupachikwa kabla ya mzizi wa kitenzi au kuwekwa kwenye mzizi {amba-} ili kuunda kiwakilishi kirejeshi cha nomino kiima.

Kupitia maelezo hapo juu, ni dhahiri kwamba wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunza Kiswahili waliathiriwa sana na miundo ya Kinyarwanda. Utafiti huu umebainisha wazi kwamba tofauti kati ya Kinyarwanda na Kiswahili ni mojawapo ya changamoto za kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi hawa. Matokeo haya hayatofautiani sana na yale yaliyopatikana katika tafiti zingine zilizotangulia utafiti huu kama vile Musau (1993), Mudhune (1994), Onyango (1997), Mutugu (2001) na Cheruiyot (2011).

Hata hivyo, kila utafiti ulibainisha tofauti za kipekee kulingana na miundo kati ya kila L1 na Kiswahili kwa wanafunzi waliohusika. Kwa hivyo, katika utafiti huu tumebainisha kuwa changamoto kubwa zilijitokeza sana katika kipengele cha urejeshi wa nomino katika vitenzi kwani kipengele hiki hujitokeza kwa namna tofauti katika Kiswahili na vile kinavyojitokeza katika Kinyarwanda. Mbali na kuwa miundo ya urejeshi ni tofauti mno kati ya Kiswahili na Kinyarwanda, matatizo ya aina hii yalitokana pia na hali kwamba Kiswahili kina miundo changamani zaidi ya kubainisha urejeshi katika sentensi kuliko Kinyarwanda kinavyofanya (Jedwali 2.7).

Tofauti zingine zilizobainishwa katika mfumo wa ngeli za Kinyarwanda na Kiswahili (§2.6), nazo zimeonekana kuwakanganya wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunza Kiswahili kwani wengi waliofanya makosa walipendelea kutumia vipatanishi vya sarufi kulingana na jinsi hali ilivyo katika Kinyarwanda. Kama tunavyopata kutokana na nadharia ya UM, hatuna budi kusisitiza kwamba wanafunzi hawa waliathiriwa sana na mfumo wa Kinyarwanda katika ujifunzaji wao wa Kiswahili kwa kuhamisha vipengele vya kimofosintaksia vya Kinyarwanda na kuvitumia katika Kiswahili.

### 4.1.2 Kuchanganya ndimi

Matokeo ya utafiti wetu yalidhihirisha pia kuwa baadhi ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi yana chanzo chake katika mchanganyiko wa maneno ya Kiswahili na ya lugha zingine kama tunavyopata katika mifano ifuatayo:

(4.4)

| | |
|---|---|
| *(a)*Kwa sababu gani bantu benye banatoka kijijini banafanya kazi kwa kufuga?* | Kwa nini wanakijiji wanapenda kufuga? |
| *(b)*Ufugaji ni kazi nzuri kwenye bantu bana hamu ya kuwa richi kwenye maisha ya kila siku* | Ufugaji ni shughuli inayosaidia watu kutajirika na kufanikiwa katika maisha yao ya kila siku. |
| *(c)*Ufugaji bunasaidia bantu ba kijijini kuona rutuba kwa kueka shamba yangu* | Wafugaji hufaidika kwa kupata mbolea ya kurutubisha mashamba yao. |
| *(d)*Kufuga kijijini si vigumu kwa sababu tuna nyasi yazo* | Kufugia kijijini ni shughuli rahisi kwani kunapatikana nyasi za kutosha. |

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba mchanganyiko wa Kiswahili na maneno ya Kinyarwanda ni mojawapo ya mambo yaliyowafanya wanafunzi waunde sentensi zenye makosa ya kimofosintaksia. Katika mifano (4.4 a-b), makosa ya wanafunzi yalisababishwa na matumizi ya nomino *bantu* ambapo walidondoa kisabiki kiambishi awali {a} na kubaki na kiambishi awali cha ngeli {ba} kinachotumika katika Kinyarwanda badala ya {wa} katika Kiswahili. Hivyo basi, ni wazi kuwa upatanishi wa kisarufi alioutumia katika sentensi yake ulirejelea kiambishi awali cha ngeli *{ba}* badala *{wa}* kinachoambikwa kwa vivumishi na vitenzi kurejelea nomino za kundi la {a/wa}.

Katika mfano 4.4 b, mwanafunzi amechanganya pia Kiswahili na Kiingereza pale anapotumia neno *richi* badala ya *tajiri*. Ingawa amekosea kwa kutumia msamiati usiofaa, ni wazi kwamba kuchanganya ndimi kwake hakukuweza kumruhusu kuzingatia upatanishi wa kisarufi unaotakikana katika Kiswahili. Hivyo basi, kosa lake lilichukuliwa pia kama kosa la kimofosintaksia mbali na kuwa la kimsamiati. Mfano (4.4 d) umechanganya viambishi vipatanishi vya Kiswahili na vya Kinyarwanda kwa kuunda kimilikishi *yazo* ambamo tunakuta mofu *{i-a-zi-o}* na kuundo kipashio *nyasi yazo*. Katika kipashio hiki, kiambishi {zi} kinachorejelea wanyama katika L1 ya mwanafunzi kimeambatishwa kwa kirejeshi {o} na kuunganishwa kwa kiambishi {i} cha kurejelea *unyasi* pamoja na mzizi {a} wa umilikisho ili kuunda kimilikishi *yazo*. Hivyo basi, ni wazi kuwa mbali na kukumbwa na changamoto ya kutumia kiambishi kinachofaa katika kurejelea wingi wa nomino

*unyasi* (nyasi), mwanafunzi amefanya makosa kutokana na hali kwamba amechanganya miundo ya Kinyarwanda na ya Kiswahili.

Kwa kuwa nadharia ya LK husisistiza kuwa mwanafunzi huzingatia michakato mbalimbali ya kisaikolojia katika jitihada zake za kuelewa na kutumia mfumo wa L2, ni dhahiri kwamba kuchanganya ndimi ni mojawapo ya michakato hiyo anayoipitia mwanafunzi Mnyarwanda anayejifunza Kiswahili. Katika hali hii, matokeo ya utafiti wetu yamedhihirisha kuwa lugha ya mwanafunzi hutawaliwa na miundo ya L1 ambapo matumizi ya neno moja kutoka L1 huathiri upatanishi wa kisarufi anaoutumia katika L2 kama tulivyodhihirisha katika mifano 4.4 a-d.

**4.1.3 Utohozi usiofaa**

Massamba (2004) anaeleza kuwa utohozi ni uundaji wa istilahi; yaani utaratibu wa kuyabadili maumbo ya maneno yaliyokopwa kutoka lugha chanzo ili yalingane na kuoana na fonolojia ya LL. Kutokana na uchunguzi wa data yetu, wanafunzi walifanya makosa kwa kuyatohoa baadhi ya maneno ya lugha mbalimbali bila sababu. Mifano katika (4.4) yaweza kutudhihirishia jambo hilo ambapo viambishi kama {ba} katika kipashio *bantu ba kijijini* hurejelea jina *bantu* lililotoholewa kutoka *abaantu* (watu) la Kinyarwanda.

Vilevile, kipashio *kazi kazuri ka kufuga wanyama* katika 3.2 b kinabainisha kwamba mwanafunzi aliathiriwa na muundo wa jina *akazi* (kazi) la Kinyarwanda ambapo {ka} ni kiambishi ngeli kinachozingatiwa katika upatanishi wa jina hili na maneno mengine yanayohusiana nalo kisarufi. Kwa hivyo, ni wazi kwamba utohozi ulikuwa

pia mojawapo ya mikakati aliyoikimbilia mwanafunzi Mnyarwanda katika jitihada zake za kuzungumza na kuandika Kiswahili.

### 4.1.4 Tafsiri

Kulingana na matokeo ya utafiti wetu, wanafunzi walifanya makosa ya kimofosintaksia yaliyotokana na kutafsiri misemo na majina ya Kinyarwanda. Katika hali hii, mwanafunzi alijaribu kujiundia sentensi za Kiswahili, lakini fikira zake zikawa zinarejelea majina ya sentensi zake katika L1. Kwa hivyo, upatanishi wa kisarufi aliouzingatia ulikuwa wa majina hayo ya Kinyarwanda au L1 badala ya Kiswahili.

**Jedwali 4.1: Upatanishi wa wanafunzi baada ya kutafsiri KN katika L1**

| Tungo za wanafunzi zenye makosa | Tungo sahihi | Tafsiri katika Kinyarwanda |
|---|---|---|
| a)*shamba ambao **u**talimwa<br>b)*huyu ndi**we**<br>c)*udevu **ru**refu **ru**mekatwa<br>d)*ufugaji **bu**tasaidia<br>e)*kijijini mwangu kinaonekana**mo….** | Shamba ambalo litalimwa<br>Huyu ndiye<br>Udevu mrefu umekatwa<br>Ufugaji husaidia<br>Kijijini mwangu mnaopatikana | Umurimá **u**záahúngwa<br>uyu ni **wé**<br>urwaánwa rureerure **rw**aakaswe<br>ubwóorozi **bu**fasha<br>Mu cyaaro cy'iwáacú habonekam**ó** |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Katika Jedwali 4.1, tungo (a) inadhihirisha kuwa wanafunzi walifanya makosa waliposhikilia kwamba jina *shamba* la ngeli ya kundi la {ji/ma} lina tafsiri yake *umurima* la kundi la *{mu/mi}* katika Kinyarwanda. Katika tungo (c) jina *udevu* (c) la kundi la {u/n} katika Kiswahili ni *urwaánwa* la kundi la *{ru/zi}* katika Kinyarwanda. Kwa hivyo, wanafunzi hawa waliunda tungo zenye kipatanishi *{u}* katika tungo (a) na {ru} katika tungo (c) kwa kuzingatia kuwa jina *umurima* (shamba) linahesabiwa katika kundi la *{mu/mi}* na kuwa *urwaánwa* (udevu) ni la kundi la {ru/n} katika

Kinyarwanda. Hivyo basi, waliunda kiwakilishi *ambao* badala ya *ambalo*, ***utalimwa*** badala ya ***litalimwa*** katika (a) na ***rumekatwa*** badala ya *umekatwa* katika (c).

Halikadhalika, tafsiri za aina hii ziliwaathiri sana wanafunzi pale waliposhindwa kutumia viambishi mwafaka vya Kiswahili kwani fikira zao wakati wa kuunda tungo zao zilikuwa zinairejelea miundo ya Kinyarwanda kama tunavyopata kutokana na mifano ya Jedwali 4.1. Katika mfano (b), mwanafunzi anapatanisha kutokana na kiwakilishi *uyu* (huyu) na kutumia kipatanishi {we} badala ya {ye} wakati ambapo katika (d) anarelejelea jina *ubwóorozi* (ufugaji) ambapo anatumia kipatanishi {bu} badala ya {u}. Katika mfano (e), mwanafunzi anazingatia muundo wa urejeshi wa viwakilishi vya mahali kwa kupachika *mo* mwishoni mwa kitenzi na kuunda kipashio *hanaonekanamo* badala ya *mnapatikana*.

Kutokana na tungo zilizotolewa katika Jedwali 4.1, ni dhahiri kuwa kabla ya kuamua kuhusu kiambishi mwafaka kinachostahili kutumiwa, wanafunzi walifikiria kwanza jina lililorejelewa katika Kinyarwanda. Mchakato huu wa kisaikolojia ulijitokeza sana kwa wanafunzi waliolinganisha maneno kwa kuyatafsiri katika L1 kiasi kwamba walishindwa kurejelea kiambishi sahihi kilichofaa kutumiwa; na matokeo yake yakawa makosa ya kimofosintaksia yaliyobainishwa katika tungo zao (Jedwali 4.1).

Mbali na hayo, uchunguzi wetu umetudhihirishia kwamba wanafunzi walifanya tafsiri za moja kwa moja katika uandishi na maongezi yao. Hali hii nayo iliathiri miundo ya tungo zao na makosa ya kimofosintaksia yakajitokeza kama tunavyopata katika mifano ifuatayo:

**Jedwali 4.2: Tafsiri za moja kwa moja**

| Muundo wa Kinyarwanda | Tungo za wanafunzi/ Tafsiri ya moja kwa moja | Muundo sahihi |
|---|---|---|
| a) Mu cyaaro cy'iwaácu amáazi aboneka ntá mafaraanga | *Kwa kijijini mwangu maji anaonekana kwa bila ya pesa | Kijijini mwangu maji hayalipwi |
| b) Ibiíndi biintu bifashá amatúungo | *Vitu vinginevyo binasaidia munyama | Vitu vingine vinavyowasaidia wanyama |
| c) Waagura ibiintu byiínshi ushaaká | *Unanunua vitu vingi unataka | Unaweza kununua vitu vingi unavyovitaka |
| d) Kóorora ní byiizá cyaane bishobora kugúkuura mu bibázo | *Kufuga ni vizuri sana vinaweza kukuokoa katika shida | Kufuga ni muhimu sana kwani kwaweza kukusaidia wakati wa matatizo |
| e) Ubuzima bw'ábaantu bó mu cyaaro nó mu mujyí bushiingiye ku bwóorozi | *Maisha ya watu kutoka kijijini na mjini bunasaidiwa sana na ufugaji | Vijijini na mijini, maisha hutegemea ufugaji/yanategemea ufugaji |
| f) Kugira ngo ntibágire ikibázo bahurá na cyó | *Ili wasiwe tatizo wanakutana nao | Ili wasikumbane na tatizo lolote |
| g) Ndaha ináama abaantu badashaaka kóorora | *Ninapa shauri watu hawataki kufuga | Ningependa kuwashauri watu ambao hawataki kufuga/ wasiotaka kufuga |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kulingana na mifano hii, ni dhahiri kwamba makosa mengi ya kimofosintaksia ya wanafunzi yametokana na tafsiri zao za moja kwa moja. Katika tungo hizi, wanafunzi walifanya makosa mengi ya kuyapanga maneno kwa utaratibu unaokubalika katika Kiswahili. Maneno katika tungo zao yameorodheshwa kama yalivyo katika Kinyarwanda bila kujali kuwa baadhi ya miundo huhitaji viunganishi, vihusishi, kugeuza kategoria za maneno au kuwa neno moja huweza kueleza kifungu cha maneno ili kuunda tungo kamili. Kwa kuwa fikira zao zilielekea kwa tafsiri walizozifanya, ndiyo maana pia walitumia vipatanishi visivyofaa katika tungo zao. Katika mfano (4.6.a), kipashio *maji anaonekana* ambapo kiambishi *{a}* cha Kinyarwanda hutumiwa badala ya *{ya}* kinachotumika katika Kiswahili huweza kututhibitishia jambo hili.

Aidha, katika Jedwali 4.2, tungo (b) inaonyesha kuwa mwanafunzi alizingatia kiambishi *{bi}* kama kipatanishi cha jina *ibiintu* (vitu) katika Kinyarwanda badala ya *{vi}*. Nayo tungo (e) inabainisha kuwa mwanafunzi alipatanisha jina *maisha* kwa

kutumia kiambishi *{bu}* ambacho hutumiwa katika Kinyarwanda kupatanisha jina *ubuzima* (maisha) la kundi la *{bu}*. Katika sentensi (d), tafsiri ya moja kwa moja ilimfanya mwanafunzi ahamishe muundo wa Kinyarwanda ambapo kitenzi jina huweza kurejelewa na kiambishi kipatanishi *{bi}* badala ya *{ku}*. Katika mfano huu, neno *vizuri* limetumiwa badala ya *kuzuri* na kipatanishi *{vi}* kimetumiwa badala ya *{ku}*.

Vilevile, baadhi ya mifano katika Jedwali 4.2 inabainisha mpangilio wa maneno usiofaa kama ilivyo katika sentensi (f). Jambo hili lilitokana na hali kwamba mwanafunzi alitafsiri moja kwa moja sentensi anayoifikiria katika Kinyarwanda. Sentensi (b), (c) na (g) zinaonyesha kuwa wanafunzi hawajali urejeshi wa katikati wa jina kiima katika kitenzi kama zilivyo sentensi za Kinyarwanda. Kwa hakika, hali hii ya kisaikojia ya wanafunzi waliofanya makosa haya hutudhihirishia kuwa ingawa walikuwa wanaandika Kiswahili, fikira zao zilikuwa zinaegemea sana kwa miundo ya Kinyarwanda na kufanya tafsiri za moja kwa moja.

### 4.1.5 Uzoefu mdogo na ukosefu wa habari

Uzoefu mdogo wa kutumia Kiswahili na ukosefu wa habari nao umejidhihirisha kama mojawapo ya vyanzo vya makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi. Ingawa tumedhihirisha kwamba baadhi ya wanafunzi walitatizika kutokana na uzembe na kutojali katika ujifunzaji wao, tumetambua pia kwamba baadhi ya miundo yao inadhihirisha makosa yanayotokana na uzoefu mdogo wa kutumia Kiswahili na ukosefu wa habari kuhusu muundo unaofaa kutumiwa. Mifano ya miundo kama hii ni pamoja na tungo katika 4.5.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

(4.5)

| | |
|---|---|
| *a)*watu wowote waliko kijijini* | watu wote waishio kijijini |
| *b)*ufugaji umeenea pahali popote kwa sababu ya nchi yetu* | ufugaji umeenea pahali pote kutokana na sera ya nchi yangu |
| *c)*kama kazi yeyote ina umuhimu na ufugaji pia una umuhimu* | ufugaji una umuhimu kama ilivyo kwa kazi zingine |
| *d)*ufugaji wa wanyama wanene kwa mfano ng'ombe, hawa wanafuna mfuno mnene kuliko wengine wanayofuga wanyama wadogo kama kuku na sungura* | ufugaji wa wanyama wanono kama ng'ombe ndio unaopendelewa kuliko ufugaji wa wanyama wadogo kama vile kuku na sungura |
| *e)*kwa ufuga kijiji mwangu ni lazima kwa kuletea watu vitu vingine kila siku, vitu vya kula, vitu vya kunywa* | ufugagi kijijini mwangu ni muhimu sana kwa kuwa unawezesha wanakijiji kupata vitu vingi vya kula na vya kunywa |

Katika tungo (4.5 a) na (4.5 b), uchunguzi wetu ulibainisha kwamba wanafunzi walitumia muundo wa *{o-ote}* badala ya *{-ote}* kwani hawana habari kuhusu matumizi ya miundo hiyo. Katika tungo (4.5 c), mwanafunzi hana habari kati ya matumizi ya muundo *{ye-yote}* na *{yo-yote}*. Ushahidi tunaoutoa katika chanzo hiki cha makosa ni kwamba miundo hii iliwakanganya wanafunzi wengi na kuwa miundo hii ni changamano zaidi kuliko miundo mingine ya vivumishi vya Kiswahili. Steinberg na wenzake (1982) wanaeleza kwamba mwanafunzi wa L2 anahitaji mazoezi ya kutosha ili aelewe miundo iliyo changamani katika lugha.

Tungo (4.5 e) inabainisha kwamba wanafunzi hawana habari kuhusu tofauti kati ya *ingi* na *ingine*. Miundo hii nayo ilionekana kuwa migumu kwa wanafunzi hawa kiasi kwamba iliwatatiza wanafunzi wengi hasa wa darasa la tano. Badala ya kutumia *vitu vingi* walipendelea *vitu vingine* wakati ambapo wanafunzi wengine walikuwa wakidondosha virejeshi katika tungo zao au wakavichanganya (4.6.c, 4.6.f, 4.6.g na 4.8.d). Kwa hivyo, uchunguzi wetu ulitudhihirishia kwamba wengi wa wanafunzi hawakuwa na habari kamili kuhusu miundo hiyo changamani na kuwa wengine walikuwa hawajaizoea na kuimudu kiasi cha kuitumia bila wasiwasi wowote.

Aidha, uzoefu huo mdogo wa kutumia Kiswahili ndio ulisababisha pia uundaji wa sentensi ndefu mno zisizojali uafikishaji unaofaa kuzingatiwa ili ujumbe utolewe na ueleweke kwa msomaji. Urefu huu uliwaathiri wanafunzi waliofanya makosa ya kutunga sentensi ndefu kwani walishindwa kupatanisha vizuri majina na maneno mengine katika tungo zao. Pengine, waliunda vipashio visivyobainisha wazi nomino kiima au kwa kuchanganya viambishi. Mifano ifuatayo huweza kutupa maelezo zaidi kuhusu chanzo hiki cha makosa.

(4.6)

| | |
|---|---|
| *a)*ufugaji kijijini ni nzuri sana mimi ninaona ufugaji ni nzuri kwa sababu mbona tumesaidia watu wote kuona mazao mengi sana hayo mazao anatuletea fedha nyingi hizo fedha zinatusaidia kuona vitu mbalimbali vitu mbalimbali binadusaidia kumaliza au kusuisha matatizo mbalimbali* | Ufugaji ni mzuri sana. Mimi naona kuwa ufugaji ni mzuri kwa sababu unasaidia watu wote kupata mazao mengi sana yanayoweza kuwaletea pesa nyingi na kusuluhisha matatizo yao. |
| *b)*mimi ninatawambia kuhusu ufugaji kijijini mwangu ni vizuri sana kwa sababu niliona kufuga wanyama yote watu walifuga hao wanyama hatakuwa na matatizo walikutana* | Ningependa kuwaambia kwamba ufugaji ni muhimu sana kijijini mwangu. Wanakijiji wanafuga wanyama wa aina nyingi ambao wanawasaidia kupambana na matatizo mengi maishani mwao. |
| *(c)*ufugaji kijijini mwangu kinasaidia watu mbalimbali binasaidia wanafunzi sana binasaidia wanafunzi kuona mazao akimemaliza kuona mazao akaenda shuleni kujifunza kwa sababu anaona vyombo bya shuleni daftari, kalamu na vitu mbalimbali mimi mbona ufugaji kwa kijijini ni vizuri kwa sababu umuhimu sana* | Ufugaji kijijini mwangu unasaidia wafugaji kupata mazao mazuri. Watoto wao huweza kupata vifaa vya shule kama vile daftari, kalamu na vitu vingine vinavyohitajika. Kwa hivyo ufugaji kijijini mwangu ni shughuli muhimu sana. |

Kutokana na mifano katika 4.6, ni dhahiri kuwa uzoefu mdogo wa wanafunzi ndio uliwafanya wafululize maneno bila kujali taratibu za uafikishaji kama vile matumizi ya herufi kubwa na/au alama vituo kama vile nukta na mkato. Tulitambua kuwa katika zoezi la masumilizi, wengi wao walikuwa wakisitasita katika matamshi yao na kujirudiarudia kama wasio na uhakika wa jambo walilotaka kuelezea kiasi kwamba tungo zao zilikuwa ndefu mno. Kwa kuwa jambo hili lilijidhirisha pia katika uandishi

wao wa insha, tuliamua kwamba wanafunzi watafitiwa walikuwa na uzoefu mdogo katika kuandika na kuzungumza Kiswahili. Changamoto hii ya kuunda sentensi ndefu ndiyo iliwafanya wanafunzi hawa sizingatie usahihi wa viambishi vinavyoambikwa kwa vitenzi na vivumishi kama tunavyopata katika mifano (4.6).

Kipashio *ufugaji kijijini mwangu kinasaidia watu mbalimbali binasaidia wanafunzi sana binasaidia wanafunzi* ....katika (4.6 c) huweza kutuonyesha jinsi ambavyo mwanafunzi alichanganya miundo tofauti ya viambishi bila kujali nomino zinazorejelewa katika tungo yake. Nao uundaji wa kipashio *ninatawambia* katika (4.6 b), ambapo anaunganisha vitenzi *ninataka* na *kuwaambia* na kudondoa {ka} katika kitenzi cha kwanza, huweza kutudhihirishia jinsi mwanafunzi aliyefanya kosa hili hajiamini katika matamshi yake na ana uzoefu mdogo katika matumizi ya Kiswahili. Hali hii ndiyo inamfanya hasa aunde kipashio kama *kwa sababu umuhimu sana* katika (4.6 c) ambapo anadondoa kitenzi kipungufu *ni* ingawa muundo huu tayari alishakutana nao katika ujifunzaji wake kwani alikuwa amewahi kuutumia katika mazungumzo yake.

Ushahidi mwingine kuhusu chanzo hiki cha makosa ya wanafunzi unajitokeza katika uchunguzi wa sentensi (4.6 a) ambapo mwanafunzi mmoja aliweza kutumia vizuri kirejeshi nafsi yambwa {tu} katika kitenzi *anatuletea* na **zinatusaidia* lakini akashindwa kukirejelea kwa namna inayofaa katika kitenzi **binadusaidia* (vinatusaidia). Kwa hivyo, mbali na kukosa habari kuhusu miundo changamani ya Kiswahili, uzoefu mdogo nao ulichukua nafasi kubwa katika kuwafanya wanafunzi

Wanyarwanda wakumbane na changamoto za kimofosintaksia katika uandishi na uzungumzi wao.

### 4.1.6 Ujumuishaji

Kulingana na misingi ya nadharia ya LK, lugha ya mwanafunzi huweza kujumuisha kanuni anazojifunza na kuzitumia pasipotarajiwa na hivyo basi akafanya makosa ya kisarufi. Norrish (1983) anasema kuwa ujumuishaji unatokana na tajiriba ya mwanafunzi katika matumizi yake ya L2. Katika hali hii, mwanafunzi anatunga sentensi zenye makosa ya kujumuisha kanuni za L2. Uchunguzi wetu wa makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi watafitiwa ulidhihirisha kwamba walizijumuisha kanuni za Kiswahili na kuzitumia pasipofaa. Wanafunzi waliofanya makosa haya hawakuweza kutambua kwamba baadhi ya kanuni zinazowaelekeza katika kutunga sentensi sahihi zina matumizi yake na mipaka wanayostahili kuzingatia ili wasifanye makosa katika maandishi na maongezi yao.

(4.7)

| | |
|---|---|
| _a)*mkono mwenyewe_ | mkono wenyewe |
| _b)*mkulima mpi_ | mkulima yupi |
| _c)*ufugaji ni umuhimu_ | ufugaji ni muhimu |
| _d)*jiwe limoja_ | jiwe moja |
| _e)*mwili msafi_ | mwili safi |
| _f)*kipofu kimoja_ | kipofu mmoja |
| _g)*udevu urefu_ | udevu mrefu |
| _h)*mbuzi zinne_ | mbuzi wane |
| _i)*ng'ombe yangu_ | ng'ombe wangu |
| _j)*nina sungura mbili_ | nina sungura wawili |

Mifano hii inadhihirisha kwamba wanafunzi walishikilia kwamba kiambishi cha ngeli; aghalabu silabi ya kwanza ya kila jina, hufanana kiumbo na kiambishi cha ngeli kinachoambikwa kwa vivumishi kama kipatanishi (**_m_**toto **_m_**dogo, **_m_**situ **_m_**kubwa). Kwa hivyo, utaratibu huo ndio umejumuishwa na wanafunzi kwa kuviunda vipashio

katika mifano (4.9 a-g) hapo juu. Mifano katika (4.7 i) na (4.9 j) inaonyesha kwamba wanafunzi walifanya makosa kwa kuzingatia upatanishi unaoyahusu majina ya ngeli za 9 na 10 *{N/N}*. Ingawa majina *ng'ombe* na *mbuzi* kimofolojia huingizwa katika kundi hili la ngeli, kisintaksia huendelezwa kwa namna sawa na majina mengine ya ngeli ya kwanza *{mu/wa}*; ndiyo maana huhesabiwa miongoni mwa makundi ya {a/wa} badala ya {i/zi}.

### 4.1.8 Uhamishaji wa ufundishaji

Kwa mujibu wa nadharia ya LK, mwanafunzi huweza kufanya makosa kutokana na jinsi anavyofunzwa (Selinker, 1974). Nao Amando na wengine (2007) wanasema kuwa uwezo mdogo wa wanafunzi wa kutekeleza kile anachofundishwa hutokana mara nyingi na uwezo mdogo wa wale wanaofundisha au vifaa vinavyotumiwa. Katika hali hii, ufundishaji ndio unaathiri lugha kadirifu ya mwanafunzi au kuchochea miundo mibovu anayoitumia. Kwa hivyo, utafiti wetu ulichunguza pia uwezo wa walimu wanaofundisha Kiswahili kwa kuwauliza maswali tofauti kuhusu kiwango chao cha masomo na tajiriba waliyo nayo katika ufundishaji wa lugha hii. Swali la kwanza lilihusiana na kiwango chao cha masomo ya ualimu.

**Jedwali 4.3: Kiwango cha masomo cha walimu**

| Kiwango cha masomo | Masomo | Jumla /3 | % |
|---|---|---|---|
| $A_2$ | Lugha za Kisasa | 3 | 33.3 |
| $A_1$ | Kiswahili | 2 | 66.7 |
| $A_0$ | Utangazaji na mawasiliano | 2 | 66.7 |

Kama tunavyopata katika Jedwali 4.3, walimu wote walibainisha kuwa walijifunza masomo ya Kiswahili katika elimu yao ingawa ni kwa viwango tofauti. Katika shule za upili, wote walijifunza Kiswahili. Wawili waliendelea na somo hili mpaka kiwango cha stashahada. Miongoni mwa walimu wote, wawili ndio waliweza

kuhitimu na kuipata shahada yao ya kwanza katika Utangazaji na mawasiliano kwani mwalimu mwingine alikuwa hajamaliza shahada yake ya kwanza wakati tulipokuwa tukikusanya data yetu. Kwa hivyo, hakuna mwalimu hata mmoja aliyekuwa na shahada yake ya kwanza katika somo la Kiswahili.

Kuhusiana na tajiriba ya walimu hawa wa Kiswahili, majibu tuliyoyapata kwa hojaji zao ndiyo haya yamewasilishwa katika Jedwali 4.4.

**Jedwali 4.4: Tajiriba ya walimu**

| **Tajiriba ya walimu katika ufundishaji wa Kiswahili** | **Jumla /3** | **%** |
|---|---|---|
| Miaka 0-2 | 0 | 0 |
| Miaka 2-5 | 2 | 66.6 |
| Zaidi ya miaka 5 | 1 | 33.3 |

Matokeo katika jedwali hili yanadhihirisha kuwa mwalimu mmoja ndiye amefundisha lugha ya Kiswahili kwa muda wa zaidi ya miaka mitano wakati ambapo wengine wawili walifundisha lugha hii kwa muda wa miaka kati ya miwili na mitano.

Swali jingine waliloulizwa walimu lilihusu vitabu vya kufundishia sarufi ya Kiswahili ambapo wote walituelezea kwamba walikuwa na tatizo kubwa la ukosefu wa vitabu vinavyoweza kukidhi mahitaji yao katika ufundishaji wa sarufi. Walimu hawa walisisitiza kwamba wao hukutana na changamoto ya kupata vitabu tofauti vya kuandaa masomo ipasavyo. Kwa hivyo, walituorodheshea vitabu vifautavyo ambavyo ndivyo walikuwa wakitumia kufundishia sarufi ya Kiswahili.

**Jedwali 4. 5: Vitabu vilivyotumiwa na walimu katika ufundishaji wa sarufi**

| Mwandishi | Mw aka | Kitabu | Mchapishaji | Wali mu /3 |
|---|---|---|---|---|
| Ahmed N. | 1997 | Matumizi ya Kiswahili | E.A.E.P. (Nairobi) | 1 |
| Gichohi W. | 1983 | Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili | Longhorn Publishers | 1 |
| Kabugi C.M. | 1997 | Tujifunze Kiswahili | FEP International | 1 |
| Kapinga C. | 1999 | Sarufi Maumbo ya Kiswahili | TUKI | 1 |
| Mgullu S. R. | 1999 | Mtalaa wa isimu | Longhorn Publishers | 1 |
| Nkwera F. | 1978 | Sarufi na Fasihi. Sekondari na vyuo | TPH | 1 |
| Niyomugabo C. | 2013 | Mafunzo ya Kiswahili, kidato 4 | Fountain Publishers | 3 |
| Niyomugabo C. | 2013 | Mafunzo ya Kiswahili, kidato 5 | Fountain Publishers | 3 |
| Niyomugabo C. | 2013 | Mafunzo ya Kiswahili, kidato 6 | Fountain Publishers | 3 |
| Wizara ya Elimu | 1986 | Kitabu cha Kiswahili, I | Wizara ya Elimu | 1 |
| Wizara ya Elimu | 1984 | Kitabu cha Kiswahili, II | Wizara ya Elimu | 1 |
| Wizara ya Elimu | 1987 | Kitabu cha Kiswahili, III | Wizara ya Elimu | 1 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kulingana na matokeo katika jedwali 4.5, ni wazi kwamba kuna uhaba wa vitabu vinavyoweza kusaidia walimu kufundisha sarufi ya Kiswahili. Walimu wote walibainisha kuwa vitabu vya mafunzo ya Kiswahili vilivyotayarishwa na Niyomugabo Cyprien na kuidhinishwa na Wizara ya Elimu ndivyo viliwasaidia sana kufundishia sarufi kwani viliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Kiswahili uliotolewa na Wizara ya Elimu na kusambazwa katika shule zote zinazofundisha Kiswahili.

Vitabu vingine vinavyobaki katika orodha hiyo, ingawa navyo vingesaidia sana, vilitajwa na mwalimu mmoja tu kwani ni vitabu ambavyo havikupendekezwa na serikali kufunzia Kiswahili. Kwa hivyo, uchunguzi wetu ulitubainishia kwamba shule zenye miundo msingi bora ndizo zilizoweza kujitafutia vitabu vingine ambavyo havikupendekezwa na serikali ili kusaidia wanafunzi wao. Mbali na vitabu vilivyosambazwa na serikali, walimu wengi walituambia kwamba hawakuwa na uwezo wa kujitafutia vitabu vingine. Kutokana na hayo, mtafiti alipenda kujua ikiwa vitabu hivyo walivyovitumia viliweza kukidhi haja yao ya kufundisha sarufi ya

Kiswahili au ikiwa kuna kasoro zozote wanazozitambua katika vitabu hivyo. Maoni yao ndiyo tumewasilisha katika Jedwali 4.6.

**Jedwali 4.6: Maoni ya walimu kuhusu vitabu vya sarufi wanavyovitumia**

| Maoni ya walimu | Jumla | % |
|---|---|---|
| Vitabu ninavyovitumiwa havinitoshelezi | 3 | 100 |
| Vitabu ninavyovitumia vinanitosheleza | 0 | 0 |
| Vitabu ninavyovitumia havina kasoro yoyote | 1 | 33.3 |
| Vitabu ninavyovitumia vina kasoro mbalimbali | 2 | 66.6 |

Usuli: Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kulingana na majibu ya walimu kuhusiana na vitabu walivyovitumia, maoni yaliyowasilishwa katika jedwali hapo juu, yanatubainishia kwamba walimu wengi hawakuridhika na vitabu walivyokuwa navyo. Asilimia 100 walihakikisha kwamba vitabu vile vilikuwa vichache mno, 33% walisema kuwa vitabu walivyokuwa navyo havikukuwa na kasoro zozote na 66.6% wakadhihirisha kwamba kasoro mbalimbali zilijitokeza. Mbali na uhaba wa vitabu vya kufunzia sarufi walivyokuwa navyo, maelezo ya walimu yalidhihirisha pia kwamba wanafunzi wao hawakuweza kupata magazeti na vitabu vingine vya kusoma kama vile riwaya, hadithi fupi, tamthilia, mashairi, na kadhalika.

Kwa hakika, uchunguzi wetu kuhusu maoni haya ya walimu ulitudhihirishia kwamba walimu walikuwa wakikumbana na changamoto ya kupata vifaa vinavyohitajika kufundisha lugha ya pili kama vile vitabu, rekodi na magazeti na kuwa hali hii iliathiri sana kiwango cha ufundishaji wao. Walimu hawa walisisitiza kwamba wanafunzi wao hawangeweza kuzoea kutumia miundo changamano ya Kiswahili kwani hawakupata fursa ya kutosha ya kusoma vitabu mbalimbali. Kwa hivyo, walishikilia kwamba makosa mengi ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi

wao yalitokana na uzoefu mdogo wa kutumia Kiswahili na ukosefu wa vifaa vinavyohitajika.

Mbali na hayo, mtafiti alipenda kujua maoni ya walimu kuhusiana na mpangilio wa vipengele vya kufundisha katika silabasi waliyoifuata. Majibu waliyoyatoa ndiyo haya tumewasilisha katika Jedwali 4.7.

**Jedwali 4.7: Maoni ya walimu kuhusu mpangilio wa silabasi ya somo la Kiswahili**

| Maoni ya walimu | Jumla /3 | % |
|---|---|---|
| Vipengele vya kufundisha havifuatani vizuri | 2 | 66.6 |
| Vipengele vya kufundisha vinafuatana vizuri | 1 | 33.3 |
| Vipengele vya kisarufi vilivyopangwa ni vichache | 1 | 33.3 |
| Vipengele vya kisarufi vilivyopangwa ni vingi | 2 | 66.6 |

Usuli : Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kulingana na majibu yaliyotolewa na walimu katika Jedwali 4.7, ni dhahiri kwamba hawakubaliani na jinsi silabasi waliyoitumia ilivyopangwa. Mwalimu mmoja ndiye alisema kuwa vipengele vya kisarufi vinafuatana vizuri. Walimu wengine wawili, yaani 66.6%, walisema kuwa vipengele havifuatani vizuri. Kuhusiana na maoni haya, walimu hawa walijitetea wakisema kwamba mpangilio uliopo hauzingatii kwamba Kiswahili huanzia rasmi katika darasa la nne kiasi kwamba baadhi ya miundo changamani hutangulia ile iliyo rahisi. Kipengele cha ngeli kwa mfano hugusiwa kijuujuu katika mtazamo wa kimofolojia na muhtasari wa somo hili hautilii maanani kipengele cha upatanishi wa kisarufi ambacho ndicho kiini cha usarufi wa tungo za Kiswahili.

Kuhusiana na vipengele vya sarufi, walimu walisema kwamba mfuatano wake ulichanganya mambo ya kufundisha kiasi kwamba haukumsaidia sana mwanafunzi kujiongezea maarifa katika kuzungumza na kuandika Kiswahili fasaha hatua kwa

hatua. Walimu walitutolea mfano na kusema kuwa mada ya kwanza katika darasa la nne huihusu historia ya Kiswahili, ya pili fasihi ilhali wengi wa wanafunzi hawa huanza kujifunza Kiswahili katika darasa hili la nne kama tulivyobainisha hapo juu.

Aidha, ni vyema kudhihirisha hapa kuwa muhtasari wa somo la Kiswahili uliotolewa na Wizara ya Elimu (2010) unabainisha kuwa somo la Kiswahili huanzia darasa la kwanza la awamu ya kwanza ya shule za upili, lakini kuwa wanafunzi wengi hutangulia ujifunzaji wa lugha hii katika darasa la nne. Walimu walitubainisha kwamba hata na wanafunzi waliokuwa wamejifunza Kiswahili katika madarasa ya awamu ya kwanza hawangeweza kukabili miundo changamani iliyopendekezwa katika silabasi ya awamu ya pili. Jambo hili lilitokana na hali kuwa katika awamu ya kwanza, somo la Kiswahili halikuwa la somo lazima na halikutahiniwa.

Kulingana na hali hiyo, wanafunzi waliobahatika kujifunza lugha hii katika awamu hiyo ya kwanza hawakuweza kuiona kama lugha iliyoweza kuwa na manufaa kwao. Hali hii ilitolewa mkazo pia na baadhi ya viongozi wa shule walioweza kuwagawia walimu fulani somo la Kiswahili bila kujali uwezo wao katika ufundishaji wa lugha hii, bali kwa kukamilisha masaa yaliyotakikana kwenye ratiba zao za masomo. Pengine, walimu watafitiwa walisisitiza kuwa shule zingine hazikuwa na somo hili la Kiswahili katika awamu ya kwanza kiasi kwamba walikumbana na changamoto kubwa kwa kufundisha wanafunzi wenye viwango tofauti katika darasa la nne.

Isitoshe, walimu hawa walibainisha kwamba muda uliotengewa kufundishia lugha hii ulikuwa mfupi sana na kutuelezea kwamba baadhi ya wanafunzi wao waliweza kuhitimu masomo yao ya shule za upili bila kuweza kuandika na kuzungumza lugha

hii. Mwalimu mmoja, yaani 33.3%, ndiye alituelezea kuwa vipengele vya kisarufi vya kufundisha vilikuwa vichache kwani wengine 66.6% walisema kuwa mbali na kuwa vipengele hivyo havikupangwa vizuri, vilikuwa pia vingi na changamani mno ikizingatiwa kuwa vilitakiwa kufundishwa kwa muda wa miaka mitatu tu. Kwa hivyo, walisema kuwa vipengele vilivyopaswa kufundishwa katika silabasi hiyo havikuwiana na muda uliotengewa ufundishaji wa Kiswahili.

Kulingana na maelezo hayo, hatuna budi kudhihirisha kwamba makosa mengi ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi Wanyarwanda katika ujifunzaji wao wa Kiswahili yalitokana na uhamishaji wa ufundishaji kama tunavyopata kutokana na nadharia ya LK. Matokeo ya utafiti huu yametubainishia kwamba wanafunzi hawa huathiriwa na jinsi wanavyofundishwa pamoja na vifaa vinavyotumiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wao wa lugha hii. Miundo potofu iliyojitokeza katika lugha yao kadirifu iliathiriwa na uwezo mdogo wa walimu na uhaba wa vifaa vya kufundishia; jambo lililokuwa limebainishwa pia katika utafiti uliofanywa na Kimenyi (2003).

Vilevile, utafiti huu umedhihirisha kuwa mpangilio wa silabasi hauwarahisishii wanafunzi kuelewa na kutumia Kiswahili kwa usahihi kutokana na mfuatano usiofaa wa vipengele vya kufundishia lugha hii, wingi na uchangamani wake hasa ikizingatiwa muda wa miaka mitatu iliyotengewa ufundishaji wa Kiswahili katika shule za upili. Mielekeo ya baadhi ya viongozi wa shule nayo ni mojawapo ya mambo mengine yaliyoweza kuzorotesha ufundishaji wa Kiswahili kwani wengi wao hawajaelewa umuhimu na nafasi yake. Baadhi ya shule za upili hazichagui

kufundisha Kiswahili kama somo lisilo la lazima na pale kinapofundishwa viongozi wengine hawajali kutafuta walimu wenye uwezo wa kukifundisha.

## 4.2 Utambuzi wa makosa ya wanafunzi na chanzo chake

Kulingana na nadharia ya UM, ni vyema kutathmini makosa yanayofanywa na wanafunzi ili kudhihirisha mikakati inayoweza kuzingatiwa na walimu katika kuyapunguza makosa hayo. Ellis (1994) anasema kuwa uchunguzi wa makosa ya mwanafunzi humsaidia mwalimu kutathmini ufundishaji wake na kufanya mipango ya masomo ya baadaye. Kwa hivyo, ingawa kazi hii haikuhusu mbinu za ufundishaji, mtafiti aliuliza walimu maswali mbalimbali yaliyomwezesha kuchunguza jinsi walivyoweza kutambua makosa ya wanafunzi wao na kuyasahihisha ili kuyapunguza.

Swali la kwanza lilitaka kujua maoni ya walimu hawa kuhusu vipengele vya sarufi vilivyowatatiza wanafunzi wao katika ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili. Kwa hivyo, maoni yao yalihifitilafiana lakini wote walituelezea kwamba kipengele cha ngeli ndicho cha kwanza kuwatatiza wanafunzi wengi. Aidha, walitubanishia kuwa matatizo mengine ya wanafunzi yalikitegemea sana kipengele hiki kiasi kwamba walikiona kama nguzo ya kuwawezesha wanafunzi wao kutumia Kiswahili fasaha. Jedwali 4.7 linaonyesha jinsi wanafunzi wao walivyotatizika katika kipengele hiki.

**Jedwali 4.8: Maoni ya walimu kuhusu ngeli zinazotatiza wanafunzi**

| Kipengele cha kisarufi | Jumla /3 | % |
|---|---|---|
| a-wa | 2 | 66.6 |
| li-ya | 2 | 66.6 |
| pa-mu-ku | 3 | 100 |
| U | 2 | 66.6 |
| u/i-zi | 2 | 66.6 |
| u-i | 1 | 33.3 |

Usuli : Matokeo ya utafiti wetu, 2014



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Kulingana na maoni ya walimu katika Jedwali 4.8, ni dhahiri kuwa ngeli ya *{pa-mu-ku}* ndiyo ya kwanza kuwatatiza wanafunzi. Asilimia 100 ya walimu wote walituelezea kwamba wanafunzi wao hushindwa kutumia viambishi mwafaka wanapotakiwa kutofautisha mahali panapozunguziwa kwa kuwa wengi huvichanganya viambishi vya mahali. Ngeli ya kwanza ya *{a-wa}* nayo ilibainishwa kama ngeli yenye utata mkubwa hasa kuhusu majina ya wanyama kama tulivyoambiwa na walimu 66.6%. Mwalimu mmoja ndiye alituelezea kwamba ngeli hii haiwakanganyi wanafunzi wake.

Ngeli ya *{li-ya}* nayo ilirejelewa na walimu 66.6% kama ngeli iliyoleta changamoto kwa wanafunzi wao hasa wanapotakiwa kutumia majina ya ngeli hii pamoja na vivumishi vya sifa au wanapotakiwa kutumia miundo ghairi kama vile *jiwe/mawe*. Wanafunzi wao hupendelea kwa mfano kutumia muundo *majiwe* kwa kujumuisha kanuni ya kuziweka nomino za ngeli hii katika wengi ambapo kiambishi {ma} hupachikwa kwa mzizi wa nomino husika. Mwalimu mmoja ndiye alituelezea kwamba ngeli hii haileti changamoto yoyote kwa wanafunzi wake. Ngeli ya *{u}* yenye umbo lisilobadilika nayo ilirejelewa na walimu 66.6% kama iliyotatanisha wanafunzi katika ujifunzaji wao. Mwalimu mmoja ndiye alisema kwamba ngeli hii haibainishi utata wowote katika ufundishaji wake.

Nayo ngeli ya *{u/i-zi}* huwakanganya wanafunzi kama tulivyoelezewa na walimu 66.6%. Walimu hawa walituelezea kwamba wanafunzi wao wanapotumia nomino kama *nguo*, *nyumba*, na kadhalika, baadhi yao huziendeleza katika wingi kama wanavyofanya kuhusu majina mengine ya ngeli ya sita. Kwa hivyo, waliweza

kuibuka na miundo kama vile *nguo/manguo* na *nyumba/manyumba* na hali hii iliathiri upatanishi wa kisarufi ulioutumiwa katika sentensi zao.

Swali lingine lilihusu kuchunguza ikiwa walimu walijua chanzo cha makosa ya wanafunzi wao ili waweze kuwaelekeza na kuwafanya wayaepuka makosa hayo au kuyapunguza. Majibu waliyotupa ndiyo haya yafuatayo katika Jedwali 4.9.

**Jedwali 4.9: Maoni ya walimu kuhusu chanzo cha makosa ya kimofosintaksia**

| Chanzo cha makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi | Jumla /3 | % |
|---|---|---|
| Muda mfupi uliotengwa kufunzia Kiswahili | 3 | 100 |
| Kufanana kwa baadhi ya miundo ya Kinyarwanda na ya Kiswahili | 3 | 100 |
| Tajiriba ndogo na ujuzi mdogo wa walimu wanaofunza Kiswahili | 2 | 66.6 |
| Mielekeo hasi ya watu kuhusu Kiswahili | 2 | 66.6 |
| Ukosefu wa vifaa vya kufunzia lugha hii | 3 | 100 |
| Mazingira ambamo wanafunzi husomea | 2 | 66.6 |

Usuli : Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kulingana na majibu tuliyoyapata kutoka kwa walimu, ni wazi kwamba wote waliafikiana kwamba muda uliotengewa kufundisha lugha hii ni mfupi sana. Wote walitueleza kwamba miaka mitatu ya kufundisha lugha hii ni michache sana. Wizara ya Elimu (2010) inabainisha kuwa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili huanzia darasa la nne la shule za upili mpaka darasa la sita. Katika kipindi hiki, mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo yote yanayotakikana ili aweze kuitumia ipasavyo kwani lengo kuu la ufundishaji wa Kiswahili ni kumpa mwanafunzi uwezo wa kutumia lugha hii katika shughuli mbalimbali za kitaifa na kimataifa, miongoni mwa malengo mengine mengi (Wizara ya Elimu).

Vilevile, walimu wote waliouIizwa walituelezea kwamba kufanana kwa baadhi ya miundo ya Kinyarwanda na ile ya Kiswahili kuliwafanya wanafunzi wengi wafikiri

kwamba lugha hizi hazina tofauti. Kwa hivyo, walimu hawa walibainisha kuwa wanafunzi wao waliweza kufanya makosa kwa kuhamisha miundo mbalimbali ya Kinyarwanda katika matumizi yao ya Kiswahili. Walimu 66.6% ndio walitubainishia kwamba ujuzi mdogo wa walimu nao ulikuwa chanzo cha makosa yaliyofanywa na wanafunzi. Katika maelezo yao walisema kwamba walimu hawakupata mafunzo ya muda mfupi ili waweze kujiongezea maarifa katika kazi yao ya ufundishaji. Amando na wengine (2008) anaeleza kuwa ili uchunguzi wa makosa ya mwanafunzi uwezekane ni lazima walimu wawe na ujuzi mkubwa wa eneo linalofundishwa, uzoefu wa kutosha katika shughuli ya ufundishaji na ujuzi kuhusu hali za kisaikolojia za wanafunzi wao.

Swala la mielekeo hasi ya baadhi ya watu kuhusu Kiswahili nalo lilibainishwa kama chanzo cha makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi. Katika kufafanua chanzo hiki cha makosa, walimu walitubainishia kwamba baadhi ya viongozi hudhalilisha na kudunisha Kiswahili kama tulivyobainisha katika (§4.1.9). Mielekeo hii pia ndiyo huwafanya baadhi ya viongozi wa shule hizi wasione kwamba vifaa vingine huhitajika ili kuwasaidia walimu wao katika ufundishaji wa Kiswahili. Mwalimu mmoja alilalamika na kutueleza haya yanayofuata:

> « *Viongozi wetu wanajua kwamba lugha ya Kiingereza ndiyo lugha tu; hawajaelewa umuhimu wa lugha ya Kiswahili (...) wanapaswa kuelewa kwamba Kiswahili ndiyo lugha yetu ya Kiafrika tunayostahili kuendeleza (....) Mtu anaweza kuishi miaka 50 bila kuvuka bara la Afrika, lakini ni vigumu afikie umri huo bila kuvuka nchi yetu kama mwananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki* ».

Swala la ukosefu wa vitabu vya sarufi lilionekana kuwakera sana walimu wote walioulizwa na kulibainisha kama chanzo kikubwa cha makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Walimu hawa

walibainisha kwamba hili lilikuwa tatizo kubwa lililofaa kusuluhishwa kabla ya mengine ili Kiswahili kipate kuendelea. Mbali na kuwa vitabu vya sarufi walivyokuwa navyo havikuwatosheleza, walimu hawa walisema pia kwamba vitabu hivyo vingesaidiwa na vitabu vingine vya kusoma, kama vile riwaya, tamthilia au magazeti mbalimbali yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili. Walituelezea kuwa wanafunzi wao wangepata uzoefu wa kutumia lugha ya Kiswahili kwa kusoma vitabu hivyo vya fasihi kwani ndivyo vinazingatia miundo mbalimbali ya lugha hii ambayo wangeweza kuiga na kuitumia katika mazungumzo na maandishi yao.

Kwa hivyo, uchunguzi wa majibu na maelezo tuliyopata kutoka kwa walimu, ulitubainishia kwamba wengi wao walifahamu chanzo cha makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi wao. Ujumuishaji wa vipengele, uhamishaji wa miundo ya Kinyarwanda katika Kiswahili na uhamishaji wa ufundishaji ndio uliozingatiwa sana kama chanzo cha makosa ya wanafunzi.

Hata hivyo, majibu waliyoyatoa yalidhihirisha kwamba wengi hawakuweza kuyaainisha makosa yote yaliyofanywa na wanafunzi wao ili waweze kuandaa jinsi ya kuyarekebisha au kuyapunguza kwa namna inayofaa. Makosa mengi yaliyobainishwa na walimu hawa yalijikita tu katika matumizi ya baadhi ya ngeli lakini hawakuweza kudhihirisha matatizo yenyewe kikamilifu na vipengele vya matumizi ya ngeli vinavyowatatiza. Wengi waliishia tu kuziorodhesha ngeli walizozifikiria kuwa zilileta changamoto kwa wanafunzi na kutoa maelezo ya kijumla kiasi kwamba tuling'amua kwamba walikuwa hawajaweza kuyachunguza makosa ya wanafunzi wao kikamilifu. Amando na wengine (2007) wanasema kuwa ni lazima

walimu washughulikie sababu ya makosa ya wanafunzi wao na jinsi wanavyoweza kuyasahihisha baada ya kuyaeleza au kuyaainisha.

### 4.3 Mikakati ya kupunguza makosa ya wanafunzi

Swali jingine lililoulizwa walimu lilitarajia kumpa mtafiti habari kuhusu mikakati iliyozingatiwa na walimu wa Kiswahili ili kupunguza makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi wao. Kwa hivyo, majibu waliyoyatoa ndiyo yamewasilishwa katika jedwali lifautalo :

**Jedwali 4.10: Mikakati ya walimu ya kupunguza makosa ya kimofosintaksia**

| **Mikakati inayozingatiwa** | **Jumla /3** | **%** |
|---|---|---|
| Mazoezi ya kisarufi darasani | 3 | 100 |
| Mazoezi darasani kuhusu utunzi wa insha | 2 | 66.6 |
| Mazoezi ya masimulizi kwa kila mwanafunzi kuhusu jambo analojichagulia mwenywe | 1 | 33.3 |
| Uundaji klabu na mazoezi ya maongezi darasani | 3 | 100 |
| Mazoezi ya kuandika au kazi za kufanyia nyumbani | 2 | 66.6 |
| Kuwaelezea wanafunzi kuhusu umuhimu wa Kiswahili | 1 | 33.3 |
| Kusahihisha kazi za wanafunzi na kuandika maelezo ya makosa waliyoyafanya | 1 | 33.3 |

Usuli : Matokeo ya utafiti wetu, 2014

Kulingana na majibu katika Jedwali 4.10, ni dhahiri kwamba walimu wote walisisitiza kuhusu mambo matatu yanayozingatiwa kuyapunguza makosa yanayofanywa na wanafunzi wao. Mazoezi ya kisarufi darasani ndilo jambo la kwanza linalofanywa na walimu katika jitihada zao za kuyapunguza makosa ya kimofosintaksia. Shughuli nyingine iliyotekelezwa na walimu hawa ilihusu kuwapatia fursa wanafunzi wao ili wajizoeze kuongea Kiswahili darasani.

Asilimia 66.6 ya walimu walituelezea kwamba mzoezi ya utunzi wa insha ni mojawapo ya mbinu wanazozitumia kupunguza makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi. Mwalimu mmoja, yaani 33.3%, ndiye aliyebainisha kwamba kila

mwanafunzi anapewa muda, angalau mara moja kwa muhula, ili awasimulie wanafunzi wenzake kuhusu jambo lolote alilowatayarishia mwenyewe. Katika hali hii, mwalimu aliweza kuwajibika kwa kumsahihishia mwanafunzi huyo makosa yote aliyoyafanya katika maongezi yake kwa kuwashirikisha pia wanafunzi wengine.

Vilevile, walimu wote walituelezea kwamba walianzisha klabu za Kiswahili katika shule zao kama njia iliyoweza kuwasaidia wanafunzi kujizoeza kutumia Kiswahili ipasavyo. Asilimia 66.6 ya walimu walisisitiza kwamba kazi za nyumbani ziliwasaidia wanafunzi wao kufanya marudio ya vipengele vya kisarufi ili kuendelea kukuza uwezo wao wa kutumia lugha hii kwa njia sahihi. Mwalimu mmoja, yaani 33.3%, alisema kwamba aliweza kuingiza mada kuhusiana na umuhimu wa Kiswahili ili kuwachochea wanafunzi wake waipende lugha hii na kuitumia ipasavyo.

Kuhusiana na uchunguzi wetu, ni wazi kwamba mikakati mingi huchukuliwa na walimu katika jitihada zao za kuyapunguza makosa ya wanafunzi wao. Mazoezi mbalimbali na uundaji wa klabu ni jambo zuri lililozingatiwa na walimu wote waliooulizwa. Vilevile, uzingativu wa kipengele cha kuingiza mada zinazoelekea kuinua mielekeo kuhusu lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi ni muhimu hasa wakati wa ufundishaji wao ingawa kilidokezwa na mwalimu mmoja, yaani 33.3%. Amando na wengine (2007) wanapendekeza kuwa ufundishaji peke yake hauwezi kutosheleza ikiwa walimu hawalengi kuwahimiza wanafunzi wao na kuwapa mawaidha yanayoweza kuwasaidia kulewa kile wanachokifanya na kuchochea utashi wao wa kujiendeleza katika shughuli yao ya kusoma.

Kazi mbalimbali zilizofanywa kuhusu ujifunzaji wa L2 kama vile Steinberg na wengine (1982) na Ellis (1985) zinaelekea kukubaliana kwamba utangamano kati ya mwalimu na mwanafunzi ni muhimu pale ambapo mwanafunzi hupewa muda wa kutosha wa kufanya mazoezi katika stadi ya kimazungumzo na ya kimaandishi. Mazoezi haya ndiyo yanamsaidia mwanafunzi kuelewa na kutumia ipasavyo kanuni za lugha anayojifunza. Kwa hivyo, ni vyema kwamba walimu wote walioulizwa walituelezea kwamba mazoezi ya aina hii ni muhimu sana katika kuyapunguza makosa wanayoyafanya wanafunzi wao. Hata hivyo, ni lazima waelewe kwamba jinsi wanavyotoa mchango katika kusahihisha makosa ya wanafunzi wao na nafasi inayopewa wanafunzi wengine ni nguzo kubwa katika kuwazoeza wanafunzi wao kutambua wao wenyewe makosa wanayoyafanya.

Isitoshe, kulingana na uchunguzi wa maoni tuliyotolewa na walimu kuhusu swala la mikakati waliyoizingatia kupunguza makosa ya komofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wao, ni wazi kwamba walimu hawa hawakutilia maanani hatua za kuyatambua na kuyaeleza makosa ya wanafunzi wao. Walisahihisha makosa kila mara yalipotokea katika kazi za wanafunzi lakini hawakupata muda wa kushughulikia makosa yaliyofanywa na wanafunzi hao, kuyatathmini na kuelewa kiwango cha utokeaji wake. Ellis (1994) anabainisha kuwa uchunguzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi ndiyo njia nzuri ya kumwezesha mwalimu kuyarekebisha na kuwahimiza wanafunzi wake wasiyarudie.

Kulingana na nadharia ya UM iliyoelekeza utafiti huu, mwalimu anatakiwa kueleza makosa ya wanafunzi wake, vyanzo vya makosa hayo ili aweze kuchukua hatua

zinazofaa katika ufundishaji wake wa baadaye. Makosa huzungumziwa darasani kwa kuwashirikisha wanafunzi wote katika usahihishaji wa kazi zao, kujitathmini na kujirekebisha wao wenyewe wakielekezwa na mwalimu. Jambo hili ndilo hurejelewa pia na Amando na wengine (2007) wanaposema kuwa mwalimu huweza kurahisisha kazi hii kwa kuwapanga wanafunzi katika makundi ambapo kila mwanafunzi atatambua kosa la mwenzake na kulisahihisha au kundi moja likasahihisha makosa ya kundi jingine. Vilevile, Amando na wengine wanapendekeza kuwa jambo hili lingewasaidia wanafunzi kujihakiki wao wenyewe na kuhakiki kazi za wengine hata wakati mwalimu hayupo katika kazi wanazozifanya wao wenyewe.

Kutokana na majibu tuliyoyapata kutoka kwa walimu, tulitambua kwamba kazi za vikundi hazikuzingatiwa sana kama mojawapo ya mikakati iliyoweza kurahisha upunguzaji wa makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi. Amando na wenzake (keshatajwa) wanasema kuwa kupitia mazoezi ya aina hii, maswala mengi huweza kuchunguzwa na mwalimu hutoa maelezo kijumla. Maelezo haya huwa mwafaka sana kuliko yale yanayoandikwa katika daftari la mwanafunzi mmoja kwani haya husomwa na mwanafunzi mmoja.

**4.3 Hitimisho**

Sura hii imebainisha chanzo cha makosa yaliyofanywa na wanafunzi na kutathmini mikakati iliyozingatiwa na walimu kwa ajili ya kupunguza makosa hayo. Kwa hivyo, tumedhihirisha kuwa makosa mengi ya kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi yalitokana na uhamishaji, kuchanganya ndimi, utohozi isiofaa, tafsiri, kutojali, uzoefu mdogo wa kutumia Kiswahili, ukosefu wa habari na ujumuishaji. Sura hii pia



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

imezungumzia na kutathimini mikakati iliyozingatiwa na walimu ili kuyapunguza makosa ya wanafunzi wao. Katika sehemu hii, tumebaisha kuwa walimu walichukua hatua mbalimbali kwa kusahihisha makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi wao kama vile kuwapatia mazoezi ya aina mbalimbali yakiwemo mazoezi ya uandishi na maongezi. Hata hivyo, tumeonyesha kuwa walimu hawa hawakutilia mkazo nafasi ya mwanafunzi katika kutambua na kuelewa makosa aliyoyafanya na yale yaliyofanywa na wenzake. Tumethibitisha kuwa hali hii ndiyo ingesaidia kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kujihakiki mwenyewe na kuzihakiki kazi za wenzake na hatimaye kujisahihisha mara tu anapofanya makosa.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura zilizotangulia tumechunguza makosa ya kimofosintaksia yanayowakumba wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda. Sura hii imehitimisha utafiti huu kwa kutoa muhtasari wa tasnifu nzima, matokeo ya utafiti, changamoto tulizozipitia na mapendekezo kadhaa kuwahusu washikadau mbalimbali wa elimu na wa ufundishaji wa Kiswahili.

## 5.2 Muhtasari wa utafiti

Utafiti huu ulinuia kuchunguza changamoto za kimofosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda. Kwa hivyo, lengo kuu la kazi hii lilikuwa kuchanganua lugha kadirifu ya wanafunzi kwa kubainisha matatizo wanayokumbana nayo katika ujifunzaji wao wa Kiswahili na mikakati inayozingatiwa na walimu wao ili kupunguza makosa yanayofanywa na wanafunzi wao. Data iliyotumiwa ilikusanywa nyanjani kupitia hojaji na mahojiano yaliyofanywa kwa kushirikisha wanafunzi wa Kiswahili wa shule tatu teule na walimu wao.

Nadharia za UM na LK ndizo zilizoongoza mtafiti katika kazi hii. Nadharia ya kwanza ilitumika kubainisha makosa, kuyaeleza na kuyathamini ili kuchunguza vyanzo vyake. Nayo nadharia ya pili imechangia pakubwa kwa kuchunguza mikakati ya kisaikolojia anayoitumia mwanafunzi katika jitihada zake za ujifunzaji wa

Kiswahili ambapo makosa ya kimofosintaksia hutokea kadiri lugha kadirifu yake inavyobadilikabadilika.

Ili kuandaa vifaa vya utafiti vilivyomwezesha mtafiti kupata data faafu, jaribio la utafiti lilifanywa katika shule ya Groupe Scolaire de Cyeza. Kwa hivyo, utafiti huo mdogo ulimsaidia mtafiti kupanga vizuri maswali yaliyotolewa kwa wanafunzi na walimu wa shule tatu teule wilayani Muhanga: Groupe Scolaire de Kirwa, Groupe Scoaliare de Nyarusange na Groupe Scolaire de Shyogwe. Vilevile, jaribio hili la utafiti ndilo lilimpa mtafiti hamu ya kuunda swala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchangua mada, upeo na mipaka pamoja na mbinu zilizotumika ili kufanikisha utafiti huu. Matumizi ya maktaba yalimwezesha pia mtafiti kuwa na ujuzi mpana katika uwanja wa ujifunzaji wa L2 kwa jumla na kuelewa eneo la utafiti kwa kusoma nadharia mbalimbali na yaliyoandikwa kuhusu mada.

Katika sura ya kwanza, vipengele muhimu ambavyo ndivyo msingi wa utafiti huu vimezungumziwa. Usuli wa mada umebainisha jinsi ambavyo mada hii ilivyoibuka, malengo na misingi ya nadharia zilizoelekeza utafiti huu zimedhihirishwa, yaliyoandikwa kuhusu mada yalibainisha uhusiano na tofauti kati ya utafiti huu na tafiti zingine zilizoutanguliana. Mbinu za utafiti zilizozungumziwa katika sura hiyo zimeangazia mwelekeo tuliouzingatia katika utafiti huu na jinsi tulivyoushughulikia ili kukidhi haja yetu ya kuzichunguza changamoto za kimofosintaksia zilizowakumba wanafunzi watafitiwa. Kwa hivyo, misingi ya nadharia za UM na LK imefafanuliwa kwa kuonyesha jinsi ilivyomwongoza mtafiti katika kazi yake.

Katika sura ya pili, mtafiti alidhihirisha mofosintaksia ya ngeli za Kiswahili na Kinyarwanda kwani ngeli ndizo nguzo katika ujifunzaji wa mofosintaksia ya lugha hizi. Mtafiti alifikiria kuwa wanafunzi wengi Wanyarwanda wanaojifunza Kiswahili katika shule za upili waliweza kukutana na changamoto za kimofosintaksia ambapo athari za L1 hujitokeza katika lugha yao kadirifu. Kwa hivyo, ilikuwa vyema mifumo ya ngeli za lugha ya Kiswahili na Kinyarwanda zizungumziwe na kulinganishwa ili kubashiri matatizo ya kimofosintaksia yaliyoweza kujitokeza katika ujifunzaji wa Kiswahili wa wanafunzi hawa.

Katika sura ya tatu, makosa ya kimofosintaksia yaliyofanywa na wanafunzi yalichunguzwa. Mtafiti alipanga makosa hayo katika kategoria tofauti kwa kuzingatia mazoezi matatu yaliyotolewa wanafunzi. Zoezi la kwanza lilihusu kuzikamilisha tungo mbalimbali kwa kutumia viambishi mwafaka vya upatanishi wa kisarufi. Zoezi la pili lilihusu utungaji wa insha ambapo wanafunzi walipewa mada "Ufugaji kijijini mwangu". Zoezi la tatu lilihusu masimulizi ya wanafunzi ambapo wanafunzi walisimulia kuhusu visa tofauti walivyovipenda. Kwa hivyo, sura hiyo ilichunguza makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi kwa kuyagawa katika vitengo tofauti vilivyozingatia pia kiwango cha utokeaji wa makosa hayo na idadi ya wanafunzi waliotatizika katika kila kategoria iliyochunguzwa.

Sura ya nne ya utafiti huu ilitathimini makosa yaliyofanywa na wanafunzi kwa kudhihirisha vyanzo vyake na kuchunguza mikakati iliyozingatiwa na walimu katika kuyapungua makosa hayo. Kwa kuwa lugha ya mwanafunzi hubadilikabadilika kutoka pale anapotumia miundo mibovu hadi pale ambapo lugha yake huelekea kuwa

sahihi, sura hii ilibainisha mikakati tofauti anayoizingatia mwanafunzi katika mchato huo wa ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 ambapo makosa mbalimbali ya kimofosintaksia hutokea.

Katika sura ya tano, mbali na kutoa muhtasari wa sura zilizotangulia, mtafiti amebainisha pia matokeo ya utafiti huu, changamoto alizokumbana nazo na kutoa mapendekezo kwa wadau mbalimbali wa ujifunzaji na ufundishaji wa Kiswahili nchini Rwanda.

### 5.3 Matokeo ya utafiti

Kazi hii ilinuia kuchunguza changamoto za kimofosintaksia zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, nchini Rwanda. Uchanganuzi ulifanywa kwa kuzingatia makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi wa Kiswahili katika shule tatu teule; Shule ya Groupe Scholaire ya Nyarusange, Shule ya Groupe Scolaire de Kirwa na Shule ya Groupe Scolaire de Shyogwe.

Kutokana na uchunguzi wetu, makosa mengi yalijitokeza katika kategoria ya mpangilio wa maneno katika tungo ambapo tumetambua tofauti ndogo kati ya lugha kadirifu ya wanafunzi wa darasa la tano na wa darasa la sita. Vilevile, kategoria ya urejeshi wa nomino katika vitenzi nayo ilionekana kuwatatiza wanafunzi wengi wa madarasa yote mawili.

Mazoezi ya masimulizi na la maandishi ndiyo yamedhihirisha makosa mengi katika kategoria hizi. Nalo zoezi la kuzikamilisha tungo kwa kutumia viambishi mwafaka lilidhihirisha kuwa baadhi ya ngeli huhitaji uangalifu mkubwa. Ngeli ambazo

zimeonekana kuwakanganya sana wanafunzi ni zile za kundi la *{pa, mu, ku}* zinazorejelea mahali, *{ku}* kuhusu vitenzijina, makundi ya *{a/wa}* kuyahusu majina yanayorejelea wanyama na ngeli zingine zenye majina yasiyoonyesha kiambishi chochote cha ngeli kama vile *chai, jangili, shamba* na kadhalika. Vilevile, miundo tofauti ya baadhi ya majina katika makundi mbalimbali ya ngeli nayo imebainisha changamoto kadha kwa wanafunzi. Majina kama *kipofu, jiwe, ukuta, ukubwa, ufa, koti,* na mengine yanakiuka utaratibu wa kawaida wa upatanishi wa kisarufi unaozingatia viambishi awali vya nomino yamewakanganya wanafunzi wengi katika utafiti huu.

Isitoshe, utafiti huu ulibainisha kuwa lugha kadirifu ya wanafunzi wa darasa la tano na wa darasa la sita huhitilafiana kidogo katika kipengele cha mpangilio wa maneno katika tungo zao. Asilimia 100 ya wanafunzi wa darasa la tano ikilinganishwa na 86.6% wa darasa la sita walikumbana na changamoto kubwa kuyapanga maneno katika maandishi yao. Aidha, zoezi la masimulizi ndilo lilibainisha matatizo mengi ya aina hii kwani wanafunzi wote kutoka madarasa yote walishindwa kuyapanga maneno kwa utaratibu unaofaa katika masimulizi yao. Wengi wao walikuwa wakiunda tungo ndefu mno zisizojali alama za vituo na uakifishaji kwa jumla ambapo walidondosha baadhi ya viunganishi na vihusishi au wakavitumia kwa njia isiyotarajiwa. Uchunguzi wa mazoezi yote matatu yaliyotolewa wanafunzi, ulitudhihirishia kwamba miundo ghairi ya vivumishi iliwatatiza wanafunzi wengi ambapo walishindwa kupatanisha nomino na vivumishi vya pekee na/au nomino na vivumishi vya sifa visivyochukua viambishi ngeli vya jina linalovumishwa kama vile *safi, tajiri, maskini*.

Kupitia utafiti huu, makundi saba ya makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi yamedhihirishwa: makosa ya uchopekaji wa vipashio katika tungo, udondoshaji wa vipashio katika tungo, mchanganyiko wa viambishi na matumizi ya viambishi visivyofaa, mchanganyiko wa aina za maneno, uradidi wa vipashio usiofaa katika tungo, uhamishaji wa vipashio, mpangilio mbaya wa maneno katika tungo na uundaji wa sentensi ndefu. Ubainishaji na uainishaji wa makosa yaliyofanywa na wanafunzi umefanywa kwa kuzingatia misingi ya nadharia za UM ambayo hushikilia kwamba makosa yabainishwe na kupangwa ili yaweze kuainishwa na kuelezwa.

Aidha, utafiti huu umebainisha chanzo cha makosa yanayofanywa na wanafunzi na kutathmini mikakati inayozingatiwa na walimu kupunguza makosa hayo. Uhamishaji wa vipengele vya sarufi kutoka L1 hadi Kiswahili umeonekana kuwa chanzo kikubwa cha makosa mengi ya wanafunzi. Kwa hivyo, uchunguzi wetu umeonyesha jinsi ambavyo LK ya wanafunzi Wanyarwanda ilivyozingatia miundo na vipatanishi vya kisarufi vya Kinyarwanda. Kuchanganya ndimi, utohozi isiofaa na upungufu wa msamiati, tafsiri, kutojali, uzoefu mdogo na ukosefu wa habari, ujumuishaji na uhamishaji wa ufundishaji ni mambo msingi yaliyodhihirishwa kama vyanzo vya makosa ya kimofosintaksia ya wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunza Kiswahili.

Isitoshe, utafiti huu umedhihirisha kwamba mikakati mbalimbali huzingatiwa na walimu ili kupunguza makosa ya wanafunzi wao. Mazoezi ya ya utunzi wa insha, yale ya masimulizi na ya kisarufi, usahihishaji wa makosa ya wanafunzi na uundaji wa klabu ni mambo muhimu yanayozingatiwa na walimu ili kuyapunguza makosa ya wanafunzi wao. Hata hivyo, utafiti wetu umethibitisha kwamba nafasi ya mwanafunzi



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

katika kuyatambua makosa anayoyafanya yeye mwenyewe na yale yanayofanywa na wenzake haizingatiwi kama njia muhimu ya kumsaidia mwanafunzi kupunguza makosa anayoyafanya. Kwa mujibu wa nadharia ya UM iliyoelekeza utafiti huu kwa kiwango kikubwa, ni lazima mwanafunzi apate nafasi ya kutosha ya kuchunguza makosa anayoyafanya mwenyewe. Jambo hili ndilo linampa uwezo wa kujihakiki na kuwahakiki wenzake kwa kuyatambua makosa yao na kuyasahihisha mara yanapotokea.

Mbali na hayo, ufanisi wa uchunguzi wa makosa ya wanafunzi kwa kuwashirikisha wanafunzi unamtaka mwalimu azingatie kazi za makundi. Kazi za aina hii ndizo zingeweza kuwasaidia walimu kuyafikia malengo mengi katika ufundishaji wao wa Kiswahili kwa kutumia muda mfupi na kushirikisha wanafunzi wengi zaidi katika kuelewa kiwango cha makosa wanayoyafanya, kuyachunguza na kuyaeleza kwa pamoja.

**5.4 Changamoto**

Mtafiti alipata changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa utafiti huu. Katika kuliunda swala la utafiti na malengo ya utafiti huu, ilimbidi mtafiti kuchukua muda mwingi kutembelea shule mbalimbali zinazofundisha Kiswahili ili kubashiri matatizo yaliyowakumba wanafunzi katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Vilevile, wanafunzi walifanya makosa mengi mno kiasi kwamba unukuzi, uainishaji na upangaji wake ulichukua muda mrefu.

Changamoto nyingine ilijitokeza pale ambapo baadhi ya wanafunzi hawakuweza kuzingatia moja kwa moja mawaidha waliyoyapata kutoka kwa mtafiti hasa kuhusu

jinsi walivyotakiwa kujihisi huru na kujibu maswali bila wasiwasi. Kwa hivyo, mtafiti alilazimika kwanza kujuika na wanafunzi hawa walipokuwa wakijifunza na baadaye kurudia mawaidha hayo na maelekezo mengine kila wakati alipotoa zoezi kwa wanafunzi wote. Jambo hili lilimfanya mtafiti achukue muda mrefu kuwatayarisha wanafunzi hawa na kuwaweka katika hali ambapo aliweza kukusanya data kama alivyonuia.

Mbali na hayo, kulikuwa na idadi ndogo ya wanafunzi ambao hawakuweza kuzungumza Kiswahili kwa kusingizia kwamba kiwango chao katika kuzungumza lugha hii kilikuwa kidogo mno. Kwa hivyo, ilimbidi mtafiti kuwachochea zaidi na kuendeleza mazungumzo yao kwa kuwauliza maswali kadhaa kuhusina na mada ambazo walikuwa wamejichagulia wao wenyewe na kuwapatia mifano mingine iliyoweza kuwasisimua zaidi. Hali hii ndiyo ilimsaidia kukusanya data kutoka kwao kwani kinasasauti kilikuwa tayari na kila mwanafunzi alipojaribu kujieleza kilikuwa kinafanya kazi.

Mwishowe, mtafiti alikutana na changamoto katika kuchunguza vyanzo vya makosa ambapo aliweza kutambua kwamba kosa moja laweza likachochewa na sababu nyingi au kosa la kimofosntaksia likaingiliana na kosa la aina nyingine. Kwa hivyo, ilimbidi achukue muda mwingi ili aweze kuchunguza vyema makosa ya aina hiyo. Ilimpasa kuirudia data mara kwa mara ili apate ushahidi wa kutosha wa kosa la mwanafunzi ili kuamua kuhusu chanzo chake.

## 5.5 Mapendekezo

Kulingana na matokeo ya utafiti wetu, tunaweza kuthibitisha kwamba mbali na mikakati ya kisaikolojia anayoizingatia mwanafunzi katika jitihada zake za ujifunzaji wa Kiswahili, changamoto nyingine nyingi za kimofosintaksia kwa wanafunzi wa shule za upili zina chanzo chake katika uhamishaji wa ufundishaji na mielekeo hasi ya baadhi ya watu kuihusu lugha hii. Hivyo basi, ukosefu wa vifaa vya kufundishia, mpangilio mbaya wa silabasi na uhaba wa walimu waliohitimu katika ufundishaji wa somo la Kiswahili umejitokeza kama mambo msingi yanayostahili kutafutiwa suluhisho ili Kiswahili kiweze kuimarishwa miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili nchini Rwanda. Kwa hivyo, kulingana na matokeo ya utafiti huu, mapendekezo yafuatayo yangepaswa kuzingatiwa.

### 5.5.1 Mapendekezo kuhusu serikali na viongozi wengine

Nchini Rwanda, Kiswahili hutumiwa kando ya lugha zingine ambazo ni Kinyarwanda ambayo ni lugha ya taifa na rasmi, Kiingereza na Kifaransa ambazo ni lugha rasmi. Kwa hivyo, serikali ya Rwanda ingepaswa kuinua hadhi ya Kiswahili kama lugha inayowaunganisha Wanyarwanda na raia wengine katika Jumuiya Afrika Mashariki. Zaidi ya hayo, lazima Kiswahili kipewe majukumu yanayotambulika kisheria ili nyanja ambamo kinatumiwa ziweze kudhihirishwa wazi. Hali hii ndiyo ingesaidia kukiendeleza na kuwanufaisha Wanyarwanda hasa wakati huu ambapo Rwanda imeshajiunga na nchi zingine katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambamo Kiswahili ndicho hutumiwa kama lingua franca.

Vilevile, Wizara ya Elimu nayo ingepaswa kuandaa vitabu vya kutosha kulingana na mazingira ambamo wanafunzi Wanyarwanda husomea ili kuwawezesha kupambana na baadhi ya changamoto zinazowakumba katika ujifunzaji wao wa Kiswahili. Hali hii ingesaidia sana kusuluhisha matatizo mengi yaliyo na chanzo chake katika L1. Hivyo basi, wataalamu mbalimbali katika mambo ya isimu na mbinu za ufundishaji wangeajiriwa ili kushirikishwa katika shughuli hiyo na pia kuandaa vifaa vingine vya ufundishaji wa stadi za kuzungumza na kuandika Kiswahili sanifu.

Matokeo ya utafiti huu pia, yameabainisha kuwa muda mfupi uliotengewa ufundishaji wa Kiswahili ni chanzo kikubwa sana cha makosa ya wanafunzi. Tumedhihirisha kwamba ni vigumu mwanafunzi aweze kumudu miundo changamani ya lugha ya pili (L2) katika kipindi cha miaka mitatu tu. Kwa hivyo, ni lazima Serikali ifikirie kurasimisha kwanza ufundishaji wa Kiswahili kuanzia ngazi za chini katika awamu ya kwanza ya shule za upili ili baadaye kiweze kuingizwa katika elimu ya msingi kwani kadiri mtoto alivyo mdogo ndivyo anaweza kujifunza lugha yoyote kwa urahisi.

Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili, silabasi ya somo hili nayo ingefanyiwa marekebisho ili kutosheleza mahitaji ya wanafunzi wa somo hili. Vipengele vya kufundisha lugha hii vingefuatana kwa utaratibu maalumu unaowarahisishia wanafunzi kuelewa somo hili na kujiongezea maarifa katika mazungumzo na maandishi hatua kwa hatua. Aidha, ni wazi kuwa ufanisi wa ufundishaji wa Kiswahili unategemea sana jinsi ambavyo wakuza mitaala na walimu wanavyoshirikiana. Kwa hivyo, kutangamana kati yao ndiko kungewawezesha

kutunga vitabu vya kufundishia, kuunda silabasi na kupanga muhtasari wa somo la Kiswahili kwa njia nzuri inayoafikiana na uwezo wa wanafunzi katika viwango mbalimbali vya ufundishaji wa sarufi ya Kiswahili.

Kama tulivyobainisha katika utafiti huu, baadhi ya viongozi wa shule za upili wana mielekeo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili ambapo wanakidhalilisha na kukidunisha. Kwa hivyo, ni lazima waelewe umuhimu wake na kukipa nafasi yake katika ufundishaji wa lugha kwa jumla. Hali hii ndiyo ingewafanya wajitahidi kutafuta vitabu vya kutosha na walimu wenye uwezo katika ufundishaji wa Kiswahili. Kwa kuwa makosa mengi yamejidhihirisha miongi mwa wanafunzi wa shule zisizo na miundo msingi imara, hasa za shule za vijijini, ni bora viongozi wa shule hizi washrikiane na walimu wao ili kujadili matatizo yanayokabili wanafunzi wao. Hivyo basi, wangeweza kutafuta suluhisho kwa baadhi ya matatizo yanayowakabili kama vile kwa kuongezea wanafunzi wao vipindi vya kuwawezesha kuzungumza na kuandika Kiswahili au kuwatuza wale wanaokitumia.

Mwishowe, utafiti huu umetubainishia kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili hufanyiwa hasa darasani ambapo mwanafunzi anamtegemea mwalimu wake tu. Kwa hivyo, ni vyema serikali ya Rwanda ikififikiria sera mbalimbali za kufundisha lugha hii kupitia vyombo vya habari na magazeti mbalimbali yaliyomo nchini. Magazeti yanayotangaza habari katika Kiswahili nayo yangeanzishwa na kusambazwa katika shule hizi ili wanafunzi waweze kujiongezea ujuzi wao katika matumizi bora ya Kiswahili. Vilevile, serikali ya Rwanda ingefikiria namna ya kushirikisha nchi ambamo Kiswahili kimeshaendelea na kuimarishwa kama vile Kenya na Tanzania

katika utunzi wa vitabu na usambazaji wa majarida na magazeti yanayoandikwa katika Kiswahili.

### 5.5.2 Mapendekezo kuhusu walimu

Ingawa utafiti huu ulibainisha kwamba mikakati mingi muhimu huzingatiwa na walimu katika kuyapunguza makosa ya wanafunzi, matokeo yake yamedhihirisha pia kwamba walimu hawa hawatilii mkazo nafasi ya mwanafunzi katika kuyatambua makosa anayoyafanya na yale yanayofanywa na wenzake. Kwa hivyo, wanastahili kuelewa kuwa nafasi ya wanafunzi katika kutambua makosa yao, kuyachunguza na kuyaeleza ndiyo njia bora ya kupunguza makosa hayo. Kazi za uandishi na uzungumzi katika makundi nazo zingetiliwa mkazo ili kumwezesha mwalimu kushughulikia mambo mengi katika muda mfupi alio nao pale ambapo mada za kuwahamasisha wanafunzi wao kuipenda lugha hii zingejadiliwa.

Kulingana na matokeo ya utafiti huu, imebainika pia kuwa walimu hawapati muda wowote wa kujiongezea ujuzi katika kazi yao ya ufundishaji wa Kiswahili. Kwa hivyo, semina na mafunzo ya muda mfupi yangeandaliwa kwa ajili yao ili kuwawezesha kupata maarifa mengine katika ufundishaji wa Kiswahili na kubadilishana mawazo kuhusu matatizo mbalimbali wanayokumbana nayo katika ufundishaji wao. Isitoshe, makongamano yangeandaliwa kwa kushirikisha wataalamu mbalimbali wa isimu na lugha, wanafunzi kutoka maeneo tofauti ili kuzungumzia baadhi ya maswala muhimu katika ufundishaji wa lugha hii nchini.

### 5.5.3 Mapendekezo kuhusu wanafunzi

Utafiti huu umebainisha pia kwamba wanafunzi wengine hufikiria kuwa Kiswahili ni sawa na Kinyarwanda na kufanya makosa ya kimofosintaksia katika maongezi na maandidshi yao. Hivyo basi, wanapaswa kujua kuwa ingawa lugha hizi zinafanana, kuna tofauti za kiisimu ambazo wanatakiwa kuzizingatia ili waweze kuandika na kuzungumza Kiswahili fasaha kwa kuepuka makosa ya kisarufi yaliyo na chanzo chake katika L1.

### 5.5.4 Mapendekezo ya kufanya tafiti zaidi

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, ni wazi kuwa mapendekezo ya kufanya utafiti zaidi yanahitajika ili kufidia vipengele kadhaa vinavyohusu ujifunzaji wa Kiswahili kama L2 kwa wanafunzi Wanyarwanda. Katika usuli wa utafiti wetu, tumebainisha kuwa kipengele cha kimofosintaksia ndicho msingi wa ujifunzaji na matumizi bora ya lugha yoyote. Hivyo basi, kimeshughulikiwa na kuonyesha makosa yanayofanywa na wanafunzi na jinsi ambavyo walimu hujitahidi kuyasahihisha. Hata hivyo, kazi yetu haikuhusu mbinu za ufundishaji zinazotumiwa na walimu hawa. Kwa hivyo, ni vyema kazi zingine ziweze kuchunguza kipengele hiki ili kuikamilisha kazi yetu.

Isitoshe, kupitia kazi hii, mtafiti alikuwa akiyakuta makosa mengine yaliyofanywa na wanafunzi katika kategoria mbalimbali za sarufi. Kwa hivyo, ni jambo jema kuwa kazi zingine zichunguze makosa hayo yanayofanywa na wanafunzi hawa hasa katika viwango vingine vya sarufi kama vile fonolojia na hata msamiati ili kuikamilisha kazi hii. Ipo haja ya kuchunguza pia lugha kadirifu za wanafunzi wa madarasa ya awamu

ya kwanza katika shule za upili ambapo Kiswahili hufundishwa kama somo lisilo lazima.

**5.6 Hitimisho**

Katika sura hii, mtafiti ameweza kuhitimisha utafiti huu kwa kutoa muhtasari wa tasnifu nzima, kubainisha matokeo ya utafiti, changamoto zilizizomkumba na kutoa mapendekezo mbalimbali kulingana na matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu. Aidha, wito umetolewa kwa wadau tofauti wa ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Rwanda ili kutoa mchango wao wa kuimarisha na kuboresha ufundishaji wa lugha hii miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili nchini humo.

## MAREJELEO


Adewole, S.M. *(1986)*. A Syntactic Basis for Noun Classification in Kiswahili. *Kiswahili*. 53 (1/2). 37-49

Alan, D., (2007). *An Introduction to Applied Linguistics: From Practice to Theory*. Edinburgh. Edinburgh University Press.

Allwright, R.L. (1975), 'Problems in the Study of the Language Teachers Treatment of Learner Error'. In Burt K.M and Dulay H.C. (ed). *New Direction in Second Language Learning, Teaching and Bilingual Education.* Washington D.C.: TESOL. 96-109.

Amando, L., Eduardo E. F., Arburim I. na Christopher P. C. (2007). Teachers' attitudes towards correcting students' written errors and mistakes, *Porta Linguarum*. 10. Universidad de Murcia. 21-30.

Ashton, E.O. (1944). *Swahili Grammar Including intonation*. London. Longman.

Basigayabo, P. (1992). Matumizi ya Kiswahili katika utangazaji nchni Rwanda: Mtazamo wa Kiisimujamii. Tasnifu ya Shahada ya Kwanza. Butare. UNR.

Bickman, L. na Rog D. (2009). *Applied Social Research*. 2nd Ed. London. The SAGE Publications Ltd.

Bizimana, S. (2002). *Imiterere y'Ikinyarwanda*: amajwi, amagambo n'interuro. T1. Butare. IRST.

Brain, J. (1969). *Basic Structure of Swahili*. Eastern African Studies Program. New York. Syracuse University.

Campbell, R. na R. Wales. (1970). The Study of Language Acquisition. In J. *Lyons (ed.) New Horizons In Linguistics.* Harmondsworth: Penguin.

Cheruiyot, C. L. (2011). Matatizo ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa Kipsigis wanaojifunza Kiswahili Sanifu : Mtazamo wa Lugha Kadirifu. Tasnifu ya Uzamili. Nairobi. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Chomsky, N. (1959). Review of Skinner Verbal behavior. *Language*. 35. 26-58.

Cook, V. (1996). *Second Language Learning and Language Teaching*. 2nd ed. New York. Oxford University Press Inc.

Corder, S.P. (1971). Idiosyncratic dialects and errors analysis. In Richards J.C. (ed). *Error Analysis : Perspectives on Second Language Acquisition*. London. Longman. 158-171.

Corder, S.P. (1974). The Significance of Learner's Errors. In Richards J.C. (ed). *Error Analysis : Perspectives on Second Language Acquisition*. London. Longman. 19-27.

Creswell, J.W. (2009). *Research Deseign. Qualitative, Quantitative and Mixed Metdods Approaches.* 3rd Ed. London. The SAGE Publications Ltd.

Dulay, H.C. na Burt M.K. (1973). Should we teach children syntax ? In *Language Learning*. 23. 235-252.

Dulay, H.C. na Burt M.K. (1974). *Errors and Strategies on Child Second Language Learning*. Tesol Quaterly. 8 (2). 129-136.

Ellis, R. (1985). *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford. OUP.

Ellis, R. (1994). *The Study of Second Language Acquisition.* Oxford. OUP.

Habwe, J. na Karanja P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili.* Nairobi. Jarada Phoenix Publishers Ltd.

James, C. (1971). An Exculpation of Contrastive Linguistics. In Nickel G. (ed). *Papers in Contrastive Linguistics*. Cambridge. Cambrigde University Press.

Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi maumbo ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam. TUKI

Karangwa, J.D. (1986). Kiswahili katika uwanja wa biashara nchini Rwanda. Tasnifu ya Shahada ya Kwanza. Ruhengeri. UNR.

Katamba, F. (1993). *Morphology.* New York. Palygrave.

Khansir, A. A. (2012). Error Analysis and Second Language Acquisition. In *Theory and Practice in Language Studies,* 2 (5). 1027-1032.

Kiango, J. G. (2002). Nafasi ya Kiswahili katika ujenzi wa jamii mpya ya Afrika Mashariki. *Nordic Journal of African Studies, 11(2).* 185-197.

Kihore, Y.M., Massamba D.P.B. na Msanjila Y.P. (1999), *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam. TUKI

Kihore, Y.M., Massamba D.P.B. na Msanjila Y.P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam. TUKI.

Kimenyi, T. (2003). Hali ya Kiswahili Katika Elimu Nchini Rwanda. Tasnifu ya Uzamili. Ergaton. Chuo Kikuu cha Egerton.

Kithuku, M. (2012). Mofosintaksia ya ngeli ya 9/10 (N/N). Tasnifu ya uzamili. Nairobi. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Krapf, J.L. (1850). *Outline of Grammar of the Suaheli Language with Special Reference to the Kinika Dialect*. Tubingen.

Lado, R. (1957). *Linguistics Across Cultures.* Michigan. The University of Michigan Press.

Massamba, D.P.B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam. TUKI.

Mbaabu, I. (1978). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Kenya Literature Bureau. Nairobi

Mbaabu, I. (1992). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi. Longman.

Mbaabu, I. (1995). *Usahihishaji wa mokosa katika Kiswahili*. Nairobi. Longhorn Kenya Limited.

Mbaabu, I. (2005). Mchango wa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) katika uendelezaji wa Kiswahili. *Kiswahili*. Toleo Maalumu la Jubilei ya Miaka 75 ya TUKI (1930-2005). Dar es Salaam. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. 94-102.

Mdee, J.S. (1986). *Kiswahili: Muundo na matumizi yake*. Nairobi. Intercontinental Publishers Ltd.

Mgullu, R. (1990). *Uainishaji wa kimofolojia wa ngeli za nomino za Kiswahili*. MULIKA, 22. TUKI. Dar es Salaam. 53-67.

Mgullu, R. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi. Longhorn.

MINEDUC. (2008). *Nine Years Basic Education Implementation. Fast Track Strageties*. Kigali.

MINEDUC. (2013). *Education Sector Strategic Plan 2013/14-2017/18*. Kigali.

Mohamed, A. M. (1988). *Sarufi mpya na mazoezi ya ziada*. Nairobi. Foundation Books Limited.

Mohamed, A.M. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi. East African Publishers.

Mudhune, E.S. (1994). A Contrastive Analysis Approach to the Learning of Swahili Morphosyntax by Luo Learners. Tasnifu ya Uzamili. Nairobi. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mugenda, O.M. na Mugenda A.G. (2003). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Methods*. Nairobi. Acts Press.

Mugenda, O.M. na Mugenda A.G. (2012). Research Methods Dictionary. Nairobi. Applied Research & Training Services.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Munyakazi, L. (1984). *La Situation sociolinguistique au Rwanda. Aspect endocentrique et exocentrique.* Tasnifu ya Uzamifu. Nice. Universite de Nice.

Musau, P.M. (1993). *Aspects of Interphonology : The Study of Kenyan Learners of Swahili.* Tasnifu ya Uzamifu. Bayreith. Bayreuth African Studies.

Mutugu, B.N. (2001). Makosa ya kileksia katika insha na chanzo chake: Uchunguzi wa shule tano za upili wilayani Kiambu. Tasnifu ya Uzamili. Nairobi. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Myachina, E.N. (1981). *The Swahili Language: A Descriptive Grammar*. London. Routledge & Kegan Paul.

Nemser, W. (1971). *Approximate Systems of Foreign Language Learners*. In Richards. J. (ed). *Error Analysis : Perspective of Language Acquisition.* 55-64.

Nkusi, L. (1983). L'augment aurait-il un rôle sémantique en Kinyarwanda? in *Le Kinyarwanda, langue bantu du Rwanda,* Etudes linguistiques. P. Jouanet (Mhariri.). 1983. SELAF. Paris. 97-112.

Norrish, J. (1983), *Language Learners and their Errors*. London. The Macmillan Press Limited.

Ntakirutimana, E. (2000). *Uhusiano kati ya Ulughamoja na Maendeleo.* Makala ya kongamano la Kimataifa. Kiswahili 2000. TUKI. 95-102

Ntawigira, P. (2011). Language use in the Educational System of Rwanda. A Case Study of Kiswahili in Secondary Schools. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Dar es Salaam. Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Obuchi, S. na Mukhwana A. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele*. Kijabe. A.I.C. Kijabe Printing Press.

Onyango, J. (1997). Uziada wa kisarufi katika Kiswahili cha wanafunzi wa Kinyala: Mtazamo wa uchanganuzi linganuzi. Tasnifu ya Uzamili. Nairobi. Chuo kikuu cha Kenyatta.

Orodho, J.A. (2009). *Elements of Education and Social Research Methods*. Maseno. Kanezja Publisher.

Polomé, E.C. (1967). *Swahili Language Handbook*. Wshngton D.C. Center for Applied Linguistics

Richards, J.C. (1974). *Error analysis: Perspectives on Second Language Acquisition.* London: Longman

Schachter, J. na Mrianne, C. M. (1977). Some Reservations Concerning Error Analysis. *TESOL Quarterly*. 2 (4). 441-451.

Seale, C. (2012). *Researching Society and Culture*. 3rd Ed. London. The SAGE Publications Ltd. London.

Selinker, L. (1972). Interlanguage. In *IRAL*. Vol X/3. Reprented in Richards J.C. (Mhariri). (1974). *Error Analysis: Perspectives on Second Language Acquisition*. Longman. London. 31-54

Shahim, N. 2011. Error treatment in TESOL Classrooms. *Jordnan Journal of Applied Science "Humanities Series". 13 (1).* 207-206.

Shimamungu, E. (1998). *Le Kinyarwanda. Initiation à une langue bantu.* Paris. L'Harmattan.

Singleton, D. na Lengyel, Z. (1995). The Age Factors in Second Language Learning Acquisition. Dublin. Multilingual Matters Ltd.

Skinner, B.F. (1957). *Verbal Behavior*. Englewood Cliffs: Prentice Hall.

Steere, E. (1969). *Swahili Exercises. Revised and partly re-written by Hellier A.B.* London. The sheldon Press.

Steere, E. (1865). *A Handbook of Swahili Language* (as Spoken at Zanzibar). London. The Sheldon Press

Steinberg, D.D., Nagata H. na Aline D.P., (1982). *Psycholinguistics, Language, Mind and World.* Second Edition, Pearson Education Limited.

TUKI. (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Dar es Salaam. Chuo  Kikuu cha Dar es Salaam.

## VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO A: HOJAJI KWA WANAFUNZI

*Darasa:*

*Shule:*

**i) Kamilisha sentensi zifuatazo kwa kutumia viambishi vinavyofaa. Ziandike sentensi hizo katika wingi pale panapohitajika.**

*Mfano: Mtoto …… (changa) ………….. (mefika).*

*Jubu : Umoja: Mtoto mchanga amefika*

*Wingi: Watoto wachanga wamefika*

1 Ng'ombe……………..(angu)……… (nakula) majani

2 Nyumba ………….(refu)…….. (tajengwa) hapa.

3 Mbuzi……..(nne)……………. (meuzwa)

4 Mkono……….. (enyewe)………(mevunjika)

5 Kisu……(angu) ……(mepotea).

6 Ukuta………. (kubwa) ……..(mebomolewa)

7 Ufa …….(le)…….(tazibwa).

8 Mchele ………….(hu) ………..(tapikwa) kesho.

9 Jiwe …….(moja)……(litupwa)

10 Koti………… (zuri)……………(tavaliwa)

11 Udevu………… (refu) …….(mekatwa)

12 Mahali ………..(enyewe) kumesafishwa.

13 Kipofu ………….(moja)………….(mefika) hapa

14 Mkulima.............(pi) ..............(mevuna)?

15 Shamba (amba)...... ..........(talimwa) ni ..............(ao).

16 Ukuni ..........(enyewe) ...........(taokotwa).

17 Chai............ (enyewe)............(mepikwa)

18 Ukubwa ............(pi) ................(nakupendeza)

19 Mahali (hu)................... mna joto.

20 Mstituni (hu) ............kunatisha

21 Maji (ha)............ ......... (tachemshwa) na mama..............(ake).

22 Mwili ........(ke) ni ..........(safi)

23 ........(yu) ndi.....muuguzi ........(enyewe)

24 Nitanunua nguo (o-ote) .......(ekundu) nifikapo mjini.

25 Wali ......(ote) ......(meliwa)

**ii) Tunga insha kuhusu mada ifuatayo (ukurasa mmoja unatosha):**

"Ufugaji kijijini mwangu".

**KIAMBATISHO B: HOJAJI KWA WALIMU**

**Shule:** ☐

**Darasa:** ☐

**Elimu:** ☐

*A2 (Cheti)*

*Masomo:*…………………………………………………………………….

*A1 (Stashahada)*

*Masomo:*………………………………………………………………………

*A0 (Shahada)*

*Masomo:*…………………………………………………………………….

**Tajiriba yako ya ufunzaji wa Kiswahili:**

*Mwaka mmoja hadi miwili* ☐

*Miaka mitatu hadi minne* ☐

*Miaka mitano au zaidi ya miaka mitano* ☐

1 Unatumia vitabu gani katika ufunzaji wako wa sarufi?

……………………………………………………………………………………………

2 Unaona kuwa vinakutosha ili kukidhi malengo yako ya masomo unayotayarisha?

i) Ndiyo ☐ Hapana ☐

ii) Toa maoni yako.

……………………………………………………………………………

3 Kuna kasoro zozote za kisarufi unazozitambua katika vitabu hivyo?

i) Ndiyo ☐ Hapana ☐

ii) Kama zipo, zitaje : ...........................................................

iii) Unafanya nini ili uweze kuepuka athari zake katika ufundishaji wako?...................

4 Una maoni gani kuhusu mpangilio wa silabasi unayofuata katika ufundishaji wako ?

i) Vipengele vya kufundisha ni vingi

ii) Vipengele vya kufundisha ni vichache

iii) Vipengele havifuatani vizuri

iv) Vipengele vinafuatana vizuri

v) Toa maoni kutetea hoja zako

.......................................................................................................

..................................................................................

## KIAMBATISHO C: KIONGOZI CHA MAHOJIANO KWA WANAFUNZI

**Simulia wenzako kisa chochote ukipendacho:** chaweza kuhusu jambo lililokufurahisha maishani mwako, siku yako ya kwanza ya kufika sekondari, safari iliyokufurahisha, michezo iliyokufurahisha, mkasa ulioshuhudia kama vile ajali, wizi, na kadhalika.

## KIAMBATISHO D: KIONGOZI CHA MAHOJIANO KWA WALIMU

1 Kuna vipengele vyovyote vya kisarufi vinavyotatiza wanafunzi wako?

2 Ni vipengele vipi vya sarufi vinavyotatiza wanafunzi wako katika ujifunzaji wao wa sarufi ya Kiswahili?

3 Ni aina gani za makosa ya kisarufi wanayoyafanya wanafunzi wako?

4 Unafikiri makosa ya kisarufi ya wanafunzi yanatokana na nini ?

5 Ni mikakati ipi unayofanya ili kupunguza makosa ya kisarufi ya wanafunzi wako?

6 Ni mapendekezo gani uliyo nayo kwa washikadau wa elimu kuhusu kukuza sarufi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili nchini Rwanda?



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY